Hakikat Kitabevi Toleo Namba: 3

# MAADILI YA UISLAM

**Ali bin Emrullah** **Muhammed Hadimi**

Toleo la Kituruki lilitolewa na

**Hüseyn Hilmi Işık**

**TOLEO LA TATU**

**Hakikat Kitabevi**
Darüşşefeka Cad. 53/A P.K.: 35
**34083** Fatih-ISTANBUL/TURKEY
Tel: 90.212.523 4556–532 5843 Fax: 90.212.523 3693
http://www.hakikatkitabevi.com
e-mail: info@hakikatkitabevi.com
-2023-

## KALIMATU TANZIH

**Subhanallah wabihamdih subhanallahil adhim**. Kalima hii ya Tanzih inapatikana katika **tarjama ya maktubaat** katika barua za 307 na 308. Wale watakaoisoma hii asubuhi na jioni mara mia hufutiwa dhambi zao. Huokoka na shida zao. Na huhifadhiwa na kutenda tena maasi.

---

Anasema Hadhrat Imam Rabbani katika juzuu ya kwanza barua ya 275 kitabu cha **Maktubaat**:

Nyinyi mmezipata neema hizi kwa  kufunza elimu za kiislam na kueneza hukmu za fikh. Katika sehemu hizo ujinga ulitopea na bid'a ilienea. Allah amekupeni mapenzi ya yale anayoyapenda. Kazi ya kueneza uislam ameipitishia kwenu. Kwa hivyo jitahidini kusomesha uislam na kueneza hukmu za fikh kwa kiasi mtakavyoweza. Mambo haya mawili ndio msingi wa furaha zote, ndio njia ya kupanda daraja na ndio sababau ya kuokoka. [Tunashukuru kwamba kuna uhuru wa kuandika na kueneza vitabu sahihi vya dini. Ni wajibu kwa kila muislam kuisaidia dola ambayo inatoa uhuru huu.]

---

## KUMBUSHO LA MCHAPISHAJI

Yeyote anaetaka kuchapisha kitabu hiki kwa lugha yake asili au kukitafsiri kwa lugha yoyote, tunatoa ruhusa yetu kwake kufanya hivyo. Wale wote wanaofanikisha jambo hili lenye faida kubwa, tunawaombea baraka kwa Allah na kuwashukuru sana. Ruhusa ya kuchapisha kitabu hiki tunaitoa kwa sharti ya kwamba kitachapishwa kwa karatasi zenye ubora toshelevu na mpangilio na usanifu wa maandishi uwe mzuri usio na makosa.

---

## TAHADHARI

Wamishionari wanafanya jitihada kubwa kuutangaza ukristo. Wayahudi wanafanya jitihada kutangaza mafunzo ya dini yao. Hakikat kitabevi; taasisi ipatikanayo huko Istanbul; inafanya jitihada ya kueneza elimu ya kiislam. Wamasoni nao wanafanya jitihada kubwa kuzipiga vita dini. Mtu mwenye busara, ufahamu na dhamira atachagua kwa uelewa wake na kulisaidia lile lililo sahihi kati ya makundi haya ili kuweza kuwaokoa viumbe wote. Hakuna lililo bora zaidi kuliko kujitolea kwa ajili ya kuwahudumia watu. Leo, vitabu vya dini vilivyo mikononi mwa mayahudi na wakristo, viitwavyo Injil na Taurati, wao wenyewe wanakubali kuwa viliandikwa na binadami. Ama Kur-an Karim imetoka kwa Allahu taala na iko safi. Mapadri wa kikristo na  marahibu wa kiyahudi wote wanatakiwa kusoma vitabu vinavyotolewa na Hakikat Kitabevi kwa uangalifu na insafu na wajaribi kuvifahamu.

# Maudhui ya Kitabu


Maudhui ya Kitabu ........ - 3 -
MAADILI YA KIISLAM ........ - 5 -
TABIA MBAYA NA NJIA ZA KUJIKOMBOA NAZO ........ - 11 -
TABIA MBAYA NA TIBA YAKE ........ - 14 -
UKAFIRI ........ - 20 -
UJAHILI ........ - 30 -
PUPA LA MALI NA ULWA ........ - 30 -
WOGA WA KUAIBISHWA ........ - 32 -
KUPENDA KUSIFIWA ........ - 34 -
BID'AT IITIKADY ........ - 34 -
MATASHI YA NAFSI ........ - 35 -
KUAMINI KWA KUIGA ........ - 39 -
RIYA ........ - 42 -
MATARAJIO MAREFU ........ - 48 -
TAMAA ........ - 50 -
KIBURI ........ - 57 -
THAMANI YA ELIMU NA WANAZUONI ........ - 75 -
KUJIDHALILISHA ........ - 80 -
KUJIONA ........ - 82 -
HASAD ........ - 84 -
CHUKI ........ - 92 -
USHAMATA ........ - 96 -
KUHAMA ........ - 97 -
WOGA ........ - 99 -
TAHAWWUR (USHUPAVU) ........ - 99 -
GHADAR ........ - 105 -
KHIYANA ........ - 105 -
KUVUNJA AHADI ........ - 106 -
DHANA MBAYA ........ - 108 -
KUPENDA MALI ........ - 110 -
TASWIF ........ - 113 -
KUPENDA WATU WAOVU ........ - 114 -
KUWAFANYIA UADUI WANZUONI ........ - 116 -
FITNA ........ - 117 -
MUDAHANA NA MUDARAA ........ - 121 -
INADI NA KUJITUKUZA ........ - 122 -
UNAFIKI ........ - 123 -

KUTOKUFANYA MAZINGATIO................................................... - 123 -
KUMUOMBEA MUISLAMU DUA MBAYA.................................... - 125 -
KUMPA JINA BAYA MUISLAMU .................................................. - 126 -
KUKATAA KUTOA MSAMAHA.................................................... - 127 -
KUITAFSIRI KUR-AN KARIM KWA MAKOSA ................................ - 128 -
KUFANYA HARAMU KWA MSISITIZO ........................................ - 130 -
KUSENGENYA ............................................................................... - 131 -
KUTOKULETA TOBA ...................................................................... - 134 -
UZINDUZI MUHIMU....................................................................... - 143 -
MAADILI YA KIISLAM...................................................................... - 144 -
SEHEMU YA PILI ............................................................................. - 144 -
UTANGULIZI ................................................................................... - 144 -
NYONGEZA YA KWANZA YA UTANGULIZI.................................. - 157 -
NYONGEZA YA PILI YA UTANGULIZI .......................................... - 163 -
ELIMU YA MAADILI NA MALEZI KATIKA UISLAM ........................ - 168 -
MLANGO WA KWANZA................................................................ - 168 -
MLANGO WA PILI ......................................................................... - 170 -
MLANGO WA TATU........................................................................ - 177 -
MLANGO WA NNE ......................................................................... - 181 -
MLANGO WA TANO........................................................................ - 184 -
MLANGO WA SITA ......................................................................... - 188 -

# MAADILI YA KIISLAM

## Dibaji

***Tuanze kitabu chetu hiki kwa jina la Allah***
***Jina la Allah ndio ngao bora. (kimbilio)***
***Neema zake hazipimiki wala hazihesabiki***
***Yeye ndie mfalme mkuu mwenye huruma na msamehevu***

Allahu taala ni mwenye huruma kwa watu wote walio duniani. Huwaumbia na kuwapelekea neema zote wanazozihitajia. Na ili waweze kupata furaha ya hapa duniani na huko akhera basi pia huwafunza yeye namna ya kuzitumia neema hizo. Imam Rabbani katika barua ya 259 anatujuvya kwamba wale makafiri ambao kamwe hawakuwahi kusikia neno kuhusu Uislam katika maisha yao hadi wakafa, basi hao hawataadhibiwa kwenye Jahannam na kwamba baada ya kuhisabiwa watatoweka kama ilivyo kwa wanyama. Ama wale watakaosikia juu ya Uislam na kuupa mazingatio basi hao wataingizwa peponi. Allahu taala ametoa nafasi ya umri mzima kwa ajili ya kufanya mazingatio. Wale ambao awali walidanganywa na nafsi zao, marafiki waovu, vitabu au njia nyengine potofu za habari wakaangukia kwenye upotevu, lakini baadae wakagutuka na kurejea kwenye imani basi hao Allah atawapa msamaha wake. Hawa atawaokoa na ule msiba wa milele. Ama wale madhalimu waovu hawatopata uongofu wake. Hawa atawaachia waendelee kuwemo kwenye shimo la upotofu walilojichagulia na kulipenda. Na wale waumini ambao kufuatana na amali zao imethibiti kwao kuingia motoni, hao kwa maamuzi yake Allahu taala baada ya kuwaadhibu kwenye Jahannam kwa kiasi ya makosa yao, basi atawaingiza peponi. Yeye Allahu taala pekee ndie muumba wa kila kitu, mwenye kukifanya kiwepo kila kiliopo na mwenye kuvilinda vyote hivyo na vitisho na majanga.

Mtu yeyote, wakati na pahala popote akimsifu na kumshukuru mtu mwengine yeyote, kwa sababu yoyote na muda wowote, basi afahamu hizo sifa na shukran zote zinamstahikia Allahu taala kwa sababu yeye Allah ndiye muumbaji asili na mteremshaji wa neema zote. Bila ya yeye kuwakumbusha, kuwapa nguvu na kuwawezesha, basi hapana mja mwenye kuweza kutenda wema au uovu. Ni yale

ayatakayo yeye tu ndio huwa na asilolitaka haliwezi kutokea. [Katika hadith qudsy anasema (**nimewaumba binadamu ili watukuke kwa kunijua mimi**). Si sahihi kusikia hadithi hii ukasema makafiri hapa duniani hawamuamini Allahu taala kwa hivyo hii hadithi haiwafikiani nao. Kwa sababu hata hao wanazuoni na mawalii wanaanza kumfahamu Allahu taala baada ya kufikia daraja fulani la elimu au umri fulani. Makafiri vile vle watamtambua Allahu taala watakapofika akhera. Hakuna ambae hatomtambua.]

Hamdu (kumhimidi Allah) maana yake ni kuamini kwa moyo na kutamka kwamba neema zote huumbwa na kuteremshwa na Allah. Shukru (kumshukuru Allah) maana yake ni kuzitumia neema katika yale yanayoridhiwa na hukumu za Uislam. Neema ni yale mambo yote yenye faida. Haya yameandikwa katika vitabu vya maulamaa wa ahlu sunna, maarufu wao wakiwa ni wale maulamaa wa madhehebu manne.

Sala na salamu zetu zimfikie kipenzi chetu, mtume wa Allah, alie mkamilifu kuliko watu wote, Muhammad aliyhi salaam pamoja na jamaa zake na masahaba zake wote "ridhwanullahi taala alayhim ajmain" walioteuliwa kupokea elimu na mwenendo wake mwema!

Waislam wanalazimika kujifunza elimu za kiislam. **Elimu za kiislam** zina matawi mawili makuu nayo ni **Elimu ya dini** na **Elimu ya sayansi**. Wanamageuzi wa dini wameiita elimu ya sayansi kwa jina la **elimu ya kireshinali** na ile ya kidini wameiita **elimu ya kiskolastiki.** Hii elimu ya sayansi pia huitwa "**hikma**". Mtume swallallahu alayhi wasallama amesema **(Hekima ni kama mali iliyompotea muislamu. Popote atakapoikuta aichukue).** Hadithi sharif hii inatuamrisha kujifunza elimu za sayansi. Elimu ya dini ina matawi ishirini, manane yakiwa ndio makuu na kumi na mbili ni madogo. Miongoni mwa hayo matawi manane makuu moja wapo ni hii elimu ya **maadili ya kiislam**.

[Wale walioelimika kisayansi na kuwa na maadili mema hao ndio **waliostaarabika**. Ama wale walioendelea kwenye elimu ya sayansi ikawawezesha kujenga viwanda vikubwa vikubwa bali wasiwe na maadili mema hao huwa watu **wasiostaarabika**, **madhalimu** na madikteta. Na wale wasio na elimu ya sayansi bali pia wakakosa na maadili hao hubakia kuwa **washenzi** na wachafu. **Ustaarabu** ni ile hali ya kuimarisha makazi na kutoa huduma kwa jamii. Hili hufanyika kwa mchanganyiko wa elimu ya sayansi, sanaa na maadili. Kwa ufupi sayansi na sanaa vinapokutana na maadili mema hutumika kwa manufaa ya binadamu na huo huwa ndio **ustaarabu**. Madhalimu hutumia elimu yao hiyo kwa kumkandamiza binaadamu. Hapa

inatupambazukia kwamba muislamu wa kweli ni mtu mwenye maendeleo na wale wasio waislamu ni wenye mashaka na huzuni katika maisha. Bila ya shaka ustaarabu ni kuweza kujenga miji kwa majumba na miundo mbinu mengine, jambo ambayo huwezekana kwa kutumia elimu ya sayansi na teknolojia. Maendeleo ya teknolojia ni kuengeza ugunduzi mpya juu ya ule uliofikiwa na kizazi kilichopita. Maisha ya binaadamu huwa ya amani na utulivu, pale tu maadili ya kiislam yanapofatwa.]

Ni fardhi kwa muislamu kusoma elimu za kiislam kwa kiasi kinachohitajika. Kuna vitabu vingi vilivyoandikwa na wanazuoni juu ya mada hii ya maadili ya kiislam. Miongoni mwavyo ni **Akhlaqi Nasiri** kilichoandikwa na Nasrudyn Muhammad Tusi, **Akhlaqi Jalali** kilichoandikwa na Jalaluddin Muhammad Dawani na **Akhlaqi Muhsini** kilichoandikwa na Husein Waizy Tusi. Mlango wa kwanza wa kitabu chetu hichi ni tafsiri ya kitabu kiitwacho **Barika** cha muandishi Abu Said Muhammad Hadimi “rahimahullahu taala”. Katika mlango huu tumebainisha zile tabia zisizo njema ambazo zimekatazwa na Uislam na tumeainisha njia za kutumia ili kujikinga bali pia kujitibu, mtu akiwanazo. Tabia hizi mbaya ni maradhi ya moyo wa muislamu na yanaweza kumsababishia kufa kwa roho na moyo kwa milele. Mlango wa pili wa kitabu chetu tutaelezea maana ya maadili na vigawanyo vyake tukiangaza kwenye mlango wa mwanzo wa kitabu kiitwacho **Akhlaqi Alai** kilichoandikwa kwa kituruki na Ali bin Amrullah “rahimahullahu taala” aliyekufa mwaka 979 Hijria sawa na [1572 miladi] huko Edirne Turkey.

Wale vijana wetu wema watakaokisoma kitabu hiki watafahamu kwamba mababu zao walikuwa ni watu wenye afya njema na maadili mazuri, wachapa kazi na waliostaarabika. Hayo yatawaokoa na uongo, uzushi na upotofu ulioandikwa na maadui wa Uislam.

Nasrudyn Tusi jina lake hasa ni Muhammad bin Fakhrudyn. Alizaliwa Tus (Mash-had) mwaka 597 Hijria na akafia Baghdad katika mwaka 672 Hijria [1273 A.D.]. Alikuwa ni Shia. Ni mmoja kati ya wale waliokuwa sababu iliyompelekea Hulagu kuiharibu Baghdad na kuuwa Malaki ya waislam. Baadae alikuwa ndie waziri mkuu wa Hulagu na alianzisha akademia na maktaba yenye uwezo wa vitabu zaidi ya 400,000. Yeye binafsi aliandika vitabu vingi sana.

Jalaludyn Muhammad Dawany “rahimahullahu taala” alizaliwa mwaka 829 hijria na kufa mwaka 908 hijria [1503 A.D.] huko Shirazi. Alikuwa ni mmoja kati ya wanazuoni mahiri na ameandika vitabu vingi

sana. Kitabu chake **Akhlaki Jalali** kimeandikwa kwa lugha ya kiajemi. Chapisho lake la nane lilichapishwa mwaka 1304 hijria [1882 A.D.] huko India. Kitabu hiki kimetafsiriwa kwa kiingereza.

Huseyn Waizy Kashify "rahimahullahu taala" alikuwa ni mlinganiaji katika mji wa Hirat. Alikuwa akitoa nasaha juu ya mlingano kw watu wanaotaka kuoana. Alikufa mwaka 910 hijria [1505 A.D.] huko Hirat.

Enyi vijana wema! Enyi wajukuu wa mashahidi walioutumia umri wao wote na waliotoa roho zao kwa ajili ya kujifunza na kueneza Uislamu na maadili yake mazuri! Mababu zenu wamekufikishieni na kukuachieni amana, mafunzo sahihi na yaliyo kamilika ya dini yenu na maadili yake hivyo jifunzeni hayo kwa hima! Wale wanaoikodolea macho nchi yenu iliyo njema na wakafanya uadui kwa nafsi, mali au maadili mema basi pambaneni nao maadui hao kwa nguvu zenu zote ili kuzihami amana hizo! Eneeni kila mahali na muwafikishie watu furaha ya milele! Eleweni kwamba dini yetu inatuamrisha kuwa na tabia njema, kupendana, kuwaheshimu wakubwa na kuwahurumia wadogo, na kuwatendea wema watu wote wenye dini na wasio na dini! Kila mwenye haki mpeni haki yake, na kila aliestahiki ujira mpeni ujira wake! Msiende kinyume na kanuni na amri za dola! Lipeni ushuru wenu kwa wakati wake! Msisahau kwamba Allah siku zote yuko pamoja na walio wakweli! Tupendane na tusaidiane ili Allahu taala nasi atusaidie!

Wanazuoni wanaeleza kwamba Allahu taala ameumba ndani ya binaadamu vitu vitatu ambavyo ni akili, moyo (maanawy) na nafsi. Vitu hivi si vyenye kuonekana. Kuwepo kwa vitu hivi tunakufahamu kutokana na athari za kiutendaji za vitu hivyo na katika yale tuyasomayo kupitia mafunzo ya dini. Akili na nafsi viko kwenye ubongo. Moyo (maanawy) nao uko kifuani upande wa kushoto, kwenye pande la nyama la moyo wa kibaiolojia. Vyote hivyo vitatu si viungo vyenye kushikika wala havikai pahali kwa kujaza nafasi. Kuwepo kwake ni sawa na kuwepo umeme kwenye tungi au kuwepo usumaku kwenye vifaa husika. Akili hufanya kazi ya kufahamu elimu ya sayansi na kubagua baina ya ile ifaayo kwa Uislam na ile mbaya, potofu. Jema na ovu hubaguliwa kwa vipimo vya Uislam. Akili yenye kuufahamu na kuufata Uislam huitwa **Aklin Salim** (akili iliyo sawa). **Ujinga** ni ile hali ya uchache wa akili na kubabaikababaika. Ama kukosa akili kabisa huwa ni **wendawazimu**. Akili iiliyosawa huutambulisha moyo (maanawy) yale yaliyosahihi yaliyofunzwa na Uislam. Moyo (maanaway) nao hujenga dhamira ya kuyatekeleza hayo na hapo ndipo mishipa ya

fahamu itokayo kwenye ubongo huanzisha msukumo wa vitendo kwa viungo mbali mbali mwilini. Matamanio ya kutenda mema au maovu kuweka makazi kwenye moyo huu (maanawy) ndio hujenga tabia. Nafsi hupenda yale mambo yenye kukipa ladha kiwiliwili bila ya kujali kwamba mambo hayo ni mazuri, mabaya, yenye faida au hasara. Matamanio ya nafsi huwa hayaendani na matakwa ya Uislam. Hata hivyo nafsi hutumia nguvu na kulazimisha mambo hayo yafanyike. Ndiyo pale huudanganya moyo na kuughilibu kuwa yale maovu yenye madhara eti ndio mazuri. Hivyo huufanya moyo utekeleze hayo maovu ili hiyo nafsi ipate kuridhisha matashi yake. Ni lazima kushikamana vyema na amri za Uislam ili kuuongezea nguvu moyo na kuidhoofisha nafsi ili isiweze kuuhadaa moyo na kumfanya mtu kuwa mwenye tabia mbaya. Kama ambavyo akili hupata nguvu kwa kuusoma Uislam basi moyo nao vile vile huengezeka nguvu kwa kuutekeleza Uislam. Katika utekelezaji wa matendo ya kiislam lazima ipatikane **ikhlas**, yaani kutekeleza ibada kwa kuwa tu Allah ameamrisha, na sio kwa sababu au manufaa mengine yoyote. Moyo kuweza kupata ikhlas hutegemea sana na wingi wa moyo huo unavyomkumbuka Allah na mja anavyotaja kwa wingi jina la Allah. Kujifunza njia sahihi ya kuleta dhikri kunahitaji kupata kiongozi (murshid) ambae utasoma kwake na ambae utajifunza kwake namna ya kuyatoa moyoni yale mawazo na hisia za kidunia zilizo kwenye akili na viungo vya mwili. Mawazo ya kidunia yanapomalizika basi moyo wenyewe huanza kumkumbuka Allah. Hii ni kama kuingia hewa kwenye chupa wakati maji yanapotoka. Kuulinda moyo na mawazo ya kidunia hutegemea na [nuru] anayoipata mwanafunzi kutoka kwenye moyo wa mwalim (murshid) wake. Nuru hii hutiririka kutoka moyo mmoja kwenda mwengine kwa fungamano la kimapenzi lililo baina ya hiyo mioyo miwili. Murshid kuwa mji mbali na mwanafunzi wake au kuwa amefariki hakuzuii kutiririka na kufika kwa nuru hiyo. **Murshid** lazima awe ni mtu aliebobea kwenye elimu ya dini, mkamilifu katika utekelezaji, mwenye ikhlas na mwanazuoni wa ahli sunna. Kuwa mtekelezaji wa amri za dini kunaupa nguvu moyo na kuidhoofisha **nafsi**. Hivyo nafsi haipendi moyo ufanye jitihada ya kutekeleza kwa vitendo maamrisho ya Uislam, kuhudhuria vikao na darsa za murshid au kusoma vitabu nya dini. Ndio maana wale wenye kuzifuata nafsi na kuzisaliti akili zao huwa hawana dini. Nafsi haifi, ila inapopoteza nguvu huwa haiwezi tena kuighururi akili.

Leo hii waislam walio duniani wamegawika makundi matatu. Kundi la kwanza ni la wale wafuasi wa masahaba ridhwanullahi alayhim. Hawa ndio **ahli sunna** na ndilo kundi lililookoka **(Firkatu**

**najiya)**. Kundi la pili ni lile la maadui wa masahaba. Hili ni kundi la mashia ambalo ni kundi ovu lililopotea. Kundi la tatu ni kundi adui kwa ahlu sunna na **shia** pia. Hili ni kundi la **mawahabi** au pia huitwa **Najdy** kutokana na kuwa chimbuko lao ni mji wa Najd huko Saudi Arabia. Hili pia huitwa kundi lililolaaniwa kwa vile wamewaita waislam kuwa ni washirikina na Mtume "swallallahu alayhi wasallam" amemlaani yule anaemwita muislamu, kafir. Kundi la mashia limeasisiwa na Wayahudi na lile la mawahabi limeasisiwa na Waingereza. Waturuki ni katika waliolinda kundi la ahlu sunna.

Bila ya kujalili yuko kundi lipi, mtu yeyote mwenye kufata matamanio ya nafsi yake na kuwa na moyo uliopotea basi huyo ataingia katika moto wa Jahannam. Kila muumini anatakiwa aseme sana **(Lailaaha illallahu)** ili kuitakasi nafsi na alete istighfari **(Astaghfirullah)** nyingi ili kuusafisha moyo. Yule mwenye kutekeleza maarimsho ya Uislam basi kwa uhakika dua zake hutakabaliwa. Asiesimamisha sala, mwenye kuwaangalia wanawake wanaotembea uchi, mwenye kula na kunywa vya haramu huyo amekwenda kinyume na mafunzo ya Uislam na dua zake hazitotakabaliwa.

| **Miladi** | **Hijria shams** | **Hijria kamar** |
|---|---|---|
| **2001** | **1380** | **1422** |

# MAADILI YA KIISLAM

## SEHEMU YA KWANZA

Sehemu ya kwanza ya kitabu chetu itaelezea aina arobaini ya tabia mbaya na namna ya kuzitibu. Maandishi haya yote yametafsiriwa kutoka juzuu ya kwanza ya kitabu cha Abu Said Muhammad Hadimy "rahimahullahu taala" kiitwacho **Barika.** Kitabu hiki ni cha juzuu mbili na kimeandikwa kwa lugha ya kiarabu. Kilichapishwa Istanbul katika mwaka 1284 hijria [1868 miladiya]. Kilichapishwa tena mwaka 1411 hijria [1991 miladiya], wachapishaji wakiwa ni Hakikat Kitabevi. Hadhrat Hadimy alifariki mwaka 1176 hijria [1762 miladiya] katika kata ya Hadim huko Konya, Uturuki.

## TABIA MBAYA NA NJIA ZA KUJIKOMBOA NAZO

Mambo yote ambayo yanampa madhara binaadamu duniani na akhera yanatokana na tabia mbaya. Tabia mbaya ndio kinara wa maovu yote. Kujiepusha na mambo ya haram huitwa **Taqwa**. Taqwa ndio ibada thamini kuliko zote kwani kitu chochote unapotaka kukipamba na kukiremba lazima kwanza ukizafishe na kuyaondoa machafu yake. Kwa hivyo bila ya kujisafisha kuepukana na madhambi, utiifu na ibada huwa havina faida. Havipewi thawabu. Ovu lililo kubwa kabisa kupita maovu yote ni **Ukafiri**. Hakuna wema wala kheri yoyote ambayo kafiri ataitenda na akafaidika nayo huko akhera. Hata kama atauliwa kwa dhulma basi kafiri hawi shahidi wala hatoingia peponi kwa hilo. Bila ya kuamini kwanza, hakuna wema wowote unaolipwa thawabu. Taqwa ndio msingi wa mema yote na kabla ya mengine yote inahitaji kujibidiisha kuwa na taqwa. Yafaa kila mtu anasihiwe na aamrishwe kuwa na taqwa. Ili tuweze kuwa na raha na utulivu, udugu na kupendana hapa duniani na huko akhera, ili kuepukana na adhabu ya milele na ili kupata furaha na neema za kudumu basi tunahitaji kuwa na taqwa.

Tabia mbaya ni ugonjwa kwa moyo na unapozidi moyo hufa; yaani husababisha ukafiri. Shirk (ukafiri) ndiyo tabia mbaya kuliko zote na ndio sumu kuu ya moyo. Yale madai ya baadhi ya wasio na imani wanaosema "Mimi moyo wangu uko safi bwana. Wewe angalia zaidi moyo wangu," ni madai yasiyo na msingi. Moyo uliokufa hauwezi kuwa safi.

Ukafiri kuna wa aina tafauti ila ulio mkubwa na muovu zaidi ni **Shirk**. Katika kuutambulisha uovu wa aina yoyote tunaweza kutumia ule uovu wa hali ya juu ili kuwakilisha maovu mengine. Kwa hivyo neno shirk linapokutwa ndani ya Kur-an Karim na hadithi sharif linaweza kuwakilisha aina zote za kufr. Katika aya ya 48 na 116 za Suratun Nisaa zinaweka wazi kwamba hakutakuwa na msamaha kwa mushrik. Aya hizi zinatambulisha kwamba makafiri watadumu milele ndani ya Jahannam.

[Shirk maana yake ni kumpa Allahu taala mshirika au kumfananisha. Mwenye kumfananisha Allahu taala na kitu chengine huitwa **Mushrik** na kile kinachofananishwa na Allahu taala huitwa **Sharik**. Mtu yeyote yule atakapoamini kuwa kuna kitu kina moja ya sifatul uluhiyya basi kitu hicho itakuwa amekifanya ni mshirika wa Allahu taala (Sharik). Zile sifa zilizo mahsusi kwa Allahu taala ambazo ni **Sifatu Dhatiya** na **Sifatu Thubutiyya** kwa pamoja huitwa **Sifatu Uluhiyya**. Kuwepo milele, kuumba, kujuwa kila kitu, kuwapa shifaa wagonjwa ni miongoni mwa mifano ya Sifatul Uluhiyya. Kuamini kwamba kiumbe chochote kile (binadamu, jua, ngombe n.k.) kina Sifatul Uluhiyya hivyo ukakiheshimu, kukitukuza au kukiomba itakuwa tayari umekiabudu kitu hicho. Kwa hilo, vitu hivyo huwa viabudiwa. Kusema maneno au kufanya matendo ya kutukuza na kuadhimisha au kufanya ibada mbele ya picha, masanamu au makaburi ya watu au makafiri hali ya kudhani kuwa wana Sifatul uluhiyya, hiyo itakuwa ni Shirk. Iwapo mtu ataitukuza picha au sanamu ya mtu mwengine kwa dhana ya kuwa huyo anaetukuzwa ni mja mwema wa Allah au ni jamadari mkubwa wa taifa; bila ya kuitakidi kua ana sifatul uluhiyya; basi hiyo haitokuwa shirk wala kufr. Ila inafaa ifahamike vyema kwamba kutukuza au kuadhimisha picha au sanamu ni haram katika Uislam hivyo anaefanya hayo anakuwa ni fasik. Na ikiwa haram hii haipi umuhimu na akawa anaichukulia wepesi basi anaweza kuwa **Murtad** kama ilivyo kwa haram nyengine zote. Mayahudi na wakristo ambao si washirikina, bado wanakua ni makafiri kwa kumkanusha kwao mtume wa Allah Muhammad swallallahu alayhi wasallam. Hawa ni **makafiri wenye kitabu**. Ila linaloweza kusemwa wazi ni kwamba wengi wa wakristo wa leo tayari ni washirikina kutokana na kitendo chao cha kumpa Issa alayhi salam sifatul uluhiyya. Wale walio katika madhehebu ya Barnabos na Aryus ni makafiri wenye kitabu ambao leo madhehebu yao hayapatikani tena.]

Gonjwa kubwa la moyo linalofuata baada ya shirk ni kuamini au kutenda **Bid'a**. Baada ya uovu wa Bid'a linalofuata katika maovu ni

jambo la kutokujiepusha na maasi. Ukiachia mbali kufr na shirk, muumini yeyote atakaefanya dhambi kubwa au ndogo na akafa kabla ya kutubia, anaweza akapata shufaa ya Allahu taala au akasamehewa kwa huruma zake tu Allahu taala bila ya sababu yoyote. Na kama hatopata msamaha wa Allahu taala basi ataadhibiwa kwenye Jahannam hata kama itakuwa ni dhambi ndogo. Dhambi zilizochanganyika na haki za waja wengine ni nzito kusamehewa na adhabu yake huwa kali zaidi. Kutomkamilishia mke mahari yake na kuwazuilia waja kujifunza dini ya haki ni mfano wa kuingilia haki za mja. Hadithi sharif inasema **(Itafika zama, binaadamu hatozingatia juu ya chumo lake kuwa linatokana na vyanzo halali au vyanzo haramu)** na katika hadithi sharif nyengine **(Itafika zama, kushikamana na Uislam itakuwa ni uzito sawa na kukamata kaa limoto mkononi).** Hivyo kujiepusha na haram zote aidha na makruh tahrimy ni jambo la taqwa. Kutotekeleza yaliyo fardhi na yale yaliyo wajibu ni jambo la haram. Kuacha bila udhuru sunna zilizokokotezwa ni makruh tahrimy. Kuacha kutekeleza yale yaliyoamrishwa katika itikadi, amal au akhlaq hupelekea mtu kuadhibiwa huko akhera. Ni wajibu kuyaepuka yale mambo ambayo yatampelekea mja kuadhibiwa, mfano kuacha sala, wanawake kutoka nje bila ya stara ya kisheria ni miongoni mwa dhambi kubwa. Kuacha dhambi yoyote ile ni jambo la lazima. Ila katika kitabu chetu hiki hatutozungumzia mambo ambayo hayatakiwi kuachwa bali tutazungumzia yale mambo yenye kulazimu kuyaacha.

Mambo yasiofaa huwa yanafanywa na moja ya kiungo cha mwili au hata kiwiliwili kizima. Kuna viungo vinane vilivyojipatia umashuhuri zaidi katika utendaji maasi navyo ni moyo, sikio, jicho, ulimi, mikono, miguu, tumbo na utupu. Moyo, ni upulizo uliofanywa juu ya pande la nyama la moyo wa kibaiolojia uliopo kushotoni kwa kifua chetu. Huu ni moyo maanawy na kama ilivyo roho si kitu chenye kugusika. Maasi hutendwa kwa nguvu za hisia zipatikanazo katika viungo husika. Hivyo wale wanaotaka kupata raha na furaha ya duniani na akhera inabidi wavizuie viungo kutenda madhambi. Moyo unahitaji kulelewa na kukuzwa hadi ufikie kuwa jambo la kutofanya maasi kwake ndiyo tabia ya kawaida. Mwenye kusimamisha sala, akajiepusha na maasi hali ya kuwa ni katika ahli sunna, basi huyo ni mtu mwema na huitwa **Muttaqy** au **Salih**. Na atapofikia kupata radhi na mapenzi ya Allahu taala basi huwa ni **Walii** Moyo ambao kuacha maasi kwake ni jambo la mpambano, huo nao huisabiwa ni uchamungu, ila kufikia daraja ya uwalii ni pale moyo unapoacha maasi kwa kuwa ndio tabia yake ya kawaida. Ili kufikia hatua hiyo moyo unahitaji kutakaswa sawa sawa.

**(Na kuusafisha moyo kunahitaji utiifu wa kanuni za Uislamu). Uislam** una mambo matatu ambayo ni elimu, matendo na ikhlas. Hii maana yake ni kujifunza maamrisho na makatazo, kuyafuata yale uliyojifunza na kufanya yote hayo kwa kutaka radhi za Allah tu bila ya sababu nyengine yoyote. Kur-an Karim imezisifia hizo amri tatu. Katika kitabu hiki tutayataja yale mambo yatakiwayo kuachwa ili kuutakasa moyo.

## TABIA MBAYA NA TIBA YAKE

Jambo la awali kwa muislamu ni kuutakasa moyo wake kwani moyo ndiyo kiongozi wa mwili wote. Viungo vyote viko chini ya amri ya moyo. Mtume "swallallahu alayhi wasallama" amesema **(Ndani ya kiwiliwili kuna pande la nyama. Likiongoka hilo basi viungo vyote huongoka na likipotea hilo basi viungo vyote hupotea. Nao ni moyo).** Maana yake ni ule moyo maanawy unaopatikana kwenye pande la nyama la moyo wa kibaiolojia. Moyo ukiwa mwema hutakasika mja na kutokana na tabia mbaya na kupambika na tabia njema. Sura na muonekano wa mtu huitwa **Jumbile** (maumbile). Nguvu zake za moyoni ndio hutengeneza mwenendo wake. Mwenendo muovu hutokana na moyo unaogonjwa. Maradhi haya ya moyo tiba yake ni nzito. Inahitaji kuzijua vyema na kuzitumia kwa umakini dawa zake. Mwenendo ni tabia na matamanio yaliyo ndani ya moyo. Nguvu hizi za moyoni ndio zenye kupelekea kwenye itikadi, maneno na harakati za binadamu. Chaguo tunalofanya katika kutekeleza mambo mbali mbali nalo pia liko chini ya uamuzi wa nguvu hizo.

Kubadilisha tabia kwa kuziacha zile ovu na kufuata zilizo nzuri ni jambo lenye kuwezekana. Hadithi sharif inasema **(Boresheni tabia zenu!).** Ni wazi kwamba Uislam hauamrishi kufanya jambo lisilowezekana. Uzoefu pia unathibitisha hilo. (Uzoefu ni moja kati ya njia tatu za kupata elimu sahihi. Njia nyengine ni kupitia mafunzo ya mitume. Na ya tatu ni ile ya kutumia vipimo). Wanadamu wanatafuitiana kiuwezo katika kubadilisha tabia zao.

Kuna nguvu za aina tatu ambazo hupatikana ndani ya roho ya binaadamu ambazo ndizo asili ya tabia. Nguvu ya kwanza ni nguvu ya upambanuzi au pia huitwa **akili** ambayo imegawika kwenye nadharia na vitendo. Nguvu ya upambanuzi wa nadharia akiwa nayo mtu katika kiwango stahili huitwa **busara**. Hii humuwezesha mtu kupambanua jema kutokana na ovu na haki kutokana na batili. Nguvu hii inapovuka na kupita daraja stahili huitwa **ujuaji**. Mtu mjuaji hulamizisha kutaka kujua yale ambayo hayawezekani kujulikana. Hulazimisha kutaka kuzitolea undani ayaat mutashabihaat. Huzungumzia maswala ya

kadhaa na kadar. Hujikita katika kufanya uchawi na hila za aina nyengine. Vyenginevyo, nguvu hii akiwa nayo mtu chini ya daraja stahiki huwa ni ujinga. Mtu **mjinga** hupata shida kupambanua baina ya jema na ovu. Upambanuzi wa vitendo akiwa nao mtu katika daraja stahili basi huitwa uadilifu. **Uadilifu** ni jambo timilifu lisilo na uchache wala wingi.

Nguvu ya pili ni **Ghadhabu**. Hii ni nguvu ya roho ya kinyama inayomsukuma mtu kufanya matendo dhidi ya vitu asivyovipenda au kuvitaka. Nguvu hii anapokua nayo mtu kwa wastani unaotakiwa humpelekea kuwa shujaa. Huitumia nguvu hii kwenye mambo ya lazima yenye faida. Mfano wa nguvu hizi ni pale waislam wanaposhuka kwenye maidani kupambana na makafiri ambao ni mara mbili au zaidi ya idadi yao wao. Nguvu hizi akiwa nazo mtu zaidi ya daraja stahiki humfanya kuwa fedhuli, mwenye ghadhabu za haraka na fujo. Uchache wa nguvu hii kwa mwanadamu humfanya awe mwoga na kushindwa hata kuchukua hatua stahili inapolazimika.

Nguvu ya tatu inayotengeneza tabia ya binaadamu ni **matamanio**. Hii ni ile hali ya roho ya binaadamu kuyataka yale mambo ambayo inapata ladha njema  hii binadamu huyatumia matashi yake ya kimaumbile kwa kuzingatia uzani wa Uislam. Nguvu hizi zinapozidi kwa binadamu hupelekea **tamaa** na ulafi. Katika hali hii binadamu hukimbilia kukidhi matashi yake au kupata chumo bila ya kujali misingi ya sharia ya Uislamu. Kwake, kupata ni lazima na hajali hata kama itakua ni kwa dhara ya watu wengine. Nguvu hii inapokuwa chache husababisha uzembe na binaadamu huwa hafanyi jitihada stahili katika kufikia mahitaji yake fulani. Hii inaweza pengine ikatokana na maradhi, haya, woga au hata kiburi alichonacho.

Mambo hayo manne yaliyotajwa hapo juu, yaani hekima, uadilifu, iffat na ushujaa, kuwepo katika kiwango stahiki, ndio msingi mkuu wa tabia njema. Wakati binadamu anaposhikamana vyema na hekima; ambayo ni moja kati ya nguvu kuu tatu; basi huzishinda tabia mbaya za ghadhabu na matamanio, hivyo kuzielekeza kwenye tabia njema za ushujaa na iffat, na kumpa furaha maishani. Kinyume chake kama nguvu hizi tatu tulizozitaja itashindikana kuziweka katika kiwango stahiki, na zikapatikana kwa wingi au uchache; hapo zitazaa tabia mbaya. Kiudhati ni kwamba hata katika hali yake ya wastani na kiwango stahiki, tabia nne njema zinazopatikana katika hali hiyo zitahisabiwa kuwa ni ovu kama zitatumika kwa malengo maovu. Mfano wa kuitumia vibaya hekima ni kama mtu kuvaa uchamungu kwa ajili ya kupata mali au ulwa. Kuswali au kushiriki jihadi kwa ajili ya kujionesha

na kutajwa. Mfano wa kuitumia vibaya iffat ni mtu kujiepusha na matamanio fulani kwa nia ya kupata tamanio jengine au kupata ulwa.

Kimsingi ni kwamba kila moja ya hizi tabia njema nne hujulikana kwa dalili zake. Hekima ina jumla ya dalili saba na ushujaa na iffat kila moja yao ina dalili kumi na moja.

**Tiba ya tabia mbaya -** Dawa ambayo ni mjarabu kwa tabia zote mbaya itajumuika kwanza katika kuligundua hilo gonjwa na madhara yake, sababu zake, yaliyo kinyume na hilo gonjwa na athari ya tiba yake. Hatua ya pili itakuwa ni kuaguliwa na kujulikana kuwepo kwa hilo gonjwa jambo ambayo mtu atalitafiti na kulijua yeye mwenyewe au kwa kwa kuaguliwa na mtaalam alie juu yake (mwanazuoni). Muumini ni kioo cha muumini mwengine. Pia ni uzito mtu kuweza kugundua mapungufu yake binafsi. Hivyo njia yenye kupendekezwa ya kumuwezesha mtu kujua mapungufu yake ni kupata ushauri kutoka kwa rafiki muaminifu. Rafiki muaminifu ni yule anaekulinda na maafa na hatari. Rafiki kama huyo kumpata ni shida sana. Ndio maana Imam shafi akasema:

***"Rafiki wa kweli na dawa ya kweli,***
***ni adimu kuvipata bure usihangaike kuvisaka."***

Naye sayyidna Omar "radhiyallahu anhu" akasema,

***"Rafiki yangu alininasihi juu ya mapungufu yangu.***
***Kwa uhakika hio ndio dalili ya udugu wa kweli."***

Kwa vile maadui zako siku zote wako katika kutafuta mapungufu yako na aibu zako ili waweze kukukosoa na kukuaibisha, hilo pia linawezakua jambo jema kwako kwa kuweza kukutambulisha aibu na mapungufu uliyonayo. Marafiki zako wanakupenda na mara nyingi huyafumbia macho makosa na mapungufu yako. Siku moja mtu mmoja alimuomba bwana Ibrahim Adham; ambae alikuwa mwanazuoni mkubwa na walii; amuelezee makosa na mapungufu yake. Bwana Ibrahim Adham akamjibu "Ni vyema utafute mtu mwengine wa kukueleza hayo kwani mimi ni rafiki yako wa muda mrefu hivyo tabia na matendo yako yote yanaonekan ni mazuri tu kwangu." Njia nyengine ya mtu kuyajua mapungufu na aibu zake ni pale aionapo aibu ya mtu mwengine basi kujichunguza na yeye binafsi ili kujigundua kama na yeye anayo aibu ile au hana. Kama atajigundua naye anayo basi atafute njia za kuiondosha. Na hii ndio maana ya hadithi iliyosema **"Muumini ni kioo cha muumini mwengine"** kwa maana ya kwamba mtu atazigundua aibu zake kupitia kuona aibu za wengine. Alipoulizwa Nabii Isa alayhissalam "Hizi tabia njema umefunzwa na nani?" alijibu

“Sikufunzwa na mtu. Niliangalia watu tu. Yale niliyoyaona ni mazuri katika wanayoyafanya nami niliyaiga. Na yale niliyaona ni maovu katika wanayoyafanya mimi nilijilazimisha kutokuwa nayo”. Alipoulizwa Luqman Hakim wapi amejifunza adabu alijibu “Nimejifunza adabu kutokana na nyinyi”. Njia nyengine ya kujifunza tabia njema ni kwa kusoma sira za salafi swalihina, masahaba watukufu na mawalii “rahmatullahu taala alayhim ajmain” na wachamungu wengine.

Mtu ajikutapo na tabia mbovu basi kwanza atafute sababu iliyompelekea kuwa na pungufu hilo. Kisha aiondoe sababu hiyo na kujihimiza kufanya lililo kinyume chake. Ni shida kwa binaadamu kuacha alichokizoea hasa kama ni jambo linalompa ladha. Hivyo kuacha tabia mbaya ni jambo la mapambano na nafsi.

Moja kati ya njia ya kutibu tabia mbaya ni kujenga kisasi na nafsi. Hii ina maana kwamba wakati wowote unapoanguka katika uovu basi kujenga tabia ya kutenda wema wenye kuikandamiza na kuidhoofisha nafsi. Mfano wake ni kula yamini kwamba iwapo utafanya ovu fulani basi utatoa sadaka kiasi fulani au utafunga au utaleta kisimamo cha usiku. Ili nafsi iepukane na mambo hayo mazito basi itajifunza kutokutenda maovu iliyoyazowea. Kujifunza juu ya madhara ya tabia mbaya kwa kusoma au kusikia ni katika njia za tiba zenye faida pia. Kuna hadithi sharif nyingi zenye kuzungumzia madhara ya tabia mbaya na miongoni mwao ni hizi:

**1. (Hakuna dhambi kubwa mbele ya Allah kuliko tabia mbaya).** Hii ni kwa sababu mwenye tabia hii haelewi kuwa ni dhambi na wala haleti toba. Na kwa vile hii ni tabia atakuwa anaendelea kuifanya na hivyo kuwa nyingi dhambi zake.

**2. (Dhambi ambayo binaadamu wanaifanya bila kigegezi wala kuchoka ni kuwa na tabia mbaya).**

**3. (Kila dhambi ina toba yake. Toba ya tabia mbaya hakuna.Binaadmu badala ya kuacha tabia yake mbaya anazidi kuifanya iwe ovu).**

**4. (Kwa namna maji ya moto yanavyoyeyusha barafu, basi ndio hivyo hivyo tabia njema huyayusha dhambi. Na kama ambavyo siki huiharibu asali, basi ni hivyo hivyo tabia mbaya huyaharibu matendo mema ya mja).**

Uadilifu, iffat, ushujaa na hekima isiyotumika kwa nia mbaya, ndio chanzo cha maadili mema. Kuwa mwenye tabia njema na kuweza kuzifanya ziwe endelevu ni lazima kufungamana na marafiki wema wenye maadili mema. Tabia za mtu hufanana na zile za rafiki yake kwani tabia ni kama maradhi ya kuambukiza. Hivyo inalazimika

kujiweka mbali na marafiki waovu. Hadithi sharif inasema **(Dini ya mtu hufanana na dini ya rafiki yake).** Yafaa kujiweka mbali na michezo isiyo na faida na mambo mengine yasiyo na faida kama mizaha na malumbano yenye dhara. Ajihimize muislamu kusoma na kufanya mambo yenye faida. Ajiepushe na mambo yenye kuharibu tabia na kusisimua matamanio ya nafsi kama kusoma vitabu vyenye kuzungumzia ngono na ukahaba na maovu mengine au kupitia njia nyengine za mawasiliano kama redio na televisheni. Azikumbuke faida za kuwa na tabia njema na hasara za kuwa na tabia mbaya na adhabu ya Jahannam. Wale waliofukuzia mali na ulwa hawakufikia malengo yao. Mali na ulwa ni lazima vitafutwe kwa malengo ya kuvitumia kwa kheri na hapo ndipo utulivu unapopatikana. Mali na ulwa visiwe ndio lengo bali viwe ni nyenzo ya kufanyia kheri. Mali na ulwa ni kama bahari yenye kina kirefu na wangapi wangapi wameangamia humo. Kumcha Allahu taala ndio meli ya kuvukia bahari hiyo. Hadithi sharif inasema **(Usiishi duniani kama mkaazi, bali ishi kama msafiri! Wala usisahau kamwe kuwa utakufa!)**. Binadamu si mwenye kudumu hapa duniani. Kila anapozama katika matashi ya kidunia ndio hivyo hivyo huzuni, mashaka na matatizo yake vinavyoengezeka. Yafaa kila wakati kuzikumbuka hadithi sharif zifuatazo:

1. **(Mja mwenye tabia njema atapata daraja ya juu siku ya kiama hata kama ni mchache wa amali).**

2. **(Moja kati ya ibada nyepesi ambayo ina ujira mkubwa ni kuwa mchache wa maneno na mwenye tabia njema).**

3. **(Mja hata kama atakuwa na amali nyingi, tabia mbaya zinaweza kumuangamiza kwenye Jahannam bali hata kumuingiza ukafirini).**

4. Mtume swallallahu alayhi wasallama alielezewa juu ya mtu ambae alikuwa akifunga mchana na kusali usiku ila alikuwa ni mwenye tabia mbaya na akiwaudhi majirani zake na rafiki zake kwa ulimi wake. Mtume “swallallahu alayhi wasallama” alisema juu ya mtu huyu **(kuwa mja wa namna hiyo si vyema. Marejeo yake ni moto wa Jahannam).**

5. Mtume amesema **(Hakika nimetumwa kukamilisha maadili mema).** Dini zote zilizoshushwa kutoka mbinguni zilifunza maadili mema. Dini hii tuliyonayo imeshushwa kuja kukamilisha hayo maadili mema kwa hivyo hatuhitajii mtu mwengine wala chanzo chengine cha kutufunza maadili wakati dini hii ipo.

6. **(Mwenye tabia njema hupata furaha ya duniani na akhera).** Hii ni kwa sababu mtu mwenye tabia njema hujilazimisha kutekeleza hakki na wajibu wake kwa Allahu taala na kwa waja wenzake.

7. **(Moto wa Jahannam hautamchoma mja mwenye tabia njema kwenye kiwiliwili chema).**

8. **(Kuwaunga wale wanaokutenga, kuwasamehe wanaokudhulumu na kuwakirimu wanaokufanyia uchoyo ni katika maadili mema).** Mtu mwenye maadili mema huwasamehe wanaomkosea na kumdhuru kwenye mali yake mwili wake au heshima yake bali pia yeye huwatendea mema.

9. **(Yule mwenye kufanya upole wakati wa ghadhabu, Allah huujaza moyo wake amani na imani).** Huondokewa na khofu na kuwa mwenye amani. Kumfanyia wema yule aliyekukosea ni miongoni mwa daraja za juu kabisa za mwenendo mwema. Ni dalili ya ukamilifu wa mwanadamu. Wale wamfanyiao uadui yeye huwafanyia urafiki. Amesema Imam Ghazali: Nimeona katika **Injili** Nabiyullahi Isa akisema (Akufanyiae uovu usimkabili kwa uovu. Akupigae shavu la kushoto, mgeuzie na la kulia. Na yule akunyanganyae koti lako basi mpe na suruali). Haya yamo hata ndani ya **Injili** iliyobadilishwa iliyo ndani ya mikono ya wakristo wa leo. Yale yaliofanywa na wakristo kwa waislam na wayahudi huko Hispania, Kudus, India na Bosnia katika dhulma na mauaji na zile dhulma wanazofanyiana wenyewe kwa wenyewe kwenye mahakama zao tumezitaja katika kitabu chetu kiitwacho **"could not answer"**. Unyama huu waufanyao unadhihirisha wazi kuwa wao si wafuasi sahihi wa Injili.

Ni wajibu kwa kila muislamu kuisafisha nafsi yake kuepukana na tabia mbaya na kuipamba kwa tabia njema. Kuacha baadhi ya tabia mbaya na kuendelea na nyengine hakumfanyi mtu kuwa na maadili mema. Tasawwuf ni njia ya kumfikisha mtu kwenye ukamilifu wa maadili. [Ile njia isiyomfikisha mtu kwenye maadili mema haiwezi kunasibishwa na tasawwuf. Kama ambavyo katika elimu zote na sanaa zote kunapatikana walio waovu na bandia basi kadhalika katika tasawwuf kuna wengi wasiojua chochote kuhusu dini ya kiislam na tabia zake njema, mashekhe bandia, waovu wenye kujinasibisha na tarika. Tusidanganyike na mashekhe kama hawa. Na wale majahil, waovu wa tabia tusisikilize redio zao wala tusisome vitabu vyao ili tusije tukaangukia kwenye mitego yao.]

Kuna tabia mbaya sitini zilizo maarufu zaidi. Miongoni mwa hizo tumezitafsiri arobaini na kuzieleza katika vigawanyo arobaini hapo chini. Mtu yeyote atakaejizuia na hizi na akaenda kinyume nazo basi atakuwa ni mwenye maadili mema.

## UKAFIRI

1. Ovu lililo kubwa kupita yote ni kumkana Allahu Taala, na kuwa mpagani. Kumkana Muhammad aliyhi salaam nao pia ni **ukafiri**. Malaika, majini na watu wote wanatakiwa kuwa waumini. Ni wajibu kuamini kwa moyo na kuyakariri kwa ulimi yale yote ambayo Allah ameyashusha kupitia mtume wake Muhammad swallallahu alayhi wasallam. **Imani** mahali pake ni **moyoni** (moyo maanawy). Na huu moyo maanawy ni nguvu iliyo juu ya pande la nyama la moyo wa kibaiolojia. Katika hali ambazo kuna kizuizi cha kutamka imani basi inasameheka kufanya hivyo. Mfano wake ni kitisho, maradhi, kutokuwa na ulimi au kukosa wakati kama kwa kufa ghafla. Kuamini kwa kuiga, bila ya kufahamu maana nako pia huwa ni imani. Ni dhambi kutokuzingatia na kufahamu uwepo wa Allahu taala. Kuikataa yoyote kati ya nguzo za imani ni ukafiri sawa na kukataa nguzo zote. Kutokuwa na elimu juu ya nguzo zote za imani lakini ukaungama kwamba zote umeziamini hiyo nayo ni imani. Ili kuweza kuwa mwenye imani ni lazima kuyaepuka yale ambayo Uislam umeyaainisha kuwa ni dalili za ukafiri. Kuibeza japo moja ya hukmu za Uislam, kuidharau Kur-an Karim, mitume au malaika ni miongoni mwa dalili za ukafiri. Kukanusha ni kile kitendo cha kutoamini au kutosadikisha baada ya kusikia. Kutilia wasiwasi pia ni sehemu ya kukanusha.

Kuna aina tatu za ukafiri. 1. Ukafiri kwa ujinga. 2. Ukafiri kwa kukanusha. 3. Ukafiri kwa hukmu.

1.) **Ukafiri kwa ujinga** ni ile hali ya kutokuwahi kusikia au kufikiria lolote kati ya yale ambayo kila mtu anayafahamu kuwa ni ya ukafiri. Ujinga nao uko aina mbili. Kuna ulio mwepesi na ule uliobobea. Mwenye ujinga mwepesi anajifahamu kwamba anaishi ujingani. Hata itikadi ovu hawezi kuwa nayo. (Kwani hana uelewa wa mambo ya itikadi). Hawa ni kama wanyama kwa sababu chenye kumpambanua mnyama na binaadamu ni elimu na uelewa. Bali hawa wanaweza kuwa wako daraja la chini zaidi ya wanyama kwa sababu Wanyama alau kwa uchache wanafahamu yale waliyoumbiwa kwao na huyaendea yale yenye faida na wao na kuyaepuka yale yenye dhara na wao. Kinyume na wajinga hawa ambao pamoja na kujua kuwa wanaishi ujingani hawajitoi katika hali hiyo ovu wala hawaielekei elimu.

[Katika juzuu ya pili, ukurasa wa 259 wa kitabu cha **Maktubaat** cha Imam Rabbany “rahimahullahu taala” anasema “Kwa kiasi ya ufahamu wangu, watu ambao wamezaliwa na kukulia milimani huko na wakawa hawakusikia chochote kuhusu dini. Wakaishi kwa imani za

kishirikina. Hao hawataingia peponi wala motoni. Baada ya kufufuliwa, watahisabiwa, kwa kiasi ya walivyodhulumiana watalipwa kwenye uwanja wa mahshar. Baada ya kila mmoja kupata haki yake, hawa watatoweka kama watakavyotoweka wanyama wengine. Hawatopewa maisha ya milele mahali popote. Kwa vile katika maisha yetu ya kila siku tunashuhudia wengi wenye akili ambao wanakosea, ninapata uzito kusema kuwa Allahu taala atawaadhibu milele hawa waja ambao kwa kutumia akili zao pekee (bila ya wahyi) walishindwa kujua uwepo wa Allahu taala." Wale watoto wa makafiri waliokufa wadogo pia watakuwa katika kundi hili la kutoweka.

Ikiwa utapita muda mrefu baada ya mtume fulani alietumwa kufa na dini ikaharibika na kupotea, wakaishi watu katika jamii ambayo haijui chochote kuhusu Uislam au mitume, basi watu hao nao hawataingizwa motoni, bali watakuwa ni wenye kutoweka. Kadhalika hali ni hiyo hiyo kwa wale watakaoishi katika nchi za kikafiri na wasisikie chochote kuhusu Uislam.]

Ni fardhi kujifunza kwa kiasi kinachohitajika yale yaliyo katika nguzo za imani na yale ya halali na haram. Kutokujifunza mambo haya ni haram. Kuyasikia mambo haya halafu ukaonesha dharau kujifunza huwa ni ukafiri. Ujinga uliobobea ni wale waliobeba itikadi zisizo sahihi. Mfano wake ni kama wanafalsafa wa kiyunani na yale makundi 72 ya kibid'a ya kiislam. Hawa ujahili wao ni mbaya zaidi kuliko wa wale wa awali. Hili ni gonjwa lisilotambulika dawa hili. Isa alayhissalam anasema "Nimetibu viziwi na mabubu. Nimefufuwa wafu. Ila ujahili uliobobea tiba yake sikuipata". Tatizo ni kwamba jahili huyu anadhani kuwa ujahili wake ndio elimu na ukamilifu wenyewe. Hajielewi kwamba ni jahili na mgonjwa wa akili hivyo hawezi kujitafutia dawa. Ni wale tu ambao Allahu taala atawaongoa wakayafahamu maradhi yao ndio watakaoweza kuokoka na janga hili.

2.) **Ukafiri kwa kukanusha** pia huitwa ukafiri wa inda. Pamoja na kujijua kuwa ni kafiri, mja huyu hufanya inda kwa kubakia kwenye ukafiri wake. Sababu ya kubakia kwenye ukafiri huweza kuwa ni kiburi, au mali, ulwa na matashi ya nafsi au kwa kuogopa kuaibishwa. Ukafiri wa firauni na rafiki zake ni wa aina hii. Hawakuamini hata baada kuishuhudia miujiza kadhaa ya Nabii Musa. Walisema "Hatuwezi kumuamini binadamu kama sisi." Hawakuukubali utume wa aliye binadamu kama wao. Wangependelea mtume awe katika malaika. La kushangaza mno ni kwamba waliukubali uungu wa Firauni ambaye ni binaadamu kama wao. Na wakawa wanamuabudu yeye. Mfalme wa Warumi aitwae Harikulas alikataa kuamini kwa kuogopa kupoteza kiti

chake cha ufalme. Wafalme wa Kirumi hupewa jina la Kaysar. Wafalme wa Uajemi hupewa jina la Kisra. Wafalme wa Uhabeshi hupewa jina la Najashy. Sultan wa Uturuki hupewa jina la Khan. Wafalme wa Kibty huitwa Firauni. Sultan wa Misri huitwa Aziz. Sultan wa Himyer huitwa Tubba. Sahaba aitwae Dihya "radhiyallahu taala anhu" alitumwa na Mtume "swallallahu alayhi wasallama" kutoka Madina kwenda Sham kwa ajili ya kumfikishia Harikulas barua ya kumlingania Uislam. Kabla ya Siku ya kufika kwake huko Sham, ulifika msafara wa kibiashara wa Makureshi kutoka Makka ukiongozwa na Abu Sufyan. Harikulas baada ya kupokea barua hiyo alimwita Abu Sufyan kwenye kasri lake na akaanza kumdadisi:

Nasikia huko Madina kuna mtu anaedai utume, je huyu mtu ni kutoka watu wenye kutambulikana au kutoka watu wa tabaka la chini? Kabla ya yeye huyu, ameshawahi kutokea mtu mwengine akadai utume? Miongoni mwa mababu zake huyu alishawahi kutokea aliyekuwa mfalme au amiri? Wafuasi wake ni katika matajiri au ni masikini wasio na uwezo? Harakati zake zinasonga mbele au zinaonekana kusuasua? Je kuna miongoni mwa watu ambao wameingia katika dini yake halafu wakaamua kutoka? Je huyu ni mtu mwongo asietekeleza ahadi anazozitoa? Katika vita anvyopambana anapata ushindi au anashindwa yeye? Baada ya Abu Sufyan kuyajibu maswala yote haya Harikulas akamweleza kuwa hayo maelezo yake yote yanaashiria kuwa huyo mtu ni mtume wa kweli. Abu Sufyan [ambae wakati huo bado alikua hajasilimu] kutokana na ukafiri wake na husda yake kwa Mtume alipachika baadhi ya maneno ya uongo. Pia aliongeza asioulizwa na kusema "Huyu mtu anadai kwamba ndani ya usiku mmoja alisafirishwa kutoka Makka hadi Masjidul Aksa."

Kabla ya Harikulas kusema chochote, mmoja wa waliokuwepo katika majlisi hiyo alisimama na kusema kwamba yeye pia alikuwepo Masjidul Aksa katika huo usiku husika. Kisha akaelezea yale aliyoyashuhudia. Siku iliyofuata Harikulas akaisoma ile barua na kumueleza Dihya kwamba ameyafahamu na kuyaamini yaliyomo ndani ya barua na amemuamini Muhammad kuwa ni mtume wa Allahu taala. Lakini anaogopa kuidhihirisha imani yake kwa umma. Akamtaka aichukue ile barua na kumpelekea rahibu fulani aliepo pale katika vitongoji vya mji ule. Alisema "Huyo ni mtu mjuzi na mweledi na ninatumai atakapoisoma tu barua hii nae ataamini." Na ndivyo ilivyotokea. Yule rahibu alipoisoma ile barua kutoka kwa mtume wa Allahu taala aliamini na kuwataka watu wa kile kitongoji aliopo nao waamini. Kilichotokea ni kwamba watu hao hawakuamini na

wakamuua huyo rahibu. Dihya alirudi kwa Harikulas na kumueleza yaliyotokea huko kwenye hicho kitongoji. Harikulas alimueleza kuwa aliyategemea matokeo hayo ndio maana hata yeye hawezi kudhihirisha imani yake. Kisha akaandika barua na kumpa Dihya kumfikishia Mtume "swallallahu alayhi wasallam" akimuelezea imani yake. Baada ya hapo Harikulas alikwenda Humsa ambao ulikuwa ndio mji mkuu na kuwakusanya viongozi wa nchi. Aliwaeleza kuwa kuna mtu amemtumia barua yenye kuelezea utume wa Muhammad. Akawasomea ile barua na kuwaeleza kuwa yeye ameyaamini yale yaliyomo. Wale viongozi waliopo pale wote walipinga. Alipoelewa kuwa hawatoamini na wataleta upinzani alirudia maneno yake na kuwaeleza kuwa aliyasema yale kwa nia ya kuwapima tu ni kiasi gani wameshikamana na dini yao. Wale wafuasi wake waliposikia hayo walifarjika na wakaporomoka kumsujudia. Harikulas akachagua ukafiri badala ya iman ili kuokoa ufalme wake. Kipindi hicho waislam walikuwa wamekwenda kwenye mji wa Muta kwa ajili ya vita ambako waislam wengi walishuhudia. Wakati Mtume "swallallahu alayhi wasallam" alipoipokea barua ya Harikulas alisema **"Anasema uongo. Hajaiacha dini yake ya Kinasrani!"** Barua ya Mtume swalallahu alayhi wasallam aliyompelekea Harikulas inapatikana katika vitabu vya **Buhari**, **Mawahib** na **Barika**.

3.) **Kufuru kwa hukumu** ni kuhukumiwa mja kuwa kafiri kwa kusema au kutenda yale mambo ambayo Uislam umeyaainisha kuwa ni alama za ukafiri hata kama mja huyo moyo wake utakuwa ni wenye kuamini au ulimi wake ni wenye kutamka imani. Hali ni hivyo hivyo kwa yule mtu ambae atavidharau, kuvidhihaki au kuvitusi vitu ambavyo Uislam umevitukuza. Vile vile kusema maneno yasiofaa kuhusu Allahu subhanhu wataala pia kunapelekea ukafiri. Mfano kusema "Allah anafatilia mambo ya viumbe hali ya kuwa amekaa juu ya Arshi". Au kusema "kama ambavyo umenidhulumu mimi basi Allah na wewe amekudhulumu." Au kusema "Yule fulani ni muislamu gani yule, kwangu mimi yuko sawa na myahudi tu". Kumshuhudisha Allah katika jambo la uongo, kuwadharau malaika, Kur-an Karim au hata herufi katika Kur-an Karim, kuikana sehemu yoyote ya Kur-an Karim, kuisoma Kur-an Karim pamoja na vitumbuizo vya muziki, kuzikataa au kuzisema vibaya aya sahihi asili za Injili na Taurati, kutumia herufi za Shazi kuisoma Kur-an Karim na kudai kwamba hiyo ndiyo Kur-an Karim yenyewe yote hayo ni kufur. Kusema maneno yenye kumdhalilisha Mtume au kudai kuwa mja mwema fulani ni bora kuliko Mtume „swallallahu alayhi wasallama", kuichukia hadithi ya mtume

iliokubalika ukweli wake na kutomuamini yeyote miongoni mwa mitume 25 iliyotajwa katika Kur-an Karim pia ni katika kufur. Kudai kwamba mitume walikua ni wahitaji pia ni kufru kwa sababu ufakiri waliokuwa nao mitume ulikuwa ni chaguo lao binafsi. Kumuamini yeyote anaedai utume ni kufru. Wakati usikiapo hadithi sharif za ukweli ukazibeza mfano hadithi isemayo **(Baina ya kaburi langu na mimbar yangu ni bustani miongoni mwa bustani za peponi)** wewe ukabeza na kuleta istihzai kwa kusema "Mimi pale sioni chochote isipokuwa kaburi, mabusati na minbar tu", kuyakebehi matukio ya akhera, kutokuamini adhabu za kaburi na adhabu za akhera na kudai kuwa haziingii akilini wala haziendani na sayansi, kutokuamini kuwa Allah ataonekana huko peponi, kutaka kumuona Allah hapa duniani na kusema "Mimi sina shida na pepo" nayo yote ni katika kufru. Mengine miongoni mwa maneno ambayo kuyasema ni dalili za kutokuamini Uislam ni kama kusema, sayansi ni bora kuliko elimu za dini ya kiislam, nikiswali nisiswali kwangu yote ni sawa, mimi sitoi zaka, laiti riba ingekuwa halali, laiti dhulma ingekuwa halali, kutoa sadaka kwa mali ya haramu halafu ukategemea upate thawabu, kumuombea dua mtu alietoa msaada kwa kutumia mali ya haramu hali ya kwamba unajua na kusema kwamba rai za qiyasi alizozitoa Imam adham Abu Hanifa „rahimahullahu taala" hazikubaliki. Katika aya ya 56 ya Suratul **Aaraf** Allahu taala anasema **(Yeye ndie apelekaye upepo kuwa bishara kabla ya kufika rehema yake (mvua). Hata hizo pepo zinapobeba mawingu mazito tunayapeleka katika mji uliokufa. Kisha tunateremsha hapo maji kwa mawingu hayo. Kwa maji hayo tukaotesha kila aina ya matunda. Basi inamaana hivi tutawafufua wafu ili mpate kukumbuka).** Aya hii inathibitisha kukubalika kwa qiyas na kwamba inafaa. Katika aya hii Allah analinganisha jambo lenye malumbano na lile lililowazi na kutambulika. Kwa vile kila mtu anaelewa kuwa majani yaliyokauka huchanua tena kutoka ardhini baada ya Allahu taala kunyesha mvua, Allahu taala anaonesha uwiano wa tokeo hili na lile la kufufuliwa tena waja baada ya kufa.

Ni kufru kutokuamini elimu za kiislam au kuzidharau elimu hizi na kuwadharau wanazuoni.

Mtu anayetaka kuwa kafiri, mara tu atiapo niya hiyo basi huwa tayari amekuwa kafiri. Mtu yeyote anaemtakia mwengine ukafiri, kwa kuwa anahisi ukafiri ni kitu bora basi mtu huyo amekuwa kafiri yeye mwenyewe. Na ikiwa atamtakia ukafiri mtu mwengine kwa kuwa huyo mtu ni dhalim na kumtamania ukafiri ili aende akadumu motoni basi mtu huyu yeye mwenyewe hatokuwa amekufuru. Ikiwa mtu kwa hiari

yake atasema maneno ambayo anajua yatamuingiza katika ukafiri basi huyo atakua amekufuru. Na kama atasema hali ya kuwa hajui kuwa yanakufurisha, kuna maulamaa wengi waliosema kuwa pia atakuwa amekufuru. Wakati mtu anakusudia kutamka neno lisilokufurisha lakini ulimi ukateleza na likatoka neno lenye kukufurisha, huyo hahisabiwi kuwa amekufuru.

Kufanya jambo la kikafiri hali ya kuwa anajua kuwa ni la kikafiri hilo husababisha ukafiri. Lau kama atafanya tendo hilo hali ya kuwa hajui kuwa ni la kikafiri, wengi wa maulamaa wanasema kwamba pia litamsababishia mtu ukafiri. Kuvaa vazi ambalo linajulikana kwamba ni maalum kwa makafiri kama kujifunga ukanda unaotumika maalum na mapadri nalo ni katika ukafiri. Kuvivaa vitu hivi kama hila ya kivita au katika kuleta suluhu na dhalim basi hali hiyo haiwi ukafiri. Ila mfanya biashara kuvaa mavazi hayo kwa lengo la kujichanganya katika nchi za kikafiri itakuwa ni kufur. Kuvaa mavazi haya kwa ajili ya kufanya mzaha, vichekesho au utani ni ukafiri pia na haitoshelezi mtu kuwa eti itikadi yake iko sawa.[1] Katika siku za sherehe za makafiri, kufanya au kutumia vitu maalum watumiavyo wao katika siku hiyo ni ukafiri. Kuwapelekea zawadi siku hiyo vitu vyenye sifa hiyo pia ni ukafiri. Ili kuwa muislamu sio lazima nafsi nayo kuamini. Iwapo jambo lenye kusababisha ukafiri limetoka kwenye nafsi na kufika moyoni ila ulimi ukaacha kulitamka jambo hilo, hiyo ni ishara ya uthabiti wa imani aliyonayo mtu. Iwapo muislamu ndani ya tamko lake au tendo lake kuna asilimia tisini na tisa ya dalili za ukafiri na ikawa bado imebakia asilimia moja ya imani mja huyo haitwi kafiri. Kinachotangulizwa mbele kwa muislamu ni kumdhania mema.

Maneno ya kujionesha yanayosemwa kwa ajili ya kudhihirisha uweledi, elimu au usanii au mzungumzaji akakusudia kuwapa mshangao, kuwachekesha kuwapendezesha au kuwadharau wengine, yanaweza yakapelekea kwenya ukafiri kwa hukumu. Maneno yanayozungumzwa wakati wa ghadhabu nayo pia yanaweza yakapelekea huko. Hivyo ni busara kwa muislamu kufikiri vyema kabla hajafungua mdomo wake kusema neno na kabla hajafanya jambo lolote. Anatakiwa aipe umbele imani yake katika kila jambo. Hatakiwi kuidogesha dhambi yoyote. Iwapo mtu atafanya dhambi ndogo na akanasihiwa alete toba naye akasema “Nimefanya lipi kubwa la kuleta toba” huo nao ni ukafiri. Iwapo binti ataolewa akiwa mdogo kabla ya

---

[1] Angalia kitabu cha Ibn Hajar kiitwacho (**Al ilaam bi kawatil islam )** ukarasa wa 363

kuvunja ungo, kisha alipofikia ukubwa na kuvunja ungo ikawa hajui kitu juu ya Uislam na imani na akashindwa kueleza chochote wakati alipoulizwa basi ndoa hiyo huwa imevunjika. Hii ni kwa sababu kusihi kwa ndoa na kuendelea kwa ndoa lazima wahusika wote wawili wawe ni waumini. Mtoto awapo mdogo huambatana na imani ya wazee wake ila anapofikia ukubwa muambatano ule humalizika na anahitajika kudhihirisha imani yake mwenyewe. Hayo ni sawa kwa mtoto wa kike na wa kiume. Mwenye kumuua muumini au kumpongeza yule mwenye kutoa amri ya kuuliwa muumini wote hao wamekufuru. Kuamua, kutilia mkazo au kuunga mkono kuuwawa mtu ambae kisheria hafai kuuwawa ni kufur. Kumpongeza dhalim kwa kumpiga au kumuua mtu bila ya haki nayo ni kufur. Kumshuhudisha Allah katika kuthibitisha mambo yasiyo ya kweli (mfano kusema “Allah anajua kuwa mimi nakupenda wewe kuliko mwanangu” hali ya kuwa si kweli, ni katika ukafiri. Iwapo muislamu mwenye cheo atakwenda chafya nawe ukamwambia **yarhamukallah** kisha akatokea mtu akakukemea na kukwambia “Ndio neno gani hilo la kumwambia muheshimiwa. Waheshimiwa hawaambiwi maneno ya kienyejienyeji kama hayo”, hiyo nayo ni kauli ya kikafiri. Mtu asieamini kuwa ni wajibu, akadharau na kuibeza sala, zaka au swaumu huyo ni kafiri. Kukata tamaa kuwa huwezi kupata rehema za Allah nao ni ukafiri. Kitu ambacho asili yake si haramu, ila kikapata uharamu kwa sababu iliyotokea baadae basi kitu hicho huwa haram. Mfano ni mali iliyochumwa kwa kitendo cha wizi au njia nyengine ya haram. Hizi kuzisema kuwa ni halal si kufru. Ulevi, nguruwe na vitu vyengine ambavyo kwa nafsi zake ni haram, itakuwa ni kufur kuvisema kuwa ni halali. Jambo lolote ambalo kwa makubaliano linajulikana kuwa ni haram, kulisema kuwa ni halal ni ukafiri. Vitu vilivyo thamini kwa Uislam kama adhana, msikiti, vitabu vya fikhi kuvidhalilisha ni kufur. [Adhana inayotoka kwenye redio au mabomba ya msikitini ni mithili tu ya adhana sio adhana zenyewe asili]. Kusali hali ya kuwa unajua kuwa huna udhu, au hali ya kuwa unajua kuwa wakati wa sala haujaingia au kuelekea upande usiokuwa wa kibla kwa makusudi nayo ni katika kufur. Kulitumia neno kafiri kama tusi na ukamtusi muislamu huo hauwi ukafiri. Ila kama tulivyoeleza kabla kumwita hivyo kwa kumkusudia kuwa ni kafiri kwa itikadi basi huo ni ukafiri kwa muitaji. Amri zake Allah huitwa ni **fardhi** na yale makatazo yake huitwa ni **haramu**. Fardhi na haramu ni katika jumla ya **hukmu za kiislam**. Kufanya jambo lililokatazwa na Uislam ni dhambi. Kutenda dhambi si ukafiri ila lile jambo zima la kwamba ile ni dhambi na inafaa isifanywe wewe ukalibeza na kuonesha dharau hapo unakuwa ni ukafiri. Kukana

kwamba ibada zinaulazima kutekelezwa na madhambi yanaulazima kuachwa ni kufru. Kuamini kuwa mapato ya nchi yenye kukusanywa ni mali ya mkuu wa nchi ni ukafiri. Kwa mtizamo wa Sadrul Islam inawezekana kwa baadhi ya wapenzi wa Allah (mawalii) kuwepo katika mahala tafauti kwa wakati mmoja. Pia baadhi ya vitabu vya fikhi vimekubalisha uwezo wa wana ndoa wanaoishi maeneo ya mbali baina yao kuweza kupata mtoto. Mwanazuoni mkubwa aitwae Omar Nasafy "rahimahullahu taala" amesema kwamba inawezekana Allahu taala akawafanyisha mawalii mambo yaliyo kinyume na kanuni za kawaida za maisha zilizozoeleka (makarama). Haya ni maneno sahihi. Kwa kawaida watu wasio na elimu wasiulizwe maswala kwa mfano Uislam ni nini? Imani ni nini? bali wapewe maelezo ya vitu hivyo kisha waulizwe kama ndio hivyo wanvyoamini. Wanandoa wawili wanaotaka kuingia kwenye ndoa yafaa kuwauliza kwa mtindo huu. Kwa kuonekana na matendo au kauli ambazo zinawapelekea ukafiri wasihukumiwe ukafiri kabla ya kuthibitishwa kwamba kwa hayo wanakusudia ukafiri na kwamba wanadharau hukmu za Uislam. Vyenginevyo inafaa wadhaniwe mema.

Iwapo muislamu atasema au kutenda kwa makusudi mambo ambayo maulamaa wote wamekubaliana kwamba ni yenye kukufurisha basi mtu huyo atakuwa kafir na huitwa **Murtad**. Baada ya kuwa Murtad, zile ibada zote na thawabu alizozichuma kabla hubatilika. Iwapo atarudi katika iman, na ikiwa ni katika watu wenye uwezo basi atatakiwa kurudia tena kutekeleza ibada ya hija hata kama alikwishafanya. Sala, swaumu na zaka hatotakiwa kuzilipa ila zile kadhaa ambazo alitakiwa azilipe kabla ya kuwa murtad atalazimika bado kuzilipa. Hii ni kwa sababu Murtad hafutiwi madhambi yaliyopita. Murtad ndoa yake huvunjika hapo hapo. Kama ataendelea kuishi na mkewe na akapata watoto kabla ya kurudi kwenye iman na kufunga tena ndoa yake, basi hao watakuwa ni watoto wa zinaa. Chochote anachokichinja murtad ni kibudu na hakiliwi. Bila ya kuleta toba kwa lile lililomtoa kwenye iman, hatoweza kurudi kwenye Uislam hata kama atatoa **shahada** na kusali. Kukikana kile kitu kilichompeleka kwenye ukafiri pia itatosha kuwa ni tendo la kutubia. Ikiwa Murtad atakufa bila ya kutubia basi atastahiki kukaa milele katika Jahannam. Hivyo inafaa tuogope sana kuanguka kwenye ukafiri na tuwe wachache wa mazungumzo. Katika hadithi sharif tunajifunza yafuatayo: **(Daima zungumza yaliyo ya kheri au kaa kimya!)**. Kuwa makini na mpole na usiwe mtu wa mchezo mchezo. Jiweke mbali na mambo yenye kupingana na dini, kanuni au yasiyo wiana na akili na

ubinadamu. Inahitaji kumuomba sana Allah akuepushe na shirk. Katika hadithi sharif tunasoma kwamba **(Iogopeni sana shirk kwani hakika shirki ni yenye kujificha kuliko sauti ya miguu ya mdudu chungu)**. Shirk iliyotajwa katika hadithi hii ni ukafiri. Ilipoulizwa ni vipi tutaweza kujinusuru na kitu kilichojificha kama hivyo ndipo yakaja mafunzo ya kutumia dua ifuatayo **(Allahumma innaa naudhu bika annushrika bika shay-an naalamuhu wa nastaghfiruka bimaa la naalamuhuu!)**. Inatakiwa kuisoma sana dua hii asubuhi na jioni. Maulamaa wamekubaliana kwamba makafiri kamwe hawatoingia peponi na watabaki milele ndani ya Jahannam. Kwa vile kafir lau kama angeliishi daima duniani kwa nia yake angedumu kuwa kafiri, basi ni hivyo hivyo huko akhera atadumu katika moto wa Jahannam. Allahu taala ndiye muumbaji na ndie mmiliki wa kila kitu. Yeye ana haki ya kufanya alitakalo katika milki yake na hakuna mwenye haki ya kumsaili kwa hilo. Kukifanyia kile alichokimiliki atakavyo haiwezi kuambiwa kuwa ni dhulma. Ndani ya Kur-an Karim Allahu taala amejieleza wazi kwamba yeye si dhalimu na kwamba hatomdhulumu yeyote miongoni mwa waja wake.

[Allahu Taala ana majina mazuri **(Asmaul husna)** ambayo ni ya azali kama alivyo yeye mwenyewe. Tunashuhudia vitu kuzuka kutoka hali ya kutokuwepo na kutoweka vikawa havipo. Vitu hivi haviwezi kuwa vimezuka tu kutoka pasipo tambulikana. Lazima awepo muumbaji mwenye kivianzisha vitu kutoka katika hali ya kuwa havikuwepo; muumbaji ambaye bila ya shaka yeye amekuwepo kila wakati bila kukosekana wakati wowote. Ili kujitambulisha kuwepo kwake, muumbaji huyu ametuma mitume akawapa na vitabu. Mitume hawa na vitabu hivi ni maarufu na majina yao yamezagaa katika vitabu vilivyojaa kwenye maktaba zote duniani. Jambo lililo uwanjani likawa linashuhudiwa na kila mtu haliwezi kukatalika. Kukana uwepo wa Allahu taala ni kukataa jambo lililo uwanjani. Kukataa kuwepo kwa Allahu taala na upekee wake ni sawa na kukataa mambo yanayotokea kila siku na tukawa tunayasoma kwenye maandishi mbali mbali. Hili si jambo analotegemewa kulifanya mtu mwenye akili iliyo sawa. Kati ya majina yake tisini na tisa yanapatikana **Muntaqim** na **Shadidul iqaab**. Kwa majina yake haya mawili ndio Allah akaumba Jahannam saba. Aidha kutokana na majina yake kama **Rahman, Rahim, Ghaffaar, Latif** na **Rauf** ndio Allahu taala akaumba pepo nane. Mambo ambayo yatapelekea kuingia motoni na yale yatakayopelekea kuingia peponi Allahu taala aliyapambanua tangu azali na kwa vile yeye ni mwingi wa rehema akawatambulisha waja wake. Allahu taala amewaonya waja

wake mara kwa mara kwamba hakika moto wa Jahannam ni mkali mno na kwamba waja hawatoweza kuuvumilia hivyo wajiepushe na sababu zitakazowapelekea kuingia motoni. Vile vile amekuwa akiwalingania sana kufanya yale mambo yatakayowapeleka kwenye neema za kudumu za peponi ambayo ndio yatakayowapa furaha ya hapa duniani na huko akhera. Ili waweze kuukubali na kuuchagua mlingano huu Allahu taala akawapa neema za akili, matakwa na uhuru wa kuchagua. Allahu taala hakumuamrisha wala hakumpangia tangu azali mtu yeyote kuingia motoni au kufanya mambo yanayoingiza motoni. Lakini Allahu taala kwa elimu yake alikwishajua tangu azali ni wepi katika binaadamu watakapofika duniani watachagua na kufuata njia ya kuelekea peponi na ni wepi watachagua na kufuata njia ya kwenda motoni. Elimu ya **kadhaa** na **kadar** ni ya azali. Allahu taala kumtaja Abu lahab kuwa ataingia motoni haitokani na kuwa Allahu taala alitaka hivyo tangu azali ila Allahu taala alifahamu tangu azali kwamba chaguo la Abu Lahab hapa duniani litakuwa ni njia ipelekayo motoni.

Kuelekea kwenye iman ni jambo jepesi. Ni wajibu kwa kila mtu kuangalia kwa mazingatio utaratibu, nidhamu na uzani uliotumika katika kuumbwa kwa kila kitu. Ukichunguza chembe ndogo za maumbile na vile viumbe vikubwa kama jua, nidhamu ya maumbile na maingiliano yao vinakulazimisha kuungama kwamba hayo hayawezi kuwa yametokea wenyewe kwa sudfa na kwamba lazima vimeumbwa na mtaalamu mahiri, mweledi, mwenye elimu na hekima na mwenye nguvu zisizo na ukomo. Mtu yoyote mwenye akili timamu na akabahatika kupata elimu ya sayansi, astronomi, bayolojia au tiba anafahamu wazi kwamba vitu hivi vilivyoepukika na kila aibu na mapungufu katika maumbile yake havina budi kuwa na muumbaji na kwamba Muhammad "swallallahu alayhi wasallam" anayeyatambulisha mambo hayo basi ndie mjumbe wa kweli wa muumbaji huyo. Mtu huyu moja kwa moja humuamini muumbaji. Hasa pale anapofahamu kwamba wakanushaji watadumu kwenye Jahannam na waumini watadumu peponi basi hukimbizia kuamini kwa mapenzi yake. Bwana Ibrahim Hakki, mwenyeji wa Erzurum, aliyefariki Sirid mwaka 1195 hijria [1781 miladia] katika kitabu chake kiitwacho **Maarifatname** kwenye kigawanyo cha tisa anaeleza yafuatayo: (Sayansi, astronomi, viwanda na mashine ni vitu vilivyovumbuliwa kwa akili na majaribio ya binadamu na kwa kupitiwa na muda elimu hii hubadilika na kuthibitishwa kuwa mengi yaliyodhaniwa kuwa ni sahihi jana kumbe si sahihi. Kwa hivyo kupatikana elimu ya zamani na mpya katika sayansi, yaliyokuwa sahihi jana na yaliyo sahihi leo,

kunathibitisha kuwepo kwa muumbaji, ambae elimu yake haina mipaka ambae ndie aliyeumba ulimwengu huu kutoka katika hali ya kutokuwepo). Na yule ambae atasoma juu ya mwenendo mwema na miujiza ya Muhammad "swallallahu alayhi wasallam" basi hatochelewa kufahamu kwamba huyo ni mtume wa Allah.]

Kila siku kuswali sala moja tu ni wepesi lakini kusali sala tano kwa siku ni uzito na watu wengi wanakwazika. Je inawezekana kwa Allahu taala mwingi wa rehema kuacha kutuamrisha yaliyo mepesi na badala yake akatuamrisha yaliyo mazito? [Jawabu nzuri ya suala hili imetolewa na mwanamke wa kiingereza aliyesilimu na tumeinukuu katika kitabu chetu **"Imani na Uislam."**]

## UJAHILI

2. Gonjwa la pili la moyo ni **ujahili**. Aina za ujahili na madhara yake tumezielezea mwanzoni mwa mada ya mwanzo.

## PUPA LA MALI NA ULWA

3. Gonjwa la tatu miongoni mwa magonjwa ya moyo ni pupa la kutaka mali na ulwa. Hadithi sharif zifuatazo hapo chini zinaagua na kuelekeza tiba ya maradhi haya:

1.) **(Madhara yanayosababishwa na pupa la kutafuta mali na ulwa ni makubwa zaidi kuliko yale yanayosababishwa na mbwa mwitu wawili wenye njaa waingiapo kwenye kundi la mbuzi).**

2.) **(Binadamu ataangukia kwenye madhara, kwa kuoneshwa kwake kidole juu ya mambo yake ya kidini na kidunia)** hii ina maana kwamba binadamu katika kutaka kwake umaarufu katika mambo yake ya kidunia na ya kidini basi humalizikia kuidhuru dunia yake na akhera yake.

3.) **(Kupenda kupongezwa kunamfanya mtu awe kipofu na kiziwi. Maovu na mapungufu yake hawezi kuyaona tena. Hasikilizi tena nasaha na ushauri mzuri apewao).**

Kupenda ulwa na umaarufu kunasababishwa na mambo matatu. Sababu ya kwanza ni kutaka kukidhi matamanio ya nafsi. Nafsi hutaka kukidhi matamanio yake kwa njia za haramu (ambapo ni wepesi kuzifikia ukiwa na ulwa). Sababu ya pili inayompelekea mtu kutaka ulwa ni kuokoa haki zake au za watu wengine kutokana na mikono ya dhalim na kuzitumia kwenye njia mustahab kama vile kutoa sadaka, na mambo mengine ya kheri na yaliyo mazuri au kuzitumia kwenye njia za halali kama vile kula, kuvaa na kuishi mahali pazuri, kuwa na watoto na kuishi maisha mazuri, kuondoa mambo yanayokwaza kwenye ibada

na kutoa huduma kwa Uislam na waislam. Mwenye kutaka ulwa kwa sababu hii, na ikawa hakufanya riya wala hakuchanganya batili ndani ya haki, ikawa asifanye mambo yaliyoharamishwa na Uislam, asiache yaliyo ya wajibu na yale ya sunna, basi itajuzu kuwa na ulwa huo bali itapendeza hasa. Kwa sababu, yale yote yenye kupelekea kwenye jambo la wajibu au sunna nayo yanakuwa ni wajibu au sunna kuyatekeleza. Allahu Taala wakati alipoelezea vipi binaadamu bora anatakiwa awe, jambo la waislam kuwa viongozi pia amelitaja. Suleiman alayhi salaam katika kuomba ufalme na mali alisema (Ewe Mola! Naomba unipe mulki ambayo hutampa mtu yeyote baada yangu!). Habari za mambo yaliyotokea katika dini zilizopita na yakawa hayakukataliwa, basi pia katika dini yetu hupewa mazingatio. Katika Hadithi sharif tunasoma yafuatayo **(Kutawala kwa haki na uadilifu kwa siku moja, ninapendelea zaidi, kuliko kupigana jihadi ya kuendelea kwa siku mia)**. Pia katika hadithi sharif nyengine **(Kutawala kwa uadilifu kwa saa moja tu ni bora kuliko kufanya ibada za sunna kwa miaka sitini).** Kuwa na cheo kisha ukachanganya haki na batili au ukafanya riyaa ni jambo lisilojuzu hata kama niya ya mtendaji ni njema kwani mambo ya haramu na yale makruh hayafai kutendwa hata kama itakuwa ni kwa nia nzuri. Baadhi ya haram kuzifanya kwa nia njema zinaweza kumalizikia kwenye dhambi zaidi. Nia njema inafaa ikiwa tu jambo linalofanywa ni la utiifu au ibada. Jambo la halal au hata fardh kufuatana na nia yake mtu linaweza likampelekea kupata dhambi. Hivyo yule anaefanya dhambi kisha akadai (Wewe tizama moyo wangu bwana. Mimi moyo wangu ni msafi. Allah anatizama mioyo yetu) ameleta madai ya uongo na yenye madhara makubwa.

Sababu ya tatu inayompelekea mtu kutaka ulwa ni kuifurahisha nafsi. Nafsi kama ambavyo inafarajika kwa kuwa na mali basi pia hufarijika kwa kuwa na cheo. Hata kama katika hali hii sharia za dini hazikuvunjwa na njia za haramu hazikutumika katika kufikia matakwa ya nafsi, bado inahofiwa kuwepo kwa uchache wa uchamungu. Baada ya kupata cheo inahofiwa sana kuwa njia za riya na kujionesha zitatumika ili kuwavutia watu. Unafiki, kuchanganya haki na batili, hila na udanganyifu pia vinahofiwa kutumika. Haifai kufanya jambo ambalo lina mchanganyiko wa halali na haramu. Sababu hii ya tatu ya kutaka ulwa, pamoja na kwamba si haramu, kwa vile ina mambo yasiyo mazuri, nayo inahitaji kujua tiba yake. Kwanza ni kufahamu kwamba ulwa ni jambo la kupita na kuzingatia madhara na hatari zake. Ili kuepukana na kiburi kinachotokana na kujikusanyia umaarufu na heshima basi yafaa baadhi ya wakati kiongozi kufanya mambo ambayo

wananchi hawatoyapenda miongoni mwa mambo halali na yenye kujuzu katika Uislamu (yatakayomsababishia alaumiwe). Inahadithiwa kuwa mmoja kati ya watu waliokuwa wakiishi maisha ya kuipa nyongo dunia (Zahid) alihisi kuwa kiongozi wa nchi na wale walio karibu nae wakionesha hamu ya kutaka kuwa karibu nae. Ili kujiepusha na hilo, siku moja aliwaalika chakula cha usiku. Wakati wa kula, zahid yule alionekana kula kwa kufakamia na kwa matonge makubwa. Yule kiongozi hakuvutika na yale aliyoyaona; ambayo hayafanani na sifa za mtu zahid; na akaamua kutokumfatilia tena yule zahid. Huku nyuma yule zahid alinyanyua mikono kumshukura Allahu taala kwa kumuokoa na lile jambo la kuwa karibu na waheshimiwa. Moja kati ya dawa mjarabu dhidi ya gonjwa hili la kupenda ulwa ni kujitahidi kutochanganyika na watu. Mbali na mahitaji ya kidini na yale ya lazima ya kibinaadamu ajitahidi mtu asijichanganye na watu. Dawa hii imetajwa kwenye hadithi sharif.

## WOGA WA KUAIBISHWA

4. Gonjwa la nne ni kuogopa kuzungumzwa vibaya na kuhuzunishwa kwa kutajwa aibu na mapungufu yako. Hii ni ya tatu katika yale mambo tuliyoyataja yenye kupelekea ukafiri kwa kukana ambapo mtu huona haya na huogopa kuwa atasemwa vibaya au kuaibishwa na wengine. Hii ndio sababu iliyomfanya Abu Talib kubaki katika ukafiri. Abu Talib alikuwa ni baba wa Sayyidna Ali "radhiyallahu taala anhu" na ami wa Mtume "swallallahu alayhi wasallam". Alifahamu kwamba yeye ni mtume lakini kwa kuogopa kusemwa vibaya na kutiwa aibu na watu, hakuamini. Wakati akiwa katika saa ya mauti Mtume wa Allahu taala alimwambia **(Ewe mjomba! Ili niweze kukuombea msamaha siku ya kiama lazima useme "Laa ilaaha illallahu"!)**. Abu Talib akajibu (Ewe mtoto wa ndugu yangu. Naelewa kuwa uyasemayo ni kweli. Lakini sitaki watu waanze kunisema kuwa nimeamini kutokana na kuogopa mauti). Kufuatana na tafsiri ya Baydhawy aya ya 56 ya suratul qasas **(Haliko katika uwezo wako, kuwaongoa uwapendao)** imeshuka katika tukio hili. Katika mapokezi mengine imepokewa kuwa makureshi walikuja kwa Abu Talib na kumwambia "Wewe ni kiongozi wetu na amri zako kwetu siku zote ni zenye kutiiwa. Ila tunakhofia kuwa baada ya kufa kwako ugomvi wetu na Muhammad "aleyhi salaam" utaendelea. Hivyo mwambie Muhammad "aleyhi salaam" asiizungumze kwa ubaya dini yetu." Abu Talib akamwita Mtume wa Allah na kumueleza yale waliyoyasema. Alipofahamu Abu Talib kuwa mtume wa Allah hatofanya suluhu nao, alisema mbele ya mtume maneno yenye kuashiria kutaka kuwa

muislamu. Mtume alipoyasikia hayo, alimtaka ami yake kuamini. (Lau kama nisingeogopa watu kunisema kwa aibu basi ningeliamini ili nawe pia upate kufurahi). Wakati akikata roho alionekana akimungunya baadhi ya maneno. Bwana Abbas "radiyallahu anhu" alikurubisha sikio lake ili kujaribu kusikia anayoyasema na kusema kuwa Abu Talib alitoa maneno ya kujuza imani yake. Jambo hili la kuwa Abu Talib aliamini ni lenye kutiliwa wasi wasi mno. Kufuatana na maulamaa wa ahli sunna, Abu Talib hakuamini na imam Abu Hanifa "rahimahullahu taala" ameeleza wazi kwamba Abu Talib alikufa kafir. Baada ya kufa kwake Ali "radhiyallahu anhu" alikuja kwa Mtume "swallallahu alayhi wasallam" akamwambia "Ami yako alie katika upotofu amekufa". Mtume akamwambia "**Muoshe, mkafini na umzike. Tutaendelea kumuombea dua hadi tutakapokatazwa."** Mtume alibakia nyumbani kwake na hakutoka nje kwa baadhi ya siku akiwa anamuombea dua ami yake huyu. Baadhi ya masahaba waliposikia hali hii ya Mtume nao wakaanza kuwaombea dua jamaa zao waliokufa hali ya kuwa ni makafiri. Ndipo ikashuka aya ya 114 ya suratu Tawba yenye kusema **(Haifai kwa mtume na wale walioamini, kuwatakia msamaha washirikina, hata kama itakuwa ni jamaa zao).** Na katika hadithi sharif **(Kafiri atakaepata adhabu ndogo kuliko wote siku ya kiama ni Abu Talib. Ataekewa kaa la moto chini ya nyayo zake ambalo moto wake utaufanya ubongo uchemke).**

Tiba ya gonjwa la kuogopa kuzungumzwa vibaya na kuaibishwa ni kufikiria ifuatavyo: Ikiwa aibu na maovu unayotajwa kwao unayo kweli, basi itakuwa ndio umepata nafasi ya kuyatambua hivyo utie nia ya kutoyafanya. Hilo litakuwa limekuletea faida na inafaa hata kuwashukuru waliokutendea. Alielezwa Hasan Basri "rahimahullahu taala" kwamba kuna mtu alikuwa akimsengenya. Alitoka Hasan Basri na kisahani chenye halua akampelekea huyo mtu na kumwambia "Nimesikia umekuwa ukinigawia thawabu zako hivyo nami nimeamuwa kukuletea zawadi ya haluwa." Imam adham Abu Hanifa "rahimahullahu taala" alipata habari kwamba kuna mtu akimsengenya. Alitoka Imam na kifuko chenye dhahabu akampelekea yule mtu na kumwambia (Kama utazidi kutupa thawabu zako basi nasi tutazidi kukuletea huu ujira). Na ikiwa aibu zako zinazotajwa ni za uongo na ni uzushi basi anaepata madhara ni huyo msemaji. Yafaa ufahamu kwamba thawabu zake unapewa wewe na dhambi zako anabebeshwa yeye. Uzushi na kupeleka maneno ni uovu zaidi kuliko kusengenya. Uzushi na Namima ni uovu zaidi kuliko kusengenya. Namima maana yake ni kupeleka maneno baina ya waislam. Angalia (Maktubati Masumiye )juzuu ya pili ukarasa wa 123.

## KUPENDA KUSIFIWA

5. Ni gonjwa la tano la moyo. Mtu hupenda **kusifiwa na kushukuriwa**. Hii inatokana na mtu kujipenda, kujitukuza na kijidhania kuwa yeye ni mwema. Kusifiwa kunampa ladha mtu kama huyu. Linalomfaa mtu huyu ni kujua kwamba kujitukuza si jambo jema na hata ukubwa nao afahamu kwamba ni wa kupita tu. Mada hii tutaizungumza kwa upana zaidi wakati tutakapozungumzia gonjwa la kiburi.

## BID'AT IITIKADY

6. Hii ni Imani iliyopotea na isiyo sahihi. Wengi wa waislam wamekumbwa na gonjwa hili. Sababu kuu ya gonjwa hili ni kule kujaribu kulazimisha kuyapatia maelezo ya kiakili mambo ambayo hayafahamiki kwa kutumia viungo vyetu vya hisia au elimu zetu za vipimo, na hatimae kuangukia katika imani isio sahihi iliyotokana na makosa ya akili zetu. Ili muislamu asije kuanguka katika janga hili anafaa ajiegemeze kwenye moja ya dhehebu mbili za kiitikadi; yaani **Maturidy** au **Ash-ary**. Kufuata mafunzo ya mmoja kati ya maimamu hawa wawili kutamkinga mtu na kukumbwa na maradhi haya kwa sababu wanazuoni wa **ahli sunna** „rahimahullahu taala", mambo ambayo akili haikuweza kuyaeleza waliyapatia ufumbuzi kwa kutumia Kur-an Karim na sunna pekee. Walitumia akili zao kwa kutafuta maana kutoka kwenye Kur-an Karim na sunna. Maana hizo ni zile ambazo walijifunza kutoka kwa Mtume swallallahu alayhi wasallam na masahaba zake kisha wao wakayaandika kwenye vitabu vyao.

[Yale yaliyoelezwa na Kur-an Karim na sunna na ikawa yenye kufahamika wazi kabisa basi inakuwa ni **ukafiri** kutoyaamini au kuyatilia wasiwasi. Zile amri ambazo hazikutambulishwa kwa wazi na ikawa zimebaki kuwa zenye shaka, basi ni **bid'a** kuzipa maana isiyokuwa yake. Wale wenye kuzipa maana isiyo sahihi Kur-an Karim na sunna huitwa **watu wa bid'a**. Wale ambao fikra na ufahamu wao binafsi wanauambatanisha na Kur-an Karim na sunna huitwa **wazandik**. Yule mwenye kuamini ufahamu wa mtu mwengine usio sahihi, nae anakuwa ni mtu wa bid'a. Ila atakapovijadili Kur-an na sunna na kusema kwamba mambo yaliyomo hayawezekani au hayakubaliani na akili yangu basi huyo atakuwa ni kafiri. Yule ambae atahalalisha lililo haramu hali ya kujidhania ametegemea hadithi au aya fulani huyo hatokuwa kafiri lakini atakuwa ni ahlu bid'a. Kusema

kuwa kuchaguliwa kwa ukhalifa wa Abubakar na Umar hakukufanyika kwa haki ni bid'a. Ila kusema kwamba makhalifa hao wawili hawakuwa na haki ya kuwa makhalifa ni ukafiri. Muhammad Shihristan "rahimahullahu taala" katika kitabu cha **Milal wa Nihal** amesema kwamba wanazuoni wa kihanafy wamefata madhehebu ya itikadi ya Abu Mansour Maturidy "rahimahullahu taala" kwa sababu naye ni mfuasi wa Imam Abuu Hanifa katika maswala ya Usul na Furuu. **Usul** maana yake ni iitaki na **Furuu** maana yake ni hukmu za kiislam. Wanazuoni wa madhehebu ya Malik, Shafi na Hanbali wamefuata madhehebu ya itikadi ya imam Abul Hassan al Ash-ary "rahimahullahu taala". Yeye alikuwa ni mfuasi wa madhehebu ya Shafii. Bwana Abdulwahab Tajudyn Subky ambae ni mtoto wa ulamaa mkubwa wa kishafi aitwae Abul Hasan Ali Subky "rahimahullahu taala" amesema "nimevipitia vitabu vya maulamaa wa kihanafi na nikakuta kuna tafauti 13 ukilinganisha na iitikadi ya Shafii. Ila tafauti nilizoziona si za kumtoa mtu kwenye njia ya haki. Hawakutafautiana katika mambo ya msingi na wote wawili wamefuata njia ya haki". Muhammad Hadimy "rahimahullahu taala" katika kitabu chake cha **Barika** ukarasa wa 317 anasema kwamba baina ya madhehebu ya Maturidi na Ash-ari pamoja na kujumuisha na zile tafauti ndogo kabisa alikuta jumla ya tafauti 73. Imeelezwa kwa kirefu katika vitabu vya **Hadika** na **Barika** kwamba watu wa bid'a ni wenye kuingia motoni.]

## MATASHI YA NAFSI

7. Hili ni gonjwa la saba miongoni mwa maradhi ya moyo nalo ni kufuata hawaya, matamanio na ladha za nafsi. Kur-an Karim imeeleza wazi wazi kwamba hili ni jambo ovu na kwamba litamkengeusha mtu na kumtoa kwenye njia sahihi kwa sababu wakati wowote nafsi inamili zaidi katika kumkanusha Allah, kufanya inadi na uasi. Mtu anapoiridhia nafsi yake kwa kila inalotaka huwa ni mwenye kuabudia nafsi yake. Mwenye kuiridhia sana nafsi yake basi huangukia kwenye ukafiri, bid'a au ufasik. Abubakar Tamistanu "rahimahullahu taala" anasema (Kuepukana na gonjwa la kuitii nafsi ndio neema kubwa ya hapa duniani, kwani nafsi ndio kizingiti kikubwa kiliopo baina ya mja na mola wake). Sahl bin Abdullah Tusteri (Basra 283 hijria) amesema (ibada yenye thamani kubwa kabisa ni kuiasi nafsi). Islam bin Yussuf Belhi alimpa zawadi Hatemul Esama (237 hijria) nae akaipokea. Wakamuuliza watu Hatemi kuhusu yeye kuipokea ile zawadi haiwi ni kufuata matamanio ya nafsi? Hatemi akajibu kama ifuatavyo (Kupokea zawadi kutoka kwake ni tendo la kujidhalilisha mimi na kumtukuza yeye. Na lau kama ningekataa basi ningekuwa nimejitukuza mimi na

kumdhalilisha yeye jambo ambalo nafsi yangu ingelipendelea sana). Katika hadithi sharif moja refu, sehemu yake ya mwisho ilimalizikia kwa maneno yafuatayo **(Mambo ambayo yatampelekea binaadamu kwenye maangamizi ni matatu. Uchoyo, kufuata matamanio ya nafsi na kujiona).** Imam Ghazali "rahimahullahu taala" anasema: "Kizingiti kikubwa kinachozuia msaada wa Allahu taala usimfike mja ni **kujiona.** Hii maana yake ni mtu kutokuziona aibu na mapungufu yake na kujitukuza kwa mazuri yake. Nabiyullahi Isa alayhi salaam alisema (Enyi wafuasi wangu! Hakika ya upepo umezima taa nyingi. Basi ni hivyo hivyo na tendo la kujiona limezima ibada nyingi na kuzipoteza thawabu zake).

Katika hadithi sharif Mtume "swallallahu alayhi wasallama" anasema **(Ninaogopa mno umati wangu kukumbwa na tabia mbili ovu. Kufuata matamanio ya nafsi na kusahau mauti na kuikimbilia dunia).** Kufuata matamanio ya nafsi kunazuia kufuata mafunzo ya Uislam. Kusahau mauti kunapelekea kuyatii matamanio ya nafsi.

Katika hadithi sharif nyengine tunasoma **(Dalili ya kuwa na busara ni kuishinda nafsi kwa kuiweka chini ya amri yako na kujitayarisha kwa yale yaliyo ya lazima baada ya kufa. Dalili ya ujinga ni kufata matamanio ya nafsi halafu ukataraji msamaha na rehema za Allah).** Kufuata matamanio ya nafsi kisha usilete toba wala istighfar na bado ukawa unategemea kusamehewa na kuingia peponi hilo huitwa **Tamanio**. Ama kujitahidi kuleta sababu zitakiwazo kisha ukategemea kuingia peponi hilo huitwa **Tarajio**. Tamanio humpelekea mtu kuwa mvivu ila Tarajio humfanya mtu akawa mchapa kazi. Yale mambo ambayo nafsi inayapenda na kuyataka huitwa **Hawaya**. Kimaumbile nafsi ni yenye kupenda na kutaka mambo maovu yenye dhara. Ubeti huu umesibu katika kuyaeleza hayo. Tahadhari na nafsi yako usiiamini aslani. Ni adui mwenye dhara kuliko shetani sabini. Madhara ya nafsi kumburuza mtu kuelekea kwenye madhara ya matendo ya haram na makruh ni yenye kuonekana wazi. Nafsi hushughulikia matashi ya kinyama tu ambayo ni mahitaji ya kidunia. Binadamu anapojikita kukimbilia zaidi mahitaji ya kidunia basi hubaki nyuma katika jambo la kujitaarisha na akhera. Jengine lilo muhimu kufahamu ni kwamba nafsi haitoshelezwi na yale ya halali, na kila utapozidi kuipa nayo itakudai zaidi na zaidi, na hatimae kukuelekeza kwenye ya haramu. Hata yale ya halali yanapotumika bila ya kiasi huweza kuleta madhara na matatizo. Mtu wa aina hii hufikiria tumbo na matashi mengine tu. Humalizikia kuwa mchoyo na wa ovyo.

[Imam Rabbani „rahimahullahu taala“ anasema: (Binaadmu ametokana na Adam. Adam ni kitu kisicho kuwepo. Wakati ambapo hapakuwa na kitu chochote isipokuwa Allahu taala, yeye alielewa kuwa vitu vitatokea kutoka kutokuwepo kwao. Hii ina maana kwamba vitu tayari vilikuwepo ndani ya elimu ya Allahu taala. Allahu taala aliziakisi sifa zake kwenye maumbile ya Adamu na ile asili ya uwepo ilidhihiri kwa kuumbwa Adam. Hivyo ile asili ya uwepo ambayo ilikuwa kwenye elimu yake tu ikawa sasa imedhihirika kwenye maumbile na hapo kuwepo kukaanza. Kwa hivyo vitu viliopo vimetokana na kutokuwepo, na kuwepo kwake kumekuja kwa njia ya Allahu taala kuakisi sifa zake kwao. Ni mfano wa tofaa kutokana na kokwa yake. Ili kuyafahamu maumbile ya binaadamu, wacha tuangalie picha ya kitu inavyoonekana kwenye kioo. Picha ya kwenye kioo ni matokeo ya kuakisi kwa mionzi inayotoka kwenye hicho kitu. Kioo ndio sawa na Adam au kutokuwepo. Roho na moyo maanawy wa binaadamu ni sawa na mwangaza. Kioo ni sawa na mwili wa binaadamu na ule mng’ao ni sawa na nafsi. Asili ya nafsi ni kisichokuwepo au Adam na wala haina uhusiano na roho au moyo maanawy). Mtu mwenye kufuata matamanio ya nafsi, siku zote yanampelekea kuacha mafundisho ya Uislam. Kwa vile wanyama hawana akili wala nafsi, hutumia mahitaji pale wayapatapo. Wao hujiepusha na yale ambayo yatadhuru mwili wao au kuwapa maumivu. Uislam haukatazi kuishi duniani kwa raha na utulivu wala hauharamishi yale matashi ya lazima na yenye faida. Dini ya Uislam inamtakia mja kuishi kwa raha na utulivu hapa duniani na huko akhera. Kwa hilo, ndio maana ikamuamrisha kufuata akili na kuikana nafsi. Lau kama mtu angelikuwa na nafsi tu bila akili, basi angekuwa ni mwenye kufuata matamanio yake tu, na ingempelekea kwenye maangamizi. Na kama nafsi isingekuwepo, basi angeonesha mapungufu katika kutafuta maisha na kuendeleza maisha kwa kupitia mafungamano ya ndoa, bali pia angekosa ujira wa jihadi dhidi ya nafsi. Njia ya kumfikisha kuwa mbora kuliko malaika ingekuwa imefungwa. Hadithi sharif inatwambia **(Lau kama wanyama wangeliyajua yale mnayoyajua kuhusu akhera, basi msingepata nyama ya kula!).** Hii ina maana kwamba lau wanyama wangelielewa juu ya adhabu za akhera kama tuelewavyo sisi, basi wangekata kula na kunywa kutokana na khofu hivyo wakabaki mifupa mitupu. Kama binaadamu nao wasingekuwa na nafsi, basi pia nao wasingeweza kula na kunywa kutokana na khofu ya yale ya akhera na wasingeweza kuishi. Ili binadamu waweze kuishi sahau iliyomo kwenye nafsi na matamanio ya dunia vinahitajika. Nafsi ni kama kisu chenye makali pande mbili. Pia ni kama dawa ambayo ina na sumu ndani yake. Yule

ambaye ataitumia dawa hiyo kwa kufuata maelekezo ya tabibu atafaidika lakini yule atakaeitumia atakavyo atadhurika. Uislam haufundishi kuiangamiza kabisa nafsi bali unafunza ni kwa vipi tutaweza kuiongoza nafsi na kufaidika nayo.]

Ili kuizuia nafsi isitoke nje ya Uislam kuna aina mbili za jihadi. Jihadi ya kwanza ni kutoisikiliza na kutokuyatekeleza yale nafsi inayoyataka. Hii huitwa **Riyadha** ambayo huwa kwa Waraa na Taqwa. **Taqwa** ni kujiepusha na yale ya haram na **Waraa** ni kujiepusha na ya haramu na kutokutumia ya halali zaidi ya uhitaji. Jihadi ya pili ni kufanya yale mambo ambayo nafsi haiyapendi. Hii huitwa **Mujahada**. Ibada zote ni aina ya Mujahada. Jihadi hizi mbili huiongoa nafsi na kumkomaza mja na kuipa ukakamavu roho. Humpeleka mja kwenye njia ya waja wakweli, mashahidi na wema. Allah si muhitaji wa utiifu na ibada za waja wake na wala hadhuriki na madhambi wanayoyatenda. Amewaamrisha yote hayo ili waweze kuziongoa nafsi zao.

Lau kama binaadamu wasingekuwa na nafsi basi hali ya ubinaadamu isngekuwepo na badala yake ungekuwa ni umalaika. Kiwiliwili kina mengi inachoyahitaji ikiwemo kula, kunywa, kulala na kupumzika. Kama ambavyo mpanda farasi anvyomuhitaji sana farasi wake na akawa anamuhudumia vyema mnyama wake, basi na binaadamu pia anauhitaji sana mwili wake hivyo ni lazima kuuengaenga vyema. Ibada hutekelezwa na kiwiliwili. Wakati mtu mmoja aliposema kuwa ataswali kucha na hatolala usiku alijibiwa kwamba **ibada zilizo bora ni zile endelevu.** Ibada iliyo endelevu inamkomaza mja kuwa mtumwa wa mola wake.

Kutia nia kuyatekeleza yaliyomo katika dini nayo ni **ibada**. Maamrisho na makatazo ya Allahu taala huitwa **hukmu za Uislam** au **hukmu za Allah**. Yale yaliyoamrishwa kutendwa huitwa **Fardh** na yale yaliyokatazwa huitwa **Haram**. Katika hadithi sharif tunasoma **(Fanyeni ibada kwa kiasi ya uwezo wenu. Ibada ifanywayo katika hali ya furaha huwa na thamani kubwa).** Kiwiliwili kikipata mapumziko basi hufanya ibada kwa upendo. Uchovu wa mwili na akili huifanya ibada isiwe ya kuvutia. Ili kuondosha uchovu inafaa baadhi ya wakati kukifurahisha kiwiliwili kwa yale mazuri yaliyo ya halali. Imam Ghazali "rahimahullahu taala" anasema (Kufanya ibada kwa wingi kunakichokesha kiwiliwili. Ifikapo hivyo ni bora kujipumzisha kwa kulala, kusoma sira za waja wema au kujifurahisha kwa kufanya starehe zilizo halali. Kufanya hivyo ni bora kuliko kufanya ibada na uchovu). Makusudio ya kufanya ibada ni pamoja na kupambana na

nafsi na kuupa utulivu moyo kwa kuuunganisha na mola wake. **(Sala humzuia binaadamu kutenda maasi na matendo maovu).** Sala iswaliwayo kwa mapenzi na furaha ndiyo yenye uwezo wa kufanya hayo. Ili kuweza kupata furaha hii ni lazima kuipatia nafsi baadhi ya matashi ya halali inayoyatamani katika kiwango kinachohitajika. Kufanya hivyo ndio kuutekeleza Uislam. Kuyafanya yale ya halali ambayo yatakupelekea kuweza kutekeleza ibada basi nayo huwa ni ibada. Ushahidi wa haya ni ile Hadithi sharif isemayo **(usingizi wa alim, ni bora kuliko ibada ya jahil).** Kusali sala ya tarawehe hali ya kuwa umeshikwa na usingizi ni makruh. Lazima isaliwe baada ya usingizi kuondoka na kuwa katika hali ya furaha. Sala inayosaliwa na usingizi husaliwa kizembe bila ya mazingatio.

[Kuwa na usingizi na uchovu ni sababu ya kuakhirisha ibada na wala sio kuiacha kabisa. Kuiacha fardhi bila ya udhuru unaokubalika ni dhambi kubwa na ni lazima kuilipa. Mambo ya wajibu pia ni wajibu kuyalipa unapoyaacha. Mwenye kuacha sunna basi hukosa ujira wa sunna hiyo. Ama kujenga mazoea ya kuacha sunna bila ya udhuru basi kutamkosesha mtu shufaa iliyoambatanishwa na sunna husika. Haijuzu kuacha kuitekeleza fardhi katika wakati wake kutokana na uchovu au kukosa furaha. Sababu hizo hazitomuokoa na dhambi na kuadhibiwa kwa kuacha kuifanya ibada katika wakati wake. Kuzibeza hukmu za Uislam yaani halali na haramu na kuacha kuzipa umuhimu, imeelezwa wazi na vitabu vya elimu ya akida kuwa ni ukafiri. Kwenye nukta hii maadui wa Uislam wamejaribu sana kuwahadaa vijana wa kiislam na kujaribu kuuvunja Uislam kwa ndani. Ili tusidanganyike na haya ni lazima kuvisoma vitabu vya elimu za Uislam vilivyoandikwa na maulamaa wa kisunna.]

## KUAMINI KWA KUIGA

8. Gonjwa la nane miongoni mwa maradhi ya moyo ni **kumuiga** mtu usiyemjua. Haifai kuwafuata wanazuoni wasio wa ahli sunna, kusikiliza maneno yao au kusoma vitabu vyao kutokana na kuhadaika tu kwa vile wanasifiwa sana au kutokana na propaganda za nguvu wanazozifanya. Bila ya mtu kuwa unamjua au kuwa umetambulishwa mtu huyo na watu unaowaamini, kumfata mtu huyo iitakadi yake, mafundisho yake na ibada zake kunaweza kukupeleka katika upotofu. Kwa kawaida hatuhitajii kumuiga mtu ili kuweza kumjua Allahu taala na uwepo wake. Mtu yeyote mwenye akili timamu aliesoma sayansi, kwa kuzingatia tu, basi atafahamu kuwa Allahu taala yupo na atapata imani. Hatuwezi tukaiona kazi yoyote iliyofanywa halafu tukakataa

kuwa ina mfanyaji wake! Huo ni ujinga uliotopea. Dini yetu imetuamrisha kuziangalia kwa mazingatio athari mbali mbali ili tuweze kupata imani. Salafi salih wamelieleza hili kwa kauli moja. Baadhi ya watu waliotokana na makundi potofu yaliyojitokeza baada miaka mia nne ya hijria, wameleta fikra kwamba mtu hahitajii kuangalia na kuzingatia maumbile yake na maumbile ya vitu vyengine. Hii si fikra sahihi. Kuleta kwao fikra hii hakubatilishi uoni wa wanazuoni wema waongofu waliokuwa kabla yao. Hivyo pamoja na kuwa mtu aliefuata imani sahihi kwa kuwaiga wazazi wake au walimu wake hukubalika imani yake, lakini bado anakuwa ni mwenye dhambi kwa kuacha kujifunza elimu zitakazompa mazingatio na kuweza kumfahamu Allahu taala. Pia kuna maulamaa wanaosema kuwa mwenye kupata imani kwa kupitia kwa wazazi au walimu hahisabiwi kuwa hakufanya mazingatio yoyote (hivyo hapati dhambi).

Katika ibada na amali ni wajibu kumchagua mmoja kati ya wanazuoni waliofikia daraja ya Mujtahid na kumfuata katika mambo yote. Hii ndio kufuata mmoja kati ya wanazuoni wa madhehebu manne. Na asipompata mwanazuoni wa ahli sunna yeye mwenyewe basi na afuate mafundisho yaliyo katika vitabu vyao. **Ijtihad** ni kile kitendo cha kuelezea yasiyofahamika kwa wepesi katika zile aya na hadithi sharif ambazo hazikuwekwa wazi. Mwanazuoni ambae anakamilisha sifa za kuweza kufanya ijtihad huitwa **Mujtahid**. Hakuna Mujtahid aliyetokea baada ya miaka mia nne ya hijria na wala uhitaji huo haukuwepo. Hii ni kwa sababu Allahu taala na mtume wake walikwishafundisha hukmu zote na kuelezea yale yote yatakayohitajika katika maisha na katika mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia yatakayotokea hadi mwisho wa maisha. Mujtahid waliyaelewa mafunzo haya na kuyafunza kwa wale waliofuata. Wanazuoni waliofuata walielezea vipi mafunzo haya yanaweza kutumika katika hali mpya zinazojitokeza, katika vitabu vyao vya fikh, tafsiri na kadhalika. Wanazuoni hawa huitwa **Mujadid** na wataendelea kutokea hadi mwisho wa maisha. Hivyo wale wanopendekeza kuleta mageuzi katika dini kwa kuengeza vitu vipya kwenye hadithi na Kur-an Karim hao ni maadui wa Uislam. Wanaleta madai kwamba “Mazingira ya kisayansi yamebadilika. Tunakabiliana na matukio mapya. Wanazuoni wanahitajika kukaa na kuandika tafsiri mpya. Ijtihad mpya zinahitajika kufanywa.” Wanadai kuwa nyongeza na mabadiliko yanahitajika kufanywa kwenye nusus (Kur-an Karim na hadithi sharif) jambo linalothibitisha kwamba hawa ni **wazandik** na maadui wa Uislam. Soma kitabu chetu kiitwacho **(Confessions of a British spy).** Maadui wenye dhara zaidi kwa waislam ni Waingereza. Baada ya

kuanza kufuata moja kati ya madhehebu manne, haifai kubadilibadili na kufuata madhehebu mengine bila ya kuwa na uhitaji maalum. Ila kama utakuwa katika mazingira ambayo ni uzito kufuata rai iliyo katika madhehebu yako, basi hapo unaweza ukafuata rai nyengine kutoka katika madhehebu manne. Haijuzu kufanya jambo kwa kukusanya rai za madhehebu manne na kuchagua ile iliyo nyepesi yao. Ibada ifanywayo chini ya utaratibu huo sio sahihi. Kwa vile hakuna mwanazuoni aliyefikia daraja ya Mujtahid baada ya miaka mia nne ya mwanzo ya hijria, haijuzu kuwaiga wanazuoni waliokuja baada ya wakati huo kwenye rai zao. Ili kujifunza madhehebu ya maulamaa waliokuja kabla ya wakati huo, ni wajibu kusoma vile vitabu vya madhehebu husika vilivyokubalika kwa kauli moja na maulamaa wa madhehebu hayo. Haifai kujielimisha kutoka katika vitabu au mafunzo ya wale ambao hawakusadikishwa na kukubaliwa na maulamaa wabobevu, wachamungu wa ahli sunna. Haifai kusoma kitabu chochote tu cha dini na ukaanza kukifuata katika ibada zako. Mafunzo na vitabu vya wanazuoni wasiokuwa wa ahli sunna haifai kuvifuata. Katika madhehebu ya Hanafi vitabu vya **Kadihan, Haniyya, Khulasa, Bazaziyya** na **Zahiriyye** na **Ibnu abidin**, na kwa madhehebu ya Malik **Muhtasar al khalil**, na kwa madhehebu ya shafii **Anwar liamalil abrar** na **Tuhfatul muhtaj** na **Alfikh alal madhahibi l arbai** chenye kuelezea madhehebu manne ni miongoni mwa vitabu vyenye kuaminika. Kujifunza ibada na **hukmu** kutoka kwenye vitabu vya hadithi ni uzito. Vitabu vya hadithi vyenye kukubalika zaidi ni **Bukhari**, **Muslim** na vilivyobaki vinne vijumuikavyo chini ya jina la vitabu sita.

Kitabu thamini chenye kuelezea Tasawuf ni **Mathnawy**. Kitabu muhimu kilichokusanya hukmu za kiislam na tasawuf ni **Maktubat** cha Imam Rabani.

Haijuzu kumfuata na kutumia kitabu chake kila mtu anaetajwa kuwa ni mwanazuoni. Vitabu mashuhuri vilivyotajwa na kuandikwa na maulamaa wa ahli sunna vimetafsiriwa na vinafaa kutumika kwa kupata **elimu za dini**. Vitabu ambavyo havikutafsiriwa kutoka kwa maulamaa maarufu, bali kufuata vitabu vya dini na tafsiri zilizobuniwa vinaweaza kumpeleka mtu kwenye maangamizi hapa duniani na huko akhera. [Musa Beykiyef kutoka mji wa Kazan, kutoka kizazi cha Moskof alikuwa ni kafiri ambae mwenyewe akijitambulisha kuwa ni muislam. Hakuwa akiamini kur-ana karim wala hadithi sharif na alibuni dini mpya ambayo ndiyo aliita Uislam. Akitumia maneno ya kupamba pamba na kuonesha kwamba waislam ni watu wasioendelea na kwamba maulamaa wa ahli sunna ni watu wenye vichwa vigumu na misimamo mikali. Akadai kuwa Kur-ani na hadithi si vitu vya kufatwa

na vijana wa kisasa waliosoma sayansi hivyo fikra alizozizaa ndio akaziita dini na kuwadanganya vijana kwa vitabu alivyoviandika. Wale waliodanganyika, hivi leo wanatoa jarida la kila mwezi kwa kituruki na humo wanaandika uovu na uongo wa kuwahujumu wanazuoni wa Ahli sunna. Tunawaombea dua waweze kusoma vitabu vya ahli sunna ili wapate uongofu.]

Dhambi la pili kubwa baada ya shirki ni bid’a. Kinyume cha bid’a ni kushikamana na sunna. Ibada kubwa kabisa baada ya kumuamini Allah ni kushikamana na imani ya **ahlu sunna**. Maana ya kuwa ahli sunna ni kwamba muislamu katika itikadi na maneno yake, vitendo, ibada zake na muamala wake na watu wengine, atafuata njia ya mtume Muhammad “swallalahu alayhi wasallam” na wale masahaba “radhiyallahu taala anhunna” tabiina na wale waliokuja baada yao katika wanazuoni wa ahli sunna “radhiyallahu taala anhum ajmaina”. Njia waliyoipita tutaijua kwa kusoma vitabu vya fikh na elimu nyengine za dini. Waislam wa kweli ni wale waliofuata njia hii. Wengi wa waislam kutokana na kufuata nafsi zao na akili zao finyu wamefuata maoni yao binafsi na baadhi ya yale waliyoyasoma kwenye sayansi na kuiacha njia ya wanazuoni wa ahli sunna na kuangukia kua **ahlu bid’a**.

[Kushikamana na mtu muovu ambaye hapendi Uislamu kunapelekea kwenye maangamizi. Mafunzo ya Muhammad “swallallahu alayhi wasallam” ndio **hukmu za Uislam**. Watu walio waovu sana ni **Wazandik**. Hawa hubeba majina ya kiislam na kuvaa vilemba na majuba makubwa. Humsifu Mtume “swallallahu alayhi wasallam” na kuusifu Uislam. Ila huvipa Kur-an Karim na sunna maana isiyo sahihi hivyo kuudhuru Uislam kwa namna wanayotaka. Hawa ni vibaraka wa Waingereza, wajinga walionunuliwa na makafiri wa makao makuu ya wamasoni huko London, kwa kulipwa pesa nyingi, na kupewa vyeti bandia na umaarufu. Waislam wenye akili, waliosoma vitabu vya ahli sunna, hawatodanganywa na vibaraka hawa. Mtume wetu alitupa habari kuwa watu hawa watatokea na kwamba watakwenda pata adhabu kali kwenye daraja la chini la moto. Tunaandika mistari hii ili kuwaokoa vijana wetu kutokana na maadui hawa waliojificha. Nasaha zetu hizi zitawafaa wale wenye akili.]

## RIYA

9. Hili ni gonjwa la tisa miongoni mwa magonjwa sitini muhimu ya moyo. Riya ni kukionesha kitu kinyume na kilivyo. Kiufupi ni kujionesha. Ni kufanya matendo ya akhera na kujionesha uko katika njia ya akhera lakini nia hasa ikawa ni kupata faida za kidunia. Kiufupi

ni kuitumia akhera ili kupata maslahi ya kidunia. [Kufanya ibada kwa kuwaonesha watu ili wakupende. Yule ambaye anafanya ibada kwa lengo la kujionesha na hali ya kwamba ana elimu juu ya hilo analofanya huyo huwa **mnafik**, na ikiwa hakuwa na elimu basi huwa mbabaishaji wa dini. Wale ambao hawana elimu ya sayansi na wakajitokeza kwamba wao ni wataalam wa fani hiyo, wakawadanganya waislam kwa kuwatolea maelezo ya kisayansi na kwa kupitia njia hiyo wakawa wanawaharibia dini yao na imani yao basi hao huitwa **wazandik** au **wababaishaji wa sayansi**.] Tutahadhari tusidanganywe na wababaishaji wa dini na wale wa sayansi. Riya itajuzu pale tu ambapo mtu ataifanya kutokana na kutozwa nguvu. Kutozwa nguvu ni kutishiwa kifo au kudhuriwa heshima yako. Wakati huo kufanya riya inakuwa ni dharura. Kutiwa jela au kulazimishwa kwa kupigwa nako ni kutozwa nguvu ila ni kwa daraja la chini. Haijuzu kufanya riya kutokana na hizi sababu za kutozwa nguvu kwa daraja la chini. Kinyume cha riya ni **ikhlas. Ikhlas ni kufanya ibada kwa ajili ya Allahu taala pekee bila ya kutegemea faida zozote za kidunia.** Mtu mwenye ikhlas wakati anafanya ibada zake huwa halimpitikii jambo la kuonesha watu kwa hivyo hata kama watu watakuwa wanaziona zile ibada zake hilo linakuwa haliidhuru ikhlas yake. Katika hadithi sharif tunasoma yafuatayo **(Mwabudu Allahu taala kama kwamba unamuona! Na hata kama wewe humuoni, elewa kwamba yeye anakuona).**

Kuwafanyia watu wema katika mambo ya kidunia ili wakupende na kukusifu nayo pia ni riya. Ila riya ya kwenye ibada ni ovu zaidi kuliko hii. Kufanya jambo hali ya kuwa hukusudii radhi za Allahu taala ndio riya mbaya kuliko zote. Kufanya ibada kwa kutegemea Allah akupe maslahi ya kidunia sio riya. Hili mfano wake ni kuomba dua ya mvua au kusali istikhara. Mfano wa haya pia ni kuchukua ujira wa uimamu, uhatibu na ualimu au kuomba dua kuondoshewa ufakiri, maradhi na matatizo mengine. Haya yamekusanya pamoja nia ya ibada na manufaa ya kidunia. Basi ni hivyo hivyo kwenda hija na ukawa na nia pia ya kufanya biashara. Katika hali hizi nia ya ibada ikikosekana basi huwa ni riya. Nia ya ibada ikiwa ndiyo kubwa zaidi basi thawabu hupatikana. Iwapo muislamu atafanya ibada kwa kuwaonesha wengine kwa lengo la kuwafundisha au kuwahamasisha, basi hio sio riya na atapata thawabu nyingi. Kufunga mwezi wa Ramadhan haiwi riya. Kuanza kusali kwa ajili ya kutaka radhi za Allahu taala kisha kati kati ikachanganyika na riya basi haitohisabika kuwa ni riya. Mtu anaesali kwa kufanya riya atakua ameondosha wajibu wake wa kusali sala ile ila sala yake itakuwa haina malipo. Kuchinja mnyama kwa nia ya kupata nyama yake hakuisabiwi kuwa ndio umefanya ibada ya

kuchinja. Haijuzu kuchinja kwa ajili ya Allahu taala na binaadamu kwa wakati mmoja. Mnyama ambae atachinjwa kwa ajili ya mtu, mfano kwa kurudi kwake vitani au kutoka hija, au kwa ajili ya mapokezi ya raisi au muheshimiwa fulani na ikawa hapakukusudiwa radhi za Allahu taala basi mnyama huyo aliechinjwa anakuwa ni kibudu na hatofaa kuliwa na muislamu. Mtu aliesimama kusali kwa kutaka radhi za Allahu taala na akakumbwa na mawazo ya kidunia ndani ya sala yake yote, basi sala yake ni sahihi. Kuvaa nguo ambayo itakupa umaarufu ni riya. Watu wa dini wanatakiwa wavae mavazi mazuri hasa katika siku za ijumaa na siku za sikukuu.

Kutoa mawaidha, nasaha au darsa kwa ajili ya kujipatia umaarufu ni shirki pia. Kusoma kwa nia ya kuwashinda watu kwenye mijadala, kudhihirisha umahiri na kujikumbia sifa ni riya. Kusoma kwa ajili ya kupata mambo ya kidunia kama mali na cheo basi nayo ni riya. Riya ni jambo la haramu. Elimu inayosomwa kwa ajili ya Allahu taala humuengezea mtu uchamungu. Humuwezesha mtu kuyagundua mapungufu na aibu zake hivyo kuepukana na mitego ya shetani. Maulamaa waitumiao dini kwa ajili ya kupata maslahi ya kidunia huitwa maulamaa waovu na makazi yao ni Jahannam. Ibada yoyote ambayo mtu anapokuwa mbele za watu anaifanya kwa mazingatio na kufuata sunna lakini anapoifanya ibada hiyo akiwa pekee akawa anaondosha njiani tu, basi hiyo nayo pia ni riya.

Kutoa hadiya thawabu zilizotokana na amali aliyoifanya mja na kumpa mja mwengine aliye hai au aliyekufa ni jambo lenye kujuzu. Kwa mujibu wa madhehebu ya Abu hanifa inafaa kutoa sadaka thawabu zilizochumwa kutokana na matendo ya hija, sala, funga, sadaka, kusoma Kur-an Karimi, maulidi au dua. Haisihi kuzifanya ibada hizi chini ya makubaliano ya kulipwa ujira. Kufuatana na madhehebu ya Shafi na Malik thawabu zilizochumwa kutokana na sadaka, zaka na hija; ambazo ni ibada zinazotekelezwa kwa mali; inajuzu kuzitoa hadiya kwa mtu mwengine. Kwa madhehebu haya haijuzu kutoa hadiya thawabu zinazotokana na matendo yanayofanywa kwa mwili kama sala, funga na kusoma Kur-an Karim. Tunasoma kwenye Hadithi sharif kwamba **(Mtu mwenye kupita kwenye makaburi, akasoma surat ikhlas kumi na moja na akatoa hadiya thawabu zake kwa maiti waliopo pale, basi ataandikiwa mema sawa na idadi ya maiti waliopo pale).** Kwa wafuasi wa madhehebu ya Abu hanifa thawabu za suratul ikhlas hizo watazitoa hadiya moja kwa moja kwa hao maiti. Ama wafuasi wa madhehebu ya Shafi na Malik wao baada ya kumaliza kusoma ikhlas watawaombea dua maiti.

Ili ibada iweze kuwa sahihi lazima ipatikane nia ya kutaka radhi za Allahu taala. Nia mahali pake ni moyoni na haitoshelezi kwa kuitamka kwa ulimi pekee. Itajuzu kama nia itatamkwa hali ya kwamba imeambatana na ile ya moyoni. Ikiwa nia iliyotamkwa kwa ulimi ni tafauti na ile iliyo moyoni basi hapa inayotizamwa ni ile ya moyoni. Tafauti na kiapo hakiko hivyo. Kiapo kinatizamwa kwa lile ulilolitaja kwa ulimi. Hakuna hadithi sharif wala habari ambayo imeeleza kuwa nia za ibada zitamkwe kwa ulimi. Hakuna imam yeyote miongoni mwa maimamu wanne aliyefunza hilo. Nia haimaanishi kukumbuka au kuileta moyoni ibada unayokusudia kuifanya. Nia ni kule kuwa na utashi na kusudio la kuifanya ibada kwa ajili ya kumridhisha Allahu taala. Nia ni ile anayokuwa nayo mtu wakati wa kuanza ibada. Kile kinachotokea moyoni kabla ya kuanza ibada mfano siku moja kabla yake hiyo haiitwi nia bali huitwa dhamira, ahadi au tarajio. Mfano wakati wa nia kwa ibada ya funga kufuatana na madhehebu ya Hanafi ni kuanzia pale magharibi ya jioni ya kabla ya siku ya kufunga inapoingia hadi ufikapo wakati wa kuanza funga alfajiri ya siku inayokusudiwa kufungwa.

Kuacha kufanya baadhi ya mambo ya halali ili usisababishe watu wengine kupata madhambi ni jambo lenye kufaa, ila kuacha sunna au mustahab kwa sababu hiyo hilo halitofaa. Mfano ili watu wasikuseme na ikawa ndio sababu ya wao kupata dhambi, ukaamua kutokutumia mswaki wakati wa sala, au kutokuvaa kilemba au kuacha kutumia kipando fulani. Mswaki ni kijiti kilichokatwa kutoka katika mti wa zaituni,mduti au mti wa erak.Kijiti hiki kitakuwa na urefu kiasi na unene kama kidole.Inajuzu kwa wanawake kutafuna ubani badala ya kutumia mswaki.Ikiwa mtu hatopata mswaki basi inajuzu kutumia kidole cha shahada na cha gumba kwa kusugulia meno. Bisri Hafi alikuwa akitembea njiani bila wiatu.

Kuacha kufanya maasi inaweza ikatokana na khofu ya Allahu taala, kuwaonea haya watu au kuacha kwa kuhofia kuwa watu wengine nao wataiga. Dalili ya kuacha maasi kwa kumuogopa Allahu taala ni kile kitendo cha kutokufanya maasi hata ukiwa peke yako. Kuwaonea haya watu ni kule kuogopa kuwa watakutaja vibaya. Kufanya maasi na ukawa ndiyo sababu ya watu wengine nao kufanya, ni uovu mkubwa kuliko kufanya maasi peke yako. Dhambi yoyote iliyoasisiwa na mtu, ataendelea kupata ujira wake muovu kwa muda itakapoendelea kuwepo hadi siku ya kiama. Katika Hadithi sharif tunasoma kwamba **(Ikiwa mja dhambi yake ataifanya kwa siri hapa duniani, basi Allahu taala nae pia atamfichia dhambi hiyo siku ya**

**malipo watu wasiijue).** Ila kuficha maasi na kundelea kuyafanya siri hali ya kujidhihirisha mbele za watu kwamba wewe ni mtu mwema hiyo ni riya.

Haijuzu kuona haya na kuacha kufanya ibada ili watu wasikuone. Maana ya kuona **haya** ni kuacha kudhihirisha maovu na makosa. Kwa hivyo haitojuzu kuacha kutoa mawaidha, kuacha kuamrisha mema na kukataza mabaya, kuacha uimamu au uadhini, kuacha kuandika au kuuza vitabu vya dini, kuacha kusoma Kur-an Karim au maulidi, kwa sababu tu ya kuona haya. Maana ya hadithi sharif isemayo **(Haya ni sehemu ya imani)** imekusudiwa kuona haya kwa kujulikana dhambi na maovu yako. Muumini anatakiwa kwanza amuonee haya mola wake hivyo atekeleze ibada zake kwa ikhlasi na umakini. Siku moja, mmoja katiya ya maulamaa wa mji wa Bukhari wakati akitembea njiani aliwaona watoto wa mfalme wakicheza mchezo mbaya. Akawakamata na kuwatandika kwa bakora yake aliyokuwa nayo mkononi nao wakakimbia. Walipofika kwao wakashitaki kwa baba yao ndipo huyu mwanazuoni akaitwa kwenye hadhara ya mfalme. Mfalme akamuuliza mwanazuoni "Hivyo wewe hujui kwamba mwenye kwenda kinyume na amri za mfalme atakwenda jela?." Mwanazuoni akamjibu "Kwani nawe hufahamu kwamba aendae kinyume na amri za Allah ataingia kwenye Jahannam." Mfalme akendelea "Wewe hii kazi ya kuamrisha mema na kukataza maovu umepewa na nani?" Mwanazuoni akamjibu "Na wewe huu ufalme umepewa na nani?" Mfalme akajibu "Mimi mamlaka haya nimepewa na khalifa." Mwanazuoni akasema "Mimi wadhifa wa kuamrisha mema na kukataza maovu nimepewa na mola wa huyo Khalifa." Mfalme akamwambia "Basi kuanzia leo nimekuchagua uwe muamrishaji mema na mkatazaji mabaya wa mji huu wa Samerkand." Mwanazuoni akajibu "Nami ninajiuzulu na huo wadhifa ulionipa." Mfalme akashangazwa mno na jawabu yake na akamuuliza "Inakuwaje unajiuzulu kutoka kwenye wadhifa ambao kabla uliutekeleza bila ya kuamrishwa wala kuruhusiwa!?". Mwanazuoni akajibu "Wewe ukinipa wadhifa unawezapia kunitengua. Ila wadhifa niliopewa na Allah hawezi kunitengua mtu yeyote." Baada ya kusikia jawabu hiyo Mfalme akamwambia "Vyema. Omba basi kutoka kwangu chochote unachotaka." Mwanazuoni akamwambia "Nirejeshee ujana wangu." Mfalme akajibu kuwa hilo haliwezi. Mwanazuoni akamwambia "Basi nipatie andiko lako ambalo litamuamrisha malaika mkuu wa motoni Malik asinichome motoni." Mfalme akajibu kwamba hilo pia haliko katika uwezo wake. Ndipo mwanazuoni akamwambia "Mimi ninae mfalme wangu ambae mambo

yangu yote ninaomba kwake. Mfalme wangu mimi kila ninalotaka kwake hunipa na hajawahi hata siku moja kunijibu kwamba jambo fulani haliko katika uwezo wake.” Mfalme “Usinisahau na mimi katika dua zako” alimalizia na kumuachia mwanazuoni aende zake.

Tunasoma kutoka katika Hadithi Sharif zifuatazo: **(Wale ambao wakiwa mbele za watu wanasali kwa umakini ila wanapokuwa peke yao wakawa wanasali kwa kuondosha njiani basi hao wamemdhalilisha Allahu taala). (Moja ya jambo ninaloliogopea sana kukukumbeni ni shirki ndogo. Shirki ndogo ni riya). (Yule mtu ambae hapa duniani anafanya ibada kwa ajili ya kuwaonesha watu ataambiwa siku ya kiama: Ewe mja muovu! Leo hapa huna thawabu yoyote. Thawabu zako kazitake kwa wale ambao ulikuwa ukifanya ibada kwa ajili yao huko duniani). (Allahu taala anasema “Mimi sina mshirika. Yeyote atakaenishirikisha, basi akatake thawabu zake kutoka kwa huyo alienishirikisha nae.” Tendeni amali zenu kwa ikhlasi kwani Allahu taala anazikubali zile amali zilizotendwa kwa ikhlas tu).** Ibada hutendwa kwa ajili ya kupata radhi za Allahu taala. Kutenda ibada kwa ajili ya kupata mapenzi au ihsan ya watu wengine hivyo ni kuwaabudu watu hao. Allahu taala anatuamrisha kufanya ibada zetu kwa ikhlas. Katika hadithi sharif Mtume “swallallahu alayhi wasallama” anatwambia **(Yule mwenye kumuamini Allahu taala pekee na akasimamisha sala na kutoa zaka kwa ikhlas, huyo atapata radhi za Allahu taala).** Wakati mtume akimpeleka Muadh bin Jabal kuwa gavana wa mji wa Yemen alimwambia **(Zifanye ibada zako kwa ikhlas. Ibada chache zinazofanywa kwa ikhlas zitakutosha siku ya kiama). (Wahongere wale ambao wanazifanya ibada zao kwa ikhlas. Hizo ni nyota za uongofu ambazo zitaondosha giza la fitna). (Mambo ambayo yameharamishwa hapa duniani ni yenye kulaaniwa. Mambo yenye thamani ni yale yanayofanywa kwa kutaka ridhaa ya Allah).** Dunia ni sehemu ya kupita tu na umri wa binadamu ni mfupi sana. Ni ujinga uliotopea mtu kuiacha dini kwa ajili ya hii dunia yenye kupita. Binadamu ni viumbe visivyo na uwezo. Bila ya kutaka yeye Allahu taala hakuna yeyote anayeweza kumsaidia au kumdhuru mwengine. Allahu taala ni mwenye kutosha kwa mja wake.

Yafaa kumuogopa Allahu taala na kutokukata tamaa na rehema zake. Tuwe na matumaini zaidi kwa Allahu taala kuliko woga. Kuwa katika hali hiyo kutatupa ladha ya ibada zetu. Vijana wanatakiwa wawe na woga zaidi, na wazee wanatakiwa wawe na matumaini zaidi. Wakati wa maradhi tunatakiwa kuwa na matumaini zaidi. Haijuzu kuwa na matumaini bila ya woga au kuwa na woga bila ya matumaini. Hali ya

kwanza ni kuonesha kujiamini sana na hali ya pili ni ya kupoteza kabisa matumaini. Katika hadithi qudsy Allahu taala anasema **(Mja wangu atanikuta kama ambavyo alikuwa akinidhania)** Katika Suratu zumar aya ya 53 katika maana ya aya tunasoma **(Allah anaghufiria madhambi yote. Yeye ni msamehevu mwenye rehema).** Kutokana na aya hii tunatakiwa tuwe na matumaini zaidi. Katika hadithi sharif zisemazo **(Hatoingia motoni yule ambae jicho lake limelia kwa kumuogopa Allah)** na **(lau kama mngeliyajua yale niyajuayo mimi, basi mngelicheka kidogo na mkalia sana)** zinatufahamisha kwamba tunatakiwa tuwe na matumaini zaidi kuliko woga.

## MATARAJIO MAREFU

10. Gonjwa hili la kumi ni ile hali ya mtu kutaraji kuwa na **maisha marefu** ili kuendeleza hawaya na matamanio yake ya kidunia. Kutaraji kuishi maisha marefu kwa ajili ya kutekeleza ibada si sehemu ya gonjwa hili. Mtu mwenye gonjwa hili hatekelezi ibada kwa wakati wake wala haharakii kuleta toba. Moyo wake unakuwa ni mgumu na huwa hayakumbuki mauti. Hata anaponasihiwa na kuwaidhia basi huwa hapati mazingatio. Katika hadithi sharif mtume wa Allahu taala anatwambia **(Likumbukeni sana lile jambo lenye kukatiza ladha za dunia).** Na katika hadithi sharif nyengine **(Lau kama wanyama wangeyaelewa yale mnayoyaelewa nyinyi juu ya akhera, basi msingepata mnyama aliyetononoka).** Akasema tena Mtume “swallallahu alayhi wasallam” **(Yule ambae atakumbuka mauti usiku na mchana, basi atafufuliwa siku ya kiama pamoja na mashahidi).** Mtu mwenye matarajio ya umri mrefu, huuangamiza umri wake kwa kutafuta mali na ulwa na huwa hakumbuki akhera. Anachofikiria zaidi ni matashi na hawaya zake. Kuwatengea watoto chakula cha mwaka haihisabiwi kuwa ni matumaini marefu ya maisha bali hii huingia katika jambo la kukidhi mahitaji ya lazima ya maisha. Akiba hii haihisabiwi kuwa ni utajiri na wala haihisabiwi katika kukamilisha mali ilazimikayo kutolewa zaka (Nasab). Kwa yule ambaye hana watoto basi inajuzu kujibakizia chakula cha siku arobaini. Kujibakizia chakula cha muda mrefu zaidi kunaharibu lile jambo zima la kumtegea Allah (tawakul). Katika Hadithi sharif tunasoma **(Bora wa binaadamu ni yule mwenye umri mrefu uliyojaa ibada)** na **(Muovu wa binaadamu ni yule mwenye umri mrefu uliojaa maovu)** na katika hadithi nyengine **(Msitamani mauti kwani hakika adhabu ya kaburi ni chungu. Kuwa na umri mrefu ukawa unafuata maamrisho ya Uislam ni jambo la faraja)** na **(Nywele zenye kuota mvi ndani ya Uislam, basi huwa nuru siku ya kiama).**

Kuwa na matarajio ya umri mrefu kunatokana na kuyapenda sana matashi ya kidunia, kusahau mauti na kuhadaiwa na siha na ujana. Ili kujitibu kutokana na gonjwa hili, sababu hizi lazima ziondolewe. Inahitaji kukumbuka kwamba mauti yanaweza yakatokea wakati wowote na kwamba siha na ujana si mambo yenye kuzuia mauti. Takwimu zinaonesha kwamba idadi ya watoto na vijana wanaokufa ni kubwa zaidi kuliko ya wazee. Ni mara kadhaa tumeshawashuhudia wale waliokuwa wagonjwa mahututi kupoa na kuendelea na maisha, na wale walio wazima kama chuma kukumbwa na mauti ghafla. Yafaa kwa yule mwenye kulijua hili kujifunza madhara yake na faida ya kukumbuka mauti. Mtume "swallallahu alayhi wasallama" anatwambia katika hadithi sharif **(Yakumbukeni sana mauti. Kuyakumbuka mauti kunamkinga mtu na kutenda dhambi na kumuokoa na yale mambo yenye madhara ya huko akhera).** Anahadithia swahaba Baraa bin Azib "radhiyallahu taala anhu": "Tulimpeleka maiti kaburini. Kisha Mtume wa Allah akakaa pembeni mwa hilo kaburi, akalia na machozi yake matukufu yakadondoka kwenye udongo. Kisha akasema **(Enyi ndugu zangu! Jitayarisheni nyote na tukio hili).** Umar bin Abdul aziz "rahimahullahu taala" alimuona mwanazuoni mmoja na akamuomba amuusie. Yule mwanazuoni akamwambia "Leo wewe ni khalifa ulitakalo una uwezo wa kuliamrisha. Ila kumbuka kuwa kesho mauti yatakuchukua" Umar bin Abdul aziz akamwambia niengeze. Akasema yule mwanazuoni "Tangu Adam alayhi salaam, mababu zako wote wameonja mauti. Sasa zamu ni yako". Maneno haya yalimliza khalifa muda mrefu sana. Na tuzisome kwa mazingatio hadithi sharif zifuatazo: **(Mwenye kutaka mawaidha basi mauti yanamtosha. Na mwenye kutaka utajiri basi kadhaa na kadar vinamtosha). (Mtu mwenye busara kuliko wote ni yule mwenye kukumbuka mauti. Huyu hupata heshima duniani na daraja kubwa huko akhera). (Muoneeni haya Allahu taala. Msipoteze muda wenu kuchuma mali ambazo zitarithiwa na wengine. Msihangaike kupata vitu ambavyo hamtovipata. Msipoteze umri wenu kwa kujenga majumba zaidi ya uhitaji wenu). (Msijenge nyumba zenu kwa vifaa mlivyovichuma kwa chumo la haramu. Vitakuharibieni dini yenu na dunia yenu).** Yafuatayo ndiyo aliyoyasema Mtume "swallallahu alayhi wasallama" kuwaambia masahaba wake wakati aliposikia kwamba sahaba wake ampendae Usama bin Zayd "radiyallahu taala anhu" amenunua mtumwa kwa mkopo wa mwezi mmoja wa dhahabu mia **(Jambo hili nyinyi halikukushangazeni! Usama nae amekuwa mja wa matarajio marefu!).** Inafaa kujinunulia mahitaji ya lazima kwa njia ya mkopo.

Katika hadithi sharif tunasoma **(Mwenye kutaka kuingia peponi asiwe na matarajio ya uhai mrefu. Asiihangaikie sana dunia ikamsahaulisha akhera. Amuonee haya Allah kwa kutokutenda maovu).** Kutaraji umri mrefu ili uweze kufaidika na ladha zisizokubalika kisheria ni haram. Bali kutaka umri mrefu kwa kufaidika na yale ya halali pamoja na kwamba sio haramu, hilo si jambo jema. Lililo bora ni kuwa na siha na afya na wala sio kuishi maisha marefu tu.

## TAMAA

11. Hili ni gonjwa la kumi na moja. **Tamaa** maana yake ni kutafuta matashi ya kidunia kwa njia zisizo za halali. Tamaa mbaya zaidi ni kutegemea kupata kutoka kwa wengine. Zile njia za halali ambazo zitampelekea mtu kuwa na kiburi na kujiona na zile zenye kumsababisha kusahau akhera na matendo ya sunna basi pia huingia katika kundi la tamaa. Kinyume cha tamaa ni **Tafwidh** yenye maana kwamba kufanya jitihada ya kupata chumo la halali na kusubiri matokeo kutoka kwa Allahu taala.

Shetani humdanganya binaadamu kwa kujaribu kumfananishia riya aione kuwa ni ikhlas na tamaa aione kuwa ni tafwidh. Allahu taala amempa wadhifa malaika mmoja katika moyo wa kila mtu. Malaika huyu humuelekeza mtu kwenye fikra njema **(ilham)** na shetani nae humuelekeza mtu kwenye fikra mbaya **(wasiwasi).** Mtu mwenye kula kutokana na chumo la halali ataweza kupambanua baina ya ilham itokanayo na malaika na wasiwasi utokanao na shetani. Yule mwenye kula haramu hatoweza kupambanua. Nafsi yake mtu vile vile humpelekea fikra mbaya moyoni mwake. Hizi ndizo huitwa **hawaya** za nafsi. Ilham na wasiwasi ni vitu vya kupita ila hawaya za nafsi huwepo kila wakati na ni zenye kuongezeka. Wasiwasi hupungua na kuondoka kwa kuomba dua na kuleta dhikri nyingi. Ila hawaya za nafsi zinahitaji mapambano makubwa. Shetani ni kama mbwa, ukimfukuza anakimbia kisha anakuja kupitia njia nyengine. Ila nafsi ni kama chui, shambulio lake ni la kuua kabisa. Ndio maana wasiwasi wa shetani ukaambiwa ni wenye kurudi nyuma **(khanas)**. Iwapo mtu ataamua kutomfuata, shetani hurudi nyuma na kutafuta wasiwasi mwengine wa kumletea. Nafsi ovu daima ni yenye kuamrisha mabaya. Shetani yeye hukuzuia kufanya jambo lenye kheri kubwa na kukutia wasiwasi ikiwa jambo ni lenye kheri ndogo. Ili akuelekeze kufanya dhambi kubwa, hukupambia kufanya kheri ndogo ndogo. Kheri hizi ndogo ndogo zilizopambwa na shetani, binaadamu humvutia na huzikimbilia kuzitenda. Katika hadithi sharif Mtume wa Allah anasema **(Haraka inatokana na shetani**

**isipokuwa katika mambo matano. Kumuozesha mtoto wa kike, kulipa deni, kumpa huduma maiti, kumlisha mgeni na kuleta toba baada tu ya kutenda dhambi).** Katika kitabu cha **Ashiatul aamal** mlango wa kutokucheleweshа sala kuna hadithi sharif isemayo **(Ewe Ali! Mambo matatu usiyacheleweshe. Isali sala mwanzo wa wakati wake unapoingia, maiti akeshatayarishwa msalie haraka, na anapotokea mchumba mwema kwa mjane au binti basi muozeshe haraka).** Kheri inayokuja kwa njia ya ilham, hufanywa pole pole hali ya kuwa na khofu ya Allahu taala na kufikiria hatima yake. Katika hadithi sharif **(Ilham inayotokana na malaika huwa ni yenye kuenda sawa na mafunzo ya Uislam na wasiwasi unaotokana na shetani huwa ni wenye kukengeuka mafunzo ya Uislam).** Binaadamu ayafanye yaliyo ni ilham na apambane dhidi ya wasiwasi wa shetani. Mwenye kuifuata nafsi huangukia kwenye wasiwasi na yule mwenye kuipinga nafsi na hawaya zake huwa wepesi kwake kufuata ilham. Katika hadithi sharif **(Shetani anampa binadamu wasiwasi. Linapotajwa jina la Allah shetani huyu hukimbia na lisipotajwa huendelea kumpa binadamu wasiwasi).** Hadithi hii inatukumbusha ulazima wa kumtaja Allahu taala. Fikra inapokuja katika nafsi ili kuweza kuibagua na kuijua jinsi yake kinachotakiwa kufanya ni kuitizama kama inawiana na mafunzo ya Uislam au haiwiani. Iwapo mtu atashindwa kupambanua basi amtafute mwanazuoni mwema amuulize. Haifai kuwauliza mashekhe waovu ambao huitumia dini kwa ajili ya kupata maslahi ya kidunia. Aidha anaweza kuulizwa yule murshid ambae inatambulika sanadi yake katika kupokea ilmu hadi kufikia kwa mtume "swallallahu alayhi wasallama". Mawalii ambao hutambulika kama **Kutbi madaar** pamoja na kwamba ni wachache lakini wataendelea kupatikana hadi siku ya kiama. Wanazuoni wa kisunna wajulikanao kama **Kutbi Irshad** hawapatikani kila sehemu na kila wakati. Ni nadir kupatikana na hutokea baada ya vipindi vya muda mrefu. Hivi leo wale mashekhe waongo na wajinga wa kitarika walioenea kila sehemu wasidhaniwe kuwa ni waongozaji sahihi. Kuanguka kwenye mitego ya mashekhe kama hao kutamfanya mtu apoteze furaha ya duniani na akhera hivyo ni vyema kuwa macho na kujihadhari nao. Fikra inapokuja katika moyo na ukaiona nafsi inaihisi chungu, basi hilo ni jambo la kheri. Na ile ambayo nafsi inaiona tamu na kutaka kuitekeleza mara moja basi jua kua hio ni shari.

Shetani ni mwenye hila nyingi. Moja kati ya hila zake ni kukwambia Allahu taala hahitajii ibada zako. Ili kuepukana na mtego

huu inafaa kuikumbuka aya ya 62 ya suratul bakara yenye maana isemayo **(faida ya amali njema ni kwa yule mtendaji).**

Hila ya pili ya shetani ni pale anapokwambia Allahu taala ni mkarimu tena msamehemu. Usijali! na wewe atakusamehe na kukuingiza peponi. Dhidi ya hila hii yafaa mtu aikumbuke aya ya 33 ya Surat Luqman yenye maana isemayo **(Msidanganyike kwa kuona Allah ni karimu, mkajiachia na kufanya maovu).** Pia akumbuke aya ya 63 ya Surat Maryam yenye maana inayosema **(Hakika pepo tutawarithisha waja wetu wacha mungu).**

Hila ya tatu ni shetani anapokudanganya kwa kukwambia "Ibada zako ziko ovyo, tena zimejaa riya. Huwezi kuwa mchamungu kwa ibada za namna hiyo. Allah anasema Katika Suratul Maida katika maana ya aya **(Allah anakubali ibada za wachamungu tu).** Wewe ibada zako hizo haziwezi kutakabaliwa. Unahangaika bure kama mnyama mwenye kuchezea bakora bila sababu." Dhidi ya hila na madai haya ya shetani muislamu anahitaji kufikiri na kujisemea yafuatayo "Mimi ninafanya ibada kwa ajili ya kutekeleza amri za mola wangu ili niepukane na adhabu zake. Wajibu wangu ni kutekeleza yale niliyoamrishwa na kukubaliwa au kutokukubaliwa niliyoyafanya hayo ni maamuzi yake Allah mwenyewe. Mimi ninachoelewa ni kwamba ibada zikifanywa kwa kuzingatia fardhi na sharti zake basi zinakuwa sahihi." Kuacha kutekeleza mambo ya fardhi ni dhambi kubwa. Ili kuokoka na dhambi hizo ni wajibu kuzitekeleza hizo ibada. Ni dhambi mtu kuwa hafanyi ibada halafu akanyanyua mikono juu kumuomba Allah amuingize peponi. Hadithi sharif inatwambia **(Mtu mwenye busara ni yule ambae anafanya ibada na kuiasi nafsi yake, ama mjinga ni yule ambae anafuata hawaya za nafsi kisha akategemea kupata rehema za Allah).** Mambo ambayo tunayahitaji kwa akhera yetu tunalazimika kuyatayarisha katika hii dunia yenye kumalizika isiyo ya kudumu.

Hila ya nne ya shetani ni pale anapokwambia, "Wewe sasa shughulikia kufanya kazi ili upate maisha bora. Ukishapata kipato kizuri na maisha matulivu, wakati huo ibada utazifanya vyema zaidi." Anakuingiza katika mtego huo ili uache kujishughulisha na ibada tangu hivi leo. Jawabu ya mtego huu ni kufahamu kwamba siku ya kufa mtu haiamui yeye mwenyewe. Vifo vyetu Allahu taala ameshaviandika tangu azali na huwenda cha kwako ikawa kimeshakaribia. Hivyo kutekeleza majukumu yako ya kiibada leo, bila ya kuakhirisha ndio uamuzi wenye busara. Katika hadithi sharif Mtume wa Allah anasema **(Ameangamia muakhirishaji)** akimkusudia yule mwenye kuacha kutekeleza majukumu yake yaleo na akayafanya kesho.

Shetani anaposhindwa kukuachisha kutekeleza ibada hukujia na hila ya kukutaka utekeleze haraka haraka fardhi zako ili usipitwe na wakati. Nia yake kwa uhakika ni kwamba uharakishe ili kuwe na mapungufu ya fardhi na sharti za ibada zako. Dhidi ya hili ni kufahamu kwamba matendo ya fardhi ni machache hivyo ni vyema kuyafanya kwa unyenyekevu na mazingatio. Na yale yasiyo ya fardhi basi kufanya machache kwa utulivu ni bora kuliko kufanya mengi bila unyenyekevu.

Hila ya sita ya shetani ni kukuelekeza kwenye riya na kukutaka ufanye ili watu waone na wapendezewe. Jawabu kwa hili ni mja kukumbuka kwamba faida na dhara hazimo katika mikono yetu wenyewe. Pia watu wengine hawawezi kutufaidisha kamwe. Hivyo kutegemea kutoka kwa watu wengine ni ujinga ulio batili. Mwenye kutoa yote yenye faida ni Allahu taala pekee, hivyo inatosha kufanya ibada kwa kumuelekea yeye pekee.

Hila ya saba anayoifanya shetani pale ambapo ameshindwa kukuzuia na ibada ni kukufanya ujione. Atakuhadaa kwa kukuonesha kwamba wewe ndie mchamungu zaidi kuliko watu wengine na kwamba wakati watu wote wameghalifika na kulala wewe umesimama unafanya ibada. Bila shaka wewe ni mja bora. Njia ya kuukwepa mtego huu ni kufahamu kwamba busara na tanabahi tulizonazo, ni ihsani Allahu taala kutupa na kama asingetupa basi tusingeweza kujishughulisha na ibada.

Hila ya nane ya sheitani ni kukutaka ufanye ibada zako siri na kwamba Allahu taala ataingiza tu ndani ya mioyo ya watu mapenzi na heshima kwako. Huu ni wito wa shetani kukuita kwenye riya ya siri. Jawabu lako kwake litakuwa ni kumwambia “Mimi ni mja wa Allahu taala naye ndiye anaenimiliki. Kwa namna apendavyo ibada zangu anazikubali na kuzikataa. Binadamu kuzijua au kutokuzijua ibada zangu haiwahusu.”

Mtego wa tisa wa shetani ni kukuhadaa kwa kukwambia kuna uhitaji gani kufanya ibada? Allahu taala ameshakadiria tangu azali kwamba watu wengine ni wema na wengine watakua waovu. Wale ambao wamekadiriwa kuwa wema hata wakifanya maovu Allahu taala atawasamehe na kuwaingiza peponi. Na wale waliokadiriwa kuwa waovu hata wafanye ibada vipi, ni bure tu. Mwisho wao wataingia motoni tu. Hivyo wewe ya nini kujichosha! Jiachie! Kwa hili ni kumjibu shetani kwamba “Mimi ni mja mwenye kuamriwa hivyo nina wajibu wa kuyatekeleza yale ayatakayo mwenye cheo cha kutoa amri” Shetani anaweza kuendelea kukuhadaa kwa kukwambia, unaweza kujilazimisha kutekeleza maamrisho kutokana na kuogopa

kuadhibiwa. Lakini jambo la kuwa watu wema hawatoadhibiwa Allahu taala ameshalikadiria tangu azali, tena kukitiacho wewe wahka ni nini! Kuujibu uzushi huu mja inafaa ajieleze yafuatayo “Mola wangu ni mjuzi wa kila kitu na anafanya alitakalo. Anampa kheri amtakae na anampa shari amtakae. Hakuna yeyote mwenye haki ya kumsaili” Iblisi siku moja alijitokeza kwa nabiyullahi Isa na kumjadili “Wewe si unasema kile alichokadiria Allahu taala tu ndio hutokea” Nabiyullahi Isa “alayhi salaam” akamkubalia hilo. Iblis akamwambia “Jitupe basi kutoka juu ya mlima huu. Kama umeandikiwa tangu azali kuwa usiumie basi hutoumia.” Isa “alayhi salaam” akamwambia “Ewe uliyelaaniwa. Ni haki ya mola kuwajaribu waja wake. Waja hawana haki ya kumjaribu mola wao.” Kwa hivyo katika hoja hii nzima ya shetani mja atakuwa na jawabu ifuatayo “Kufanya ibada ni faida kwangu. Kama nimekadiriwa kuwa ni mja mwema basi thawabu zangu zitazidi na daraja langu litaongezeka. Kama nimekadiriwa kuwa mja muovu nitaepukana na adhabu za kuacha ibada. Kufanya ibada katika hali zote mbili mimi hakunipelekei kwenye madhara”. Allahu taala ni mwenye hekima, hivyo kuwaadhibu wenye kufanya ibada haiwiani na hekima yake. Pia kuacha kufanya ibada kwa kuwa ulikwishakadiriwa tangu azali kuwa ni mtu mwema, si jambo lenye manufaa. Kwa vipi basi lipendelewe hilo? Mtu yeyote mwenye busara hukimbilia kufanya lile lenye faida na kuacha lile lisilo na faida. Kama nimeshakadiriwa kuwa ni muovu basi nitapendelea niingie motoni hali ya kwamba nilikuwa mtii kwa mola wangu kuliko kuingia motoni hali ya kwamba nilikua muasi kwa mola wangu. La muhimu zaidi ni kwamba Allahu taala ameahidi kuwaingiza peponi wale wafanyao ibada na kuwaadhibu wale wasiotenda. Ahadi yake Allahu taala kuwa ni ya kweli na kwamba yeye habadili lile aliloliahidi ni jambo ambalo wamekubaliana wanazuoni wote kwa kauli moja.

Allahu taala kila kitu amekiwekea na sababu yake katika kuumba kwake na huo ndio mfumo wake katika uumbaji. Huweza kuubadilisha huu mfumo katika baadhi ya mambo machache yajulikanayo kuwa ni muujiza na makarama. Ibada kuwa ndiyo sababu ya kuingia peponi ni jambo lililoainishwa. Hii ina maana kwamba neema za peponi ni ujira wa matendo mazuri yaliyofanywa. Kuna hadithi sharif isemayo **(Hakuna mja yeyote atakaeingia peponi kwa sababu ya ibada zake).** Ifahamike kwamba ujira ni kitu chengine na sababu ni kitu chengine.

Hila ya kumi ya shetani ni kukudanganya kuwa kufanya ibada ni jambo lilokadiriwa tangu azali na kudra ya Allahu taala haigeuki. Kufanya au kuacha ibada ni jambo ambalo binaadamu tayari

amekadiriwa na ni lazima kwake kutokea. Madai haya ya shetani ni kama yale yaliyopita kwamba kuwa mtu mwema au mbaya ilikwishakadiriwa tangu azali. Kama umekadiriwa kuwa mwema basi utakuwa mwenye kufanya ibada na kama umekadiriwa kuwa muovu hutofanya. Juu ya hili jawabu litakuwa kama ifuatavyo: Ni kweli kabisa kwamba Allahu taala anaumba kila kitu vikiwemo yeye binadamu bali pia na matendo yake. Lakini katika matendo yake binaadamu, Allahu aala amempa sehemu ya uhuru wa kuamua lipi anataka kulifanya na lipi hataki. Hizi ni nguvu za maamuzi ya moyoni na wala sio nguvu zenye kuumba kitu kikaonekana nje. Nguvu za kuumba kitu anazo Allahu taala pekee na yeye ndie mwenye uhuru wa kuamua uliokamilika. Katika nidhamu yake, Allahu taala amejiamulia kuumba matendo kwa njia ya kutumia uhuru usio kamili wa binaadamu. Hivyo binaadamu kwa kutumia uhuru wake usiokamili huamua katika moyo kutenda jambo zuri au baya, na Allahu taala kwa ujuzi wake usio na mpaka akalifahamu hili na kwa uhuru wake uliokamilia akaamua kuliumba, likatokea na likaonekana nje au akakataa kuliumba hivyo likawa halikutokea. Mbali na nidhamu hii, Allahu taala anaweza kuumba matendo mengi tu ambayo hayakuamuliwa na uhuru usiokamilika wa binaadamu ila katika hali ya kawaida mwenendo wake na nidhamu yake ya kiungu inafuata nidhamu hiyo. Kuna baadhi ya wakati kuna mambo yanayotokea kinyume na nidhamu maarufu ya kiungu ijulikanayo. Hii hutokea katika yale mambo tunayoyaita miujiza ambayo huoneshwa na mitume au **makarama** ambayo huonesha na waja wema wa Allah wateule.

Mambo hayatokei kupitia uhuru usiokamilika wa binaadamu pekee. Binaadamu anaweza akaamua jambo lakini lisitokee nje. Allahu taala naye kwa matashi yake, si katika mwenendo wake kuyaumba matendo bila ya mwanadamu husika kuamua kwa uhuru wake usiokamili. Hivyo binadamu si mwenye kutozwa nguvu na Allahu taala katika kuamua yale ayatakayo. Binadamu hutumia uhuru wake usiokamili kufanya jambo kisha Allahu taala kwa utashi wake ndio jambo hilo huliumba na kulitoa nje. Shetani anchojaribu kumuhadaa binadamu ni kumuonyesha kwamba Allahu taala akitaka ndio anaweza kufanya ibada na asipotaka hawezi. Na kwamba binaadamu ni mwenye kutozwa nguvu katika kufanya au kuacha kufanya jambo fulani. Hivyo binadamu akitenda au asitende, matokeo yatakuwa ni kama vile yalivyoamuliwa azali kwenye kadhaa na kadar. Ukweli katika hili ni kwamba, pamoja na kwamba mambo yanatokea kama yalivyokadiriwa tangu azali lakini kutokea kwake kumetokana na

matashi yake mwenyewe binaadamu kwa kutumia uhuru usiokamilika aliopewa. Yeye mwenyewe binaadamu ndiye alietaka kuwa jambo hilo alifanye au asilifanye. Maana ya kusemwa kuwa Allahu taala amekadiria matendo ya waja tangu azali ni kwamba, mambo gani mja ataamua kuyafanya Allahu taala ameyajua na kuyapitisha tangu azali. Haya yameandikwa kwenye Lawhil mahfoudh. Jambo kuwa limeandikwa kwenye Lawhil mahfoudh haioneshi kuwa mja ni mwenye kutozwa nguvu kwao. Mmoja wa wanazuoni wakubwa bwana Abdulhakim Efendi anasema (kadhaa na kadar iliyoandikwa tangu azali ni kule kujua kwake Allahu taala ni lipi waja wake watataka kulifanya tangu azali, na wala haimaanishi kwamba amemuamulia binaadamu kutenda ayatendayo tangu azali) Yani kadhaa na kadar ni elimu ya azali na wala sio amri ya azali. Sio amri iliyokwisha hukumiwa bali ni elimu iliyokwisha hukumiwa. Ikiwa mtu mmoja atayajua yale ambayo mtu mwengine atayafanya katika siku fulani, naye akataka kwamba mtu yule ayafanye na akayaorodhesha katika karatasi, hii haimaanishi kwamba huyo mtu analazimika kuyatenda hayo. Wala huyu aliyetakiwa kufanya hawezi kuleta madai kumwambia mwenziwe kwamba "Ulijua kuwa nitafanya, ulikuwa unataka kuwa nifanye na ukaandika kwenye karatasi. Kwa hivyo wewe ndie uliyeyafanya haya''. Hayo si madai sahihi kwani huyo mtendaji aliyafanya kwa utashi wake. Ni kweli kwamba huyo mwenziwe aliyajua, aliyataka na kuyaandika kwenye karatasi, lakini hakuyafanya. Hivyo Allahu taala kujua tangu azali, na kutaka jambo litokee na kuliandika kwenye Lawhil mahfoudh haimaanishi kumlazimisha mja kulifanya. Allahu taala ameliandika katika Lawhil mahfoudh tangu Azali kutokana na kuwa yeye atalitaka litokee kwa kujua kwake kuwa mja atapitisha maamuzi ndani ya moyo wake ya kufanya jambo hilo. Elimu ya azali ya Allahu taala ni yenye kufuata yale ambayo mja kwa utashi wake atataka kuyafanya. Kutokea kwa matendo ya mja kunategemea elimu hii na kutaka kwake Allahu taala, na kuumba Allahu taala hilo tendo alilolitaka mja litokee. Mja asipotumia uhuru wake kuamua kufanya jambo, elimu ya Allahu taala imelifahamu hilo tangu azali, hivyo Allahu taala halipitishi jambo hilo wala haliumbi. Hivyo elimu hii inafuata kile kijulikanacho. Lau kama binadamu asingepewa uhuru usiokamili na ikawa mambo yote anaamuliwa na Allahu taala kikamilifu basi tungesema kuwa binadamu ni mwenye kutozwa nguvu katika mambo yake. Kufuatana na madhehebu ya ahlu sunna matendo ya binaadamu yanatokea kupitia matakwa yake pamoja na matakwa ya Allahu taala.

[Moyo (maanawy) wa binaadamu si kitu chenye kugusika. Ni kama mawimbi ya umeme na sumaku. Hauwekeki pahali ukachukua nafasi. Nguvu yake inaathiri kwenye pande la nyama la moyo wa kibaiolojia uliopo kushotoni kwa kifua chetu. Akili, nafsi na roho navyo ni mfano wa moyo si vyenye kugusika. Vyote hivi vitatu vina mahusiano na mafungamano na moyo. Macho, masikio, pua, mdomo na ngozi vinapokea hisia kama rangi, sauti, harufu, ladha ujoto na kupitia mishipa ya fahamu huvipeleka kwenye ubongo. Ubongo unautambulisha moyo juu ya hisia hizo. Akili, nafsi, roho na matashi ya shetani pia huja kwenye moyo. Moyo ndio unachagua, kutaka na kuamua lipi lifanyike. Moyo ukishaamua, unautambulisha ubongo na kwa kupitia mishipa ya fahamu ubongo unavitambulisha viungo vyengine. Ndipo viungo, kwa kutaka Allahu taala, vinaweza kutekeleza lile lililotakiwa na kuamuliwa na moyo.]

## KIBURI

12. Gonjwa la kumi na mbili la moyo ni **kiburi**, nacho ni kujitukuza na kujiona bora kuliko wengine. Moyo unapata raha kwa kujihisi kuwa ni bora kuliko wengine. **Kujiona** pia ni aina ya kujitukuza ila katika hili tafauti na kiburi ni kwamba mtu hajilinganishi na wengine bali hujiona yeye mwenyewe au ibada zake kuwa ni bora tafauti na uhakika ulivyo. Kiburi ni jambo lisilokubalika na ni haramu. Ni alama ya mja kumsahau muumbaji wake. Katika hadithi sharif tunasoma kuwa **(Hatoingia peponi yule mwenye alau chembe ndogo ya kiburi).** Kinyume cha kiburi ni **Tawadhuu** yenye maana ya kujiona sawa na wengine. Hii ni tabia yenye kupendeza mno. Katika hadithi sharif tunasoma kwamba **(Ahongere yule mwenye tabia ya tawadhuu).** Tawadhuu haina maana ya mtu kujidunisha kwa wengine. Si kujidhalilisha wala kuwa masikini. Ni kuchuma mali ya halali na kutoa sadaka nyingi. Ni kutambuana na wanazuoni na wataalamu wa kisayansi. Ni kuwaonea huruma mafakiri. Katika hadithi sharif tunasoma **(Mwenye kufanya tawadhuu, mwenye kuchuma chumo la halali, mwenye tabia njema, anaeamiliana na watu wote kwa upole na kutokumfanyia ubaya mtu yeyote, huyo ni mja mwema). (Mwenye kufanya tawadhuu kwa ajili ya Allah, Allahu taala humpandisha daraja.)** Inajuzu kumfanyia kiburi akufanyiae kiburi. Allahu taala ndiye mmiliki wa kiburi na ametukuka mbele ya waja wake. Kumfanyia kiburi mwenye kutakabbar ni thawabu na kumfanjia upole mtu mwenye kiburi ni kujifanyia dhulma. Pia inafaa kuwafanyia kiburi wale waliopotea na kuacha njia ya haki na kwa matajiri. Kiburi hiki hakilengi kujitukuza lakini kinakusudia kutoa mazingatio kwao. Kujilabu mbele ya maadui katika vita ni jambo lenye

kufaa. Mtu mwenye kutoa sadaka anatakiwa awe na mchanganyiko wa raha, furaha na kiburi kidogo. Kiburi chake kisiwe kwa yule fakiri anaempa sadaka bali kiwe ni dhidi ya mali anayoitoa kwa lengo la kuidhalilisha na kuidogesha. Hadithi sharif inasema **(Mkono wenye kutoa umetukuka kuliko ule wenye kupokea).** Inajuzu kufanya kiburi kwa wenye kufanya riya. Pamoja na kwamba ni vyema kufanya tawadhuu kwa walio chini yako lakini haijuzu kufanya hivyo kwa kupita mpaka. Inafaa kufanya tawadhuu ya daraja la juu mbele ya mwalimu au mwanazuoni lakini haifai kufanya hivyo mbele ya watu wengine. Hadithi sharif inasema **(Kupita mpaka katika tawadhuu, si tabia ya muislam).**

Kiburi kibaya kuliko vyote ni kile mja anachomfanyia Allahu taala. Hivyo ndivyo alivyokuwa Namrudh. Alijitangazia uungu na alipopelekewa mtume na Allahu taala kwa ajili ya kumnasihi, alimrembea kwenye moto. Firauni pia alikuwa ni miongoni mwa wajinga hao. Alijitangazia uungu wa Misri na kuwaeleza watu kwamba yeye ndie mola wao mkuu. Allah alimpelekea Musa alayhi salaam ili amnasihi lakini hakumuamini. Matokeo yake Allahu taala alimzamisha katika bahari ya Suez. Watu kama hawa wasioamini kwamba hii dunia ina muumbaji huitwa **Wapagani.** [Katika kila zama wajinga kama hawa walipatikana. Watu kama Mao na Stalin, wameua mamilioni ya watu. Wamewaua na kuwatesa wanazuoni wa Uislam na kuviangamiza vitabu vyao, bali pia wamewakandamiza raia wao na kuwapa maisha ya kitisho. Kutokana kuweza kwao kufanya kila walitakalo kwa mabavu basi walifurutu ada. Walijidhania kuwa tayari wana sifa sawa na mola muabudiwa na walifikia kulitamka hilo. Walipiga marufuku kuingiza na kusoma vitabu vya Uislam ndani ya nchi zao na wakawaua wale wenye kutangaza dini. Hatimae hawakuokoka na ghadhabu za Allahu taala, nao pia wameangamia kama wenzao. Kama ilivyo kwa madhalimu wote waliopita katika historia, na wao vile vile leo wanakumbukwa kwa laana na chuki. Na wale madhalimu na madikteta ambao walinyakuwa uongozi katika baadhi ya nchi za kiarabu chini ya mwamvuli wa mapinduzi na mageuzi, walikuwa ni watu waliodanganywa akili zao kwa propaganda mbaya, na wakamalizikia kuwaiga hao wapagani kwa kuupiga vita Uislam. Hawakusoma vitabu vya kihistoria ambavyo vinathibitisha kuwa mwisho wa madhalimu ni mbaya! Hawakuzingatia adhabu zitakazowakumba hapa duniani na huko akhera!]

Kuna wengi tuliowasikia ambao wamefanya kiburi dhidi ya Allahu taala. Mfano wa maneno yenye kiburi walioyasema ni haya: “Huyo

mtume anaeambiwa ametumwa na Allah ndio huyu!" na "Lau hii Kuran Karim ingeshushwa kwa mmoja kati ya waheshimiwa wa Makka. Si ingekuwa vyema zaidi!" Katika wakati wote wamekuwepo watu wanaowafanyia kiburi na kuwabeza wanazuoni wa kiislam. Kiburi hiki ni vita vilivyotangazwa na huyu mtumwa, mja dhaifu asiyejiweza kwa chochote, ambaye hayajui hata yale yatokeayo ndani ya mwili wake, dhidi ya mfalme wake, mwenye nguvu zisizo mpaka, aliye mmiliki wake na mola wake mlezi. Kuna wakati Ibilisi nae alionesha kiburi mfano wa hiki. Wakati Allahu taala alipowaamrisha Malaika wamsujudie Adam, Iblis yeye alikwenda kinyume na mola wake na kumjibu "Iweje mimi nilisujudie dongo! Mimi ni mbora zaidi kuliko yeye huyo. Mimi umeniumba kwa moto wakati yeye huyu umemuumba kwa tope." Kwa kuona nuru inayotoka katika moto wakati wa kuwaka kwake basi akadhani kuwa moto ni bora kuliko maji na dongo. Uhalisia ni kwamba utukufu haumo katika kujitukuza bali umo katika kufanya tawadhuu. Peponi kuna dongo, nalo litanukia kama miski. Peponi hakuna moto. Moto utatumika kwa kuadhibu kwenye Jahannam. Moto unatumika kuangamizia wakati dongo hutumika kujengea. Viumbe wanaishi juu ya dongo. Madini na hazina nyengine hupatikana chini ya ardhi. Kaaba imejengwa kwa udongo. Pamoja na kwamba mwangaza wa moto unaleta mchana na kumaliza kiza cha usiku, matunda na mauwa yote yanamea ardhini. Aliye mbora wa viumbe vyote Muhammad "swallallahu alayhi wasallama" kwake ni kwenye udongo.

Katika hadithi sharif **(Allahu taala anasema, Kiburi, ukubwa na utukufu ni vyangu pekee. Yeyote atakaetaka kushirikiana na mimi katika haya basi nitamtupa motoni na wala sitamuonea huruma)** na wakati mtume sallallahu wasallama aliposema **(Hatoingia peponi yule ambae ana lau chembe ndogo ya kiburi ndani ya moyo wake)** waliuliza masahaba "Je kupenda kuvaa nguo nzuri na viatu vizuri ni kutakabbar." Nae mtukufu wa daraja akajibu **"Allahu taala ni mzuri na anapenda mambo mazuri."** [Yale yote yanayofanywa kwa ajili ya kuwa msafi na mtanashati na kuwa usionekane ovyo mbele ya watu huitwa uzuri. Vitu vya lazima vitumikavyo kufikia uzuri huitwa ni mahitaji ya lazima ya kujinadhifishia. Kufanya mabadiliko katika mwili au kuvaa mavazi ya ghali kwa ajili ya kujitukuza kwa wengine huko huitwa kujipamba na vitu vitumikavyo huitwa mapambo. Hivyo ni vitu visivyo vya lazima kwa mahitaji ya kulinda afya na heshima yake mtu. Wanaume haijuzu kutumia vitu vya mapambo mahali popote na wanawake haifai kuyatumia mbele ya wanaume wasio maharim wao.] Hadithi sharif isemayo (Allahu taala mambo yake yote ni mazuri na

anawapenda wenye tabia nzuri) inatudhihirishia kwamba kama ilivyo kwa wenye dhambi nyengine, watu wenye kiburi hawatoingia peponi bila ya kuadhibiwa kwanza. Wale ambao hawatokuwa wameingizwa peponi bila ya shaka watakuwa wako motoni kwa sababu hizo ndizo sehemu mbili pekee za kupelekwa watu huko akhera. Wale wenye imani alau ndogo hawatadumu motoni bali hatimae wataingizwa peponi. Wale waumini ambao watafanya madhambi makubwa kisha wasilete toba, na wakawa hawakupata shufaa wala msamaha, basi hao wataadhibiwa motoni kwa uzito wa dhambi zao, kisha wataingizwa peponi. Katika hadithi sharif Mtume wa allah anasema **(Muumini ambae hana kiburi, khiyana, wala hana haki ya mtu mwengine basi ataingia peponi bila hesabu)** na **(Kuwa na haki ya mja mwengine ni aibu na ni mapungufu kwa muumini).** Kukopa kwa ajili ya mahitaji ya lazima ya nyumbani na kulipa mara tu upatapo ni wajibu. Katika hadithi iliyopita kilichokusudiwa ni deni lililochukuliwa bila ya kuwa na uhitaji wa lazima na likawa halikulipwa baada ya kupata uwezo, deni lilokopwa kwa njia za haram, deni la mahari na deni lililotokana na kazi ya kusomesha elimu ya dini. Wakati mtume "swallallahu taala alayhi wasallam" akikata roho alisema **"Ewe Ali! Kuna myahudi fulani ananidai. Mlipe huyo."** Alikuwa amekopa ngano kwa myahudi hivyo akausia akalipwe. Mmoja kati ya masahaba ambae aliwahi kuwa mwanazuoni mkubwa wa kiyahudi, lakini baadae akasilimu baada ya kuzungumza na mtume na kugundua kua ni mtume wa kweli, bwana Abdullah bin Salam "radiyallahu taala anhu" siku moja alikuwa amebeba mzigo wa kuni mgongoni kwake. Waliomuona wakamuuliza kwa nini anajipa mashaka yale na hali ya kuwa yeye ni Tajiri mwenye mali nyingi. Akawajibu kuwa anajaribu kuiokoa nafsi yake na kiburi. Tajiri kuacha kumpa ujira mchukuzi na kuamua kubeba mzigo yeye mwenyewe ni kujidogesha na kujidunisha. Afanyapo hilo kwa lengo la kupambana na nafsi yake na kufikia tabia njema ni jambo zuri na lenye thawabu. Katika hadithi sharif mtume wa Allahu taala anasema **(Watu watatu hatazungumza nao Allahu taala siku ya kiama na atawaadhibu adhabu kali. Anaezini uzeeni, mtawala asemae uongo na fakiri mwenye kiburi).** Wakati Sayyidna Umar "radhiyallahu anhu" alipofanya ziara katika mji wa Sham, siku ya kuwasili kwake alitoka Gavana wa sham, Abu Ubayda bin Jarrah "radhiyallahu taala anhu" kumlaki akiwa pamoja na viongozi, wakuu wa vikosi vya ulinzi na watu wengine. Katika safari hiyo yeye Umar "radhiyallahu anhu" alikuwa akipanda ngamia wake kwa kupokezana na mtumwa wake. Wakati wanaingia na kulakiwa na watu wa Sham, ilikuwa ni zamu ya huyo mtumwa kupanda, hivyo waliingia hali ya kua mtumwa yuko juu ya

ngamia na khalifa wa waislam ameshika hatamu za ngamia huyo. Wakati wakiingia palikuwa na mto mdogo wa kuvukwa hivyo khalifa wa waislam alivua viatu vyake akakunjia kunjia na kupita. Gavana wa Sham Abu Ubayada bin Jarrah “radiyallahu anhu” akamwambia “Ewe khalifa wa waislam, mbona unafanya hivyo! Watu wote wa Sham, wakiwemo Warumi wametoka ili kumuona khalifa wa waislam. Wote wanakuangalia wewe hivi sasa. Hawatovutiwa na hilo.” Umar akamjibu “Ewe Abu Ubayda! Haya uyasemayo yanaweza kuwa na madhara makubwa kwa hawa waliohudhuria hapa. Watakaosikia watadhani kwamba utukufu wa mtu unapimwa kwa kipando alichopanda na uzuri wa mavazi yake na mapambo yake. Hawatofahamu kwamba utukufu ni kuwa muislamu na kutekeleza ibada. [Sisi tulikuwa ni dhalili, tumekandamizwa na wafalme wa kiajemi.] Allahu taala akatutukuza kwa kutufanya waislam. Utukufu huu aliotupa Allahu taala kama tutauacha na kutafuta utukufu katika jambo jengine, Allahu taala atatufanya tuwe dhallili tena na atatudhalilisha kuliko vitu vyote. Utukufu unapatikana kwenye Uislam. Mwenye kuufuata Uislam huwa mtukufu. Yule asieridhika na hukumu za Uislam na akatafuta utukufu, utulivu na furaha kupitia vitu vyengine huyo atakuwa dhalili.” Tawadhuu ni moja ya amri za Uislam. Mwenye kufanya tawaadhuu, hutukuka na kupanda daraja. Mwenye kiburi hudhalilika.

Katika hadithi sharif tunasoma **(Wale walio na kiburi hapa duniani, siku ya kiama watatolewa makaburini dhalili na wamedogeshwa kama mdudu chungu. Watakuwa na umbile la binaadamu mwenye udogo wa mdudu chungu na watadharauliwa na watu wote. Wataingizwa kwenye moto wa Jahannam chini kabisa kwenye pango liitwalo Bolis. Pango hilo limepewa jina hilo kwa sababu ni pango ambalo waingiao humo hukata tamaa ya kutoka tena. Wataadhibiwa kwenye moto huo na watakapoomba maji ya kunywa basi watanyeshwa usaha wa watu wa motoni).** Siku moja Gavana wa mji wa Madina Abu Hurayra “radhiyallahu taala anhu” alikuwa akipita njiani hali ya kuwa amebeba mzigo wa kuni. Muhammad bin Ziyad “rahimahullahu taala” akamfahamu na kuwaambia wale aliokuwa nao wakae pembeni kumpa njia Gavana. Wale waliofatana nae wote walishangazwa kwa kuona ile tawadhuu ya kiongozi huyo. Tunasoma katika hadithi sharif kwamba **(Alitokea mtu mmoja katika umati zilizopita, alikuwa akiburura nguo yake chini kwa kiburi alichonacho. Tabia hii ilimkasirisha Allah hivyo ardhi ilimmeza mtu huyo)** na katika hadithi nyengine Mtume anasema

**(Kupanda punda, kuvaa nguo ya kitambaa cha kaniki na kukamua maziwa mnyama ni dalili kwa mtu anayefanya haya kuwa hana kiburi).**

Kiburi kina sababu saba kuu. Elimu (hata ya dini), ibada, nasabu, uzuri, nguvu, mali na cheo. Sifa hizi zikipatikana kwa mtu jahil basi zinaweza kumsababishia kiburi.

Elimu husababisha kiburi, lakini pia ndiyo dawa yake. Kiburi kinachotokana na elimu ni sugu kupoa. Elimu ni kitu chenye thamani kubwa hivyo mtu alie na elimu hujidhani yuko juu na mtukufu. Mtu mwenye dhana kama hio basi ni sahihi elimu yake kuiita ujahil. Elimu ya kweli ni ile itakayomuezesha mja kuyaona mapungufu na udogo wake na kuufahamu utukufu na ukubwa wa yule aliyemuumba. Humuongezea woga kwa muumbaji wake na tawadhuu kwa waja wenziwe. Humuongezea hima ya kulinda haki za waja wenziwe. Elimu ya namna hii huitwa elimu yenye manufaa nayo ni fardhi kujifunza na kuifundisha. Elimu hii inapelekea kufanya ibada kwa ikhlas. Tiba ya elimu yenye kusababisha kiburi ni kujua mambo mawili. La kwanza ni kujua kwamba, ili elimu iwe na thamani na utukufu basi inategemea na uzuri wa nia ya mja. Mja awe anajifunza kwa nia ya kutokana na ujinga na kuepukana na hawaya za nafsi. Na wala asisome kwa kutaka kutambulika kwa kuwa imam, mufti au shekhe. La pili aelewe kwamba elimu lazima iambatane na amali na kuwafundisha wengine na yote hayo yafanywe kwa ikhlas. Elimu isiyo na amali wala ikhlas ni yenye madhara. Katika hadithi sharif tunasoma kwamba **(Elimu ambayo hakujifunza mtu kwa ajili ya Allahu taala, itamuweka juu ya moto wa Jahannam).** Mfano wa elimu hiyo ni ile iliotafutwa kwa ajili ya mali, cheo au umaarufu. Kusoma elimu ya dini kwa ajili ya kupata maslahi ya dunia ni sawa na kula kinyesi kwa kutumia kijiko cha dhahabu. Wenye kuitumia dini kwa ajili ya kupata maslahi ya kidunia ni wezi wa dini. Katika hadithi sharif tunasoma kuwa **(Wenye kutumia elimu ya dini kupata maslahi ya kidunia, hawataisikia harufu ya pepo).** Inajuzu kujifunza elimu za sayansi ili kupata maslahi ya kidunia, bali ni lazima kufanya hivyo. Katika hadithi sharif tunasoma **(Wenye elimu katika umma huu watagawika makundi mawili. Kundi la kwanza ni lile ambalo litakuwa na faida kwa binaadamu. Hili ni lile kundi la wale wasiotegemea malipo ya kidunia. Mja huyu ataombewa dua na samaki walio baharini, wanyama walio ardhini na ndege walio hewani. Kundi la pili ni la wale ambao elimu yao haiwafaidishi watu bali ni ya kupatia maslahi ya kidunia. Hawa watapigwa minyororo ndani ya Jahannam).** Kur-an Karim inatutambulisha kuwa vinamsabihi

Allahu taala vyote vilivyopo ardhini na duniani. Hadithi sharif inatwambia **(Wanazuoni ni warithi wa mitume).** Hii ina maana kwamba mwanazuoni wa kweli ni yule alie kwenye njia na mwenye kufuata yale aliyokuja nayo Mtume "swallallahu alayhi wasallam". Mwanazuoni mwenye kufuata mafunzo ya Uislam ni nuru yenye kuwaangazia walio pembeni yake. Katika hadithi sharif tunasoma kwamba **(Siku ya kiama ataletwa shekhe na kutumbukizwa motoni. Wale wanaomfahamu mle motoni watamkusanyikia na kumwambia "Wewe duniani ulikuwa ukifunza amri za Allah, vipi umeingia kwenye adhabu hii?". Naye atajibu "Nilikuwa nikiyafanya yale niliyokuwa nikiyakataza. Na sikuwa nikiyatekeleza yale niliyokuwa nikiyaamrisha. Ndio maana leo ninaadhibiwa.").** Na katika hadithi sharif nyengine **(Wakati nilipopelekwa safari ya Miraji huko mbinguni, niliwaona watu wakikatwa ndimi zao kwa mikasi ya motoni. Nikamuuliza Jibril hao walikuwa ni nani. Akanieleza kuwa hao ni makhatibu na watoaji mawaidha ambao walikuwa wakiamrisha mambo hali ya kuwa wao hawayatekelezi).** Na tunasoma aidha kwenye hadithi nyengine kuwa **(Mazabbaniya (watesaji) wa motoni wataanza kuwatesa mahafidh waliofanya maovu kabla ya wale wenye kuabudia masanamu kwa sababu dhambi yenye kufanywa kwa kujua ni mbaya zaidi kuliko yenye kufanywa kwa ujinga).** Masahaba kutokana na elimu zao wakiogopa dhambi zote, kubwa na ndogo. Mahafidh waliotajwa katika hadithi hii itakuwa ni wale waliohifadhi Taurati kwa sababu waislam waliofanya dhambi hawatoadhibiwa zaidi ya makafiri. Pia inaweza kuwa ni mahafidh wa umma huu ambao wamekufuru kwa kutokuyapa umuhimu madhambi na kutokujiepusha nayo. Katika hadithi sharif Mtume wa Allah anasema **(Iwapo wanazuoni hawatojichanganya na viongozi wa kisiasa, na wakawa si wenyekukimbilia kukusanya mapato ya kidunia basi watakuwa ni mikono miaminifu ya mitume. Ama watakapojichanganya na wana siasa na wakaanza kujikusanyia mapato ya kidunia basi watakuwa wameifanyia hiyana amana hii).** Kama ambavyo mweka amana analazimika kuhakikisha kwamba mali aliyoachiwa iko salama, basi ni hivyo hivyo kwa wanazuoni, wanalazimika kuhakikisha kuwa elimu ya dini haiharibiwi. Siku moja wakati Mtume „swallallahu alayhi wasallama" akifanya tawaf kwenye Kaaba aliulizwa ni mtu gani aliye muovu zaidi. Naye akajibu **"Usiulize aliye muovu! Uliza aliye mzuri. Mwanazuoni muovu ndie mtu muovu zaidi."** Hii ni kwa sababu mwanazuoni afanyapo dhambi, huifanya hali ya kuwa anajua. Nabiyullahi Isa alayhi salam amesema (Mwanazuoni muovu ni sawa na jabali lililopo kwenye njia ya maji. Jabali lenyewe

halichuruzishi maji wala haliruhusu maji yaliyopo kupita). Mwanazuoni muovu ni kama msingi wa maji machafu. Ukiuangalia juu umejengwa vyema na unapendeza ila ndani umejaa uchafu. Katika hadithi sharif tunasoma kwamba **(Mtu atakaepata adhabu kali zaidi siku ya kiama ni yule mwanazuoni ambae elimu yake haikumfaidisha chochote).** Na hii ndio sababu itakayowafanya wanafiki; wale makafiri wanaojidhihirisha kama waislam; waingie kwenye shimo la chini kabisa la motoni kwani wao pamoja na kusikia na kufahamu, walifanya inadi na kuchagua ukafiri. Mtu mwenye elimu ya dini, ima itampelekea kupata furaha ya milele au ataangukia kwenye balaa lisilo na mwisho. Mtume wa Allah anasema katika hadithi sharif **(Baadhi ya mahabusu wanaoadhibiwa motoni watatoa harufu mbaya kiasi ya kwamba mahabusu wenzao watakirihika zaidi na harufu hiyo na itawachukiza kuliko hata adhabu ya moto. Watawauliza hao wanukaji, kwa nini wanatoa harufu kirihifu kama hiyo. Nao watawajibu kwamba wao walikuwa ni wanazuoni wasiotekeleza yale wayajuayo).** Bwana Abu Dardaa „radhiyallahu taala anhu“ anasema (Mwanazuoni asiyefuata ilmu yake, haitwi mwanazuoni). Iblisi alikuwa na elimu ya dini ya kutosha ila hakutekeleza kufuatana na ilmu yake. Mfikirie mtu aliepekee jangwani na akawa na panga nyingi na silaha nyengine, jasiri na mwenye kujua kuzitumia silaha hizo. Iwapo atavamiwa na simba na asizitumie silaha hizo, basi je silaha hizo zitakuwa na faida yoyote?. Basi ni hivyo hivyo kwa elimu ya dini. Hata kama utajifunza masuala laki moja lakini kama hukuyatumia hayatokupa faida. Mtu mwenye maradhi thakili, hata kama dawa yake itapatikana, bila ya kuitumia dawa hiyo hawezi kupata faida.

Hadithi sharif inatwambia **(Katika zama za mwisho, wengi wa wale wafanyao ibada watakuwa ni wajinga wa dini yao. Na wale viongozi wa dini wengi watakuwa ni waovu).** Viongozi wa dini watakuwa waovu kwa kujichanganya kwao na watawala kwa ajili ya kupata maslahi ya kidunia. Sufyan Thawry „rahimahullahu taala“ anasema "Ndani ya Jahannam kuna bonde ambalo ndani yake wataadhibiwa wale viongozi wa dini wenye riya na waliojichanganya na watawala" Anasema tena Sufyan "Elimu yangu ilikuwa imesonga mbele sana kiasi ya kwamba nilikuwa ninaweza kuifasiri aya tukufu kwa njia thalathini tafauti. Siku moja nikahudhuria mualiko wa chakula wa sultan. Chakula kile kiliniathiri na tahamaki nikawa nimeyasahau yale yote niliyokuwa nikiyajua." Muhammad bin Salama „rahimahullahu taala“ anasema (Mwanazuoni mwenye kusubiri

kwenye mlango wa mtawala kwa ajili ya manufaa ya kidunia, ni mbaya zaidi kuliko nzi aliye juu ya kinyesi).

Katika hadithi sharif tunasoma kwamba **(Yule ambae amepewa elimu na Allahu taala kisha asiwasomeshe wengine basi siku ya kiama atafungwa pingu za moto).** Hiyo itakuwa ndio hali ya wanazuoni wenye kuficha elimu yao. Katika suratu Nisaa aya ya 5 isemayo **(Mali yenu msiwape wajinga)** imepewa katika maana kuwa msiwape elimu zenu wanafiki na mabazazi.

Mtume wa Allah anatwambia katika hadithi sharif **(Uislam utaenea kila pembe. Wafanya biashara wa kiislam watavuka bahari bila pingamizi na farasi wa jeshi la kiislam watatembea kwenye miji mengine. Kisha baadhi ya wanazuoni wataanza kuzunguka na kusema "Je yuko alienizidi mimi kwa usomi. Kuna yeyote anayejua zaidi yangu!?" Hao ndio kuni za Jahannam).** Hadithi inatufahamisha kwamba wenye kutafuta elimu kwa lengo la kufanya riya na kiburi wataingia motoni.

Hadithi sharif inasema **(Yeyote mwenye kujitangazia uanazuoni ni jahil).** Mwenye kutoa jawabu kwa kila suala, mwenye kuelezea kila akionacho na mwenye kuuza elimu yake kila pahali basi huyo anadhihirisha ujahili wake. Yule mwenye kusema sijui, ninahitaji kujifunza kwanza ili niseme, anadhihirisha kuzama kwake kwenye elimu. Wakati mtume "swallallahu alayhi wasallama" alipoulizwa ni ipi sehemu bora zaidi alijibu **(Sijui. Allahu taala atakaponijulisha nitakujibuni).** Alipomuuliza suala hili Jibril nae akampa jawabu hilo hilo. Nae alipomuuliza Allahu Taala akaelezwa kuwa ni **Miskiti.** Katika suratul Aaraf aya ya tano katika maana ya aya tunasoma **(Fanya msamaha na uamrishe mema)** mtume alimuuliza Jibril maelekezo ya aya hii nae Jibril akamwambia hafahamu mpaka akamuulize Mola wake. Mara nyengine alipokuja akamueleza yale Allahu taala aliyoyaamrisha katika hiyo aya kwamba **"Yule ambae anajiweka mbali nawe, wewe mkurubie. Yule mwenye kukunyima, wewe mkirimu. Na yule mwenye kukudhulumu, wewe msamehe."** Shabi "rahimahullahu taala" alipoulizwa na mtu mmoja akajibu "sijui", yule mtu akamwambia "Wewe ndie Mufti wa Iraq, haipendezi kujibu sijui". Shabi akasema "Malaika wakubwa wamejibu sijui. Kuna tatizo gani na mimi kutoa jawabu hiyo!" Imam Abu Yusuf "rahimahullahu taala" alipoulizwa na akasema sijui wakamwambia "Unachukua mshahara kutoka mfuko wa mali ya waislam lakini ukiulizwa unasema sijui". Akajibu imam Abu Yusuf "rahimahullahu taala" "Mshahara ninaochukua ni kwa kadiri ya yale ninayoyajua. Lau kama ningechukua

mshahara na kwa yale nisiyoyajua pia, basi pesa zilizo katika mfuko wa mali ya waislam zisingelitosha.” Kufanya urafiki na jahili asiefuata nafsi yake ni bora kuliko kufanya urafiki na kiongozi wa dini mwenye kuifuata nafsi.Mwenye kufanya kiburi kwa kuwa ni mwanazuoni basi hiyo ni dalili ya ujahili.Hii ni kwa sababu elimu inampelekea mtu kwenye tawadhuu na kumuweka mbali na kiburi.

Kufanya kiburi ni haram. Kutakabbar ni sifa ya Allahu taala na ni mahsusi kwake. Mja kwa kiasi atakavyojidhalilisha kwa mola wake ndio daraja yake inavyopanda na kwa kiasi atakavyojitukuza ndio anakuwa dhalili mbele ya Allahu Taala. Mtu asiyejua madhara ya kiburi ni makosa kumwita mwanazuoni. Elimu ya mja inapoongezeka na uchamungu wake ndio unaongezeka na huzidi kuogopa kutenda maasi. Ndio maana mitume wote; Allahu taala awawie radhi; walikuwa ni watu wenye tawadhuu, wakimuogopa sana Allah na hawakuwa na kiburi wala kujiona. Kuwafania kiburi wadogo au mafasik pia haifai. Mwenye kiburi pekee ndio inapasa nae kumfanyia kiburi. Mtu alie na elimu amuonapo asie na elimu yafaa ajiambie kwamba “Huyu akifanya maasi ni kutokana na kutokujua kwake ila mimi ninafanya maasi hali ya kuwa ninajua.” Na amuonapo mwenye elimu yafaa aseme “Huyu ana elimu kuliko mimi na anaifanyia kazi. Matendo yake anayafanya kwa ikhlas. Mimi bado sijafikia hivyo.” Na amuonapo mwenye umri zayidi yake yatakiwa afikirie kwamba mwenziwe ameshafanya ibada zaidi yake na awaonapo wadogo kuliko yeye afikirie kuwa hao ni wachache wa madhambi akilinganisha na yeye mwenyewe. Na anapowaona wale walio sawa nae kiumri yafaa aseme “Ninayajua madhambi yangu ila siyajui matendo yake. Udhalili umo ndani ya dhambi zinazotambulika.” Na atakapowaona watu wa bid’a na makafiri yafaa afikirie na kusema “Mwisho wa mja unajulikana wakati wa pumzi yake ya mwisho. Mimi yangu siijui itakuwaje” Asiwafanyie kiburi watu hao ilapia asiwaoneshe mapenzi. Wale ambao wanaeneza ukafiri na bid’a na kuleta mabadiliko katika dini, hao ni maadui wa sunna za Mtume swallallahu alayhi wasallama. Wanachofanya ni kuizima nuru ya sunna na kueneza upotofu wa bid’a, kuwataja vibaya maulamaa wa ahli sunna, na kuzifasiri kimakosa aya na hadithi za mtume kwa lengo la kuupiga vita Uislam kwa ndani.

[Vitabu vyote vinavyochapishwa katika taasisi yetu ya uchapishaji, ni tafsiri ya vitabu vya maulamaa wa ahli sunna “rahimahumullahu taala” na wala si mawazo yetu binafsi. Katika vitabu vyetu tunawafahamisha vijana utukufu wa wanazuoni wa ahli sunna “rahimahumullahu taala” na kwamba ili kuweza kupata furaha ya

duniani na akhera njia pekee ni kufuata njia iliyoainishwa na wanazuoni wa ahli sunnatu waljamaa “rahimahumullahu taala”. Katika kutoa huduma hii hatutegemei manufaa yoyote ya kidunia. Watu wa bid’a na wale wanaopinga madhehebu wanaweza wasipendezwe na vitabu vyetu hivyo wakazuia kuenea na kusomwa kwake. Wanaweza wakatoa uzushi wa kishetani dhidi ya vitabu vyetu. Kwa vile hawana elimu, hawawezi kupata mapungufu ya kielimu ndani ya vitabu hivi. Hawawezi kuleta madai kwamba vitabu hivi vinachapishwa kwa kutafuta pesa au manufaa mengine ya kidunia. Kilichobakia ni kusema tu kwamba vitabu hivi ni viovu visisomwe. Tunapowauliza uovu huo uko wapi watuoneshe basi jawabu lao huwa, sisi tumesikia tu, hivyo ndio inavyosemwa. Alhamdulillah! Vijana walioamka hawahadaiwi na madai ya vizabizabina hao; na kila siku zikiendelea wasomi wa vitabu hivi wanazidi. Haifai kuwapenda waharibifu na vizabizabina hawa.]

Inafaa mtu kutoyasahau madhambi yake na kufikiria kadar yake vipi imeandikwa tangu azali na ni upi mwisho wake. Ni yupi aliye mbora huko akhera, hilo haliwezi kujulikana hapa duniani. Kuna wana dini ambao pumzi yao ya mwisho ilimalizikia katika ukafiri na kuna makafiri ambao walimalizikia kuwa waumini. Mtu kujidhania kuwa yeye ni wa peponi na kwamba kafiri ni wa motoni (kabla uhai haujamalizika) ni sawa na kudai kuwa anajua ya ghaib; jambo ambalo ni kufur. Malazi ya mtu kuwa ni ya peponi au ya motoni yanajulikana baada ya kumaliza uhai wake. Vipi uhai wake binadamu utamalizika ni katika elimu ya ghaib. Hivyo haifai kwa mtu yeyote kufanya kiburi.

**SUALI:** Kuwakataza maovu na kuwanasihi makafiri na watu wa bid’a ni jambo la lazima. Je mtu ambae amejidunisha kwa watu hao vipi ataweza kuwanasihi? Aidha katika ada za kiungu ni kwamba mtu atakufa kwa namna ambavyo maisha yake aliyaishi na kama imetokea kinyume cha hivyo ni nadra sana. Na pia ni kwamba Allah anawasifu waumini na kwamba wao ni bora kuliko makafiri. **JAWABU:** Kutokuwapenda makafiri ni kutokana na kwamba Allahu taala ametutaka tusiwapende na wala sio kwa kuwa sisi ni watukufu zaidi. Mfalme anapompeleka mwanawe sehemu, humpa mlinzi afatane naye na huyu mlinzi hupewa ruhusa ya kumkemea na kumpiga huyo mwana wa mfalme kama atafanya kosa kubwa. Huyu mlinzi anapompiga huyo mtoto anafahamu kwamba yeye si mwenye utukufu zaidi yake wala hafanyi kiburi kwa hilo. Muumini kutokumpenda kafiri inafanana na hilo. Allahu taala anawafahamisha waumini kwamba utukufu hauko katika dhati yao bali uko kwenye imani yao. Yeyote

atakaekuwa na imani basi atapata utukufu. Utukufu wa milele unategemea maisha ya mja yalivyomalizika.

Ili ibada iwe na thamani nayo hutegemea masharti yake. Muislamu hapitishi muda wake ovyo kwenye mambo yasiyo na faida. Anasema Sayyidna Abubakar "radhiyallahu anhu" "Kwa kuhofia kwetu tusije tukaanguka kwenye dhambi moja tu basi tukiacha kufanya mambo sabini ya halali" Hivyo haifai kuziamini sana ibada tunazofanya wala kujitukuza kwa wingi wa ibada. Ili ibada itakabaliwe inahitaji nia iliyotakasika na kwamba ibada ile iwe imefanywa hasa kwa kutaka radhi za Allahu taala. Kuipata ikhlas hii sio rahisi. Kuitakasa nafsi kunakuja na taqwa. Taqwa nayo hupatikana kwa kujiepusha na maasi. Mtu ambae hajaitakasa nafsi yake, ni uzito kuweza kufanya ibada zake kwa ikhlas.

Kujisifu na kutakabari kutokana na mababu zake mtu ni ujahili na ujinga uliotopea. Kabil, mtoto wa Adam alayhissalam na Kan'an, mtoto wa Nuh alayhissalam, hawakuokoka na ukafiri kwa kuwa baba zao ni mitume. Mababu zao wanaojitukuza kutokana nao, hivi sasa wao ni gao la mchanga tu. Je! ni jambo la akili mtu kujisifia kwa sababu ya gao la mchanga. Asijisifu mtu kwa wema wa mababu zake ila ajitahidi kuwa mwema kama wao na kufuata njia yao.

Wanawake wengi hufanya kiburi kutokana na uzuri wao. Uzuri si kitu cha kudumu, unafifia haraka na wala si kitu kilicho kwenye milki yake binaadamu. Ni ujinga mkubwa kujigamba kwa kitu ambacho hufifia na kuondoka. Uzuri wa nje utakuwa na thamani pale tu utakapokwenda sambamba na usafi wa moyo yaani tabia njema. Usafi wa moyo hujidhihirisha kwa kufuata mwenendo wa Mtume swallallahu alayhi wasallam. Binaadamu asipoupa thamani usafi wa moyo na uzuri wa tabia basi huwa hana tafauti na wanyama bali anaweza akawa daraja la chini kuliko wanyama. Anakuwa ni kama mashine mbovu iliyopasukapasuka na kujaa uchafu. Mashine ambayo kila wakati inahitaji maangalizi, ukarabati na usafishwaji. Je! yafaa kwa mtu kama huyu kufanya kiburi!? Kinachofaa zaidi kwake ni kuwa na tawadhuu.

Kufanya kiburi kutokana na nguvu na ujana ni ujinga. Wanyama viungo nyao vya hisia na makanikia vina nguvu zaidi kuliko binadamu. Kwa mantiki hiyo basi wanyama walitakiwa wawafanyie kiburi wanaadamu. Ni nani ana uhakika kwamba kijana siku zote atabaki mwenye nguvu na hatakumbwa na maradhi, madhara au ajali? Je kuna yeyote alieshuhudiwa kudumu daima na ujana, nguvu na harakati

zake? Katika hali hii basi je ni jambo la akili kweli kufanya kiburi kwa kitu cha mpito, kinachokuwepo kwa muda mfupi sana, kitu ambacho hata wanyama wanacho?

Haipendezi hata kidogo kwa binaadamu kufanya kiburi kutokana na mali, watoto, cheo na ulwa. Hivi si sehemu yake binaadamu bali ni vitu vya mpito vyenye kuja na kuondoka. Ni vitu ambavyo hata watu waovu wenye maadili mabaya pia wanaweza kuwanavyo. Pengine watu wa aina hiyo wawe navyo zaidi. Lau kama hivi vingekuwa ni vitu vitukufu vya kufanyia kiburi, basi hao watu waovu wasio na maadili nao wangekuwa ni bora kuliko wale watu wasio na vitu hivyo. Kama ingekuwa mali ni nyenzo ya utukufu basi tungetakiwa na wezi nao pia tuwatukuze wanapoiba na kumiliki mali.

**Hikdi** pia isiwe ni sababu ya kufanya kiburi. Hikdi maana yake ni kuwa na uadui wa moyoni na kuweka chuki. Ni mtu kumchukia mtu mwengine aliye daraja sawa au daraja ya juu zaidi kuliko yeye. Kwa vile hawezi kumfanya kitu basi humfanyia kiburi. Haoneshi tawadhuu mbele ya mtu ambae anatakiwa kumfanyia hivyo. Hakubali maelekezo sahihi na nasaha za mtu huyo. Hupenda kujionesha mbele za watu kuwa yeye ni bora kuliko mtu huyo. Hata anapomkosea basi huwa hamuombi radhi.

**Hasad** nayo inaweza kuwa ni sababu ya kiburi. Hasidi hutaka neema aliyonayo mtu fulani imuondokee ili aipate yeye. Hakubali maelekezo sahihi na nasaha za huyo mwenziwe. Hadiriki hata kumuuliza kitu kwa lengo la kujifunza. Pamoja na kufahamu kwamba huyo mwenziwe yuko juu kuliko yeye, basi pia humfanyia kiburi.

**Riya** nayo pia hupelekea kwenye kiburi. Hujionesha kwa tendo la riya na kuwafanyia kiburi watu asiowajua mbele ya watu wengine. Kwa kawaida wanapokua pekee huwa si mtendaji wa jambo hilo. Kuwaokoa watu hawa na kiburi inahitajika kwa watu wenye elimu kuvaa mavazi yanayokwenda sambamba na heshima yao. Katika hili Imam adham Abu Hanifa “rahimahullahu taala” akiwataka wasomi wavae vilemba vikubwa na Majuba yenye mikono mipana. Ni jambo la ibada kwa mtu kupendeza kwa mavazi mazuri mbele ya watu anaowapa nasaha na kuwawaidhi ili aheshimike. Wasipompa heshima hawawezi kumsikiliza kwa sababu watu wajinga humhukumu mtu kwa mavazi yake, hawafahamu elimu na mwenendo wake.

Watu wengi hawajifahamu kwamba ni wenye kiburi hivyo ni vyema kuzijua alama za kiburi. Kupenda watu wakusimamie unapoingia sehemu fulani ni dalili ya kiburi. Iwapo mwanazuoni

anaefahamu kwamba watu wanamuheshimu ikawa anaridhia kusimamiwa na watu ambao anawapa nasaha basi hicho si kiburi. Kupenda kuwa katika hali ya kukaa na watu wakawa wamekusimamia mbele yako ni kiburi. Imam Ali “radhiyallahu anhu” anasema “Mwenye kutaka kumuona mtu wa motoni basi na amtizame yule ambaye amewasimamisha wengine mbele yake hali ya kuwa yeye amekaa” Masahaba “ridhwanullahi alayhim” wakimpenda Mtume “alayhi wasallam” kuliko kitu chochote ila hawakuwa wakimsimamia Mtume aingiapo kwa sababu wakifahamu kwamba Mtume swallallahu alayhi wasallam hakuwa akilipenda hilo. Ila mwanazuoni anapoingia ni vyema kusimama kwa ajili ya kuonesha utukufu wa elimu. Yahya bin Kattan “rahimahullahu taala” baada ya kusali sala ya laasiri alikaa hali ya kuwa ameegemea mnara wa msikiti. Wakaja kwake baadhi ya wanazuoni maarufu wa wakati wake akiwemo Ahmad bin Hambal “rahimahullahu taala”. Wote wakaanza kumuuliza maswala mbali mbali katika elimu ya hadithi hali ya kuwa wamesimama mbele yake. Yahya akawa anawajibu. Hakuwaambia wakae wala wao wenyewe hawakuthubutu kukaa. Mazungumzo yao yaliendelea hadi wakati wa sala ya magharibi. Kijana mwenye elimu akae sehemu ya juu kuliko mzee asie na elimu. Mwanafunzi asianze kusema kabla ya mwalimu wake, na iwapo mwalimu hayupo basi asikae sehemu yake. Watembeapo, asitembee mbele yake. Ikiwa mtu anajihisi anapenda watu wamsimamie lakini ikawa anapambana ili jambo hili litoke ndani ya nafsi yake, hili huhisabiwa kuwa ni tashi la kimaumbile au hata wasiwasi wa shetani. Hali zote hizi mbili haziisabiwi kuwa ni dhambi kwa sababu ni jambo ambalo liko nje ya uwezo wake.

Kuwa na utashi kwamba utembeapo kuwe kuna kundi la watu linakufuata nyuma basi hiyo ni dalili ya kiburi. Kupenda kwamba wewe uwe umepandia mnyama na wanafunzi wako wanatembea kwa miguu ni alama ya kiburi. Mtume wa Allah “swallallahu alayhi wasallama” siku moja alikuwa akienda kuyatembelea makaburi ya Bakii huko Madina. Baadhi ya masahaba “ridhwanullahi alayhim" wakamuona na wakaanza kumfata nyuma. Mtume wa Allah “swallallahu alayhi wasallama” alisimama na kuwataka wapite mbele naye akatembea nyuma yao. Alipoulizwa sababu ya kufanya hivyo alijibu **(Nilizisikia sauti za nyayo zikitembea nyuma yangu. Nikaamua kufanya vile ili nisije nikapatwa na chembe ya kiburi ndani ya moyo wangu).** Kiuhakika ni kwamba hilo lisingempa kiburi mtume wa Allah ila alifanya hivyo ili liwe ni somo la vitendo kwa masahaba zake. Abu Dardaa “radhiyallahu taala anhu” anasema “Mtu mwenye kiburi, kwa kiasi

ambacho watu wanaotembea nyuma yake wanaongezeka, ndio hivyo hivyo masafa baina yake na Allahu taala yanavyoongezeka.”

Kutokuwatembelea jamaa zako ni alama ya kiburi. Kuwatembelea watu walio chini kuliko wewe ni dalili ya tawadhuu.

Kutokupenda mtu akae ubavuni kwako, kutokukaa na mgonjwa, kutokufanya shughuli za nyumbani mwako mwenyewe, kutokwenda wewe mwenyewe kununua vitu vya mahitaji ya nyumbani kwako, kutokuivaa tena nguo ambayo ulikwisha wahi kuivaa, zote hizi ni alama za kiburi. Kadhalika kutokutaka kuonekana na sare ya kazi wakati uko kazini. Kutokuhudhuria mialiko ya watu masikini hali ya kuwa ya watu matajiri unahudhuria nacho ni kiburi. Kutokuwapatia mahitaji ya lazima watoto na jamaa, kutokukubali maneno ya ukweli unayoelezwa na kuleta mjadala, kutokuwashukuru wenye kukukosoa na kukuonesha mapungufu yako haya yote kama yatafanyika mbele ya watu itakuwa ni riya na kama mtu atayafanya akiwa pekee au akiwa na mhusika tu basi itakuwa ni kiburi.

Ili kuweza kuwa mwenye tawadhuu ni lazima ajue binadamu wapi alitokea kuja duniani na wapi anaelekea, na kwamba kabla hakuwepo. Kwanza alikuwa ni mtoto mchanga asiyeweza kufanya lolote. Na hivi sasa yuko chini ya tishio la kuweza kuumwa na kupoteza maisha wakati wowote. Hatima yake ni kufa, kuoza na kugeuka udongo. Chakula cha wanyama na wadudu. Sawa na yule aliye katika chumba cha mahabusu akisubiri kunyongwa. Maumivu anayoyapata wakati anasubiri kuuwawa ni sawa na hii jela iitwayo dunia. Ni sehemu ya kusubiri tu, muda wowote itampeleka mtu kwenye adhabu. Atakufa awe mzoga, chakula cha wadudu na atakabiliana na adhabu ya kaburi kisha atafufuliwa ili kupata adhabu ya siku ya kiama. Basi ni lipi linalomfaa zaidi mtu ambaye anaishi na woga wa kudumu motoni; kiburi au tawadhuu? Muumbaji wa wote, mwenye kukidhi mahitaji yao, anaewalinda na madhara yote, atakae wahisabu siku ya kiama, atakaewaadhibu, mwenye nguvu na uwezo usiopimika ambae hana mshirika wala mfanana nae, mmiliki na muweza pekee Allahu taala anasema **(Wenye kiburi siwapendi. Niwapendao ni wale wenye tawadhuu).** Kiumbe ajizi, ambae hana uwezo wa kufanya lolote, aliye mnyonge, ni lipi kati ya haya lililo sawa kwake kufanya? Mja mwenye akili anayejifahamu na kumfahamu mola wake anaweza kweli kufanya kiburi? Binadamu kila wakati anatakiwa adhihirishe mbele ya mola wake unyonge wake na kushindwa kwake. Kila pahala na kila wakati adhihirishe haya kwa kufanya tawadhuu. Abu Sulayman Darani “rahimahullahu taala” anasema “Ikiwa watu wote watataka

kunitukana na kunidharau hadi niwe chini ya daraja nililo hivi sasa hilo hawatoweza. Kwa sababu katika daraja lolote watakalofikiria kunishusha kwa matusi na dharau zao, mimi ni dhalili zaidi na niko chini zaidi ya hilo" Je binadamu anaweza kujidhania kuwa yuko daraja ya chini kuliko watu wote; hata Firauni na Iblisi? Kwa sababu hawa wawili; na madhalimu wengine wa binaadamu na Uislam waliokuja siku za karibuni kama Stalin na Mao; ndio waovu wa makafiri wote. Walidai uungu na kutesa na kuuwa mamilioni ya watu kwa ajili ya kufikia matakwa yao. Bila ya shaka hawa ndio makafiri wakubwa. Allahu taala hawa amewaghadhibikia na na amewashusha kwenye daraja ovu kabisa la ukafiri. Ila mimi amenivisha rehema zake na kunipa uongofu na imani. Lau angelitaka (Allah) angelifanya kinyume na haya lakini Alhamdulillah hakufanya hivyo. Pamoja na hayo, nimefanya dhambi nyingi hadi kufikia umri huu, dhambi ambazo hajawahi kufanya mtu yeyote. Sijui hali yangu itakuwaje wakati wa pumzi yangu ya mwisho. Haya ndiyo yafaayo mja kuiambia nafsi yake kwa kuonesha tawadhuu.

Katika hadithi sharif tunasoma **(Allahu taala ameniamrisha niwe mwenye tawadhuu. Mmoja wenu asimfanyie mwengine kiburi).** Katika hadithi hii tunafahamu kwamba wale wasio waislam wanaoishi katika nchi ya kiislam chini ya maridhiano maalum au wageni wanaoingia katika nchi ya kiislam kwa ruhusa mfano watalii, wafanyabiashara na wawekezaji, haifai kuwafanyia kiburi.

[Hadithi hii pia inatufahamisha kwamba katika nchi za makafiri zisizo chini ya muafaka maalum hairuhusiwi kwa muislamu kuzidhuru mali zao, roho zao, heshima zao, kufanya wizi katika nchi hizo, kupinga sharia za nchi, kuwatukana wafanyakazi wa idarani, kuvunja amani na utulivu wa nchi, kutolipa kodi au nauli katika vyombo vya usafiri au kufanya lolote ambalo liko kinyume na utukufu na uzuri wa mwenendo wa kiislam. Katika nchi hizi za kikafiri, kutokupinga sharia zao za kikristo haimaanishi kuwa ndio kuwakubali wao kuwa ulul amri. Amri ambazo zinapelekea kumuasi Allah hazipingwi.Hii ikiwa ni kwa ulul amr au kwa makafiri amri zao hazipingwi. Kwenda kinyume na amri za serikali popote ulipo, hiyo husababisha fitna. Kusababisha fitna ni haramu. Katika vitabu vya fikhi mlango wa "Ikrah" na pia katika juzuu ya tatu ya kitabu cha Muhammad Ma'asum "rahmatullahi alayhi" kwenye barua ya 55 maelezo ya suala hili yanapatikana. Kuna baadhi ya watu ndani ya nchi za kiislam au zile za kikafiri, ambao wameacha mafunzo haya ya mtume swallallahu alayhi wasallama, nao huwafanzia vitendo vya utovu wa adabu makafiri na kwenda kinyume na mipango ya kiidara ya nchi, basi huwa wamefanya dhambi, bali pia kuufanya Uislam na

waislam waonekane washenzi. Wanakuwa wameufanyia Uislam khiyana kubwa.

Jihadi maana yake ni **kuamrisha mema na kukataza mabaya.** Jihadi ni ya aina mbili. Ya kwanza ni ile ya kuutambulisha Uislam kwa makafiri na kuwaokoa kutokana na madhara ya ukafiri. Ya pili ni ile ya kuwafunza waislam dini yao ili waweze kuepukana na yale ya haram. Zote hizi aina mbili za jihadi zinafanyika kwa njia tatu. Njia ya kwanza ni kwa kiwiliwili. Na hii inajumuisha kufanya jihadi kwa kutumia njia zote za kivita ili kupambana na madikteta na watawala ambao wanawazuia wanyonge kufikiwa na habari ya Uislam na kuwaelekeza kwa mabavu kwenye ukafiri kwa kuwakandamiza na kuwafanyia mateso ya aina tafauti. Kupambana na madikteta na wakoloni hao kwa kutumia vifaa vya kisasa kabisa hadi kuwashinda na kuyaondoa makucha yao kutoka kwa wale walio dhaifu waliodhulumiwa na kuwatoa kwenye utumwa. Kisha kuwafunza uzuri wa Uislam na kuwaita waingie katika dini. Wasipotaka, wataruhusiwa kuishi pamoja na waislam ndani ya nchi, chini ya amri ya Uislam ya haki usawa na uadilifu hali ya kupewa haki sawa na waislam na kuruhusiwa kuendelea na dini zao. Jihadi hii ya silaha hufanywa na dola. Jeshi la nchi na vikosi vya ulinzi ndio hufanya hilo. Bila ya idhini ya dola haijuzu kwa muislamu yeyote kuwavamia au kuwapiga vita makafiri. Muislamu ambae atamuua kafiri alie katika maafikiano maalum na dola anastahiki kupewa adhabu ya kiwango cha juu kabisa. Hapa inafahamika kwamba jihadi katika Uislam haimaanishi kubomoa miji na kuua watu. Jihadi ni kuwafahamisha watu Uislam kwa upole ili waupende na kwa hiari zao waingie kwenye dini. Mtume „swallallahu alayhi wasallama“ na masahaba „ridhwanullahi taala anhu ajmaina“ na dola za kiislam za kikweli kama vile dola ya Othman, kwa namna hio ndio zilipigana jihadi. Hawakuwavamia wanyonge wasio na silaha. Wao walipambana na madikteta, wakoloni na wale wanaobeba majina ya kiislam katika watu wa bid’a ambao walizuia Uislam usiwafikie wanyonge na wasiutambue.

Wadhifa wa pili wa vikosi vya ulinzi na jeshi la kiislam ni kuilinda nchi ya kiislam na raia wake dhidi ya makafiri na wale wenye itikadi mbovu za kibaguzi wenye nia ya kuuangamiza Uislamu. Katika suratul Anfal Allahu taala anawaamrisha waislam kutafiti na kuzijua silaha zinazozalishwa katika dola za kikafiri ili nao waweze kuzalisha katika kipindi ambacho hakuna vita. Dola isiyofanya haya huwa haikufuata maamrisho ya Uislam. Huku ni kutokufanya matayarisho ya kujibu

hujuma za maadui jambo ambalo litasababisha maelfu ya waislam kupoteza maisha na Uislam kudhoofika.

Aina ya pili ya jihadi katika Uislam ni kutumia njia zote za habari na mawasiliano katika kuufikisha na kuufahamisha Uislam. Hili hufanywa na wanazuoni wa kiislam kwa msaada na usimamizi wa dola. Katika zama zetu hizi maadui wa kiislam wakiwemo makafiri, wamisionari, wamasoni, wakomunisti na wapinga madhehebu wanatumia njia zote za habari na mawasiliano kuupiga vita Uislam. Wanatumia uongo na uzushi ili kuwahadaa watu na wale wajinga miongoni mwa waislam kwa lengo la kuuangamiza Uislam. Ilitokea katika mwaka 1992 wakristo kubuni maswala 11 na kuyapeleka katika miji yote ya waislam. Huko Bangladesh wanazuoni waliyajibu masuala hayo yote na kuwafedhehesha viongozi wa dini ya kikristo. **Hakikat Kitabevi** walioko Istanbul wameziingiza jawabu hizi chini ya mlango uitwao **"Alkadhibul jadydatul hiristiyaniyyah"** katika kitabu kiitwacho **"Asswiratul mustaqim"** na kukipeleka kitabu hiki duniani kote. **Kadiyani, Bahai,** wafuasi wa **Mawdudy, kundi la tabligh, kundi la salafi, kundi la wasio** na **madhehebu na Wahabi** wamefuata Uislam usio sahihi kutokana na kutoa maana zisizo sahihi kutoka katika Kur-an Karim na hadithi sharif. Makundi haya yote huchapisha vitabu, vitini na vipeperushi, aidha hurusha matangazo ya redio kueneza imani zao zisizo sahihi. Wanatumia mamilioni ya pesa kwa ajili ya kazi hii. Kwa upande mmoja wanawadanganya wale waislam wa kweli wa **ahli sunna**; na kuuvunja Uislam kupitia ndani. Na upande mwengine wanaeneza duniani Uislam usio sahihi. Hivyo wale wageni wa dini wanaotaka kuingia Uislam wanabaki kuduwaa hawajui wafate lipi. Matokeo yake ima wanaghairi kuwa waislam au wanaangukia kwenye njia isiyo sahihi hali ya wenyewe kujidhani tayari wamekuwa waislam sahihi.

Jihadi yenye thamani kubwa leo kwa waislam wa kweli wa ahli sunna ni kutumia njia zote za habari kueneza Uislam sahihi duniani kote ili kupambana na maadui wa nje na ndani ya Uislam, wenye kufanya propaganda potofu zenye kuvuruga.

Aina ya tatu ya jihadi ni ile inayofanywa kwa dua. Ni lazima (fardhi ayn) kwa waislam wote kufanya jihadi hii na kuiacha ni dhambi. Jihadi hii pia hufanyika kwa kuwaombea dua wale wenye kufanya jihadi ya aina ya kwanza na ya pili. Dua yoyote yenye kuombwa kwa ikhlasi basi kwa hakika hupokelewa.

Aina hizo tatu za jihadi zilizotajwa ikiwa zitafanywa kwa kutegemea msaada wa Allahu taala na kufuata misingi ya dini basi bila ya shaka msaada wa Allahu taala utapatikana. Allahu taala hawezi kupokea dua zetu iwapo matayarisho ya lazima ya jihadi zikiwemo silaha, mazoezi ya ukakamavu na mapenzi baina yetu hayakupatikana. Ili dua ikubaliwe kwanza tunalazimika kukamilisha matayarisho ya lazima ya jambo husika. Na hiyo ndiyo maana ya kutawakal. Na kama tulivyosisitiza ili jihadi ifanikiwe lazima misingi ya dini ifuatwe. Uislam unasisitiza kwamba kabla ya jihadi kufanyika lazima matayarisho makini yafanyike. Ili kuweza kuingia katika aina ya kwanza ya jihadi basi matayarisho ya vifaa vya kisasa vya kivita na namna ya kuvitumia lazima yafanyike. Pia lazima kuwepo utiifu wa makamanda wa jeshi kwa serikali na kuepuka kuleta migawanyiko. Kila muislamu anatakiwa asaidie taasisi za ulinzi kwa kiasi ya uwezo wake. Vile vile ni wajibu kuzisaidia kimali jumuia na taasisi mbali mbali za maulamaa wa ahli sunna wenye kujishughulisha na aina ya pili ya jihadi. Hii itakuwa ni jihadi ya mali. Wale wenye kufanya jihadi kwa miili yao na mali zao, Allahu taala amewaahidi pepo siku ya kiama. Ali Muhammad Belhi, katika kitabu chake kilichochapishwa kwa lugha ya kiajemi mwaka 1411 Hijria; **Muuftiyyi mujahid**; ameelezea kwa kirefu maswala ya jihadi.]

Katika hadithi sharif Mtume wa Allah anatwambia yafuatayo **(Miongoni mwa wale waliopata neema, wenye kuonesha tawadhuu na wakajua mapungufu yao, wakachuma chumo la halali na kutumia katika njia za kheri, na wenye kuweka sambamba elimu ya fikh ne hekima [yaani tasawuf] wenye kuchukua tahadhari juu ya halali na haramu, wenye kuwaonea huruma mafakiri, wenye kutekeleza amali zao kwa kutaka radhi za Allah, wenye tabia njema na wasiomfanjia uovu mtu yeyote, wenye kutekeleza amali zao kwa elimu,wenye kugawa ziada katika mali yao na wale walio wachache wa maneno wote wahongere).**

Tawadhuu inayofanywa kwa dhihaka, riya, unafiki, woga, au kwa nia ya kupata mali au cheo ni katika tabia mbaya. Ili kuepukana na tabia hiyo mbaya ni lazima kujiepusha na yale maovu yasababishayo hilo. Mtu aliyetakasika na maovu hayo na akawa na tawadhuu basi huyo ndie mwenye mwenendo mwema.

## THAMANI YA ELIMU NA WANAZUONI

Katika kitabu kiitwacho **Riyadhun nasihin** (kimeandikwa na Muhammad Rabhami mwaka 835 hijria na kuchapishwa Bombay

mwaka 1313 hijria kisha kikachapishwa tena na Hakikat Kitabevi ya Istanbul mwaka 1994) kilichoandikwa kwa kiajemi, kuanzia ukurasa wa 356 muandishi anasema:

Katika kitabu cha **Mirshadul ibaad minal mabdai ilal miad** (Muandishi ni Najmudyn Abu bakar Razi, alikufa mwaka 654) imeandikwa hadithi sharif isemayo **(Mwenye kujifunza elimu kwa lengo la kupata heshima mbele ya wanazuoni au kwa lengo la kulumbana na wajinga ili apate umaarufu basi kamwe hatoingia peponi).** Hadithi sharif hii inatufahamisha kwamba, mwenye kutafuta elimu kwa ajili ya kupata mali, cheo au kukidhi matashi yake ya kinyama na asieitumia elimu kwa ajili ya kutekeleza amali zake, huyo huwa si mwanazuoni wa kiislam. Katika hadithi sharif nyengine **(Mwenye kujifunza elimu kwa ajili ya dunia basi atapata mali na ulwa duniani ila malipo yake ya akhera yatakua ni moto).** Elimu kama hiyo haina faida na inafaa kujiweka nayo mbali. Kama tunavyosoma katika hadithi sharif nyengine **(Ewe mola, nilinde na elimu isiyo na faida).** Elimu ambayo muislamu analazimika kujifunza huitwa elimu ya kiislam. **Elimu ya kiislam** imegawika sehemu mbili ambazo ni **elimu ya dini** na **elimu ya sayansi**. Wanamageuzi wa dini wameiita elimu ya dini kuwa ni **elimu ya kiskola** na ile ya sayansi wameiita kuwa ni **elimu ya kimantiki**. Elimu isiyo na faida nayo ni ya aina mbili. Aina ya kwanza ni ile impelekayo mtu motoni kama ambavyo imeainishwa hapo juu. Na ya pili ni ile elimu ya sayansi itolewayo bila elimu ya dini. (Mateso yaliyofanywa na dola kongwe ya kirumi dhidi ya wayahudi kwa kuwatupa kwenye mazizi ya simba, mateso ya kinyama yaliyofanywa na wakristo katika zama za kati huko Palestina, mauaji ya halaiki yaliyofanywa na Hitler huko Ulaya na yale yaliyofanywa Asia na wakoministi wa Kirusi na Kichina, uvamizi wa Waingereza katika nchi mbali mbali na kuwagawa wananchi wake na kutia choko choko na ugomvi baina yao, yote yalitekelezwa kutokana na aina ya pili ya elimu ya sayansi). Allahu taala anawataja hawa madhalimu, maadui wa binadamu ambao wameendelea sana kwenye elimu ya sayansi, kuwa ni sawa na punda. (Ndani ya **Taurati** na injili **"kama punda waliobeba mizigo."**) Wanasayansi hawa madhalimu ambao hawana elimu ya maadili ya kiislam, hawako katika njia ya haki. Allahu taala hayuko radhi na watu hawa. [Hadithi sharif iliyo katika kitabu cha **Kunuzu dakaik** inasema **(Mbora wenu ni yule aliyejifunza Kur-an Karim kisha nae akawafunza wengine)**. ] Katika kitabu kiitwacho **Mishkat** tunasoma hadithi sharif isemayo **(Kila muislamu mwanamke na mwanamme ni fardhi kwake kujifunza elimu ya dini).** Hii ni amri ya

kujifunza elimu zenye manufaa kwa kutaka radhi za Allahu taala. Kuwafunza elimu watu wasiofaa ni sawa na kumvisha nguruwe mkufu wa dhahabu. [Hadithi sharif iliyoandikwa kwenye karatasi ya kalenda itolewayo na Turkiye Gazetesi ya tarehe 12 Juni 1995 inasema **(Kitakapokaribia kiama wanazuoni wa uhakika watapungua. Kutakuwepo viongozi wa dini wajinga ambao watatoa fatwa kwa kutumia rai zao na kuwapoteza watu kuelekea njia potofu).** ] Na katika hadithi sharif nyengine tunasoma **(Utafika wakati, watu watawakimbia viongozi wa dini kama wanavyoukimbia mzoga wa punda ulio barabarani).** Hii inahabarisha namna ambavyo hali za watu zitakavyoharibika na kuwa mbaya. Elimu ni kitu ambacho Allahu taala amekitukuza. Lakini wale wenye kuiabudu dunia, ambao utotoni hawakupata malezi ya wazee wawili wala hawakupata elimu ya madrasa, utu uzimani nako hawakupata heshima ya kuhudhuria darsa za wanazuoni wa kweli wala kusoma vitabu vyao, basi huwa hawaogopi hatari itokanayo na mapungufu waliyo nayo katika dini wala hawajishughulishi kusoma na kujifunza kutoka katika vitabu vya wanazuoni wa uhakika. Watu hawa fikra zao ziko katika kupata mali na ulwa tu bila ya kujali wanapata kwa njia ya halali au ya haramu. Hawawezi kutafautisha kati ya haki na batili na hawajui thamani ya wanazuoni wa kweli. Kwa mtizamo wao, mawaidha na vitabu vya wanazuoni wa uhakika ni sawa na kuuza manukato kwenye soko la wanyama au kumuuzia kioo kipofu. Ni sawa pia kama kumsomea Abu lahab surat **Taha**, au kumpa muhuni njiani mfuko wenye vito vya thamani au kumuuzia wanja kipofu. Mtu mwenye akili timamu hafanyi mambo haya. Allahu taala anawasema watu hawa wasio na uelewa kuwa **(Hawa ni kama wanyama, bali ni dhalili zaidi ya wanyama)**. Katika hadithi sharif iliosimuliwa na Anas bin Malik inasema **(Mtu yeyote atakaemtukana mwanazuoni bila ya haki, basi Allahu taala atamdhalilisha na kumdogesha mbele ya watu wote. Na yule atakaemuheshimu mwanazuoni, Allahu taala nae atamtukuza na kumpandisha daraja kama mitume).** Katika hadithi sharif nyengine **(Mtu yeyote atakaepandisha sauti yake juu ya sauti ya mwanazuoni, Allahu taala atamdhalilisha duniani na akhera. Na atakapojuta akaleta toba, atasamehewa).** Inafahamika hapa kwamba ni lazima kuwaheshimu wanazuoni wa kweli.

***Umeumbwa kwa tone la maji kumbuka!***
***Si vyema, sawa na wanazuoni kujiweka!***
***Angalia Mustafa anatamka!***
***Heshima kwa mwanazuoni, nami kwangu hufika!***

Fahamu vyema kwamba wanazuoni ndio wanaomuokoa mtu kutoka kwenye upotevu na njia isiyo sawa. Bila ya kuwa na muongozi huwezi kuiona njia sahihi. Hivyo ni lazima kuwatafuta wanazuoni wa kweli wa ahli sunna na vitabu vyao walivyoviandika. Nabiyullahi Musa alayhi salaam, pamoja na daraja la juu la elimu alilokuwa nalo, na kuwa na heshima ya kuwa ni msemeshwa na Allahu taala, lakini bado alifatana na Yusa alayhi salaam ambae alikuwa ni mwanafunzi wa Hidr, ili kupata elimu zaidi. Haya yanatajwa katika Suratul **Kahf**. Aidha pamoja na kwamba Nabiyullahi Musa alayhi salaam alikuwa na uweledi mkubwa wa elimu ya mantiki, alimfata Hidr alayhi salaam ili kupata elimu zaidi. Katika tafsiri ya Buhari ameyaeleza haya kwa urefu. Kwa hivyo ewe ndugu yangu! Kuna jambo la muhimu zaidi kuliko elimu na wanazuoni ambalo ndio unapotezea kwake umri wako wenye thamani?! Je hufahamu kwamba dini yetu imetuamrisha kuithamini elimu, kuwaheshimu wanazuoni na kuwa pamoja na wale walio katika njia ya Allah?! Kwa hivyo usipoteze umri wako katika mambo yasiyo na faida. Katika hadithi sharif tunasoma **(Mwanazuoni mwenye elimu sahihi na anaetekeleza amali zake kufuatana na elimu yake basi ana tafauti ya daraja moja tu baina yake na mitume. Hiyo daraja moja ndio hicho cheo cha utume).** Hivyo ili kuweza kufikia cheo hicho ni lazima kufanya hima katika kutafuta elimu.

***Ewe mwenye furaha ya kutafuta elimu!***
***Usiipitishe bure dakika ya umri wako muhimu!***
***Tambua thamani ya nasiha zangu adhimu!***
***Atapatwa na majuto asiejua yake kima!***

**HIKAYA:** Kadhi Imam Abu Yusuf alikuwa na mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka kumi na tano. Akimpenda sana mtoto wake. Siku moja ghafla tu yule mtoto alikufa. Akawaagiza wanafunzi wake washughulikie maiti ile ya mwanawe kwani yeye alikuwa anahudhuria darsa kwa mwalimu wake na asingependa kukosa kuhudhuria. Baada ya kifo chake Abu Yusuf, kuna watu walimuona ndani ya ndoto akiwa kasimama mbele ya kasri refu sana. Kasri lake lilirefuka sana kwenda juu na kuikaribia Arshi. Alipoulizwa ni la nani kasri lile alijibu kuwa ni lake. Alipoulizwa amelipataje alijibu ni kutokana na mapenzi yake ya elimu na watu wenye kujishughulisha kusoma na kusomesha. Ewe ndugu yangu! Ili uweze kupata utukufu wa akhera na duniani jifunze elimu.

***Ili kuwa na furaha kila wakati***
***Ili kupata heshima kila pahali***
***Jihimize kupata elimu***
***Jihimize kuvaa taji la elimu***

**HIKAYA:** Mwalimu wa muandishi wa kitabu cha Riyadhu nasihina, mwanawe mkubwa wa kiume alikuwa ni mcha mungu sana. Wakati akikata roho huyo mtoto, baba yake alikuwa pembeni ya kitanda chake. Alipokwisha kata roho alimfunika. Kwanza akaenda zake darasani na kusomesha juzuu moja katika somo la hadithi kisha akarudi na kuanza kushughulikia mambo ya mazishi. Hapo zilisikilika sauti zikitoka kwenye milima iliyouzunguka mji zikisema (Ahadi ya mwanangu imefika na amekufa. Kwa vile hili ni jambo linalotokana na maamuzi yake Allahu taala basi mimi nimeridhiya. Hakuna jengine linaloweza kufanyika. Hivyo ndivyo zilivyo amri na kadhaa za Allahu taala). Katika hadithi sharif iliyosimuliwa na Hassan bin Atiyya "radhiyallahu anhu" tunasoma **(Asiehuzunika kwa kifo cha mwanazuoni basi huyo ni mnafiki. Hakuna msiba mkubwa kwa watu kuliko kifo cha mwanazuoni. Mwanazuoni anapokufa mbingu na vilivyomo ndani yake huomboleza kwa muda wa siku sabini).** Mwanazuoni wa kweli anapokufa basi huwa pameingia pengo katika dini, pengo ambalo halizibiki hadi siku ya kiama. Katika hadithi sharif nyengine tunasoma **(Binadamu ima awe mwalimu, au mtafuta elimu au mwenye kuwapenda hawa. Asie katika watatu hawa basi ni sawa sawa na nzi alie katika zizi la wanyama).** Kwa hivyo tujitahidi tusiwe katika hili kundi la nne.

Mshairi anasema

***Kitachomuokoa binadamu na Jahannam ni elimu***
***Mali asiyoweza kukuibia mtu ni elimu***
***Usitake kitu chengine zaidi ya elimu***
***Kutakachokupa yote uyatakayo duniani na akhera ni elimu*.**

Katika fatwa za Baldaji Imam Sadru shahid (Sadru Shahid Husamadyn Umar aliuwawa shahidi mwaka 536 Hijria huko Semerkand) anasema **(Iwapo mtu atamdhihaki mwanazuoni, basi ndoa yake huvunjika hapo hapo).** Yeyote atakaemwita mwanazuoni kwa majina kama mjinga, jahil, nguruwe au punda, mtu huyo atachapwa viboko. Na kama atamwita hivyo kwa nia ya kumtukana basi ndoa yake huwa imevunjika. Imam Muhammad naye anaongeza kwa kusema iwapo mtu atasema neno lenye kupelekea ukafiri basi ndoa yake huvunjika hapo hapo. Mwenye kuitukana elimu na wanazuoni huwa kafiri. Tunamuomba Allahu taala atupe sote elimu yenye faida na atuweke mbali na elimu isiyo na faida. Elimu yenye faida ni ile aliyokuja nayo mtume wa Allah swallallahu alayhi wasallam. Elimu hii inapatikana katika vitabu vya wanazuoni wa ahlu sunna.

## KUJIDHALILISHA

13. Ni jambo la kumi na tatu katika tabia mbaya. Tawadhuu inapopita mipaka huwa ni **kujidhalilisha** yenye maana ya kujifanya duni. Kujidhalilisha ni haramu. Kama zilivyo haramu nyengine inaweza nayo ikajuzu kufanywa katika hali ya **dharura.** Miongoni mwa dharura ni kama kuokoa dini, roho, mali na heshima yake mtu dhidi ya dhalim. Kutafuta njia nyepesi ya kutatua tatizo pale penye shinikizo na mashaka ni jambo ambalo linajuzu.

Kujidhalilisha ni moja kati ya tabia mbaya. Mfano wa kujidhalilisha ni kama pale mwanazuoni anapojiwa na mshona viatu, kisha mwanazuoni akamnyanyukia huyo mshona viatu na kumuweka katika sehemu yake anayokaa, isitoshe, wakati wa kuondoka akamsindikiza hadi mlangoni na kumuekea sawa viatu vyake alivyovaa. Kama angelisimama kwa kumpokea tu kisha akakaa, naye akamuonesha pahala pa kukaa, kisha akamuuliza hali kwa vizuri, kama ana maswala yake akayajibu kwa uso wa bashasha, kama ni mualiko akaupokea mwaliko wake, kama ni matatizo akamuonesha njia ya utatuzi, basi hapo atakuwa amefanya tawadhuu. Katika Hadithi sharif **(Mwenye kumsaidia nduguye katika dini kwa tatizo lake, analipwa thawabu sawa na za hija** [ya nafila] **na umra)**. Hadhrat Hassan “radhiyallahu taala anhu” alimuomba Thabit Binany “rahimahullahu taala” kumtatulia shida yake. Thabit alipomjibu kwamba nitakufanyia muda mwengine kwani sasa niko kwenye itikaf msikitini alimwambia “Wewe hujui kuwa kumtatulia nduguyo muislamu shida yake kunakupa malipo zaidi ya kutekeleza [nafila] hija na umra?” Hadithi hii inatumika kuwa ni msingi wa kueleza kuwa ni jambo lenye ujira kwa watu wenye vyeo kuwasaidia watu wenye mahitaji na kwa walimu kuwasaidia wanafunzi wao kwa hali na mali. Mtu ambae anamiliki mlo wake wa siku moja basi kuomba inakuwa ni kujidhalilisha na ni haramu kwake. Mtu ambae anamiliki mlo wake wa siku moja, akaomba kwa ajili ya mtu mwengine ambae hamiliki mlo wa siku moja au kumuombea mwenye deni basi hilo halitokuwa kujidhalilisha. Kujifanya kutoa zawadi ndogo ili uweze kupata zawadi kubwa zaidi nayo pia ni kujidhalilisha. Zawadi ya aina hiyo imekatazwa katika Kur-an Karim. Kilicho bora ni kutoa zaidi ya kile ulichopokea. Ila haijuzu kutoa kwa lengo la kuwa upate kikubwa zaidi. Kwenda katika karamu ambayo hukualikwa pia ni kujidhalilisha. Hadithi sharif inasema **(Kutokwenda katika mualiko ni dhambi. Kwenda katika mualiko bila kualikwa ni wizi).** Ni wajibu kwenda katika mualiko wa harusi iwapo hakuna mambo ya haramu yanayofanywa. Ni sunna kuhudhuria aina nyengine za mialiko mtu

anapoalikwa. Haijuzu kwenda katika mialiko inayofanywa kwa nia ya riya, kujionesha na kutafuta fahari. Kufanya urafiki na wakuu wa nchi, matajiri na mahakimu kwa lengo la kupata manufaa nako ni kujidhalilisha isipokuwa katika hali ya dharura kama tulivyotaja kabla. Watu kama hawa unapokutana nao kuwasalimia kwa kuwasujudia au kuwapigia magoti pia ni kujidhalilisha. Kufanya hivyo ni dhambi kubwa. Na kama atafanya hivyo kwa nia ya kuabudu basi hiyo itakuwa ni kufuru. Hili ni kujifananisha na salam za mayahudi. (**Fakir** maana yake ni mtu muhitaji. Katika Uislam huyu ni mtu ambae anaweza kukidhi mahitaji yake ya lazima lakini hana ziada hata ya kuweza kuchinja mbuzi mmoja). Ufakiri aliouomba mtume kwa Allahu taala na akausifu haukuwa ufakiri wa mali bali ulikuwa ni ule ufahamu aliokuwa nao mtu ndani ya akili yake kwamba yeye ni muhitaji kwa Allah kwa kila jambo na kila wakati. Katika kitabu kiitwacho **Durrul maarif** kilichoandikwa na Abdalla Dahalawy "rahimahullahu taala" anasema (Katika tasawuf, fakiri ni yule ambae hana matashi mengine zaidi ya kumridhisha Allahu taala). Mtu kama huyu hata anapokosa mlo wake wa siku hufanya subira na kukinai. Huyaridhia matendo na maamuzi ya Allahu taala. Anafanya kazi kutafuta riziki, kwa kuwa Allahu taala ametuamrisha tufanye hivyo. Kazi zake hazimzuii kufanya ibada wala hazimfanyishi yale yaliyo haramu. Anatimiza masharti ya Uislam katika uchumaji wake na katika matumizi yake. Kwa mtu kama huyu, utajiri na umaskini vyote vina faida kwake. Vyote vinampelekea kupata furaha ya duniani na akhera. Yule ambaye mwenye kuifata nafsi na akawa hawezi kufanya subira na kukinai, huyo haridhii kadhaa na kadar ya Allahu taala. Akiwa fakiri atalalamika kuwa kapewa kichache na akiwa tajiri pia hatotosheka atataka zaidi. Kile alichokichuma atakitumia kwa njia za haramu. Ufakiri na utajiri huwa ni sababu ya matatizo kwake hapa duniani na huko akhera.

Kufanya shughuli za viwandani, biashara, kazi halali za mshahara kama kuchunga wanyama, kutunza bustani, kazi za kwenye ujenzi na uwashi na shughuli za uchukuzi na upagazi si katika mambo ya kujidhalilisha. Mtume "swallallahu alayhi wasallam" na mawalii "rahimahumullahu taala" walifanya kazi hizo. Ni fardhi mtu kufanya kazi kwa ajili ya kujikimu yeye mwenyewe na familia yake. Ni halali mtu kufanya kazi ili apate chumo zaidi kwa nia ya kuwasaidia wengine. Idrisa alayhi salaam alikuwa ni fundi charahani. Daud alayhi salaam alikuwa ni mfua vyuma. Ibrahim alayhi salaam akijishughulisha na kilimo na kuuza vitambaa. Mtu wa mwanzo alietengeneza vitambaa ni Adam alayhi salaam. [Maadui wa dini wameandika kuwa watu wa

mwanzo walivaa majani na kuishi kwenye mapango. Maandishi hayo hayana ushahidi.] Isa alayhi salaam alikuwa ni mshona viatu. Nouh alayhi salaam alikuwa ni fundi seremala. Saleh alayhi salaam alikuwa fundi wa mikoba. Mitume "alayhimusalawatu wataslimat", wengi wao walifanya kazi ya kuchunga wanyama. Katika hadithi sharif tunasoma kuwa **(Kwenda kununua mwenyewe mahitaji ya nyumbani kwako, kisha ukayabeba na kuyapeleka ni dalili ya kutokuwa na kiburi).** Mtume "swallalllahu taala alayhi wasallama" alifanya kazi ya kuuza na kununua bidhaa. Alifanya kazi ya kununua zaidi. Alifanya kazi kwa mshahara, pia aliwahi kufanyisha kazi watu wengine. Aliingia katika mikataba ya kazi za ushirika na ifananayo na hayo katika zama zake. Alifanya kazi ya uwakala pia aliwapa kazi mawakala wengine. Alitoa na kupokea zawadi. Alikopa pesa na alichukua mzigo kwa mkopo. Alianzisha wakfu. Hakuwahi kumkasirikia mtu kwa mambo ya dunia wala hakuwahi kufanya jambo la kumkasirisha mwengine. Aliwahi kuapa na kuwaapisha wengine. Alipoapa alitekeleza na pale asipotekeleza alitoa kafara. Akifanya utani ila matani yake yalikuwa ni ya mambo ya ukweli yenye faida. Kuona haya na kukwepa kuyafanya hayo tuliyoyataja hapo juu ni dalili ya kiburi. Watu wengi hukosea hapa kwa kushindwa kutafautisha tawadhuu na kujidhalilisha. Katika hili nafsi imewahadaa watu wengi.

## KUJIONA

14. Hii ni tabia ya kumi na nne iliyo ovu. Hii ni kuyapenda matendo yako mazuri na ibada zako na kujifaharisha kwa hayo. Kuijua thamani ya matendo mazuri na ibada unazotenda na kuwa na woga wa kuzipoteza haiwi kujiona. Kukumbuka kwamba hizo ni neema ambazo Allahu taala amekupa ukafurahi kwa hilo pia sio kujiona. Kujiona ni hali ya kutokukumbuka kuwa hayo uliyonayo ni neema itokayo kwa Allahu taala na ukadhani kuwa yanatokana na ujanja wako binafsi hivyo ukafurahia kwa hilo na kujifakharisha. Kinyume cha kujiona ni **Minnat** yenye maana kwamba mtu anafahamu kuwa neema ni ihsan itokayo kwa Allahu taala na wala haitokani na nguvu na ujanja wake binafsi. Ni fardhi kufikiri kama hivyo wakati mtu yuko kwenye hatari ya kujiona. Na iwapo hayupo katika hatari hiyo basi ni mubaha kufikiri hivyo. Sababu kuu zenye kumpelekea mtu kwenye kujiona ni ujinga na kujisahau. Ili kuweza kuokoka na kujiona inalazimu mtu kukumbuka kwamba mambo yote yanatokana na matakwa ya uumbaji wake Allahu taala na kwamba akili, elimu, utendaji ibada, mali, cheo na neema zote kubwa zenye mfano wa haya ni ihsan itokayo kwa Allahu taala. **Neema** ni vile vitu vyenye faida ambavyo humpa ladha mtu kuwa

navyo. Neema zote hutolewa na Allahu taala wala hakuna mwengine anaeweza kuziumba na kuzitoa. Katika vita vya Hunayn baadhi ya masahaba “ridhwanullahi taala alayhim ajmaina” walipoona ukubwa wa jeshi lao walisema kuwa hawawezi kushindwa katika vita hivyo. Mtume “swallallahu alayhi wasallam” aliposikia kauli hiyo hakuipenda na alihuzunika. Kutokana na hilo mwanzoni mwa vita hivyo Allahu taala hakushusha nusra yake na waislam walianza kwa kushindwa. Hatimae Allahu taala alishusha huruma zake na ndipo waislam wakashinda. Wakati Daud alayhi salam alipoomba dua kwa kusema (Ewe mola wangu! miongoni mwa watoto wangu kuna wale ambao hakuna usiku uliopita bila ya wao kusali au mchana bila ya wao kufunga) Allahu taala alimjibu **(Lau kama nisingetaka mimi, na kama nisingewapa nguvu, basi wasingeweza kufanya lolote kati ya hayo).** Usemaji huu wa Daud haukuwa sahihi katika haki yake Allahu taala, na inatajwa kuwa ni sababu ya yeye kufikwa na yale maafa yaliyotajwa katika vitabu vya historia. Mambo yanayompelekea mtu kufanya kiburi tumeshayataja kabla ambayo ni hayo pia yanayompelekea mtu kujiona. Kuzishukuru neema za Allahu taala pia ni katika neema kubwa.

Madhara na matatizo ya kujiona ni mengi. Kunapelekea kwenye kiburi. Kunapelekea kusahau dhambi. Dhambi nazo zinaufanya moyo uingie kiza. Mwenye kufikiri dhambi zake basi hazitukuzi ibada zake na hufahamu kwamba kuweza kufanya ibada ni ihsan itokayo kwa Allahu taala. Mtu mwenye kujiona husahau ghadhabu na adhabu za Allahu taala. Huwa hamshauri mtu wala kuuliza, hivyo hafaidiki na busara za watu wengine.

Katika hadithi sharif tunasoma **(Mambo matatu yanampelekea mtu kwenye maangamizi. Ubakhili, matashi ya nafsi na kujiona).** Bakhili huzuilika kutoa haki na wajibu alionao kwa Allah na viumbe wenziwe kutokana na ubakhili wake. Mwenye kufuata hawaya za nafsi na yule mwenye kujiona bila shaka hilaki na maangamizi vitawakumba. Imam Muhammad Ghazali “rahimahullah taala” anasema (Maovu yote yanaongozwa na mambo matatu: husda, riya na kujiona. Pambana kuusafisha moyo wako na mambo haya). Mwenye kujiona hutumia sana neno mimi. Kwenye mijumuiko hupenda kuwa safu za mbele na hupenda rai yake ifatwe.

Katika Hadithi sharif tunasoma **(Msipofanya dhambi, nakhofia mnaweza kuanguka kwenye dhambi kubwa zaidi, nayo ni kujiona).** Mwenye kutenda dhambi nafsi yake hunyongeka hivyo anaweza kuleta toba. Mwenye kujiona hughururika na elimu yake na amali yake. Hujikweza na huwa mgumu kuleta toba. Allahu taala anazipenda zaidi

sauti za manunguniko za waliotenda madhambi kuliko sauti za majigambo za watendao mema. Lililo ovu zaidi kwa mwenye kujiona ni kupendezwa na makosa yake na hawaya za nafsi yake. Huwa mwenye kufuata yale yalio ndani ya nafsi yake na hapokei nasaha za watu wengine. Watu wengine wote anawadhania ni wajinga hali ya kuwa yeye ndie mjinga zaidi. Watu wa bid'a na wale wapinga madhehebu hivi ndivyo walivyo. Itikadi zao na amali zao mbovu wanazidhani kuwa ndio sahihi na kushikamana nazo kwa nguvu. Dawa ya watu wenye kujiona kama hawa ni ngumu kupatikana. Masahaba "ridhwanullahi alayhim" walimuuliza mtume wa Allah maana ya aya ya 108 ya suratul maida isemayo **(Zishughulikieni nafsi zenu. Hatokudhuruni aliyepotea endapo wenyewe mtakuwa katika uongofu).** Katika kuwajibu mtume wa Allah aliwaambia **(Zielezeni amri za Uislam na makatazo yake. Na yule ambae atajiona na kutokusikilizeni basi nyinyi shughulikeni na kuziongoa nafsi zenu).** Dawa ya kujiona imetayarishwa na maulamaa wa ahli sunna. Lakini hawa wagonjwa wa maradhi haya kwa vile hawajijui kuwa wanalo hili gonjwa na wanajidhani kuwa wao ni wazima, basi huwa hawazikubali nasaha na miongozo ya hao matabibu hivyo wanaendelea kuwemo ndani ya hilo janga. Uhakika ni kwamba hawa wanazuoni wanatoa dawah hii kama walivyoipokea kutoka kwa Mtume "swallallahu alayhi wasallama" bila kubadilika wala kuharibika. Wajinga na majahil wanandhani kwamba dawah hii wameitengeneza wenyewe hao wanazuoni. Hivyo hufanya majivuno na kujidhani kwamba wao ndio wako kwenye njia ya haki.

## HASAD

15. Hili ni gonjwa la kumi na tano. Hasad ni kupata wivu usiomithilika wa kutaka mja mwenzio aondokewe na neema aliyopewa na Allahu taala. Kutaka mwenzio aondokewe na kitu kisicho na faida au chenye madhara hiyo si hasad bali ni Jitihada. Pindi ikiwa kiongozi wa dini anaitumia elimu yake kwa kupata mali, cheo na kufanyia maasi, basi kutamani elimu hiyo imuondokee sio hasad. Ikiwa mtu anaitumia mali yake kwa mambo ya haramu, kwa kuudhuru Uislam na kwa kueneza bid'a na maasi, basi kutamani mtu kama huyo aondokewe na mali hiyo pia si hasad, bali ni jitihada katika dini. Ikiwa mtu atahisi hasad ndani ya moyo hali ya kwamba hali hiyo ya hasad haipendi na akawa anahuzunika inampomjia moyoni, basi mtu huyo huwa hapati dhambi. Fikra au kumbukumbu ipitayo moyoni haihisabiwi kuwa ni dhambi. Mtu kupitiwa na kumbukumbu moyoni ni jambo ambalo hawezi kulizuia. Iwapo mtu amejiwa na hasad moyoni na akawa hahuzuniki au kwa makusudi akafanya hasad basi hapo

atapata dhambi na hilo ni jambo la haram. Na ikiwa hasad hii akaiainisha kwa maneno au vitendo basi dhambi zake huzidi. Katika hadithi sharif tunasoma **(Binadamu hatookoka na vitu vitatu. Dhana mbaya, kuamini ishara mbaya na hasad. Unapopatwa na dhana mbaya, usifanye mambo chini ya dhana hiyo. Ukikumbwa na imani ya dalili mbaya, fanya jambo lako kwa kumtegemea Allah. Na unapokumbwa na hasad kwa mtu fulani basi usimdhuru mtu huyo).** Katika hadithi sharif hii tunafahamu kwamba moyo kukumbwa na hasad siyo haram bali kuiridhia kuwepo moyoni mwako na kuiendeleza ndiyo haramu. Katika kitabu kiitwacho **Hadika** imeandikwa: Fikra inayokuja moyoni inapita katika daraja tano. Daraja ya kwanza ni kwamba fikra haikai moyoni bali hutolewa hapo hapo. Hii huitwa Hajiz. Katika daraja ya pili fikra huendelea kuwepo moyoni kwa muda. Hii huitwa Hatira. Katika daraja la tatu moyo huwa katika kujisaili kati ya kulitenda au kutokulitenda lile inalolifikiri. Hii huitwa Hadithu nafsi. Daraja la nne ni moyo kuchagua kulifanya lile inalolifikiri. Hii huitwa Hamm. Hatua ya tano ni kupata nguvu lile chaguo na kurasimishwa kuwa uamuzi. Hii huitwa Azm na Jazm. Katika daraja la kwanza la pilli na la tatu malaika hawaandiki thawabu wala dhambi. Inapofikia daraja la nne (hamm) likiwa ni tendo zuri basi tayari thawabu huandikwa. Ikiwa ni tendo baya katika daraja hii ya nne kama ataliacha basi huandikiwa thawabu na kama ataliendeleza akifika daraja la tano (Azm) ataandikiwa dhambi, lakini kama kitendo hakikutendeka basi atasamehewa. Hadithi sharif inasema **(Uovu unaopita moyoni usiposemwa au kufanywa husamehewa).** Wakati mtu anapopitiwa moyoni na itikadi ambayo ni kufr au bid'a, kama atahuzunika na kuitoa moyoni hapo hapo, kwa fikra hii ya muda mfupi hawi kafiri. Iwapo mtu ataamua kuwa baada ya miaka kadhaa atakuwa kafiri au akaweka sharti kwamba likitokea jambo fulani atakuwa kafiri, basi mtu huyo, muda huo huo alipopitisha maamuzi hayo tayari amekuwa kafiri. Hali ni sawa na hiyo kwa mwanamke alieamua kwamba baada ya miaka kadhaa ataolewa na mwanamme kafiri.

[Dhambi za kutenda jambo la haramu ni kubwa zaidi kuliko zile za kupitisha uamuzi wa kufanya hivyo. **Haram** ni yale mambo ambayo Allahu taala ameyakataza na dhambi ni ule ujira anaoandikiwa aliefanya haram. Kufanya dhambi maana yake ni kufanya tendo ambalo litastahiki kwao kupewa adhabu, yani kutenda haramu. **Thawabu** ni ule ujira wa akhera watakaopewa waliofanya mema. Allahu taala ameahidi kuwalipa ujira mzuri wale wafanyao ibada na mambo mema. Si wajibu wala si lazima kwa Allahu taala kuwapa ujira

huko akhera wale waliofanya ibada na kutenda mazuri. Lakini Allahu taala kutokana na huruma zake, ameahidi kutoa malipo hayo. Allahu taala haendi kinyume na ahadi alizozitoa na kwa uhakika huzitekeleza.]

Hadithi sharif inasema **(Binaadamu humpitikia katika moyo kufanya haram ila asipofanya kwa kumuogopa Allah basi haandikiwi dhambi. Atakapolifanya lile la haram ndipo huandikiwa dhambi).**

Ni haram mtu kutia nia kuwa kafiri au kuwa mtu wa bid'a. Muda huo huo tayari anakuwa hivyo alivyonuia kwa sababu mambo mawili haya yaliyo maovu nia yake pia ni haram. Fikra ya kufanya haram ni ovu kwa sababu inapelekea kwenye uovu. Nia yenyewe sio uovu ila ikitekelezwa ndio uovu unapatikana. Iwapo nia haitotekelezwa uharamu wake na dhambi yake huondoshwa kutokana na huruma zake na rehema zake Allahu taala ambazo amezitoa hasa kwa umati wa Muhammad „swallallahu alayhi wasallama".

Mja kutamani apate kheri kama aliyopata mtu fulani, bila ya kutaka imuondokee huyo mwenziwe basi hii siyo hasad. Huo ni **wigo**. Hili ni jambo zuri. Ni wajibu kumuangalia na kumuiga mtu ambaye anajihimiza kufanya mambo mema na kuacha yaliyo mabaya. Ni makruh kufanya wigo katika mambo ya kidunia.

Hadithi sharif inasema (**Allahu taala ana ghera kwa mja wake. Mja muumini nae ana ghera kwa mja mwenziwe muumini).** Allahu taala amekataza zina kutokana na ghera yake. Allahu taala anasema **(Enyi wana wa Adam! Nimekuumbeni nyinyi kwa ajili yangu na yote yaliobaki nimeyaumba kwa ajili yenu. Hivyo hayo yasikughafilisheni mkanisahau mimi muumba wenu).** Katika Hadithi qudsy nyengine **(Wewe nimekuumba kwa ajili yangu. Usipoteze muda kwa mambo mengine. Mimi ni dhamana wa riziki yako. Usijipe huzuni).** Wakati Yusuf alayhi salaam aliposema "Utakapokwenda kwa mfalme huko na mimi jina langu litaje", tendo hilo liliigusa ghera ya mola na matokeo ikawa ni yeye kuendelea kukaa jela kwa miaka kadhaa. Ibrahim alipoonesha furaha kubwa kwa kuzaliwa Ismail basi naye aliigusa ghera ya Allahu taala matokeo yakawa ni kutakiwa amchinie huyo mwanae. Kuna mifano kadhaa kwa Allahu taala kuonesha ghera kwa baadhi ya mawalii wake aliowapenda. **Ghera** ni kule kukataa kuwa asipewe mtu mwengine jambo ambalo ni haki yako wewe kupewa. Allahu taala kufanya ghera maana yake ni yeye kutoridhia mja wake kufanya matendo maovu. Wadhifa wa mja sio kufanya alitakalo bali ni kuwa mtumwa wa Allahu taala, nayo ni kutekeleza aliyoamrishwa na kuyaacha aliyokatazwa. Kufanya kila analolitaka ni haki mahsusi ya

Allahu taala pekee. Kwa hivyo mja anapotaka nae awe anafanya kila analolitaka, huo unakuwa ni uvamizi wa haki ya Allahu taala. Wakati muumini anapofanya maasi basi inafaa yeye mwenyewe ajishangae. Aonekane kuwa amefadhaika, mapigo ya moyo yamezidi na pumzi zimempaa. Moyo wa muumini ni maskani ya Allahu taala na sehemu ya tabia njema. Kwa hivyo kuyapa nafasi maovu katika moyo ni kuchanganya yale mazuri yaliyomo na huo uovu. Inatakiwa moyo usiyaridhie haya na uyakatae kwa jitihada yote. Raisi wa maansari Sa’d bin Ubada “radhiyallahu taala anhu” aliuliza “Ewe mtume wa Allah “swallallahu alayhi wasallama”! Kama nitamfumania mke wangu na mwanamme juu ya kitanda lakini ikawa sina mashahidi wanne, je siwezi kumuua?” Mtume “swallallahu alayhi wasallama” akamjibu **“Ndiyo. Huwezi kumuua.”** Sa’d akasema “Hata kama mashahidi wanne ni lazima lakini mimi nahisi moyo wangu hautochukua hilo. Hapo hapo nitamuua” Mtume “swallallahu alayhi wasallama" akasema **“Je mmemsikia raisi wenu. Ni mwenye wivu sana. Mimi nina wivu zaidi ya yeye. Allahu taala ana wivu zaidi yangu.”** Hii ina maana ya kwamba hairuhusiwi kuwa na wivu kama huo. Mimi pamoja ya kuwa nina wivu zaidi yake, lakini sitoki nje ya mipaka ya Uislam. Pamoja na kwamba Allahu taala ana wivu zaidi lakini dhambi hiyo ya zinaa haitolei hukumu hapo hapo, ndicho alichotaka kukieleza mtume wa Allah. Mtume “swallallahu alayhi wasallama” anatoa ishara kuwa kitendo cha Sa’d kutaka kutoa adhabu hapo hapo, sio sahihi. Inafaa kwa kila muislamu kutoa adhabu ya kuadhiri wakati analiona lile kosa linafanyika. Haitosihi kutoa adhabu hiyo baada ya kwamba tendo limeisha na ni mahakama ndio inayoweza kutoa adhabu wakati huo. Mwenye kuona wazinifu wakitenda tendo akaamua kuwaua analazimika kutoa mashahidi wanne mahakamani na wala hakitofaa kiapo pekee. Na akishindwa kuleta mashahidi basi atahukumiwa yeye kwa mauaji.

Haifai kwa mwanamke kumuonea wivu mke mwenziwe. Siku moja mtume “swallallahu alayhi wasallama” alitoka chumbani kwa bibi Aisha. Bibi Aisha “radhiyallahu anha” akadhania kuwa amekwenda chumbani kwa mke mwengine hivyo akaingia wivu. Mtume “swallallahu alayhi wasallam” aliporudi akamkuta amenuna na kumuuliza **“umeingia wivu”.** Bibi Aisha akajibu “Mnyonge kama mimi kwa vipi nisiingie wivu kwa mtu kama wewe ambae ndie mbora na mwenye huruma wa viumbe wote.” Mtume “swallallahu alayhi wasallama” akamwambia **“Umekumbwa na wasi wasi wa shetani”.** Mama Aisha akauliza “Kwani nami nina shetani pembeni yangu, ewe

mjumbe wa Allah?" na mtume akamjibu **"Ndio, unae".** Mama Aisha akauliza tena "Ewe mjumbe wa Allah, na wewe pembeni yako pia unae shetani?" Akajibu mtume wa Allah **(Ndiyo, nami ubavuni kwangu ninae ila Allahu taala amenikinga mimi na wasi wasi wake)** kwa maana ya kwamba shetani wake amesilimu na anamkumbusha mambo mema. Katika hadithi sharif tunasoma **(Allahu taala amenipa mimi neema mbili ambazo hajampa mtu yeyote. Shetani wangu alikuwa kafiri naye akamfanya muislamu. Amewafanya wake zangu wote wawe ni wasaidizi kwangu katika kuueneza Uislam).** Shetani wa Adam alayhi salaam alikuwa kafiri. Mkewe bibi Hawa alidanganywa na kiapo cha shetani wakiwa peponi na kumsababisha Adam afanye makosa.

Ghera ya binaadamu kwa mola wao ni kule kukataa kwao kutenda maasi.

Kinyume cha hasad ni **Nasaha** nayo ni kutaka neema aliyopewa mja aendelee kuwa nayo na imletee faida duniani na akhera. Nasaha ni wajibu kwa kila muislamu. Katika hadithi sharif tunasoma **(Mwenye kusababisha kutokea kwa jambo la kheri, anapata ujira sawa na mwenye kulitenda)** na katika hadithi sharif nyengine **(Hajaamini bado yule asiemtakia nduguye muislamu yale mazuri ambayo yeye anayataka)** na hadithi sharif nyengine **(Msingi wa dini ni kunasihiana).** Kunasihiana maana yake ni kuelezana kuwa Allahu taala yupo nae ni mmoja tu, na kwamba yeye ana sifa zote nzuri na za ukamilifu, na kwamba hana sifa za aibu na mapungufu, na kwamba ni lazima kumuabudu kwa ikhlasi, na kwamba ni lazima kujitahidi kupata ridhaa zake kwa kadiri ya uwezo wake mtu, na kwamba haifai kumuasi, na kwamba inatakiwa kuwapenda mawalii wake na kuwachukia maadui zake, na kwamba inafaa kuwapenda wanaomtii na kuwachukia wanaomuasi, na kwamba inatakiwa kuziheshimu neema zake na kuzishukuru, na kwamba yeye ni mwenye huruma na rehema kwa viumbe vyote, na kwamba haifai kumtaja kwa sifa ambazo hana. Kushukuru maana yake ni kuzitumia neema ulizopewa na Allahu taala katika njia ambayo mola mtoaji anairidhia. Kunasihi juu ya Kur-an Karim maana yake ni kuamini yale yaliyotajwa ndani ya Kur-an Karim, kutekeleza yale yaliyoamrishwa, kutokutoa tafsiri isiyo sahihi kwa kutumia maoni binafsi, kujitahidi kuisoma sana na kwa usahihi, kuwajusa watu kwamba haisihi kuikamata bila ya udhu. Kunasihi juu ya mtume "swallallahu alayhi wasallama" ni kueleza kwamba ni wajibu kuyaamini yale yote aliyokuja nayo Muhammad "swallallahu alayhi wasallama", kumuheshimu yeye na jina lake, kutekeleza na kueneza

sunna zake, kujipamba na sifa zake njema, kuwapenda jamaa zake, masahaba wake na umma wake. Kunasihiana juu ya dola ni kuwanasihi wengine kwamba ni lazima kuwasaidia viongozi ambao wanamheshimu muumba na kuihifadhi dini yake na wenye kutoa uhuru kwa watu kutekeleza dini yao. Ni kuwanasihi viongozi juu ya kuwa juu ya njia sahihi na ya ukweli na kutunza haki za waislam. Kuwanasihi wananchi kutokupingana na viongozi na kutokuvunja sharia. Na kuwaombea dua viongozi ili waweze kuuhudumia Uislam na watu wote kwa jumla. Kushirikiana nao kwa hali na mali wakati wa mapambano ya jihad dhidi ya makafiri na kuwaombea dua kama uko mbali. Na kulipa zaka na kodi. Na kutokutumia silaha kwa kufanya mauaji. Na kuwanasihi viongozi kwa upole bila kuonesha upinzani hata kama wanachofanya ni kula haki na kukandamiza na kutokuwasababisha wakaacha njia ya haki na kutenda uovu zaidi. Ni kuwaeleza watu wote kwamba ni wajibu kuwatii wakuu wa nchi. Ni kuwaeleza watu wote kwamba ni lazima kufuata sharia za dini na kusoma vitabu vya sharia na maadili vilivyoandikwa na wanazuoni wa ahli sunna “rahmatullahu taala alayhim ajmaina”. Kutoa nasaha kwa watu wote ni kuwanasihi kutekeleza yale yote yenye faida nao duniani na akhera na kujiepusha na yale yenye dhara hapa duniani na akhera. Kuwanasihi kutosababisha madhara kwa mtu yeyote na kutokuwafunza watu yale usioyajua na kuwasitiri aibu zao. Kuwataka kwa upole kutekeleza yale yote yaliyo lazimu na kuyaacha yale yaliyokatazwa. Kuwataka kuwa na huruma kwa wadogo na heshima kwa wakubwa na kuwatendea watu yale ambayo wao wanapenda kutendewa na kuacha kuwatendea yale ambayo wao hawapendi kutendewa. Na kuwataka watu wasaidiane kwa hali na mali.

Katika hadithi sharif mtume “swallallahu alayhi wasallama” anasema **(Wale wasiowasaidia waislamu, na wale wasiofanya kazi kwa ajili ya maslahi na mazuri ya waislam basi huwa si miongoni mwao. Wale wasiotoa nasaha juu ya Allah, Kur-an Karim, mtume wa Allah, mkuu wa nchi na waislam wote kwa ujumla basi si mmoja wao).**

Wivu huondoa malipo ya ibada. Anasema mtume “swallallahu alayhi wasallama” katika hadithi sharif **(Tahadharini na wivu. Wivu unaangamiza mema ya mtu kama moto unavyoangamiza kuni).** Mtu mwenye wivu atamsengenya yule amuoneaye wivu. Atamdhuru kwenye mali yake na nafsi yake. Hivyo siku ya kiama, thawabu zake zitachukuliwa na kupewa yule mtu aliemdhuru, ili kumlipa kwa madhara yaliyompata. Wakati mtu anapoona neema zinamfika mtu

anaemuonea wivu basi hupata mashaka ya moyo na hukosa usingizi. Watu wafanyao mema wanalipwa mara kumi ya ujira ila kwa mtu mwenye wivu huangamiza tisa kati ya hayo na kubakiwa na moja tu. Hakuna dhambi lolote ambalo inaangamiza malipo ya mema yote yaliyotendwa isipokuwa ukafiri. Kutenda mambo ya haramu kwa kuyachukulia wepesi au kufanya matendo yenye kuritadisha na kumfanya mtu awe kafiri, kutaangamiza malipo yote aliyopewa mja kutokana na amali zake. Mtume “swallallahu alayhi wasallama” anasema katika hadithi sharif **(Nyinyi waislam mmeambukizwa maradhi mawili makubwa kutoka kwa umma zilizopita. Wivu na kunyoa. Wakati ninaposema kunyoa sikusudii kunyoa nywele au vichwa vyao. Ninakusudia ni kuinyoa dini kwa kuing'oa kwenye mizizi na kuitokomeza yote kwa ujumla wake. Ninakuapieni kwamba yeyote asie na imani hatoingia peponi. Ili muwe na imani ni lazima mpendane. Na ili muweze kupendana lazima msalimiane mara kwa mara).**

[Hadithi sharif hii inatuonesha umuhimu wa kusalimiana na kutuamrisha kufanya hivyo. Wakati waislam wawili wanapokutana ni sunna mmoja wao kusema **‘Assalamu alaykum’** na ni wajibu kwa yule aliesalimiwa kujibu kwa kusema **‘wa alaykum salam.’** Haijuzu kusalimiana kwa kutumia maamkizi yanayotumika na makafiri au kwa kutumia mkono, mwili au ishara nyengine tu. Iwapo patakuwa na masafa baina ya waislam wawili, basi itafaa kwao kuamkiana kwa kupeana salam au kwa kupungiana mkono kwa kunyanyua mkono wa kulia hadi kufikia usawa wa nyusi za macho. Wakati unasalimiana na makafiri itafaa kusalimiana nao kwa maamkizi yao ili kuepusha fitna. Kuanzisha fitna ni haram. Kuepusha fitna kwa kufuata maelekezo ya hapo juu yanayohusu namna ya kumsalimia kafiri kuna ujira mkubwa.]

Imetajwa katika hadithi sharif kwamba **(Muislamu hupata mazuri lakini anapokumbwa na wivu yale mazuri yote huhama).** Na katika hadithi nyengine Mtume wa Allah anasema **(Wenye wivu, wabeba maneno, na wafanyao ukuhani hawako na mimi).** Wabeba maneno ni wale watu ambao kwa makusudi hueneza maneno ya fitna baina ya waislam kwa lengo la kuwagombanisha. [Kufanya ukuhani ni kuagua yasiyojulikana.] Hatutakiwi tuwaamini wapiga ramli wanaojaribu kutoa maelezo juu ya yale yasiyojulikana. Inadhihirika kuwa watu wenye wivu hawatapata msamaha utakaoombwa na mtume na hawatakuwa na haki ya kuomba msamaha huo.

Mtume wa Allah anasema katika hadithi sharif **(Watu wa aina sita wataulizwa juu ya mambo sita, wataadhibiwa kwenye uwanja wa**

**hesabu kisha watavurumishwa motoni. Kiongozi wa nchi ataulizwa kwa dhulma, kabila la warabu wataulizwa kwa ghera, kiongozi wa kabila dogo ataulizwa kwa kiburi, mfanya biashara ataulizwa kwa kutokua muaminifu au hadaa, watu wa vijijini wataulizwa kwa ujinga na wenye elimu wataulizwa kwa hasad).** Ni wajibu kwa mfanya biashara kujua maana halisi ya riba, hadaa, uongo, kula mali ya wengine kinyume na misingi ya biashara na kujifunza njia za kuepukana na mambo hayo yaliyokatazwa. Watu wa vijijini, bali na waislam wote kabisa, wana wajibu wa kujifunza elimu ya itikadi ya ahli sunna na elimu ya lazima ya dini. Hadithi sharif hii inatufunza kuwa hasad hupatikana zaidi kwa watu wenye elimu ya dini katika jamii. Kitabu cha **Tafsirul Kabir** kinaeleza yafuatayo: (Hasad ni mafungu kumi. Tisa kati yao yako kwa watu wa dini. Mazito ya dunia ni mafungu kumi. Tisa kati yao yako kwa wacha mungu. Udhalilifu ni mafungu kumi. Tisa kati yao yako kwa wayahudi. Tawadhuu ni mafungu kumi. Tisa kati yao yako kwa wanasara. Matashi ya ngono ni mafungu kumi. Tisa yako kwa wanawake na moja liko kwa mwanamme. Elimu ni mafungu kumi. Moja liko Iraq. Iman ni mafungu kumi. Tisa yako Yemen. Akili ni mafungu kumi. Tisa anayo mwanamme. Baraka za kidunia ni mafungu kumi. Tisa yako Damascus). Haya aliyoyaandika Fakhrudyn Razi katika kitabu chake hiki ni kutegemea na ule wakati alioishi yeye. Kabla Mtume swallallahu alayhi wasallama hajaupa utukufu ulimwengu kwa kuja kwake, ilikuwa ni tabia ya wayahudi kuomba dua kwa kusema maneno yafuatayo wanapotoka kwa ajili ya vita “Ewe mola! Tunakuomba kwa baraka za mtume wako mtukufu ambae umeahidi kumleta na ambae unampenda sana” Dua zao zilikuwa zikijibiwa na Allahu taala akiwashushia nusra yake. Wakati Mtume “swallallahu alayhi wasallama” alipoanza kulingania walifahamu kuwa ndie yeye huyo mtume alieahidiwa lakini walimkataa kutokana na hasad yao. Hasad yao iliwapeleka wao na wafuasi wao kwenye majanga na maafa yasiokwisha na adhabu.

Allahu taala ametutaka tujilinde na shari za shetani na zile za hasidi anapohusudu.

Mtume wa Allah anasema katika hadithi sharif **(Mnapoomba mahitaji yenu kwa walionacho basi ombeni kwa siri kwani watu hao hufanyiwa hasad).** Iwapo itagundulika kuwa mahitaji yako yanatekelezwa basi utafanyiwa hasad. Mtu akiwa na jambo lake la siri, ni hiari yake kulificha au kulidhihirisha ila mara nyingi wale wenye kulidhihirisha humalizikia kujuta. Mtu huwa ni mmiliki wa maneno yake kabla ya kuyasema na anakuwa na khiari kuyasema au

kutokuyasema. Ila baada ya maneno yale kutoka mdomoni mwake anakuwa ni mtumwa wa yale aliyoyasema. Watu mara nyingi hawazidhibiti siri zao kama wanavyodhibiti mali zao. Kuna msemo usemao "Iweke siri dhahabu yako, imani yako na mtizamo wako."

Mtu mwenye hasad hawezi kubadilisha mipango ya Allahu taala. Hivyo ni bure hujitia wasiwasi na kujichosha kisha na dhambi alizozichuma zinakuwa ni hasara nyengine. Hadhrat Muawiya "radhiyallahu anhu" alimnasihi mwanawe akamwambia (Jiepushe sana na hasad. Madhara utakayojisababishia wewe mwenyewe binafsi kwa kufanya hasad ni makubwa na ya haraka kuliko yale atakayoyapata huyo mtu unaemfanyia hiyo hasad). Sufyan Athawry "rahmatullahi taala alayhi" amesema "Asie fanya husda huwa na akili nyoofu''. Mwenye kufanya hasad hapati alitakalo wala hapati heshima kwa watu. Hasad inaharibu fahamu na kupunguza umri wa mtu. Asma anasema alikutana na mwana kijiji ambae ni mzee katika umri wa miaka mia na ishirini. Akamuuliza siri ya kuishi kwake umri mrefu nae akamjibu kuwa hajawahi kumfanjia hasad mtu yeyote. Abuleyth Semerkandy "rahmatullahi taala alayhi" anasema "Watu watatu dua yao haitakabaliwi. Mwenye kula haramu, mwenye kusengenya na mwenye husda."

Mtu mwenye kufanyiwa hasad hapati madhara yoyote hapa duniani au akhera bali anapata faida. Yule mwenye kufanya hasad hupata huzuni na msongo wa mawazo kwa kuona yule anaemfanyia husda neema zake haziondoki bali zinaongezeka. Ili kujiokoa na hasad inahitaji kumpelekea zawadi, kumnasihi na kumpongeza yule unaehisi husuda juu yake. Pia kumfanyia tawadhuu na kumuombea dua neema zake ziongezeke.

## CHUKI

16. Hili ni gonjwa la kumi na sita kati ya magonjwa ya moyo. Chuki ni hali ya kutokumpenda mtu na kubeba moyoni kinyongo na hisia za uadui dhidi yake. Ni haram kubeba hisia za uadui kwa mtu ambae anakunasihi. Kinachotakiwa ni kupokea nasaha zake na wala sio kumfanyia chuki. Kwa vile anachofanya yeye ni kutekeleza amri ya Allah hivyo inafaa kumpa heshima na kumpenda. Si haram kufanya chuki kwa mtu dhalim. Mtu anaekufa na deni, ikiwa warithi wake hawakulilipa basi atalipishwa siku ya kiama. Kumsamehe dhalim ni katika ubora. Katika vita vya Uhud wakati Mtume swallallahu alayhi wasallama alipopata jaraha usoni na kuvunjwa jino lake masahaba "radhiyallahu taala anhum ajmaina" walihuzunika sana na kumtaka

Mtume “swallallahu alayhi wasallama” awaombee makafiri laana ili waadhibiwe. Mtume wa Allah akawajibu **(Sikutumwa nije niwalaani watu. Nimetumwa kuja kuwaombea watu dua njema na kuwa ni rehema kwa watu wote).** Adui zake aliwasamehe na hakuwalaani.

Hadithi sharif inasema **(Mali haipungui kwa kutoa sadaka. Allahu taala anawatukuza wenye kusamehe. Wale wenye kusamehe kwa kutaka radhi za Allah, yeye huwapandisha daraja).** Amesema Ghulabady kwamba sadaka iliyotajwa katika hadithi sharif hii ni ile ya fardhi yaani zaka. Wenye kufanya tawadhuu hupata thawabu zaidi katika ibada zao na katika matendo yao ya utiifu. Huwa wanasamehewa makosa yao kwa haraka. Kimaumbile binaadamu anayo roho ya mnyama na matamanio ya nafsi. Anapenda mali na pesa. Ghadhabu, kisasi na kiburi hujitokeza. Katika hadithi sharif hii dawa ya tabia hizo mbaya inaelezwa. Inaamrisha sadaka na zaka. Inasafisha ghadhabu na visasi kwa kuamrisha kusamehe. Hadithi sharif inaamrisha kusamehe kikamilifu bila ya masharti. Msamaha kamilifu huwa hauna masharti. Ni msamaha wa ujumla na wala sio wa sehemu tu ya jambo husika. Ni vizuri mno kwa mwenye kusamehe katika hali ya kuwa anao uwezo wa kugombania haki yake. Kusamehe katika hali ya kuwa huna uwezo pia ni vizuri ila kusamehe hali ya kuwa uwezo wa kudai unao inakuwa bora kwa sababu ni jambo gumu kulifanya na nafsi inafunzika zaidi. Kumsamehe aliekudhulumu inaonesha daraja kubwa ya upole, huruma na ushujaa. Kumpa zawadi asie kutendea wema pia ni daraja ya juu ya ihsani. Kumfanyia wema aliekufanyia ubaya ni daraja la juu la ubinaadamu. Sifa hizi huweza kumbadilisha adui na kumfanya awe rafiki. Nabiyullahi Isa “alayhi salaam” amesema (Niliwahi kusema kuwa mwenye kuvunja jino nae avunjwe jino. Mwenye kukata sikio au pua nae sikio lake au pua yake ikatwe. Lakini sasa ninasema anaekufanyia uovu usimfanyie uovu. Anae kupiga shavu la kulia mgeuzie na la kushoto). Sheikh Ibn Araby “kaddasallahu taala sirrahul aziz” (Muhyiddin Ibn Arabi alikufa mji wa Sham mwaka 561 hijria) anasema “Yule mwenye kumtendea wema aliemtendea ubaya, huwa ameshukuru neema alizonazo. Yule mwenye kumtendea uovu yule aliemtendea wema huwa amezikufuru neema alizopewa. Kuchukua haki yako kutoka kwa alie nae bila ya kuongeza kitu hiyo huitwa **Intisar**.” Kusamehe ndiyo daraja la juu la uadilifu na intisar ni daraja lililo chini yake. Uadilifu ndiyo daraja ya juu ya watu wema. Kusamehe baadhi ya wakati hutafsiriwa na dhalim kuwa ni udhaifu hivyo kusababisha kuongezeka kwa dhulma. Intisar siku zote inapelekea kupungua kwa dhulma au hata kutoweka kabisa. Katika

nyakati kama hizo ni bora na ni thawabu zaidi kufanya Intisar kuliko kusamehe. Kuchukua haki yako na ziada kutoka kwa alie nayo hiyo huitwa **Jeuri** na hiyo ni dhulma. Wenye kufanya jeuri wametajwa kupata adhabu. Kumsamehe aliekudhulumu kunakupelekea kupata mapenzi ya Allahu taala. Kuchukua haki yako kutoka kwa dhalim bila ya kuzidisha ndio uadilifu. Uadilifu unatakiwa ufanywe hata kwa kafiri. Kusamehe kwa kiasi cha uwezo wake mtu ni katika tabia njema. Mtume wa Allah „swallallahu alayhi wasallama" alimsikia mtu akimtakia dua mbaya dhalim, akasema **(Umefanya Intisar)**. Lau kama angefanya msamaha ingekuwa bora zaidi. Katika hadithi sharif iliyo mwisho wa juzuu ya mwisho ya kitabu cha **Barika** inasema **(Mwenye mambo matatu, huingia peponi kupitia mlango wowote anaotaka: mwenye kulipa haki ya mja, mwenye kusoma suratul ikhlas mara kumi na moja baada ya kila sala, mwenye kufa hali amemsamehe muuaji).** Mmoja wa wanazuoni ambaye alisema kuwa Dhulkarnain si mtume; alimsifu kuwa na sifa nne muhimu walizokuwa nazo mitume. Nazo ni: Akisamehe hali ya kuwa nguvu anazo. Akitimiza ahadi anayoitoa. Daima akisema ukweli. Rizki yake alikuwa haitayarishi siku ya kabla yake. Kwa kiasi ya wingi wa dhulma basi ndio wingi wa thawabu za kusamehe.

Kuna maovu kumi na moja yanayochochewa na chuki: Hasad, kufurahia majanga ya wengine, kukata udugu, kudharau, uwongo, kusengenya, kutoa siri za wengine, kufanya istihzai, kutesa, kutolipa haki na kuzuia msamaha.

Mwenye chuki hukumbwa na madhambi ya uongo, uzushi, ushahidi wa uongo, kusengenya, kumdhuru mwengine bila ya haki, kula haki ya wengine na kukata ziara. Hadithi sharif inasema **(Mtu ambae hana mambo matatu, anategemewa kusamehewa makosa yake yote. Kufa kabla ya kukumbwa na shirki na kufr, kutokufanya uchawi na kutokuwa na chuki).** Hadithi sharif hii inaonesha kuwa uchawi hauna nafasi katika Uislam.

Kufanya uchawi ni haram. Mwenye kuamini kuwa anaweza kufanya kila kitu kupitia uchawi basi huwa kafir. Kutokuamini kuwepo athari za uchawi pia ni ukafiri. Inatakiwa kuamini kwamba uchawi kama ilivyo kwa dawa, athari yake inatokea kwa kutaka kwake. Kuamini kuwa kila ukitakacho Allahu taala atakifanya, hilo ni jambo la dhambi ila sio kufur. Dawa ya uchawi imeelezwa kwa urefu katika kitabu kiitwacho **Saadeti abadiyye**.

Katika hadithi sharif tunasoma **(Allahu taala anasamehe watu wote katika usiku wa nusu ya shaaban isipokuwa mshirikina na mushahin).** Mushahin ni yule mtu wa bid'a apingae madhehebu.

[Mtu yeyote asiyefuata itikadi ya ahlu sunna waljamaa huwa mtu wa bid'a. Yule asie katika moja ya madhehebu manne huwa ametoka katika kundi la ahlu sunna. Yule aliyejitenga na itikad ya ahlu sunna atakuwa kafiri au mtu wa bid'a. Makafiri ni aina nyingi na kundi baya zaidi ni la washirikina. Mshirikina ni yule asiyeamini Allahu taala na siku ya mwisho. Wapagani, wamasoni na wakoministi ni miongoni mwa washirikina. Watu wa bid'a si makafiri ila kama watabeba itikadi zilizopotoka, kukana yale mambo ambayo yamethibitishwa wazi wazi katika Kur-an Karim na sunna basi wengi wa wanazuoni wamesema kuwa katika hali hizo watakuwa makafiri. Katika Kur-an Karim na sunna neno mushrik limetumika kwa maana ya kafir. Kwa mfano Allahu taala aliposema hamsamehe mushrik maana yake ni kwamba kafiri yeyote hatosamehewa. Watu wa bid'a wasipobeba itikadi potofu hawatakua makafiri na watabaki kuwa waislam. Ila madhara ya hawa watu wa bid'a kwa Uislam ni makubwa kuliko hata madhara yasababishwayo na makafiri. Viongozi wa dini wenye kupinga madhehebu, wafuasi wa Mawdudy, wafuasi wa Ibn Taymiyya waitwao salafi na wafuasi wa Seyyid kutub ni mfano wa makundi hayo. Katika kitabu kiitwacho **Hujjatul Islam** kilichoandikwa na mwanazuoni wa kihindi, mufti Mahmoud bin abdulghayur Pishawury "rahimahullahu taala" na kuchapishwa mwaka 1264 hijria [1848 milady], katika risala yake ya **Tuhfatul araby wal ajamy** anasema, ni wajibu kwa waislam kuwafuata mujtahid. Katika suratun Nahl aya ya 43 na suratul Anbiyaa aya ya 7 zinasema katika maana ya aya **(waulizeni wenye elimu, ili muelimike).** Tunasoma katika suratu Tawba aya ya 100 katika maana ya aya **(Allah amewaridhia Muhajir wa mwanzo, Ansari na wale wanaowafuata).** Aya hizi zinatuamrisha kufuata. Muadh bin Jabal "radhiyallahu taala anhu" alipochaguliwa gavana wa Yemen alisema (Wakati nisipopata dalili kutoka katika Kur-an Karim na hadithi sharif nitafanya ijtihad na nitaamrisha kwa kiasi ya ufahahmu wangu). Mtume "swallallahu alayhi wasallama" alivutiwa na jawabu hii na kamuombea dua. Miongoni mwa wanazuoni wa Maliki huko Misri ni Ahmed Shihabudyn Karafy "rahimahullahu taala" aliyefariki mwaka 684 hijria [1285 miladia ] . Mwanazuoni huyu alisema, ameandika Jalaludyn Suyuty rahimahullahu taala katika kitabu kiitwacho **Jazilul mawahib** kwamba (Imefikiwa Ijmaa kwamba mtu ambae ni mpya katika Uislam anaweza akamfuata mwanazuoni yeyote amtakaye). Kama ambavyo wanazuoni

wa hadithi wanaposema kuwa hadithi ni sahihi inakubalika hivyo, basi ni hivyo hivyo inavyotakiwa kwa wanzuoni wa fikh, wanaposema kwamba jambo fulani la fikh ni sahihi inabidi ikubalike hivyo. Kutoka suratun Nisaa aya ya 58 tunasoma katika maana ya aya **(Na pale msipowafikiana katika jambo la dini, basi lirudisheni kwenye Kur-an Karim na sunna).** Amri hii inaelekezwa kwa wanazuoni waliofikia daraja ya Mujtahid. Ibn Hazm na wanamageuzi wa dini wanasema (Si halali kufanya taklid [kumfuata] mtu yeyote alie hai au aliekwisha kufa. Kila mtu lazima afanye ijtihad). Maneno haya hayana thamani kwa sababu hawa si katika ahli sunna. [Imeelezwa mwishoni mwa kitabu chetu **Ashaddul jihad** kwamba Ibnu Hazm ni mpotevu na asiefungamana na madhehebu.] Ni wajibu kwa mufti kuwa mujtahid. Mufti ambae si mujtahid mutlaq ni haram kwake kutoa fatwa. Kwa hivyo inafaa kunukuu fatwa za mujtahid. Haijuzu kutaka fatwa mpya kutoka kwa mufti ambaye si mujtahid. Imeandikwa katika mlango wa saumu wa kitabu cha **Kifaya** kwamba haijuzu kwa mtu ambae si mujtahid kufanya jambo kwa kufuata hadithi aliyoisikia kwa sababu hadithi hiyo inaweza kuwa Mansukh (imefutwa) au ikawa ina maelezo zaidi ambayo yeye hayajui. Tafauti na fatwa inayotolewa na mujtahid, hii inakuwa imeelezwa na iko wazi zaidi na imezingatia viwango vya dalili zilizotumika. Maelezo yenye kufanana na haya yanapatikana katika kitabu kiitwacho **Taqrir.** Tafsiri kutoka kitabu kiitwacho **Tuhfatul arabi wal ajami** inamalizika hapa.]

Moja kati ya sababu za chuki ni ghadhabu. Wakati mtu anapoghadhibika na akawa hawezi kulipa kisasi basi hufanya chuki. Ghadhabu inatokana na mwendo wenye kasi wa damu. Kughadhibika kwa ajili ya Allah inafaa kwa sababu hii inaonesha ghera aliyonayo mtu kwa dini yake.

## USHAMATA

17. Ushamata maana yake ni kupata furaha wakati nduguyo muislam anapofikwa na maafa na ni gonjwa la kumi na saba la moyo. Mtume “swallallahu alayhi wasallama” anasema katika hadithi sharif **(Usiwe na ushamata kwa nduguyo muislamu. Ukiwa na ushamata basi Allahu taala ataliondoa tatizo hilo kutoka kwake na kukupa wewe).** Haitokuwa ushamata ikiwa mtu atapata furaha kwa kusikia kifo cha dhalim kwani hiyo ina maana ya kuokoka na dhulma na shari zake. Ila kuwa na ushamata kutokana na aina nyengine za majanga au msiba unaompata adui si jambo linalojuzu. Na inazidi uovu wake kama itadhaniwa kuwa msiba au janga hilo limemfika kutokana na mtu fulani kwa mfano kwa dua ya mtu fulani anaedhaniwa utukufu. Hili

linapelekea kujiona kwa huyo mdhaniwa. Kinachofaa kudhani ni kwamba maafa yanayomkuta dhalim ni hukmu ya uungu kutokana na uovu wake mwenyewe alioutanguliza. Hivyo inafaa kumuombea dua ili hayo maafa yamuondokee. Katika hadithi sharif mtume swallallahu alayhi wasallam anasema **(Dua ya muumini kwa nduguye muumini hutakabaliwa. Malaika atasema "Mola akupe na wewe hayo uliyomuombea mwenzio" na malaika wengine wataitikia Amin. Dua ya malaika haitokataliwa).** Na ikiwa dhalim amekumbwa na maafa ambayo yanamzuia kuendeleza udhalimu wake basi kufurahi kwa hilo hautokuwa ushamata na wala haitokuwa dhambi bali itakuwa ni ghera ya dini. Ghera ya dini ni dalili ya msimamo thabiti alionao mtu kwa dini yake. Si vyema kufanya ghera kwa nia ya kukidhi matamanio ya kinyama. Kwa ujumla kufurahi kutokana na balaa linalomfika dhalim si jambo jema ila kwa vile hili litamzuilia kuendelea na dhulma ndio maana furaha ikajuzu.

## KUHAMA

18. Hili ni gonjwa la kumi na nane. Kuhama maana yake ni kukata urafiki na mtu na kuwa na tafauti nae. Mtume „swallallahu alayhi wasallama" anasema **(Si halali kwa muumini kumuhama nduguye muumini kwa zaidi ya siku tatu. Baada ya siku tatu ni wajibu kwake kumfata na kumsalimia).** Ikiwa atajibu salamu yake basi watapata ujira wote wawili na ikiwa hatojibu basi dhambi zitabaki kwa huyo aliekataa kujibu. Haifai kwa muumini mwanamke au mwanamme kughadhibika na kuvunja mahusiano na muumini mwengine kwa sababu za kidunia tu. Na wale wasio waumini ambao wako chini ya dhima ya dola ya kiislam nao wanaingia katika hukumu hiyo hiyo. Wasio waislam nao haifai kuwahama kwa sababu za kidunia.

[Inafaa kuamiliana nao kwa wema, bashasha, maneno mazuri, kutokuwadhalilisha na kuwapa haki zao kama inavyostahiki. Iwe ni muislamu au kafir, Iwe ni katika dola ya kiislam au katika nchi isiyo na muafaka na dola ya kiislam, haijuzu kwa mtu yeyote kuchukua mali ya mtu mwengine, kumuua au kumfanyia matendo yatayompotezea heshima yake. Makafiri wanaoishi ndani ya nchi za kiislam, au makafiri wanaotembelea nchi za kiislam kama watalii, wafanya biashara na wengineo, inalazimika wapewe haki sawa na za waislam katika kuamiliana nao. Wanatakiwa wawe huru kutekeleza yale ya dini yao na ibada zao. Uislam umewapa makafiri uhuru huu. Waislam wanatakiwa wafuate amri za Allah na wasifanye maasi. Wasipinge kanuni za serekali na wasifanye makosa. Wasisababishe fitna katika

jamii. Wawatendee wema waislam na makafiri na walinde haki zao. Wasimdhulumu mtu yeyote wala kumtesa. Muislamu anatakiwa kila pahali na kila mtu amuoneshe tabia zake njema zilizotukuka, ili iwe ni sababu ya kila jamii kuupenda na kuuheshimu Uislam.]

Watu waliogombana ni vizuri kabla ya siku tatu kukutana na kusuluhishana. Imetajwa siku tatu ili kuwapunguzia watu uzito na baada ya hapo wanaanza kupata dhambi na zinaendelea dhambi hizo hadi watakapopatana. Mtume wa Allah anasema katika hadithi sharif **(Nenda kwa uliye gombana naye mkapatane. Kama amekudhulumu msamehe. Kama amekutendea uovu wewe mtendee wema).** Anayesema **'Assalamu alaykum',** hupata mema kumi. Asemae 'Assalamu alaykum warahmatullah,' hupata mema ishirini. Ama yule asemaye 'Assalamu alaykum warahmatullahi wabarakatu', hupata mema thalathini. Na katika kujibu salam basi fadhila zake ziko hivyo hivyo. Wale waliodumu na ugomvi zaidi ya siku tatu basi wanakosa msamaha wa Allah na wanastahikiwa na adhabu. Inafaa bali ni mustahabu kumhama mtu ili iwe ni nasaha na funzo kwake kutokana na uovu anoufanya. Kukosana na mtu kwa ajili ya Allah inawezekana. Katika hadithi sharif tunasoma **(Miongoni mwa ibada zenye thamani kabisa ni kupenda kwa ajili ya Allahu taala na kuchukia kwa ajili ya Allahu taala).** Allahu taala alimuuliza Musa alayhi salaam "Umefanya nini kwa ajili yangu mimi?" Musa "alayhi salaam" akajibu "Kwa ajili yako nimesali, nimefunga, nimetoa zaka na nimelitaja sana jina lako." Allahu taala akamwambia "Sala kwako ni burhani na inakulinda na kutenda maovu. Funga kwako ni ngao, inkulinda na moto wa Jahannam. Zaka nayo itakuwa ni kivuli kwako siku ya kiama na itakupa wewe raha. Dhikri siku ya kiama itakuwa ni mwangaza kwako na kukuondolea kiza. Je kwa ajili yangu mimi umefanya nini?" Musa akasema "Ewe mola wangu! Naomba unitambulishe. Nifanye lipi ili liwe lako wewe?" Allahu taala akamwambia "Ewe musa! Je umewapenda wapenzi wangu na kuwakataa maadui zangu?" Hapo Musa "alayhi salaam" akafahamu kwamba ibada aipendayo zaidi Allahu taala ni kupenda kwa ajili yake na kuchukia kwa ajili yake. Inajuzu kumhama kwa muda mrefu yule mwenye kufanya maasi na maovu. Katika kisa mashuhuri inafahamika kwamba Ahmad bin Hambal „rahimahullahu taala" alimuhama ami yake na wanawe kwa kuwa walipokea zawadi ambayo wanajua ilitokana na haramu. Mtume „swallallahu alayhi wasallama" aliwahama wale watu wa tatu na familia zao kwa kuacha kwao kushiriki katika vita vya Tabuk.

## WOGA

19. Woga ni gonjwa la kumi na nane. Kuitumia ghadhabu katika kiwango kinachohitajika huitwa **ushujaa.** Kuitumia ghadhabu chini ya kiwango kinachohitajika huitwa **woga.** Anasema Imam Muhammad bin Idris Ashafy „rahimahullahu taala", "Mtu mwenye kufanya woga pahala panapohitaji ushujaa ni kama punda. Mtu anaekataa hukumu iliyotolewa na kadhi ni kama shetani." Mtu mwoga haoneshi jitihada wala hima kwa jamaa zake na mkewe. Hawezi kuwalinda. Anaridhia mateso na dhulma. Hata akiona haramu inatendeka hukaa kimya. Anabaki na tamaa ya mali ya watu wengine. Haoneshi uthabiti katika mambo yake na apewapo majukumu hayapi umuhimu wa kutosha. Katika Suratu Tawba Allahu taala anausifia ushujaa na kujitoa muhanga. Katika suratu Nur Allahu taala anaamrisha kutokutenda huruma wakati wa kuwapa adabu stahiki wazinifu.

Na katika hadithi sharif mtume wa Allah anasema **(Lau kama binti yangu mpenzi Fatima ataiba basi nitaukata mkono wake).** Katika suratul Fath Allahu taala anasema kuhusu masahaba watukufu radhiyallahu anhum ajmaina kwamba **(Wana ghadhabu kwa makafir)** akiwasifia namna ambavyo wakikabiliana na makafiri kwa nguvu bila woga katika vita. Katika suratu Tawba aya ya 74 katika maana ya aya **(Na kuwa mgumu dhidi ya makafiri)** kwa maana ya kwamba tusiogope wakati wa uvamizi wa makafiri. Katika hadithi sharif Mtume "swallallahu alayhi wasallama" anasema **(walio na kheri zaidi kwa umma wangu ni wale wenye uvumilivu kama chuma).** Ni lazima kuwa na ushujaa dhidi ya maadui wa waislam na Uislam. Haijuzu kuwa muoga dhidi yao. Kuogopa na kukimbia hakubadilishi kudra ya Allahu taala na wakati wowote mtu ahadi yake ikifika basi popote alipo Izrail "alayhi salaam" ataichukua roho yake. Lakini pia haijuzu kujiingiza kwenye jambo la hatari. Sehemu yenye hatari kuingia au kubakia peke yako ni dhambi.

## TAHAWWUR (USHUPAVU)

20. Hili ni daraja la ghadhabu lililopita kiwango stahiki kinachotakikana. Ghadhabu zake na vishindo vyake vinapita mpaka. Kinyume chake ni kuwa mpole na latifu. Mtu mpole hakasiriki wala hakurupuki wakati akutanapo na mambo yenye kukasirisha. Muoga ni yule ambae hujidhuru katika hali kama hiyo. Mwenye ghadhabu katika hali kama hii hujidhuru yeye na kuwadhuru wengine. Na alie na hali hii ya tahawwur hufanya mambo kama mtu aliepoteza akili na huweza hata kumpelekea kwenye ukafiri. Katika hadithi sharif tunasoma

**(Ghadhabu inaharibu imani).** Mtume “swallallahu alayhi wasallama” hakuwahi kuonekana kughadhibika kwa mambo ya kidunia. Ghadhabu zake zilikuwa ni kwa ajili ya Allah. Mtu anapoghadhibika akumbuke kwamba huyo anaetaka kumfanyia lolote, na yeye anaweza kurejeshea kwa hilo hilo au hata zaidi ya hilo. Binaadamu anapoghadhibika moyo wake hutetereka na hilo huonekana kwenye mabadiliko yake katika uso, ambao huwa mbaya na wa kutisha.

Kudhibiti ghadhabu huitwa **Kazm** na hili ni jambo lenye faida na alienalo amebashiriwa pepo. Mwenye kufanya kazm kwa ajili ya Allah, akasamehe kwa aliyotendewa na asilipize kisasi, basi huyo hupendwa na Allahu taala na imeelezwa kuwa pepo imeandaliwa kwa ajili yake. Katika hadithi sharif tunasoma kwamba **(Yeyote yule ambae atajizuia na ghadhabu kwa ajili ya Allahu taala, basi nae atamzuilia na moto).** Na katika hadithi sharif nyengine tunasoma kwamba **(Mambo matatu akiwa nayo mja basi Allahu taala humhifadhi mja huyo na kumpa himaya yake, humpenda na kumpa rehema zake. Mwenye kushukuru neema aliyoipata, mwenye kumsamehe aliemdhulumu na mwenye kudhibiti hasira zake).** Kushukuru neema maana yake ni kuzitumia kwa namna ambavyo Uislamu umeagiza. Na katika hadithi sharif nyengine **(Mtu ambaye amepandwa na ghadhabu, lakini akaamua kuwa mpole hali ya kuwa nguvu ya kufanya analotaka anayo, Allahu taala anatia utulivu na imani ndani ya moyo wake)** na katika hadithi nyengine **(Mwenye kudhibiti ghadhabu zake, Allahu taala atamsitiria aibu na maovu yake).** Imam Ghazali “rahimahullahu taala” anasema (kuwa mpole ni bora zaidi kuliko kuwa mwenye kuishinda ghadhabu). Na katika hadithi sharif mtume amesema **(Ewe Mola! Naomba unipe elimu. Unipambe kwa upole. Unipe na Taqwa na unifanye mzuri kwa afya njema).** Abdullah ibn Abbas „radhiyallahu taala anhumaa“ alikwaruzana kidogo na mtu fulani. Katika kulipoza hilo ibn Abbas alimuuliza huyo mtu “Una shida yeyote tafadhali ili nikusaidie.” Hapo yule mtu aliona haya na kumtaka radhi ibn Abbas kwa lile lililotokea. Mtoto wa Hadhrat Hussein, Zeynulabidin Ali „radhiyallahu taala anhuma“ siku moja naye alikwaruzana kidogo na mtu. Basi alivua jokho lake na kumpa huyo mtu kama zawadi. Nabiyullahi Isa “alayhis salaam“ alipopita mbele ya mayahudi na wakamsema kwa maneno mabaya yeye aliwajibu kwa maneno mazuri. Walipomuuliza mbona umewapa maneno mazuri hali ya kwamba walikupa maneno mabaya? Nabii wa Allah akawajibu (Kila mtu hutoa kile alichonacho, kumpa mwengine) Mtu alie mpole mwenye utulivu huwa na furaha. Yeye husifiwa na kila mtu.

Katika hadithi sharif tunajifunza yafuatayo **(Ghadhabu zinatokana na wasi wasi wa shetani. Shetani ameumbwa kwa moto. Moto nao huzimwa kwa maji. Kwa hivyo mnapopatwa na ghadhabu tieni udhu).** Mtu anapokumbwa na ghadhabu, asome Audhu, Bismillahi na Qul audhu mbili. Mtu anapokumbwa na ghadhabu akili yake hufunikwa na hutoka nje ya Uislam. Mtu aliyekumbwa na ghadhabu kama yuko wima basi inafaa akae kitako. Katika hadithi sharif tunasoma **(Mtu aliekumbwa na ghadhabu kama yuko wima basi na akae na kama ghadhabu zitaendelea basi alale ubavu).** Mtu aliye wima kuchukua hatua ni wepesi lakini akikaa uwezekano hupungua na alalapo hupungua zaidi. Ghadhabu zinatokana na kiburi na mtu alalapo kiburi hupungua. Mtu anapoghadhibika imeamrishwa kupitia hadithi sharif asome dua ifuatayo **(Allahumma ghfirly dhanby, wadh-hab ghaydha qalby wa ajirny mina shaytan).** Maana ya dua hii ni kwamba (Ewe Mola! Nighufirie madhambi zangu, na unitoe ghadhabu katika moyo wangu na unikinge na shetani).

Hadithi isemayo **(La Taghdhab)** imekataza kughadhibika. Asighadhibike mtu kwa ajili ya dunia au akhera. Wakati mtu anapoghadhibika fahamu yake huharibika na baadhi ya viungo vyake hupata maradhi. Daktari hawezi kupata dawa ya maradhi haya. Dawa pekee ya maradhi hayo ni kufuata hadithi sharif isemayo usighadhibike. Mwenye kughadhibika huwaumiza watu kwa maneno yake na vitendo vyake jambo ambalo linawasababishia nao kupata maradhi ya fahamu. Hatimae ndani ya nyumba inakuwa hakuna raha wala mafahamiano. Inaweza kupelekea kuvunjika kwa ndoa bali hata kutokea mauaji. Ikiwa katika nyumba hakuna mtu mwenye ghadhabu basi nyumba hiyo huwa na furaha na utulivu. Iwapo atapatikana mtu mwenye ghadhabu basi nyuma hiyo hukosa raha na utulivu. Ugomvi kati ya mume na mke au mama na watoto bali hata uadui unaweza ukapatikana. Kitu kitakachosaidia kuleta furaha na utulivu ni kufuata hukmu za kiislam. Hukmu za kiislam hata kafiri akizifuata basi zitampa utulivu na furaha hapa duniani.

Majahili na wajinga wanadhania kuwa ghadhabu ndio ushujaa, ujana dume na ndio tendo linaloonesha hima. Wanaipamba ghadhabu kwa maneno hayo mazuri. Wanajaribu kuonesha kuwa ghadhabu ni kitu kizuri na kuisifu kwa hikaya zenye kuonesha kwamba kuna watu wakubwa ambao walifanya ghadhabu. Hili linaashiria uchache wa akili. Ndio maana mgonjwa ni haraka kughadhibika kuliko alie na afya, mwanamke anamtangulia mwanamme na mzee anampita kijana kwa ghadhabu. Alie chini ya miaka thalathini huitwa kijana, alie baina ya

miaka thalathini na hamsini huitwa mtu mzima na alie juu ya miaka hamsini huitwa mzee.

Haifai kusikiliza mawaidha makali yenye ushawishi ambayo hayatokani na vitabu vya dini bali yanatokana na akili ya mzungumzaji tu. Haya pia huleta ghadhabu. Dawa ya hili ni kuzungumza yaliyo sahihi kwa upole. Hadhrat Hassan na Hussein "radiyallahu taala anhumaa" walikuwa wakitembea jangwani na wakamuona mzee akitia udhu wake hali ya kuwa akifanya makosa katika hilo. Kutokana na umri wake walipata uzito kumweleza kuwa udhu wake hauko sahihi. Hivyo wakatafuta njia ya busara na kumwambia "Mzee! sisi tunabishana ni nani kati yetu anatia sahihi udhu wake. Tunaomba tutie udhu mbele yako kisha wewe utuamulie yupi kati yetu udhu wake ni sahihi." Akaanza Hasan kisha akafuatia Husein, wote wakatia udhu vyema hali ya kuwa yule mzee anawaangalia makini. Kisha yule mzee akawambia "Wanangu! Namna sahihi ya kutia udhu ndio kwanza ninajifunza kutoka kwenu hivi sasa." Ibrahim alayhi salaam aliwaalika chakula watu mia mbili miongoni mwa wale wenye kuabudia jua. Baada ya kumaliza kula wakamwambia "Chochote utakachotuamrisha tutafanya." Akawambia "Mimi nina ombi moja tu kwenu. Nataka mumsujudie mola wangu alau mara moja" Wakaanza kushauriana baina yao kwa kusema "Huyu ni mtu mwema aliye mashuhuri kwa ukarimu na mialiko, yafaa tusimkatalie. Wacha tulete hiyo sijda moja halafu tutarudi tukaiabudu miungu yetu. Hakuna dhara." Wakati wakiwa kwenye sijda Ibrahim alayhi salaam alimuelekea mola wake na kusema (Ya Rabbi! uwezo wangu mimi umefikia hapa. Hakuna la ziada ninaloweza kufanya. Kuwafikisha hawa kwenye uongofu na furaha ni wewe pekee uwezaye. Wajaalie hawa wawe waislam). Dua yake ilitakabaliwa na wote wakawa waislam. Mtu mwenye nia ya kufanya jambo la haramu atanasihiwa kwa siri. Mtu mwenye kukutwa anatenda haram ataelezwa hapo hapo lakini kwa lugha iliyo nzuri na maneno laini. Kumnasihi mtu yeyote kwa siri ni jambo lenye kuleta athari zaidi.

Kutokufahamu vyema maneno ya mtu pia kuna sababisha ghadhabu. Kwa hivyo kuzungumza kwa uchache na uwazi na kuacha kutumia maneno yenye kutia wasiwasi ndio lilio bora zaidi. Kuzungumza kitu kwa mafumbo kunampa uzito msikilizaji na kunamchoma. Kuamrisha mema kuna masharti matatu: La kwanza ni kutia nia ya kuamrisha yale ayatakayo Allahu taala na kukataza asiyoyataka. La pili ni kulijua vyema jambo unalolizungumzia na la tatu ni kuwa tayari kufanya subira kwa yale yatakayokusibu. Ni vyema

kuzungumza kwa ulaini na kuepuka lugha kali. Lugha kali yenye mijadala huleta fitna. Katika ukhalifa wake, siku moja Umar “radhiyallahu anhu” alikuwa akitembea katika mji wa madina yeye na Abdullah ibn Masoud “radiyallahu anhu” wakati wa usiku. Kutoka kwenye nyumba moja akasikia sauti ya mwananmke akiimba. Alipochungulia mlangoni akamuona mzee ambae mbele yake kulikuwa na chupa za ulevi na ubavuni kwake kuna mwanamke anaimba. Hapo hapo akachupa dirishani na kuingia ndani. Aliposimama tu yule mzee akamwambia “Ewe Amiril muuminina! Hebu kwanza naomba unisikilize” Umar akamjibu “Haya sema”. Yule mzee akasema “Mimi hapa nimemuasi Allah kwa kosa moja ila wewe amri zake tatu umezivunja.” Umar akamuuliza “Ni zipi hizo?” Yule mzee akasema “Allahu taala anatukataza kuchungulia majumbani mwa watu ila wewe umechungulia kwenye mlango. Allahu taala anatukataza kuingia majumbani mwa watu bila ya idhini ya wenyewe lakini wewe umeingia bila idhini. Allahu taala anatuamrisha tuingie majumbani kupitia milangoni na tutoe salamu lakini wewe umechupa dirishani na hata salamu hukutoa” Umar “radhiyallahu anhu” akamjibu kwa insafu na uadilifu akamwambia “Umesema kweli”. Akamsamehe na kutoka nje hali ya kuwa analia. Akamuomba msamaha na kutoka nje hali ya kuwa analia.

Ni lazima kumdhania vyema mwenye kutoa nasaha kwa waislamu wote. Maneno yake tujitahidi kuyatafsiri vyema. Ni jambo lenye ujira kuamini kwamba waislam ni wema na wenye kheri. Kutokumuamini muislamu na kumdhania vibaya ni miongoni mwa tabia ovu. Tujitahidi kufahamu neno tunalolisikia na tusilolifahamu inafaa tuulize. Haifai kumdhania vibaya msemaji mara tu usikiapo. Katika wasiwasi ambao shetani anautia mioyoni mwa watu basi amefanikiwa sana katika hili jambo la kuwafanya watu wadhaniane vibaya. Kumdhani mtu vibaya ni haram. Ikiwa neno hulipatii maana nzuri basi ni vizuri kudhani kwamba msemaji amelisema kwa makosa au kuna kitu amekisahau katika uelezaji.

Wakati fakiri anamuomba maskini na akawa asimpe basi wote wawili wanaweza kukumbwa na ghadhabu.

Kumwambia mtu kitu au kumuuliza wakati ameshughulika, yuko kwenye msongo wa mawazo, yuko kwenye huzuni au matatizo basi hilo linaweza likamletea ghadhabu. Kilio na kelele za mtoto au kelele za mnyama pia zinasababisha ghadhabu. Kughadhibika kwa sababu hizo ni vibaya. Kuna hata wanaovighadhibikia vitu visivyo na uhai. Hii ni mbaya zaidi. Mfano wake ni mtu kulichoma moto shoka au kulivunja

kwa kuwa tu alipotaka kukata kigogo kiliteleza au hakikukatika kwa pigo moja. Wapo ambao wanaonekana kujidhuru kwa kujighadhibikia wenyewe. Kujighadhibikia kutokana na mapungufu uliyoyafanya kwenye ibada inafaa na ni jambo zuri lioneshalo hima uliyonayo kwenye dini. Kughadhibika kutokana na amri na makatazo yanayotolewa na mkuu wa nchi, mtume wa Allah “swallallahu alayhi wasallama” au Allahu taala ni vibaya zaidi. Yanaweza yakasababisha ukafiri. Hadithi sharif isemayo **ghadhabu huharibu iman**, inamaanisha kwamba ghadhabu kwa Allah na mtume wake husababisha ukafiri.

Kughadhibika kutokana na matendo ya haramu yanayofanywa ni vizuri, inaashiria hima katika dini. Ila unapoghadhibika haitakiwi kufanya mambo yasokubalika kidini na kiakili. Kumwita mtu kafiri, mnafiki, asie na wivu (dayuuth) na majina mengine machafu ni haramu. Pamoja na kwamba imeruhusiwa kumwita jahil au mjinga yule mwenye kufanya tendo la haramu lakini lililo bora zaidi ni kumnasihi kwa upole na maneno mazuri. Hadithi sharif inasema **(Kila wakati Allahu taala anawapenda wenye maneno laini).** Inalazimika kwa vyombo vya dola na polisi kutumia nguvu kuzuia matendo maovu ila kutumia nguvu nyingi za ziada kwa kupiga au kutesa hiyo itakuwa ni dhulma. Kuzuia kufanya maovu kunaweza kufanywa na vyombo vya dola au mtu mwengine mwenye uwezo. Jambo la kutoa hukumu kama vile kifo na kuvunjiwa nyumba hutolewa na vyombo husika vya dola tu. Kutoa adhabu zaidi ya inayostahiki ni dhulma. Nguvu za dola kutumika kuwaadhibu wale wenye kuamrisha mema na kukataza mabaya ni haramu.

Kinyume cha ghadhabu ni upole. Upole maana yake ni kutokughadhibika nalo ni bora kuliko kuishinda ghadhabu. Katika hadithi sharif tunasoma **(Kuonesha upole kwa jambo lenye kusababisha ghadhabu kunapelekea mapenzi ya Allah).** Na katika hadithi nyengine **(Allah anawapenda wenye tabia za haya, upole na iffat na anachukia wenye kusema maneno machafu na wenye kuomba kwa lugha ya msisitizo).** Iffat maana yake ni kutotamani mali ya mtu mwengine. Rasulullahi “swallallahu alayhi wasallama” akiomba sana dua ifuatayo **(Ewe mola! Naomba unipe elimu, upole, taqwa na afya).** Elimu yenye manufaa ni elimu ya tawhidi, fikhi na maadili. Afya ni kuepukana na mambo ya bid’a katika itikadi na dini, kuepukana na mapungufu katika amali na ibada, kuepukana na matamanio ya nafsi, kuepukana na hawaya na wasi wasi wa moyo na kuwa na kiwiliwili kisicho na maradhi. Walimuuliza Mtume “swallallahu alayhi wasallama” ni ipi dua iliyo bora zaidi nae akawajibu **(Ombeni afya kwa Allahu taala. Baada ya imani hakuna jambo bora kuliko afya).** Kupata

afya kunahitaji kuleta istighfari nyingi. Tunasoma na kujifunza katika Hadithi sharif zifuatazo: **(Kuweni wenye elimu na usikivu. Mnaposoma na mnaposomesha tumieni maneno laini. Elimu na kiburi haviendi sambamba). (Mwenye kufuata maamrisho ya Uislam na akawa mpole haunguzwi na moto wa Jahannam). (Kuwa mpole kunaleta baraka. Kuwa mzembe katika kazi kunaleta kughafilika). (Hapapatikani kheri kwa mtu asiekuwa mpole). (Upole una mpa mtu pambo na kumuondoshea mapungufu).**

Hakuna haja ya kumghadhibikia adui na inatosha kusema kwa sauti hafifu: Allah akupe jaza unayostahiki. Allahu taala humpa adhabu kali yule atendae dhulma.

Hadithi sharif **(Elimu inapatikana kwa kusoma. Upole unapatikana kwa hima. Allahu taala humpa anachotaka yule mwenye kujitahidi kufanyakazi kwa ajili ya jambo jema. Na yule mwenye kujilinda na maovu basi humlinda).**

## GHADAR

21. Hili ni gonjwa la ishirini na moja pia ni sababu inayopelekea ghadhabu. **Ghadar** ni kutokutekeleza kufuatana na ahadi na wakati uliopangwa. Ikiwa kifungo kimefanywa na upande mmoja tu hiyo huitwa **Waad**. Na ikiwa kifungo ni cha pande zote mbili hiyo huitwa **Ahadi**. Waad uliopewa nguvu kwa kiapo huitwa **Mithaq**. Baada ya watu wawili kuahidiana kisha mmoja akavunja ahadi bila ya makubaliano na mwenziwe hiyo ni ghadar. Mkuu wa dola kama atahisi makubaliano aliyoyafanya na makafiri yanalazimika kuvunjika basi inalazimu awape habari na haitojuzu kwake kwenda kinyume na makubaliano kabla ya kuwapa taarifa. Katika hadithi sharif tunasoma **(Mwenye kufanya ghadar, atapata adhabu mbaya siku ya kiama).** Kufanya ghadar ni haram. Hata ahadi walizopewa makafiri zinalazimu kutimizwa.

Katika hadithi sharif tunasoma **(Hana imani asiye na uaminifu. Asietimiza ahadi yake hana dini).** Katika hadithi sharif hii tunafahamu kwamba mwenye kuondoa uaminifu hawezi kuwa na imani kamili na kama hakulipa umuhihu jambo la uaminifu basi imani haibakii.

**Allahumma innaka afuwwun, karimun tuhibbul afwa faafuany**

## KHIYANA

22. Hili ni gonjwa la moyo la ishirini na mbili ambalo pia husababisha ghadhabu. Ni haramu kufanya khiyana na ni moja kati ya alama za unafiki. Khiyana kinyume chake ni uaminifu. Khiyana maana

yake ni kufanya jambo litakaloharibu uaminifu baada ya kwamba ulikwishatambulika kuwa muaminifu. Muumini ni yule mtu ambae ana uaminifu kwa mali na roho za wengine. Uminifu na khiyana kama ambavyo unakuwa kwa mali, basi pia unaweza kua kwa neno. Katika hadithi sharif tunasoma kwamba **(Mtu mwenye kushauriwa ni muaminifu).** Hii ina maana kwamba mtu huyu ni mwenye kuaminiwa kuwa anasema kweli na yale anayoambiwa anayadhibiti na hawaelezi wasiohusika. Ni wajibu kwake kusema kweli. Kama ambavyo mtu humkabidhi mali yake mtu anaemuamini, basi na ushauri vile vile inatakiwa afanye na mtu ambae ni msema kweli na mwenye kudhibiti maneno. Katika surat Ali Imran aya ya 159 katika maana ya aya **(Taka ushauri kwanza kwa jambo unalotaka kulifanya).** Kutaka ushauri kuna mkinga mtu na majuto. Mtu anaetakiwa ushauri ni lazima kujua hali ya watu, muda na mazingira ya nchi wanayoishi. Hii huitwa elimu ya siasa. Zaidi ya hayo anatakiwa awe mtu wa fikra, busara na uoni wa mbele na awe mtu mwenye afya. Ni dhambi kwa mtu anaeshauriwa kueleza asiyoyajua au kueleza kinyume na anayoyajua. Iwapo atafanya hivyo kimakosa basi haitokuwa dhambi. Kutaka ushauri kwa mtu ambae hana hizo sifa zilizotajwa hapo juu basi ni dhambi kwa wote hao wawili. Kutoa fatwa bila ya kuwa na elimu ya dini na dunia kunapelekea kulaaniwa na malaika. Kutoa amri kwa jambo ambalo unalijua kuwa lina dhara ni khiyana.

[Katika kitabu cha **Hadika** imesemwa: Amesema Abdullah bin Masoud “radhiyallahu taala anhu” (Jambo la kwanza litakaloponyoka na kupotezwa katika dini ni uaminifu. Na la mwisho litakalopotezwa ni sala. Wataendelea kusali watu hali ya kuwa hawana dini). Katika hadithi sharif tunasoma **(Mtu yeyote atakaemuua rafiki yake, basi huyo si katika umati wangu. Hata kama aliyeuliwa atakuwa kafiri)**.]

## KUVUNJA AHADI

23. Hili ni gonywa la ishrini na tatu. Kutokutekeleza ahadi kunaleta ghadhabu. Kifungo kilichofungwa na upande mmoja huitwa **Waad** na kile kilichofungwa na pande mbili huitwa **Ahadi** kama tulivyotangulia kusema. **Waid** ni ile ahadi iliyotolewa juu ya kuleta dhara au adhabu. Kutokutekeleza waid ni ihsan na **ukarimu**. Kuweka waad wa uongo ni haram na kuuvunja waadi huu pia ni dhambi. Ila waad huu ukitekelezwa ule uharamu wa uongo huondoka. Na ndio hivyo hivyo katika mauzo fasid. Ni wajibu kwa mauzo kama hayo kuyavunja na kuyaacha. Makubaliano yanapovunjwa na toba ikaletwa basi dhambi huwa hazibaki. Ila makubaliano ya hayo mauzo kama hayakuvunjwa

basi dhambi zake huwa mara mbili. Kutekeleza waadi ni jambo la lazima.

Katika hadithi sharif mtume wa Allah anasema **(Alama za mnafiki ni tatu, kusema uongo, kutotekeleza waadi na kufanya khiyana).** Ikiwa mtu atashindwa kutekeleza waadi kutokana na sababu zisizo mikononi kwake basi huo hautokuwa unafiki. Yule aliyepewa amana ikiwa ya mali, neno au siri na akaifanyia khiyana basi huyo atakuwa mnafiki.

Katika **Bukhari** mtoto wa Amr bin As "radhiyallahu taala anhu" ametaja hadithi sharif isemayo **(Alama za mnafiki ni nne: anapoaminiwa hufanya khiyana, husema uongo, huvunja waadi, atoapo ahadi hatekelezi na hutoa Ushahidi wa uongo mahakamani).** Ibn Hajar anasema unafiki maana yake ni kutokuwa sawa baina ya yale mtu anayoyadhihirisha nje na yale yaliyo moyoni mwake. Maneno yake na matendo yake hayafanani. Kufanya unafiki katika mambo ya itikadi ni ukafiri na kufanya unafiki katika maneno na vitendo ni haram. Kufanya unafiki katika itikadi na imani ni ukafiri mbaya zaidi kuliko aina nyengine za ukafiri. Inafaa kuweka waadi kwa nia ya kuutekeleza siku zijazo, bali ni thawabu. Waad kama huo kuutekeleza ni mustahab si wajibu na kutoutekeleza ni makruh. Katika hadithi sharif inaelezwa **(Mtu yeyote ambae atatoa waadi kwa nia ya kuutekeleza kisha akashindwa basi hatopata dhambi).** Katika madhehebu ya Hanafi na Shafi kutotekeleza waadi bila ya sababu ni Makruh na unapokuwa na sababu basi inajuzu. Katika madhehebu ya Hanbali kutekeleza waadi ni wajibu na kutotekeleza ni haram. Kufanya jambo ambalo ni sahihi kufuatana na madhehebu manne ni uchamungu.

Ni wajibu kwa muislamu kuyapenda na kuyaheshimu madhehebu yote manne na kutokufuata kwa ushabiki (Taasub) dhehebu fulani. Kufanya **talfik** kwa madhehebu yote manne ni jambo ambalo halijuzu kwa kauli moja. Talfik maana yake ni kwamba wakati unapofanya ibada fulani ukaitekeleza katika hali ya kuropoa na kutumia ruhusa na wepesi unaopatikana katika madhehebu zote nne. Ibada hii haitokuwa sahihi kwa madhehebu yoyote kati ya madhehebu manne. Kukusanya ruhusa zilizo katika madhehebu moja ukafuata katika utekelezaji wako wa amali inajuzu.

[Wakati unapofanya ibada ni wajibu kufuata moja kati ya madhehebu manne. Katika kila madhehebu kuna njia nyepesi za kufanya ibada fulani na kuna njia nzito za kufanya ibada hiyo hiyo. Njia nyepesi huitwa **ruhusa** na njia nzito huitwa **azma**. Mtu mwenye nguvu

na ambae hali inamruhusu ni bora kutumia njia nzito katika kufanya amali. Jambo hili linaipa uzito nafsi, kuikandamiza na kuifanya iwe dhaifu. Ibada zimeletwa ili kuidhoofisha nafsi na kuivunjavunja. Kwa sababu nafsi ni adui wa binaadamu na ni adui wa Allah. Lazima kuidhoofisha ili kuipunguza makali yake. Hata hivyo haitakikani kuiua nafsi kikamilifu kwa sababu kwa upande mwengine nafsi pia ni kitumishi cha mwili. Mtumishi jahil na mjinga. Kwa mtu aliye dhaifu, mgonjwa au muda haumruhusu basi ni bora kutumia ruhusa katika ibada zake. Na ikiwa katika ibada hiyo hakuna njia rahisi katika madhehebu yake basi itajuzu kutumia njia rahisi zilizo katika dhehebu nyengine tatu.]

## DHANA MBAYA

24. Ni gonjwa la ishirini na nne. Kudhania kuwa dhambi yako haitasamehewa ni kufanya dhana mbaya (sui dhanni). Kumdhania muumini kuwa ni mtenda maovu (fasik) pia ni dhana mbaya. Kutokumpenda kwa kuwa unajua kuwa ni mfanyaji mambo ya haramu haiwi dhana mbaya. Hii ni kuchukia kwa ajili ya Allahu taala nayo huleta thawabu. Wakati unapoiona aibu ya nduguyo muislamu inafaa kumdhania mema na kujaribu kumuokoa na aibu ile. Fikra inayopita kwenye moyo au wazo haliwi dhana mbaya. Katika maana ya aya ya Suratul hujurat aya ya 12 tunasoma **(Enyi mlioamini! Jiwekeni mbali na dhana, kwani baadhi ya dhana zinapelekea kupata dhambi).** Katika hadithi sharif mtume wa Allah anatueleza yafuatayo **(Msifanye dhana mbaya kwani hiyo itakupelekeeni kwenye maamuzi yasiyo sahihi. Msichunguze mambo ya siri ya watu wengine, mapungufu yao msiyaone, msifanye mabishano, msifanye hasad, msifanye uadui baina yenu, msisemane, pendaneni kama ndugu kwa sababu muislamu ni ndugu wa muislamu mwenziwe. Hamdhulumu bali humsaidia. Hamdhalilishi).** Ni haramu kwa muislamu kumuua muislamu mwengine. Katika hadithi sharif tunasoma **(Muislamu hahujumu mali, nafsi wala heshima ya muislamu mwengine. Allah haangalii miili yenu, nguvu zenu, wala uzuri wenu. Amali zenu pia haangalii. Huangalia mioyo yenu).** Allahu taala anaangalia ikhlas na taqwa tuliyonayo moyoni. Ili ibada ziweze kulipwa na Allahu taala lazima zikamilishe masharti lakini pia zifanywe kwa ikhlas. Ni uzandik kusema kuwa ibada haitizamwi nia yake na kwamba kama itakuwa sahihi matendo yake tu basi inatosha. Ibada, kheri au jambo jema lolote ambalo halikufanywa kwa kutaka radhi za Allah, basi jambo hilo mlipaji wake hatokuwa Allah. Na kusema kuwa (Allahu taala anaangalia moyoni tu, lolote linalofanywa kwa nia njema Allah

atalilipa) ni kauli potofu inayotolewa na baadhi ya mashekhe wapotofu wa tarika.

[Wanafanya maovu na maasi hali ya kudai kuwa mioyo yao ni safi. Wanadai kuwa kila lifanywalo kwa nia njema huwa ni ibada na wema. Watu hawa wenye kuwahadaa waislam na wakajikusanyia muridi, wakawa wanafanya maasi ya wazi kabisa, haifai kuwafuata wala kuwapenda. Hawa kuwasema wazi kuwa ni mafasik haiwi dhana mbaya.]

Katika hadithi sharif tunasoma **(Mdhanieni Allahu taala dhana njema).** Na katika suratu Zumar aya ya 53 katika maana ya aya inasema **(Enyi waja wangu mlioziangamiza nafsi zenu kutokana na wingi wa madhambi! Msikate tamaa na rehema za Allah. Hakika Allah anasamehe madhambi yote. Hakika yeye ni mwingi wa maghfira na rehema).** Ikiwa masharti yote ya toba yatafuatwa basi kufuru na dhambi za aina zote husamehewa. Allahu taala akipenda anaweza kusamehe madhambi yasiyokuwa ya kufuru, bila ya hata mja kuleta toba. Katika hadithi qudsy tunasoma **(Mimi nitamtendea mja kwa namna ile anayonidhania).** Yule ambae ataleta toba hali ya kudhani kwamba Allah anamtakabaliya, basi Allah atamtakabalia toba hiyo.

[Ujumbe ambao Allahu taala anawapa mitume wake wote "swalawatullahi taala alayhim ajmain" huitwa **Wahyi** nao ni wa aina mbili. Ujumbe ambao unafikishwa kwa mitume kupitia kwa Malaika aitwae Jibril kuwafikishia huitwa **Wahyi matluu**. Katika wahyi huu maneno na maana yake, vyote viwili vinatoka kwa Allahu taala. Kur-an Karim ni mfano wa wahyi huu. Aina ya pili ya wahyi ni ile iitwayo **Wahyi ghayri matluu**. Allahu taala huupitisha wahyi huu katika moyo wa mtume wake alayhi salaam, kisha naye huwaeleza wale waliopo kwa kutumia maneno yake. Kauli hii huitwa **Hadithil qudsy**. Maneno yaliyo katika hadithi qudsy ni ya mtume. Katika hali ya kuwa maneno na maana ya kauli, vyote viwili vikawa asili yake vimetokana na mtume, basi kauli hiyo huitwa **Hadithi sharif**.]

Katika hadithi sharif tunasoma **(Kumdhania Allahu taala mema ni ibada)** na katika hadithi sharif nyengine tunasoma **(Ninaapa kwa yule ambae hakuna mola zaidi yake, dua yoyote yenye kuombwa hali ya kumdhania mema Allahu taala basi itakubaliwa)** na katika hadithi nyengine tunasoma **(Siku ya kiama Allahu taala ataamrisha kuwa mja fulani aingizwe motoni. Wakati akipelekwa huko mja atageuka nyuma na atasema "Ewe Mola wangu, mimi duniani daima nilikuwa nikidhani mema kuhusu wewe". Allahu taala ataamrisha asipelekwe**

**motoni na atasema "Mimi nitamlipa kwa namna dhana yake ilivyokua kwangu").**

Muumin ambaye hajulikani kuwa ni mwema au muovu basi ni vyema kumdhania kheri. Iwapo uwezekano wa kuwa mwema au muovu uko sawa basi hiyo huitwa **shaka**. Na iwapo uwezekano hauko sawa, ule upande uliozidi huitwa **Dhana** na ule uliopungua huitwa **Wahmu**.

## KUPENDA MALI

25. Hili ni gonjwa la ishirini na tano. Kuchuma mali kwa njia zisizo za halali ni jambo lililoharamishwa.

Ni makruh kukusanya mali ya halali kuliko uhitaji wake mtu. Na asipoitolea zaka huwa ni sababu ya kuadhibiwa. Hadithi sharif inasema **(Allahu taala anawalaani wale watumwa waliotawaliwa na dhahabu na fedha).** Mtumwa siku zote anajitahidi kumridhisha bwana wake. Kwenda mbio kwa ajili ya kutafuta mali ni uovu zaidi kuliko kukimbilia shahawa za nafsi. Mtu atamsahau Allahu taala kwa ajili ya kutafuta mali basi hayo huitwa **mapenzi ya dunia**. Moyo usiomkumbuka Allah, huwa maskani ya shetani. Moja kati ya njia za shetani ni kumfanya binaadamu akadhani kwamba yale anayoyafanya ni ya kheri kwa hivyo yeye ni mja mwema. Mtu kama huyo huwa ni mtumwa wa nafsi yake. Mtume wa Allah anasema katika hadithi sharif **(Umma zote zilizopita kila moja imepewa fitna yake na fitna ya umma wangu mimi ni kukusanya mali na pesa).** Watu watakimbilia dunia na kuisahau akhera.

Hadithi sharif inasema **(Allahu taala alipoumba dunia, aliwakadiria wanadamu umri wao, ahadi zao za kifo na riziki zao).** Binaadamu riziki yake haibadiliki; haizidi wala haipungui. Na kama ambavyo yeye binaadamu anaitafuta riziki, basi na riziki pia inamtafuta muhusika wake. Kuna mafakiri wengi ambao wanaishi maisha mazuri na ya furaha kuliko matajiri. Wale wenye kushikamana na dini na wakamuogopa Allahu taala, basi yeye huwapa riziki kwa namna wasioitegemea. Katika hadithi Qudsy tunasoma **(Ewe dunia! Yule atakaenihudumia mimi basi wewe kuwa mtumwa wake. Na yule atakae kuhudumia wewe basi mfanyie uzito).** Na katika hadithi sharif Mtume wa Allah anasema **(Ewe Mola! Wale wanaonipenda mimi, wape mali ya kheri. Na wale wanaonifanyia uadui wape mali nyingi na watoto wengi).** Kuna myahudi alikufa akaacha kasri moja na watoto wawili. Wale watoto walishindwa kupatana namna ya kugawana lile

kasri na wakaanza kugombana. Basi mara sauti ikatoka kwenye ukuta na kuwaambia “Msigombane kwa ajili yangu. Mimi nilikuwa mfalme. Nimeishi sana. Ndani ya kaburi nilikaa miaka mia na thalathini. Kisha dongo langu likatengenezewa mtungi ambao ulitumika miaka arobaini ndani ya nyumba. Kisha mtungi huo ukavunjika na mapande yake yakarembewa. Kisha dongo langu likatumika kutengenezea matofali yaliyojengewa ukuta huu. Msigombane bure, nyinyi pia mtakujakua kama mimi.”

Hasan Chelebi “rahimahullahu taala” katika kitabu chake kiitwacho **Mawaqif** anasema: Hadhrat Hasan na Hadhrat Husein wakati wakiwa wadogo waliumwa wote wawili pamoja. Hadhrat Ali na Hadhrat Fatima “radhiyallahu taala ajmain” na binti mtumishi wao wa nyumbani wakaweka nadhiri kwamba watakapopoa hao watoto basi watafunga siku tatu. Basi wakapoa wale watoto nao wakaanza kufunga. Lakini wakajikuta kuwa hawana chakula kwa ajili ya futari ndani ya nyumba yao. Hivyo wakenda wakakopa vibaba vitatu vya ngano kwa myahudi. Siku ya mwanzo Hadhrat Fatima akachukua kibaba kimoja akasaga unga na kutengeneza mikate mitano. Kabla ya kufika wakati wa kufutari akaja fakiri akaomba chakula. Hivyo wakampa hiyo mikate na wao wakalala na njaa. Siku ya pili ya funga yao, bibi Fatima akatengeneza tena mikate lakini akatokea yatima kuomba chakula. Wakampa yeye mikate hiyo nao wakalala na njaa. Siku ya tatu bibi Fatima akitengeneza tena mikate lakini na mara hii akatokea mtumwa na kuomba chakula, nao wakampa yeye hiyo mikate. Allahu taala akashusha aya kuwasifu kwa nadhiri yao na utoaji wao huu. Mtu kubakisha mali kwa ajili ya mahitaji yake ya dharura tu na akaigawa ile ya ziada hiyo huitwa **Zuhud**.

[Kumpa mtu haki yake mau kumlipa deni lake huo ni **uadilifu**. Kumpa mtu zaidi ya haki yake hiyo ni **Ihsan**. Kumtatulia mtu tatizo lake kwa kumpa mali ambayo wewe mwenyewe pia unaihitaji hiyo huitwa **Ithaar**.]

Rakaa mbili zinazoswaliwa na mwanazuoni Zahid ni bora kuliko swala zote zinazoswaliwa na asiekua zahid kwa umri wake wote. Baadhi ya masahaba “radhiyallahu taala anhu ajmain” waliwaambia baadhi ya matabiina: nyinyi mnafanya ibada zaidi kuliko masahaba wa mtume “swallallahu taala alayhi wasallama” lakini kwa kuwa wao walikuwa na zuhd kuliko nyie, wao ni bora zaidi. Kuipenda dunia maana yake ni kutumia njia zisizo halali kwa ajili ya kupata pesa ili kukidhi matashi ya nafsi na mambo mengine yenye kuleta ladha za kidunia. Kuikimbilia dunia ni kukimbilia kivuli kwa sababu madhara ya

matashi ya dunia ni mengi kuliko faida zake. Pia matamu hayo hayabaki, huondoka haraka. Kuyapata pia ni shida. Yale yasio na faida kabisa huitwa mchezo na upuuzi.

[Mambo ambayo anayahitaji mtu ili asife, asipoteze kiungo au asipate maumivu haya huitwa **dharura**. Mambo ambayo anayahitaji kwa ajili ya raha ya mwili na roho, kwa ajili ya kutoa zaka, sadaka, kukopesha, kwenda hija, kuchinja na kufanya mema na mazuri mengine haya huitwa **mahitaji**. Yale yaliyozidi mahitaji basi huwa ni mapambo. Ikiwa kile kilichozidi mahitaji kitatumika kwa kujionesha na kufanya kiburi basi hakitokuwa ni mapambo bali kitakuwa ni haram. Kufanya kazi ili kupata kima kiitwacho dharura ni fardhi. Kufanya kazi kwa kupata kima kiitwacho mahitaji ni sunna na hii huitwa ni **kinaa**. Kufanya kazi ili kumiliki kima kiitwacho mapambo ni halali. Kutumia njia zinazokubalika na dini kwa kuchuma kima kiitwacho mahitaji au mapambo huwa ni ibada. Kinyume chake kama vitachumwa kwa njia zisizokubalika na dini basi itakuwa ni haramu. Kinachochumwa kwa njia hizo huwa ni mambo ya kidunia.]

Katika hadithi sharif Mtume wa Allah anasema **(Mambo ya kidunia yamelaaniwa. Mambo yanayofanywa kwa ajili ya Allah na yale anayoyaridhia hayo hayakulaaniwa).** Mambo ya kidunia hayana thamani yoyote mbele ya Allahu taala. Riziki inayochumwa na kutumiwa kwa kufuata hukumu za Allahu taala haiwi mambo ya kidunia bali huwa ni neema za kidunia. Katika neema za kidunia, iliyo bora kabisa ni mke mwema. Mtu mwenye imani na kufuata maamrisho ya Allahu taala huyo huitwa mja mwema **(salih)**. Mke mwema humlinda mumewe asifanye maovu. Humsaidia kufanya ibada na matendo mema. Mke asie mwema ana madhara. Huwa ni wa mambo ya kidunia. Katika hadithi sharif tunasoma **(Nimependezeshewa katika neema za dunia, wanawake na manukato)** na katika hadithi sharif nyengine Mtume wa Allah anasema **(Lau kama mambo ya kidunia yangekuwa na thamani mbele ya Allah alau ya ubawa wa nzi, basi kafiri yeyote asingepata hata tone la maji).** Makafiri hupewa mali nyingi ambayo inazidi kuwasukumiza kwenye madhara. Katika hadithi sharif tunasoma **(Thamani ya muumini mbele ya Allah inapungua kulingana na wingi wa mambo ya kidunia aliyolimbikiza)** na katika hadithi nyengine **(Mapenzi ya dunia yakiongezeka, madhara ya akhera pia huongezeka. Mapenzi ya akhera yakiongezeka madhara ya dunia nayo hupungua).** Hadhrat Ali "radhiyallahu taala anhu" anasema dunia na akhera ni kama mashariki na magharibi. Kila ukiukaribia upande mmoja basi unazidi kuwa mbali na upande

mwengine. Tumsikilize mtume wa Allah anavyosema katika hadithi sharif zifuatazo: **(Kuyakimbilia mambo ya kidunia ni sawa na kutembea juu ya maji, je kuna uwezekano miguu isirowe? Mambo yenye kuzuia kuufata Uislam huitwa mambo ya kidunia). (Allahu taala akimpenda mja basi humfanya aipe nyongo dunia [Zahid] na aipende akhera. Yeye humtambulisha mapungufu yake). (Mwenye kuipa nyongo dunia hupendwa na Allah. Mwenye kuzipa nyongo mali za wengine hupendwa na watu). (Kuikimbilia dunia ukaipata ni uzito. Kuikimbilia akhera ni wepesi). (Kuipenda dunia ndio msingi wa maasi yote)** yaani inapelekea kwenye kila aina ya makosa na maovu. Mtu mwenye kuitafuta dunia kwanza huanguka kwenye mambo yenye shubha, kisha akaingia katika mambo ambayo ni makruh, tahamaki huanza kufanya yale ya haram na hata kuangukia katika kufur. Sababu ya umati zilizopita kutoiamini mitume yao ni mapenzi ya dunia. Mapenzi ya dunia ni kama mvinyo, mwenye kuunywa huwa hazinduki ila wakati wa mauti. Wakati Nabiyullahi Musa "alayhi salaam" alipokuwa anakwenda kwenye Jabal Tur alimuona mtu akilia mno. Akasema "Ewe mola mja wako analia kwa kukuogopa wewe." Allahu taala akamwambia "Hata alie machozi ya damu huyo sitamsamehe. Kwa sababu huyo ni mwenye kuipenda sana dunia" Katika hadithi sharif Mtume wa Allah anasema **(Mwenye kuchuma halali duniani, akhera atakwenda hesabiwa, Mwenye kuchuma haramu duniani, akhera atakwenda adhibiwa)** na katika hadithi sharif nyengine **(Allahu taala asipompenda mja, humtumilisha mali yake katika mambo ya haramu).** Kujenga nyumba kwa ajili ya kufanya kiburi ni katika hayo. Katika hadithi sharif tunasoma **(Yeyote atakaejenga nyumba kwa pesa za halali basi atapata thawabu kwa muda wote ambao watu wanafaidika na jengo hilo).** Inajuzu kujenga jengo refu kwa ajili ya kukimbia unyevu na kutafuta hewa safi, ila ni haramu kujenga jengo refu kama hilo kwa nia ya kujionesha na kufanya kiburi. Imam adham Abu Hanifa anasema (Nguo na nyumba za wanazuoni na wakuu wa nchi inafaa ziwe za mapambo ili wasitukanwe na majahili na ili wadhihirishe nguvu na azma kwa maadui).

## TASWIF

26. Ni gonjwa la ishirini na sita. Taswif ni kuchelewesha kufanya mambo ya kheri. Kuharakiza kufanya mambo ya kheri ni musaaraa. Hadithi sharif inasema **(Leteni toba kabla hamjafa. Fanyeji mambo mema kabla kizuizi hakijakufikieni. Mkumbukeni sana Allahu taala. Toeni haraka zaka na sadaka. Kwa kufanya hivyo mtapata riziki na msaada wa mola wenu mlezi).** Na katika hadithi nyengine tunasoma

**(Jueni thamani ya mambo matano kabla ya kufikwa na matano mengine. Thamani ya uhai kabla ya kifo, thamani ya afya kabla ya maradhi, thamani ya kuichuma akhera uwapo bado duniani, thamani ya ujana kabla hujazeeka na thamani ya utajiri kabla hujafukarika).** Mtu ambae hatoi zaka na haitumii mali yake kwenye njia ya Allahu taala, hupata majuto makubwa anapofukarika. Katika hadithi sharif tunasoma **(Mwenye kuchelewesha mambo ya kheri atahiliki).**

[Imam Rabbani "rahimahullahu alayhi" aliingia chooni na baada ya muda mfupi aligonga mlango kwa nia ya kumwita mtumishi wake. Yule mtumishi hali ya kudhani kuwa labda amesahau kumuwekea maji au tambara la kujitoharishia alifukuzia mbio kule mlangoni. Baada ya kufika Imam Rabbani alipenyeza shati kwenye mlango akampa na kumwambia "Shati hii mpelekee sadaka mtu fulani" Yule mtumishi akamwambia "Bwana wangu we! Kwahilo si ungelisubiri mpaka ukatoka chooni. Ya nini kujikalifisha kama hivyo!" Imam akamwambia "Fikra ya kulitoa hili shati sadaka imenijia nikiwa chooni. Lau kama ningechelewesha mpaka nitoke, naogopa shetani angenitia wasiwasi na kujaribu kunifanya niache kuifanya amali hii ya kheri."]

## KUPENDA WATU WAOVU

27. Hili ni gonjwa la ishirini na saba. Mwenye kufanya maovu huitwa fasik (mtu muovu). Uovu mkubwa kuliko wote ni kufanya dhulma. Kwa sababu hufanyika hadharani na huhusisha haki ya mja mwengine. Katika surat Ali Imran aya ya 57 na aya ya 140 zinasema katika maana za aya **(Allahu taala hawapendi madhalimu).** Na katika hadithi sharif Mtume wa Allah anasema **(Kumuombea dua dhalim aishi muda mrefu, ni kutaka Allahu taala aendelee kuasiwa).** Sufyan Athawry "rahimahullahu taala" aliulizwa "Kuna dhalim jangwani anahiliki kwa kiu, je tumpe maji?". Akajibu "Msimpe" Ikiwa dhalim anaishi katika nyumba ambayo amemnyanganya mtu mwengine basi ni haramu kuingia nyumba hiyo. Yeyote mwenye kufanya tawadhuu kwa mtu fasik basi hupoteza theluthi mbili ya dini yake. Kwa hivyo yule mwenye kumfanyia tawadhuu dhalim anafaa afahamu tangu sasa vipi hali yake itakuwa siku ya kiama. Kumbusu mkono au kumpigia magoti dhalim ni dhambi. Ila kwa mtu muadilifu inafaa. Abu Ubeyda bin Jarrah alimbusu mkono Hadhrat Umar "radhiyallahu anhuma". Mtu ambae chumo lake kubwa ni la haramu, haifai kuingia nyumbani kwake ukakaa wala haijuzu kumsifu kwa maneno au vitendo. Ila itajuzu kumwendea kwa lengo la kujiokoa nafsi yako au kumuokoa mtu mwengine kutokana na dhulma zake. Wakati uko nae haijuzu kusema

yasio ya kweli mbele yake wala kumsifu. Ikiwa ataonekana kuelekea kwenye haki basi inafaa anasihiwe. Inajuzu wakati anapokujia dhalim kumpokea kwa kusimama ila kwa lengo la kuonesha utukufu wa dini na uovu wa udhalim ni bora kutokufanya hivyo. Ikiwezekana, inafaa kumpa nasaha dhalim. Ni vyema kila wakati kukaa mbali na mtu dhalim. Katika hadithi sharif tunasoma **(Unapozungumza na mnafiki, usimwite "bwana wangu").** Kumpa heshima kafir na dhalim, kumsalimia kwa unyenyekevu na kumwita kwa majina kama Ustadh ni kufuru.

Mwenye kumuasi Allahu taala huitwa **Fasik** na yule mwenye kuwafanya wengine wamuasi Allahu taala na kusababisha kuenea kwa maasi huitwa **Fajir**. Fasik anaejulikana kufanya maasi haifai kumpenda na ni dhambi kumpenda mtu wa bid'a mwenye kueneza itikadi isiyo sahihi na mwenye kuzuia dini isisomwe. Katika hadithi sharif Mtume wa Allah anasema **(Iwapo uwezo wa kumzuia fasik asifanye uovu wake upo, na ikawa hakutokea hata mtu moja kumzuia, basi Allahu taala atawaadhibu watu wote hao duniani na akhera).** Umar bin Abdulaziz "rahimahullahu taala" anasema (Pamoja na kwamba Allahu taala hamuadhibu mtu kwa sababu ya madhambi ya mtu mwengine,lakini ikiwa mtu atafanya maasi mbele ya watu na ikawa wasimzuie basi Allahu taala atawaadhibu wote) Allahu taala alimshushia wahyi mtume Yusha "alayhisalatu wassalam" na akamwambia "Katika kaumu yako watu salih arobaini elfu na watu fasik sitini elfu nitawaadhibu". Yusha akamuuliza "Ya rabbi! Hao mafasik utawaadhibu kutokana na maovu yao. Je hao salih kwa nini unawaadhibu?" Akajibu Allahu taala "Hao ninawaadhibu kwa sababu hawakuchukia yale niliyoyachukia mimi. Walikula na kunywa pamoja na mafasiki." Si lazima kuwaamrisha mema madhalimu na watu wa bid'a ikiwa kwa kufanya hivyo kutasabisha fitna na kuleta dhara kwa mali, nafsi, watoto na Uislam kwa ujumla. Wale wenye kufanya dhambi kwa uwazi kabisa inatosha kuwachukia kwa moyo tu na inalazimu kuwapa nasaha kwa upole na lugha nzuri.

Yeyote ambae anafanya maasi na mambo mazuri hupewa jina kufuatana na wingi wa yale anayoyafanya. Ikiwa yote yako sawa basi atapendwa kwa mazuri yake na atachukiwa kwa maovu yake. Ama yule mwenye kusababisha na wengine kufanya maasi, inabidi azuiliwe na vyombo vya dola.

[Mwenye kufanya amali kwa ajili ya kupata mapenzi ya Allahu taala na akampenda Murshid, huyo huwa mja **salih**. Na yule ambae atayapata hayo mapenzi ya Allahu taala huyo huwa ni **Walii**. Na yule

walii ambae anawasaidia wengine kufikia mapenzi ya Allahu taala basi huyo huitwa **Murshid**. **Misingi ya Uislam ni mitatu: elimu, amali na ikhlasi**. Elimu za kiislam zimegawika sehemu mbili, elimu ya dini na ya sayansi. Wanamageuzi wanaiita elimu ya dini kuwa ni **elimu ya kiskola** na ile ya sayansi wanaiita **elimu ya kimantiki**. Elimu ya dini haiji tu kama kuangukiwa na embe kichwani. Inabidi kujifunza kutokana na maneno na matendo ya Murshid wa uhakika na kujifunza kupitia vitabu vya ahli sunna wa ukweli. Kiama kitakapokaribia Murshid wa kweli hawatopatikana ila kutakuwa na viongozi wa dini wengi walio majahil, waongo na waovu. Hawa hawatofanya shughuli za dini kwa ajili ya kupata radhi za Allahu taala bali watakuwa wanatafuta pesa, vyeo na umaarufu. Watajiweka karibu na watu matajiri na wakuu wa nchi. Tusije tukahadaiwa na wezi hawa wa ndani ya dini. Tujitahidi kusoma vitabu vya maulamaa wa Ahli sunna. Moja kati ya madhambi yenye madhara makubwa kwa wakati wetu na wakati wote ni kuzuia kusomwa dini. Kuangalia michezo ya kipuuzi kunazuia dini isisomwe. Vijana wasiposoma vitabu vya dini wanakuwa majahil na wanaleleka bila dini wala imani. Baba na mama walio waislam inawalazimu kuwaokoa watoto wao na janga hilo. Kwa hivyo inalazimu kuviingiza nyumbani mwao vitabu vinavyoandikwa na Hakikat Kitabevi na kuwalazimisha watoto kuvisoma. Ikiwa baba na mama hawatotekeleza wadhifa wao, basi watoto wao watakuwa makafiri na kuingia motoni.]

## KUWAFANYIA UADUI WANZUONI

28. Hili ndilo gonjwa la ishirini na nane. Kuzidhihaki elimu za kiislam na wanazuoni wa kiislam "rahimahumullahu taala" ni ukafiri. Mwenye kumsema vibaya na kumkashifu mwanazuoni huwa ni kafir aliyeritadi. Inafaa kumchukia mtu kutokana na maasi na bid'a. Kuchukia kutokana na mambo ya kidunia ni dhambi. Kutokuwapenda watu wema pia ni dhambi. Katika hadithi sharif tunasoma **(Mambo matatu yanazidisha imani. Kumpenda Allahu taala na mtume wake kuliko kitu chochote, kumpenda muislamu ambae wewe hakupendi na kuwachukia maadui wa Allahu taala).** Ni lazima kumpenda zaidi muumini mwenye kutekeleza mema mengi zaidi kuliko yule anaetekeleza mema machache. Inalazimika kuwa na chuki zaidi kwa yule kafiri na fasik mwenye maasi mengi zaidi na ambaye anasaidia kuenea kwa maasi. Katika vitu vya mwanzo tunavyotakiwa tuvifanyie uadui kwa ajili ya Allah basi ni nafsi zetu. Inapozungumzwa kuwapenda watu wema maana yake ni wewe kufuata njia yao. Miongoni mwa alama za imani ni kupenda kwa ajili ya Allahu taala na kuchukia kwa ajili ya Allahu taala. Katika hadithi sharif tunasoma **(Miongoni mwa**

**waja wa Allahu taala, kuna waja ambao si mitume ila mitume na mashahidi watawaonea gere siku ya kiama. Hawa ni waja waumini ambao hawajuani, wanaishi mbali baina yao, lakini wanapendana kwa ajili ya Allah).**

Katika hadithi sharif tunasoma **(Binaadamu, huko akhera atakuwa pamoja na ampendae hapa duniani).** Huwezi ukapata penzi la mtu ambae huko nae. Ili kuiweka dini yake mtu kwenye usalama, inalazimu kuwa na marafiki waaminifu walio wema. Mayahudi na manasara wakisema kwamba wakiwapenda mitume "alayhimusallamu wataslimat". Ila hawakufuata njia za mitume na wakachagua njia za makasisi na marahibu wao ambazo hazikuwa sahihi. Hivyo huko akhera hawatokuwa na mitume na wataingia kwenye Jahannam. Katika kitabu chetu kiitwacho **(could not answer)** tumeelezea kwa urefu kuhusu mayahudi na wakristo. Roho zilizotukuka huzinyanyua roho za wapenzi wao na roho zilizodhalilika, huzishusha daraja roho za wapenzi wao. Hivyo ni wapi mtu roho yake itakwenda baada ya kufa, hilo atalifahamu kwa kujitizama ni nani wapenzi wake hapa duniani. Mtu anapenda kwa ajili ya kuitii nafsi na maumbile, kutokana na wema aliotendewa au kwa kutaka radhi za Allahu taala. Wale wapendanao hapa duniani, kwa namna roho zao zinavyoashikiana na kuvutana basi na akhera hali itakuwa ni hiyo hiyo. Anas bin Malik "radhiyallahu anhu" anasema "Hakuna hadithi iliyowafurahisha zaidi waislam kuliko hiyo hadithi iliyotajwa hapo juu." Wale wanaowapenda makafiri, watakwenda nao motoni pamoja. Mtu hawezi kujizuia kufuata njia ya mtu anaempenda. Dalili kubwa ya kumpenda mtu ni kuyapenda ayapendayo na kuyachukia ayachukiayo.

## FITNA

29. Hili ni gonjwa la ishirini na tisa. Fitna ni kusababisha balaa na madhila na kuleta ugomvi baina ya watu. Katika hadithi sharif tunasoma **(Fitna imelala. Allah amlaani yule atakaeiamsha).** Ni fitna kubwa kuwachochea watu waiasi dola au kuasi kanuni zake. Kuchochea fitna ni haramu na ni dhambi kubwa kuliko kumuua mtu kwa dhulma. Kuiasi dola hata kama inadhulumu ni haramu na hata kuwasaidia kuleta uasi wale wenye kudhulumiwa basi pia ni haramu. Madhara na madhambi ya kufanya uasi ni makubwa kuliko madhara na dhambi za dhulma.

Imam kuleta kisomo kirefu katika sala kuliko inavyohitajika ni kuchochea fitna. Iwapo maamuma wote watakuwa wameliridhia hilo haitokuwa kuleta fitna na itakuwa ni jaiz. Viongozi wa dini na

makhatibu kuandika au kuwaidhi mambo ambayo waislam hawatoyafahamu basi pia ni kuleta fitna. Kila mtu aelezwe kwa kiasi ya ufahamu wake. Kuwaamrisha watu kufanya ibada wasiyoiweza nako ni kuzusha fitna. Hata kama ni kauli dhaifu lakini kifaacho ni kuwaamrisha watu yale wanayoyaweza. Inalazimu vile vile tusichochee fitna wakati wa kuamrisha mema. Hakuna amri iliokuja kwamba mtu ajisababishie hatari kwa ajili ya kuamrisha mema. Pia kusababisha madhara kwa dini au kwa watu wengine ni jambo lisilotakiwa. Ila inajuzu kuamrisha mema katika hali ya kujua kwamba inaweza ikakusababishia dhara katika baadhi ya manufaa yako ya kidunia. Hiyo ndiyo jihad. Na ikiwa anajihisi mtu hatoweza kufanya subira kwa hilo basi ni bora kutolifanya. Wakati fitna inapozuka tujitahidi kubaki ndani na kutoonana na mtu. Fitna ikitukumba inabidi kufanya subira.

Katika kitabu chake Imam Rabbany "rahimahullahu taala" juzuu ya pili barua ya sitini na nane anasema: Ewe mtoto wangu, nimeshaandika mara kwa mara kwamba huu ni wakati wa kuleta toba kutokana na dhambi zetu na kumuomba msamaha mola wetu. Katika wakati wetu huu ambao fitna zimeenea, inafaa kujifungia ndani usionane na mtu yeyote. Fitna imekuwa kama mvua na imeenea kila pahala. Katika hadithi sharif mtume wa Allah anasema **(Kabla ya kiama kuja fitna itaenea kila pahala. Dhulma ya fitna itagubika kila pahala kama giza la usiku. Zama hizo basi, mtu atatoka kwake asubuhi hali ya kuwa ni muumini na atakaporudi tayari atakwisha kuwa kafiri. Yule atakaerudi kwake jioni muumin basi asubuhi ataamka hali ya kuwa ameshakuwa kafiri. Wakati huo basi aliekaa ni bora kuliko aliesimama na mwenye kutembea ni bora kuliko anaekimbia. Wakati huo basi vunjeni mishale yenu na kateni pinde zenu na pigeni panga zenu kwenye jiwe. Na akujiapo mtu nyumbani kwako, kuwa kama yule aliye bora miongoni mwa watoto wawili wa Adam).** Wakati masahaba "radhiyallahu taala anhum ajmaina"" waliposikia haya, wakamuuliza mtume "swallallahu alayhi wasallama" ni lipi anawausia waislam wa wakati huo. Mtume akawajibu **(kuweni kama fanicha za nyumba zenu)** na katika mapokezi mengine **(Wakati wa fitna kama huo, msitoke nje ya majumba yenu).** [Hadithi hii iko katika kitabu cha Abu daud na Tirmidhy.] Hivi sasa tunaona namna makafiri wanaoishi katika nchi za kikafiri wanavyowafikishia madhila na mateso waislam katika miji mbali mbali mfano mji wa Negrekut. Wanawadhililisha kwa mambo yasiyoweza kutajwa. Madhila kama haya yataonekana sana katika zama za mwisho. Barua ya sitini na nane maelezo yake yamemalizikia hapa.

Katika muhtasar wa **Tadhkira Kurtuby** imeandikwa hadithi sharif isemayo **(Msisababishe fitna. Fitna inayosababishwa kwa mdomo ni mbaya kama ile inayosababishwa kwa upanga. Fitna inayosababishwa na watu waovu, madhalimu kwa kusengenya, kusema uongo na kuzushia wengine ina madhara zaidi kuliko fitna inayofanywa kwa upanga).** Wanazuoni wote wanakubaliana kuwa haifai kufanya uasi dhidi ya dola na kanuni zake hata katika hali ya kuokoa mali na roho yake mtu. Hadithi sharif inatuamrisha kuwa na subira kwa serikali iliyo dhalim. Anaeleza Imam Muhammad "rahimahullahu taala" kwamba Mtume "swallallahu alayhi wasallama" akisoma dua ifuatayo **(allahumma inny as-aluka fiilil khayrat wa tarkil munkarat wa hubbul masakyn wa idhaa aradta fitnatan fi qawmy fatawaffany ghayra maftun).** Maana ya dua hii ni kwamba (Ewe Mola! Nijaalie niwe mwenye kutenda mema na kuacha mabaya. Unijaalie niwe mwenye kuwapenda maskini. Na utakapotaka kuleta fitna katika jamii basi naomba uichukue roho yangu kabla hiyo fitna haijaja). Imam Kurtubi "rahmetullahi alaih" alisema, kwamba lengo la hadithi hii ni kuonyesha umuhimu wa kukaa mbali na kutossiriki wakati wa fitna inapotokea na kwamba mauti ni bora kuliko kushiriki katika fitna.

Katika kitabu cha **Mishkat** tunasoma hadithi sharif zifuatazo: **(Wakati wa fitna, kuweni pamoja na waislam na kiongozi wao. Msiungane na waasi wala wale walio sahihi. Bakieni hivyo hadi mauti yatakapokukuteni). (Wakati wa fitna, fuateni serikali yenu. Hata kama itakudhulumuni, ichukue na mali zenu basi itiini). (Wakati wa fitna shikamaneni na Uislam. Jiokoeni nafsi zenu. Msitoe ushauri kwa wengine. Jifungieni majumbani mwenu na zifungeni ndimi zenu). (Fitna inapozuka watu wengi huuwawa. Asiejiingiza katika fitna huokoka). (Msichanganyike na wanafitna mtapata utulivu. Na atakaekumbwa na fitna basi afanje subira, atapata utulivu). (Allah atamuuliza mja wake siku ya kiama: wakati ulipomuona mfanya dhambi kwa nini hukumkataza? Mja atajibu niliogopa madhara na uadui wake na nilitegemea msamaha na maghfira yako).** Hadithi sharif hii inaonesha kwamba wakati nguvu za adui zinapofurutu ada basi inajuzu kuacha kuamrisha mema.

Katika sherehe ya **Shir-atul islam** anasema: Kuamrisha mema na kukataza mabaya ni fardhi kifaya. Kuamrisha sunna na kukataza makruh ni sunna. Yule ambaye anafanya ovu hakatazwi kwa mkono bali hukatazwa kwa maneno. Huelezewa madhara ya lile ovu analolifanya. Yule ambaye anajitayarisha kufanya ovu, huyo hukatazwa kwa mkono. Kukataza kwa mkono au mdomo kufanywe katika hali ambayo haitosababisha fitna. Lazima ijulikane kabla ikiwa

kweli kukataza huko kutaleta manufaa. Hata kwa kufikiria basi pia itatosha kuwa ni kufahamu. Ila itakuwa hapana faida ikiwa haikutendwa kwa hisia za kupenda kwa ajili ya Allahu taala na kuchukia kwa ajili ya Allahu taala. Ikiwa kuamrisha mema kutaachwa bila ya udhuru maalum basi dua huacha kukubaliwa na kheri na baraka huhama. Nusra haipatikani katika jihadi na katika matatizo mengine. Mwenye kufanya dhambi siri, hiyo humuathiri mfanyaji pekee. Ila dhambi ikifanywa dhahiri huathiri watu wote. Mtu kutajwa kwa ubaya na mtu mwengine hakumfanyi kuwa ni mbaya. Kumtaja mtu kwa ubaya ni usengenyaji na ni haramu kwa msemaji na msikilizaji. Kumwita mtu kuwa ni muovu inahitaji ushuhuda wako binafsi au ushuhuda wa mashahidi wawili waadilifu, kuthibitisha uovu wake. Mtu anapoona dhambi inatendeka na asiizuie hali ya kwamba uwezo anao hali hiyo huitwa **Mudahana**. Imepokewa katika hadithi sharif kwamba wenye kufanywa mudahana watafufuliwa siku ya kiama hali ya kuwa ni kima na nguruwe. Kuwanasihi viongozi wa nchi walio madhalimu ni moja kati ya jihadi kubwa. Isipowezekana kuwanasihi kwa mdomo basi tuyachukie matendo yao. Mihimili ya dola hukataza kwa vitendo, wanazuoni hukataza kwa mdomo na waislam wengine mioyo yao ikataze (kwa kuchukia). Kuamrisha mema kufanywe kwa nia ya kupata radhi za Allah, jambo alisemalo mtu alijue marejeo yake (kitabu) lilikotokea na afanye hivyo bila ya kusababisha fitna. Si wajibu, bali pia inaweza kuwa haramu kuamrisha mema hali ya kujuwa kuwa haitapatikana faida au itasababisha fitna. Katika wakati kama huo ili kutoleta fitna basi inafaa mtu abakie nyumbani kwake na asiungane na wafitinishaji. Ikiwa kutatokea fitna au ikiwa serikali inafanya dhulma na ufisadi basi ni lazima kuhama katika nchi hiyo. Iwapo itashindikana kuhama basi inafaa kujitenga na kutokujiunga upande wowote au kuchanganyika na yoyote. Ikiwa anahisi kuwa maneno yake hayatoleta faida na yanaweza yakaleta fitna basi kuamrisha mema itakuwa si wajibu bali ni mustahabu. Na iwapo anahisi maneno yake yataleta faida lakini pia yanaweza kusababisha fitna basi pia si wajibu kuamrisha mema katika hali hiyo. Ikiwa fitna yenyewe itakuwa ndogo sana, itakuwa ni mustahabu kuamrisha mema. Iwapo fitna itakuwa kubwa na yenye madhara basi hapo ni haramu kuamrisha mema. Ni wajibu kuamrisha mema kwa upole kwani ukali huleta fitna. Haifai kuwaelekezea silaha wala kuwadhulumu na kuwatesa waislamu na makafiri walio chini ya dhima. Yamekamilia maelezo kutoka kitabu cha **Shir’a.**

## MUDAHANA NA MUDARAA

30. Hili ni gonjwa la thelathini. Mudahana ni kutokumzuia mwenye kufanya haramu hali ya kuwa uwezo wa kufanya hivyo unao. Hii inaweza kutokana na kumuheshimu yule mwenye kufanya haramu au watu walio karibu nae au pia inaweza sababu ikawa ni kuichukulia wepesi dini. Ikiwa haitozua fitna kwa kuleta dhara kwa dini na dunia au kuwadhuru wengine, basi ni lazima kuwazuia wenye kufanya haramu au makruh. Kutokuzuia na kukaa kimya ni haram. Kufanya mudahana ni dalili ya kuridhika na lile linalofanywa. Kukaa kimya ni jambo linalopendeza katika hali zake nyingi ila katika jambo la haki na kheri haitakiwi kukaa kimya. Wakati mtume alipoulizwa "Ewe mtume wa Allah! Katika umma zilizopita kuna walioangamizwa kwa tetemeko la ardhi na wakabaki chini ya ardhi. Ila miongoni mwao mbona mlikuwa na watu wema?" Mtume wa Allah akajibu **(Ndio. Wema pia waliangamizwa kwa sababu wakati Allah alipokuwa akiasia wao walinyamaza na hawakujitenga na waasi).** Katika hadithi sharif nyengine tunasoma **(Baadhi ya watu katika umati wangu watatoka makaburini na sura za kima na nguruwe. Hawa ni wale waliochanganyika na watenda maasi wakawa wanakula nao na kunywa nao)** na katika hadithi nyengine **(Wakati Allahu taala anapompa elimu mwanazuoni, basi pia huchukua ahadi kwake kama anvyochukua kwa mitume).** Kwa maana ya kwamba anachukua ahadi ya kuwa kila inapolazimika hatorudi nyuma katika kuieleza ilmu. Katika hadithi sharif tunasoma kwamba **(Mtu yeyote ambae Allahu taala amemruzuku ilmu na ikawa asiieleze inapolazimika, basi siku ya kiama atavikwa shingoni mwake kikuku cha motoni).** Na tunasoma katika suratul Bakara aya ya 159 katika maana ya aya **(Wale tuliowapa elimu na uongofu kisha elimu yao wakaificha kwa watu, basi hao hulaaniwa na Allah na wengine wenye kulaani).** Tunafahamu katika aya hii kwamba kufanya mudahana ni haramu. Kinyume cha mudahana ni jitihada. Katika suratul Maida aya ya 54 katika maana ya aya inasema **(Wenye kufanya jihadi katika njia ya Allah, hawahofii lawama za wenye kulaumu).** Ili kuonesha jitihada katika dini basi ni wajibu kufanya jihadi kwa ajili ya Allah kwa nafsi, mali, maneno na kalamu. Katika hadithi sharif tunasoma **(Sema ukweli hata kama unauma).** Mtu zahid (alieipa nyongo dunia) mmoja alipowaona watu wakipiga ala za muziki mbele ya khalifa wa nne wa Amawy; Marwan; alizichukua hizo ala za muziki akazivunja. Khalifa akaamuru aingizwe kwenye chumba chenye simba. Alipoingizwa tu chumbani humo akaanza kusali. Wale simba wakamjia na kuanza kumramba. Walinzi

walipoyaona hayo walimtoa na kumrudisha kwa khalifa. Khalifa akamuuliza “Hukupata woga katikati ya simba kama wale.” Akajibu “Hapana, hilo halikupita akilini mwangu. Isipokuwa usiku kucha niliupitisha nikiwaza.” Khalifa akamuuliza “Ulikuwa ukiwaza nini?” Akajibu “Vile ambavyo wale simba walivyokuwa wakiniramba. Mate yao ni najsi au si najsi? Allahu taala amezikubali sala zangu au amezikataa?”

Pamoja na kwamba uwezo unao, kuacha kuamrisha mema na kukataza mabaya kwa kuhofia fitna au kupata dhara wewe mwenyewe au watu wengine, hiyo huitwa **Mudhaaraa** nalo ni jambo lenye kuruhusiwa. Inajuzu kufanya mudhaaraa katika hali ya kwamba moyo unayo azma ya kukataza haramu na katika hali kama hiyo thawabu za sadaka zinapatikana. Unapofanya mudhaaraa ni vyema kuwa na lugha nzuri na uso wenye bashasha. Mudhaaraa unaweza kutumika kama ni mbinu ya usomeshaji. Imam Ghazali rahimahullah anasema “Kuna watu wa aina tatu: Aina ya kwanza ni kama chakula, ni lazima kwa kila mtu na kila wakati. Aina ya pili ni kama dawa, ni lazima kwa baadhi ya wakati. Aina ya tatu ni kama maradhi. Hayahitajiki bali huvamia watu na kuwaambukiza. Kujikinga na watu kama hawa ni lazima kufanya mudharaa.” Mudharaa ni jambo linalojuzu, na baadhi ya wakati ni mustahabu kulifanya. Mtu ambae nyumbani kwake hafanyi mudhaaraa kwa mkewe basi hatopata raha wala utulivu ndani ya nyumba. Siku moja mgeni alifika kwa mtume wa Allah “swallallahu taala alayhi wasallam” nae akasema **(Mkaribisheni ndani. Ni mtu muovu huyo).** Alipofika ndani alizungumza nae kwa upole na bashasha. Alipoondoka aliulizwa kwa nini alizungumza nae kwa upole, nae akajibu **(Watu ambao watapata malazi mabaya sana huko akhera ni wale ambao watu waliwapa heshima hapa duniani ili wajilinde na madhara yao).** Na katika hadithi sharif nyengine tunasoma **(Mtu ambae anafanya mambo ya haramu bila kimeme, kama ambavyo inafaa kumsengenya basi pia inafaa kufanya mudhaaraa kujiepusha na shari zake. Ila mudhaaraa usifanyike kama sehemu ya mudahana).** Mudhaaraa ni kuyatoa muhanga manufaa ya kidunia kwa ajili ya kujinusuru kutokana na madhara. Mudahana ni kuitoa muhanga dini ili kupata manufaa ya kidunia. Wakati unapomfanyia mudhaaraa mtu dhalimu, haifai kumsifu yeye au dhulma anayoifanya.

## INADI NA KUJITUKUZA

31. Hili ni gonjwa la thalathini na moja ambalo ni kukataa ukweli wakati unapousikia. Abu Jahil na Abu Talib walifanya inadi kwa

kutokuuamini na kuukataa utume wa Muhammad „swallallahu alayhi wasallam". Inadi inatokana na choyo, husda, riya au hata tamaa. Katika hadithi sharif mtume wa Allah anasema **(Allah anamchukia sana mwenye kufanya inadi dhidi ya haki).** Na katika hadithi sharif nyengine tunasoma **(Muumini anakuwa wakar na mpole).** Wakar ni yule ambae anawafanyia wenziwe wepesi katika mishughuliko yao ya kidunia. Katika mambo ya kidini anakuwa madhubuti kama jabali. Jabali linaweza kufanya ufa baada ya muda ila muumini katika dini yake hafanyi ufa.

## UNAFIKI

32. Hili ni gonjwa la thalathini na mbili. Unafiki maana yake ni kutofanana kati ya uhakika wa yaliyo ndani na yale yaliyojitokeza nje. Unafiki katika dini maana yake ni kujitangazia uumini hali ya kuwa ndani ya moyo ni kafiri. Unafiki wa kidunia ni kudhihirisha urafiki hali ya kuwa moyoni una uadui. Ukafiri mbaya kuliko wote ni unafiki wa kidini. Mkuu wa wanafiki katika mji wa Madina akiitwa Abdalla bin Ubay bin Sululu. Walipouona ushindi wa waislam katika vita vya Badr, nao wakajitangazia kuwa ni waislamu. Ila uhakika ni kwamba mioyo yao haikuamini. Katika hadithi sharif mtume wa Allah anasema **(Allahu taala na malaika wawape laana wale wenye kuwaonesha waislam urafiki kwa maneno yao lakini wakawafanyia uadui kwa matendo yao)** na hadithi sharif nyengine inasema **(Alama za mnafiki ni tatu: husema uongo, hatekelezi ahadi na hufanya khiyana kwenye amana).** Mtu kama huyu hata kama akisali basi bado ni mnafiki.

## KUTOKUFANYA MAZINGATIO

33. Hili ni gonjwa la thalathini na tatu. Binaadamu anatakiwa kuyakumbuka maasi yake na kuleta toba, na kuyakumbuka mema yake na matendo yake ya utiifu na kumshukuru Allahu taala kwa hilo. Kuzingatia usanii wa hali ya juu, mpangilio na mshikamano ulio katika maumbile yake binafsi na yale ya viumbe wengine kutamuezesha mja kujua kuwepo kwa muumbaji Allahu taala na ukubwa wake. Vile vyote vilivyoumbwa, kwa umoja wake huitwa **Aalam** (walimwengu).

[Aalam ni wa vigawanyo vitatu: **Aalamil Ajsaad** ni vitu vyenye viwiliwili. **Aalamil Arwah** ni ulimwengu wa kiroho. **Aalamil Mithal** ni ulimwengu baina ya viumbe vyenye kiwiliwili na ule ulimwengu wa roho. Huu si ulimwengu wa uwepo wa vitu bali ni ulimwengu wa uonekano wa vitu. Kila kiumbe kina muonekano wake katika ulimwengu huu. Aalamil Arwah ni vitu vilivyo nje ya Arshi. Hivi si vitu

vyenye maumbo yenye kugusika. Hivi pia huitwa **Aalamil amr**. Aalamil Ajsaad ni vitu vyenye maumbo yenye kugusika ambavyo pia huitwa **Aalamil khalq**. Nayo inagawika makundi mawili, dogo na kubwa. Binaadamu ndiyo kundi dogo na viumbe vyote vilivyobaki vinajumuika pamoja katika kundi kubwa. Kila kilicho katika kundi kubwa basi kina mfano na mfanano wake katika kundi dogo. Moyo wa binadamu ni mlango unaofungukia kwenye Aalamil Arwah. Mlango huu umeharibika na kufungwa katika mioyo ya makafiri kwa hivyo makafiri hawana habari juu ya Aalamil Arwah wala hawawezi kuzipata. Njia pekee ya kuupa moyo uhai na kuweza kufunguka kwenye Aalamil Arwah ni kumuamni Allahu taala na kuwa muislamu. Inalazimu kwa muumini kufanya jitihada ili moyo wake uingie katika ulimwengu huu wa roho na kujiboresha ili aweze kudumu humo. **Tasawwuf**; ambayo ni moja kati ya matawi manane ya elimu za kiislam; imejikita katika kutoa mafunzo haya. Wale mabingwa katika fani hii hujulikana kama ni **Walii** na **Murshid**. Murshid alie mashuhuri kabisa ni Imam Rabbany Ahmad Faruk aliyefariki India mwaka 1034 hijria sawa na 1624 miladi.

Haiyumkiniki kwa mtu mwenye akili timamu aliesomea utabibu, akaona namna ya ustadi wa sanaa ya maumbile, mpangilio mzuri na uwiano unaopatikana katika utendaji kazi wake, halafu ikawa asiamini uwepo, ukubwa, elimu na uwezo wa Allahu taala. Asieamini ni mtu asie wa kawaida, mwenye kichwa kigumu, jahil au mwenye inadi, mwenye kufuata hawaya na mtumwa wa nafsi yake au dhalim mwenye kupenda kudhulumu na kutesa wengine. Kama utayaangalia maisha ya makafiri basi utakuta yanaangukia katika hali hizo tulizotaja.]

Hadithi sharif inatwambia **(zingatieni nidhamu ya uumbaji ili mpate imani).** Kwa kusoma astronomi na kuyaona maumbile ya dunia, mwezi na jua na nyota nyengine kwa namna zinavyoelea kwenye anga kwa utaratibu na nidhamu ya hali ya juu na hesabu ya masafa yaliyo baina yao, basi ni lazima imani ya mtu kuongezeka. Katika kuumbwa majabali, mito, bahari, mimea, wanyama na hata vimelea vidogo vidogo kuna faida maalum. Hakuna kilichoumbwa bure bure tu bila ya sababu yoyote. Mawingu, mvua, umesa na radi, maji yaliyo chini ya ardhi na vitu vitowavyo nishati, bali kila kilichoumbwa kina manufaa na wadhifa maalum kinaofanya. Viumbe hivi vyote ambavyo vinatoa huduma kwa binaadamu ni vichache sana ambavyo binaadamu huyu ameweza kuwa na utaalamu navyo hadi sasa. Ikiwa ni vichache tu kati ya viumbe vilivyoumbwa na Allahu taala ndio akili ya binaadamu imeweza kuvichambua basi ni vipi akili hiyo itaweza kumchambua Allah muumbaji! Wale wanazuoni walioweza kuufahamu ukubwa

wake na sifa zake walipigwa na butwaa wakasema "Kumfahamu yeye ni kule kufahamu kutowezekana kufahamika kwake" Mmoja kati ya watu wa kaumu ya Musa "alayhi salaam" alimuabudu Allah kwa miaka thalathini. Kulikuwa na wingu ambalo likimfunika na kumkinga na jua. Siku moja wingu lile lilitoweka na akabaki juani. Alipomueleza mama yake tukio hilo akamwambia pengine kuna dhambi aliyoifanya. Yeye alikana kwamba hana dhambi yoyote aliyoifanya. Mama yake akamwambia "Je hukuangalia mbingu na mauwa? Je ulizingatia juu ya ukubwa wa muumbaji wa vitu hivyo?" Mtoto akajibu "Nimeangalia ila sikufanya mazingatio." Mama yake akamwambia "Basi kuna dhambi gani kubwa kuliko hiyo! Inabidi utubie sasa hivi." Mtu mwenye akili timamu hatakiwi kudharau kufanya mazingatio. Kuna yeyote mwenye uhakika kwamba hadi kesho bado atakuwa yuko hai? Allahu taala hakuumba chochote bila ya faida. Zile faida ambazo binaadamu bado hawajazigundua ni nyingi zaidi ya zile wanazozijua. Mazingatio yako ya aina nne. Kuzingatia usanii wa hali ya juu uliotumika katika kuumba viumbe na faida zao. Hii humpelekea mja kumjua Allahu taala na kumpenda. Kuzingatia malipo mema yaliyoahidiwa, kunampelekea mja kufanya ibada. Kuzingatia juu ya adhabu kali zilizotolewa habari yake, kunampelekea mja kumuogopa Allahu taala na kuto kumtendea uovu mtu yeyote. Kuzingatia neema na ihsan alizofanyiwa hali ya kuwa yeye ameghafilika na kuzama kwenye madhambi kunamfanya mja aone haya kwa mola wake. Allahu taala anawapenda wale wenye kufanya mazingatio juu ya viumbe vilivyo mbinguni na ardhini. Hadithi sharif inasema **(Hakuna ibada kubwa kuliko kufanya mazingatio)** na hadithi nyengine inasema **(Mazingatio ya mara moja ni bora kuliko ibada za miaka sitini).** Mazingatio yameelezwa kwa kirefu na Imam Ghazali katika kitabu chake kiitwacho **Kimyai saada** kilichoandikwa kwa kiajemi.

## KUMUOMBEA MUISLAMU DUA MBAYA

34. Hili ni gonjwa la thalathini na nne. Katika hadithi sharif tunasoma kwamba **(Msiziombee nafsi zenu na watoto wenu dua mbaya. Ikubalini kudra ya Allah. Ombeni dua Allah akuongezeeni neema).** Na katika hadithi nyengine tunasoma **(Dua mbaya ya baba na mama kwa mtoto wao na dua mbaya ya mtu aliyedhulumiwa kwa dhalim huwa haikataliwi).** Mwenye kumuombea muislamu awe kafiri basi atakuwa kafiri yeye mwenyewe. Kumuombea dhalim afe kafiri ili akapate adhabu isio na mwisho sio ukafiri. Nabiyullahi Musa aliomba dua kama hiyo na ikatajwa ndani ya Kur-an Karim. Imam adham Abu Hanifa "rahimahullahu taala" ameeleza kuwa kumuombea dua

muislamu awe kafiri ni ukafiri. Kumuombea dua mbaya asiekuwa dhalim ni haramu. Inafaa kumuombea dua dhalim kwa kiasi ya udhalimu wake. Kima cha kujuzu kwa jambo ni kiasi ya lile kosa. Ni bora zaidi kutokumuombea dua mbaya dhalim, kufanya subira au hata kumsamehe. Kafir aliye chini ya dhima, au kafiri mwengine yeyote kumuombea Allah ampe umri mrefu haifai. Itajuzu kumuombea umri mrefu ilia pate muda wa kusilimu au kuendelea kulipa jizya kwa waislam. Mwenye kumsalimia kafiri kwa unyenyekevu naye huwa kafiri. Kutumia neno lenye kutukuza kwa kafiri (mfano: ustadh) pia ni ukafiri.

## KUMPA JINA BAYA MUISLAMU

35. Hili ni gonjwa la thalathini na tano. Kumbandika muislamu jina baya au kumwita kwa jina baya alilobandikwa na wengine sio jaiz. Hüseyn Hilmi Isik "rahmetullahi alayhi" la Siddik Gümüs. Katika hadithi sharif tunasoma **(Mwenye jina baya alibadili kwa lililozuri).** Mfano Asiya abadilishwe aitwe Jamila. Inajuzu kumbandika muislamu jina zuri. Haipendezi kuwaita watoto majina yenye maana ya sifa kama Rashid na Amin. Majina kama Nurudin na Muhyidin, yana uongo na bid’a. Kuwaita mafasik, majahil na murtad kwa majina kama hayo ni makruh kwa sababu hayo ni majina yaliyobeba sifa. Hawawezi kuitwa hata kwa majaaz. Imesemwa kwamba inajuzu kuwaita watoto kwa majina haya ili majina yawaathiri na yawapelekee kuwa na sifa kama yalivyo hayo majina. Wanazuoni wema walio mashuhuri kuwataja majina yao kwa kuambatanisha na majina haya inajuzu na ina faida.

[Ibn Abidin “rahimahullahu taala” katika juzuu ya tano ya kitabu chake anasema kwamba jina lililo bora kabisa ni Abdullah, kisha Abdulrahman, kisha Muhammed, kisha Ahmed, kisha Ibrahim. Kuita baadhi ya majina ya Allahu taala kama Ali, Aziz na Rashid pia inafaa, ila wakati majina haya yanapoitwa lazima yaitwe kwa heshima. Kuyatovukia adabu majina haya kwa kukusudia ni ukafiri. Mfano jina la Abdulkadir kuliita Abdulkoydu, Hassan kuliita Hasso, Ibrahim kuliita Ibo, hii ni kuyadhihaki majina haya. Pamoja na kwamba kuyaita hivyo majina haya bila ya kukusudia kuyadhihaki si kufuru, linalofaa ni kuepuka mambo ambayo yanafanana na kufuru. Ikiwa mtoto atakufa mara tu baada ya kuzaliwa, haifai kuzikwa bila ya kupewa jina. Jina la Abdulnabii pamoja na kwamba linajuzu kuita, ni vyema kuliepuka. Hadhrat Sayyid Abdulhakim Arwasy, alikua akitoa mawaidha kila siku ya Jumanne, Alhamisi na Jumamaosi baada ya sala ya laasiri katika msikiti wa Beyazit, kwa muda wa miaka ishirini na tano hadi alipokufa mwaka 1362 hijria [1943 miladi]. Katika moja ya waadhi wake alisema

“Mtoto ana haki tatu kwa wazee wake. Anapozaliwa kupewa jina zuri la kiislam. Anapopata akili kufunzwa kuandika elimu na sanaa. Anapobaleghe kutafutiwa mchumba mwema muislamu mwenye dini na tabia njema na kumuozesha” Ni thawabu kubwa kwa wazee, jamaa bali hata kwa majirani kuwatafutia watoto wa kike wachumba sahihi. Hivi leo huko Ulaya na Amerika, wanatolewa watu waliokosa malezi, wasio na nasabu, maadui wa Uislam, waliopewa vyeti bandia na kubandikwa vyeo vya profesa. Watu hawa hutumwa kwenye nchi za kiislam na kufanywa walimu kwenye skuli za sekondari na vyuo vikuu. Vijana wetu wanaoathirika na kuanguka kwenye mitego ya watu hawa hubakia hawana dini wala madhehebu. Vijana hawa ni tishio kwa taifa na huweza kufanywa mahaini na wauaji kwa wepesi.]

## KUKATAA KUTOA MSAMAHA

36. Hili ni gonjwa la thalathini na sita. Kukataa kutoa msamaha wakati muislamu mwenzio anapokuomba ni makruh. Katika hadithi sharif tunasoma **(Kukataa kutoa msamaha wakati muislamu mwenzio anapokuomba ni dhambi).** Kukubali samahani na kusamehe makosa ni katika sifa za Allahu taala. Yule asiejipamba na sifa hizi Allahu taala humughadhibikia na atamuadhibu. Kuna njia tatu za kuomba msamaha. Kujilaumu kwa kusema “Kwa nini nimefanya!” au kusema “Nimefanya kwa sababu fulani, laiti nisingefanya.” Au kusema “Nimefanya kweli. Sitarudia tena”. Pia unaweza kukanusha kuwa hukufanya. Kukiri kuwa umefanya na kwamba hutarudia tena ni njia ya kuleta toba. Muumini huwa anasubiri aombwe msamaha ili asamehe. Mnafiki huwa anapenda aibu za mwengine zienee. Katika hadithi sharif mtume wa Allah anasema **(Kuweni wenye heshima. Msifanye vitendo vichafu. Wanawake wenu pia wafanyeni wawe na heshima)** na katika hadithi nyengine **(Ikiwa nyinyi mtajiheshimu basi wanawake wenu pia watajiheshimu. Kama mtawafanyia ihsan baba zenu na mama zenu basi nanyi watoto wenu watakufanyieni ihsani. Yule ambaye hatakubali kutoa msamaha kwa ndugu yake muislamu basi hatokunywa katika hodhi la Kawthar).** Hadithi sharif hii inamhusu yule muislamu ambae hajui kuwa nduguye muislamu amefanya kosa, wala hajui kuwa huwo msamaha anaouomba ni wa uongo. Kwa sababu kutomkubalia msamaha wake mtu kama huyu ni kumdhania vibaya. Ikiwa atajua kuwa msamaha anaoutaka ni wa uongo na akamkubalia basi huko ni kusamehe ambako katika hali hii ni mustahab na wala si wajibu.

## KUITAFSIRI KUR-AN KARIM KWA MAKOSA

37. Kutafsiri maana yake ni kukashifu na kuweka wazi, kutambulisha na kuelezea. **Taawil** maana yake ni kurejea. Tafsiri ni kukipa maana kitu. Taawil maana yake ni kuchagua maana moja kati ya maana nyingi zilizopo. Haijuzu kutafsiri kwa uoni na rai binafsi. Tafsiri inafanywa kwa kufuata mapokeo na taawil inafanywa kwa uwezo binafsi wa upambanuaji. Katika hadithi sharif tunasoma **(Mwenye kuielezea Kur-an Karim kwa mtizamo wake binafsi atakuwa amefanya makosa hata kama atapatia).** Ni makosa kutafsiri Kur-an Karim kwa mtu ambae hana elimu ya yale mambo muhimu yanayotakiwa kuyajua ili kuweza kuitafsiri Kur-an Karim. Miongoni mwa hayo ni kujua habari zilizokuja kutoka kwa mtume wa Allah „swallallahu alayhi wasallam“ na masahaba „radhiyallahu anhum“, tafsiri zilizotoka kwa wanazuoni na mtindo wao wa kutafsiri, lahaja ya makureshi, hakika na majazi, mujmal na mufaswal, kuweza kupambanua umumy na khususy, kujua sababu za kushushwa kwa aya na nasikh na mansukh. **Tafsiri** maana yake ni kufahamu makusudio yaliyomo ndani ya maneno ya Allahu taala. Hata kama maana itakayoletwa itakuwa sahihi, ikiwa njia iliyotumika sio sahihi basi hilo ni kosa. Na kama maana itakayotolewa itakuwa si sahihi basi hiyo ni kufur. Kuitaja hadithi sharif kabla ya kuijua kuwa ni sahihi au si sahihi ni dhambi, hata kama itatokea kuwa sahihi. Kunukuu hadithi sharif kutoka kwenye vitabu vya wanazuoni wa hadithi ni lazima kwanza uwe umepata ijaza kutoka kwa wanazuoni wa hadithi. Hadithi sharif inasema **(Mwenye kutunga maneno kisha akadai kuwa ni hadithi, atapata adhabu katika moto wa Jahannam).** Pia si sahihi kuchukua tafsiri kutoka vitabu vya tafsiri ya Kur-an Karim na kueleza au kuandika bila ya kupata ijaza ya wanazuoni wa tafsiri. Ila yule aliyekamilisha masharti ya kutafsiri tuliyoyaeleza hapo juu, anaweza kunukuu tafsiri na hadithi bila ya kupata ijaza ya kimaandishi. Haisihi kutoa ijaza kwa malipo ya pesa. Wale waliokamilisha masharti ni wajibu kuwapa ijaza. Kuwapa ijaza wasio na viwango ni haram.

Katika hadithi sharif tunasoma **(Yule mwenye kutafsiri Kur-an Karimi hali ya kuwa si mtaalamu wa hilo basi atapata adhabu ya moto)** na katika hadithi sharif nyengine **(Mwenye kutafsiri Kur-an Karim kwa mtizamo wake binafsi basi atapata adhabu ya Jahannam).** Watu wa bid'a hufanya hivyo ili kuthibitisha itikadi zao zilizo batili. [Mashia, mawahabi, kikundi cha tabligh, wafuasi wa Mawdudy na wafuasi wa Sayyid Kutub ni mfano wa makundi hayo. Yusuf Nabhany „rahimatullahi aleyh“ ameelezea kwa kirefu juu ya tafsiri kama hizi

katika kitabu chake kiitwacho **Shawahidul hak.** Hali ni hiyo hiyo kwa wale wazandik wanaotoa maana ya Kur-an Karim kwa mitizamo yao binafsi, na wakaleta madai kuwa mbali ya hii maana ijulikanayo, Kur-an Karimi ina maana nyengine ya ndani. Kuna na wale ambao maana ya maneno ya Kur-an Karim huyatafsiri hali ya kuyabadilisha eti kufuatana na wakati, hali na mahali.

Miongoni mwa wanazuoni wa dola ya Uthman, Nuh bin Mustafa Konewy „rahimahullahu taala" aliekufa Cairo mwaka 1070 hijria [1660 miladia] alitafsiri kitabu kiitwacho **Milal wa Nihal** kilichoandikwa na Muhammad Shihristan. Katika tafsiri hiyo anasema: Kundi la **Ismailiya** wamechukua jina hilo kutoka kwa mtoto mkubwa wa Imam Jaffar Sadik ambae akiitwa Ismail. Kundi hili pia huitwa **Batiniyya** kutokana na madai yao kwamba mbali ya hii maana ya wazi, Kur-an Karim pia ina maana ya ndani. Maana ya batin wanasema ni kwamba Kur-an Karim ina maana ya ndani, ni bahari isiyo na mipaka. Wakaiacha maana ya dhahiri wakafuata maana waliyoibuni wao wenyewe na kuiita maana ya ndani. Na la uhakika ni kwamba mtume „swallallahu alayhi wasallama" alikwishaieleza maana iliyo dhahir na wazi ya Kur-an Karim. Kuiacha maana hiyo na kubuni maana nyengine ni ukafiri na uzandik. Kwa kutumia hila hiyo wanajaribu kuupiga vita Uislam. **Majusi** (waabudia moto) katika kuuzuia Uislam usienee, kiongozi wao Hamdan Kurmut alianzisha fikra ya kibaguzi na kuunda dola ya **Karamita**. Waliwaua mahujaji na kuliondoa Hajaril Aswad kutoka Kaaba na kulipeleka Basra. Walisema kwamba pepo ni kufaidi ladha za dunia na moto ni kushikamana na mafunzo ya dini. Mambo ya haram wakayapa jina la sanaa njema. Yale maovu na machafu yaliyokatazwa na Uislam wakayahudhurisha mbele ya vijana kama mafunzo ya morali na kuwatumbukiza vijana kwenye uovu. Dola yao iliudhuru sana Uislam.Katika mwaka 372 hijria [983 miladia] ghadhabu za Allahu taala ziliwashukia na wakatoweka.]

Tafsiri ni lazima ifanywe kwa misingi ya mapokezi. Ili kuweza kufanya tafsiri ni lazima kujua elimu kumi na tano zifuatazo: Lugha, nahw, sarf, Ishtiqaq, maan, bayaan, badii, kiraa, usulidyn, fikh, asbabu nuzul, nashi na mansuh, usuli fikhi, hadithi na ilmul qalb. Haijuzu kwa mtu asie na elimu hizi kutafsiri Kur-an Karim. **Mawhiba** au **Ilmul qalb** ni elimu ambayo Allahu taala anawapa wanazuoni wachamungu bila ya kupitia mtu wa kati. Katika hadithi sharif tunasoma kwamba **(Yule mwenye kufanya amali kwa kutumia elimu yake, Allahu taala humfunza yale asiyoyajua).** Asie na hizo elimu kumi na tano zilizotajwa hafai kutafsiri Kur-an Karim na kama atatafsiri basi atakuwa

anatafsiri kwa muono wake binafsi na atastahiki kwenda kupata adhabu ya Jahannam. Hadithi Sharif inasema **(Atakayemuabudu Allahu taala siku arobaini kwa ikhlasi, basi Allahu taala ataujaza moyo wake hekima. Na hekima hiyo atakuwa akiieleza).** Wenye kutafsiri aya mutashabih wanatafsiri kwa uoni wao binafsi. Tafsiri ya watu wa bid'a iko hivyo.

Elimu iliyomo ndani ya Kur-an Karim ni mafungu matatu. Fungu moja Allahu taala hakumtambulisha yeyote kati ya waja wake. Uhakika wa dhati yake na sifa zake na mambo ya ghaib yanaingia katika fungu hili. Fungu la pilli ni zile siri alizomfungulia mtume wake pekee. Haya ni yale mambo ambayo Mtume „swallallahu alayhi wasallama" aliwatambulisha wale tu ambao aliruhusiwa na Allah kuwatambulisha. Fungu la tatu ni lile ambalo Allahu taala amemfungulia mtume wake na kumtaka awafunze watu wote. Fungu hili nalo lina vigawanyo viwili. Kigawanyo cha kwanza ni yale mambo ambayo kujifunza kwake ni kwa kusikia tu. Mfano wa hili ni kiama na hali zake. Kigawanyo cha pili ni kile kinachotegemea kusoma ukafahamu maana na kuona ukazingatia. Elimu ya Uislam na imani inaingia katika kigawanyo hichi. Hata wale maimamu mujtahid, walishindwa kufahamu kwa uhakika maana ya baadhi ya Nass ambazo hazikuwekwa wazi na matokeo yake wakahitilafiana. Na kutokana na hilo yakapatikana madhehebu mbali mbali katika utekelezaji wa amali. Maana ya Kur-an Karim wanayoitoa wale wenye sifa kumi na tano zilizotajwa haiitwi tafsiri bali huitwa **taawil** kwa sababu ndani ya maana hizo kuna rai zao. Yaani kutokana na maana kadhaa alizofahamu alitumia rai yake kuchagua moja. Maana aliyochagua ikiwa haikuwiana na maana ya wazi ya Kur-an Karim na hadithi au haikukubaliana na chaguo la Ijmaa basi maana hiyo huwa ni mbovu (fasid). Mwishoni mwa kitabu cha **Barika** wakati muandishi alipokuwa akielezea uharamu wa kucheza ngoma, alieleza (Hatukuamrishwa kufanya amali kwa kufuata vitabu vya tafsiri. Tumetakiwa tufuate vitabu vya fikh).

## KUFANYA HARAMU KWA MSISITIZO

38. Kufanya haramu kwa makusudi, hata kwa uchache, huko ni kufanya msisitizo. Kukusudia huja kwa kutia nia, kutaka na kuamua. Kupitisha uamuzi na kufanya hata kama itakuwa ni mara moja basi huwa msisitizo. Ikiwa mara kwa mara atakusudia mtu na kuamua lakini asilifanye hilo jambo, hio haitokuwa kufanya msisitizo. Ikiwa mtu atakusudia mara kwa mara na kutenda kisha akajuta na kuleta toba basi hio haitokuwa kufanya msisitizo. Kama atarejea kufanya tena na

akaleta toba tena pia haitokua kufanya msisitizo. Kama mtu ndani ya siku moja atarejea kosa mara kadhaa lakini ikawa kila afanyapo analeta toba, hiyo nayo haitokuwa kufanya msisitizo. Kila afanyapo toba ni lazima ajute kwa dhambi alioifanya, aache mara moja kufanya hiyo dhambi na akusudie kuto kuirejea tena dhambi hiyo. Kuleta toba kwa ulimi tu bila kupatikana haya masharti matatu, inakuwa ni toba ya uongo. Kufanya msisitizo katika dhambi ndogo huwa ni dhambi kubwa na inaipita dhambi kubwa iliyofanywa mara moja tu. Inapofanyika toba, dhambi kubwa pia husamehewa. Kuzichukulia wepesi dhambi ndogo hiyo ni dhambi kubwa. Kitendo cha kuzungumzia na kusifia namna ulivyotenda dhambi ndogo nayo pia ni katika dhambi kubwa. Ni dhambi kubwa kumuhisabu katika kundi la alim na la watu wema, yule mwenye kufanya dhambi ndogo. Hata ufanyapo dhambi ndogo, inapasa kuogopa sana adhabu za Allahu taala. Ikiwa hutomuonea haya Allahu taala na kuogopa adhabu zake basi huwa dhambi kubwa.

## KUSENGENYA

39. Hili ni gonjwa la thalathini na tisa. Kumzungumza muumin au asie muumin alie chini ya dhima hali ya kuwa mwenyewe hayupo, kwa lengo la kumtia ubaya hiyo huitwa **Ghiba** (usengenyaji). [Ikiwa jambo alilotiliwa ubaya analo kweli basi hiyo ndiyo ghiba na kama hana basi hiyo ni **Iftiraa** (uzushi, singizio). Kama ambavyo kusengenya na kuzusha ni dhambi kubwa kwa msemaji, basi pia ifahamike kuwa ni dhambi kubwa kwa msikilizaji vile vile. Msemaji na msikilizaji wataadhibiwa katika moto wa Jahannam. Ni wajibu kumnyamazisha msemaji na kama hakunyamaza ni wajibu kunyanyuka mahali hapo na kuondoka na kuwatakia dua njema wazungumzaji.] Ghiba ni haram. Ikiwa msikilizaji hamjui anaezungumzwa hiyo huwa siyo ghiba. Mwenye kufanyiwa ghiba huhuzunika. Ikiwa yatatajwa mapungufu yaliyo katika mwili wake, nasabu yake, mwenendo wake, kazi zake, maneno yake, dini yake, dunia yake, mavazi yake nyumba yake bali hata mnyama wake wakati hayupo, bila shaka atapata huzuni atakaposikia. Kusema kwa mafumbo, ishara, vitendo au maandishi ni sawa na kumwambia mtu kwa mdomo. Wakati yanapotajwa mapungufu ya mtu, halafu wale watu wa dini waliopo, wakasikiliza na wakamalizikia kusema "Alhamdulillah, sisi hatuko hivyo" basi hiyo nayo ni daraja kubwa ya ghiba. Wakati anazungumzwa mtu ukasema "Alhamdulillah, Allah sisi hakututoa haya kama hivyo" kwa lengo la kumtia ubaya anayezungumzwa basi pia ni ghiba mbaya sana. Kumtaja mtu kuwa ni mzuri sana kisha ukaengeza kusema kuwa lau kama angekuwa hana mapungufu fulani angezidi kuwa mzuri, hio pia ni aina ya ghiba.

Tunasoma katika Suratul Hujuraat aya ya 12 katika maana ya aya **(Na msisengenyane).** Ghiba imefananishwa na kula nyama ya mtu aliekufa. Katika hadithi sharif tunasoma **(Siku ya kiama daftari la mtu litafunguliwa. Mja atasema "Mola wangu! Wakati nilipokuwa duniani nilifanya amali fulani. Naona humu haikuandikwa" Nae atajibiwa kuwa hayo yamefutwa kutoka katika daftari lake na ameandikiwa yule aliemsengenya).** Na katika hadithi sharif nyengine **(Atakuja mtu siku ya kiama na atakapofungua daftari lake la mambo mema akute amali ambazo hakuzifanya duniani. Ataelezwa kwamba hizo zimetoka kwa wale waliomsengenya duniani).** Anasema Abu Hurayra "radhiyallahu anhu" kwamba "Tulikuwa tumekaa na Mtume wa Allah "swallallahu alayhi wasallam" siku moja. Mmoja wetu akasimama na kuondoka. Ikasemwa: Ewe Mtume wa Allah, hali yake si nzuri ndio akondoka" Akasema Mtume wa Allah **(Rafiki yenu mmemsengenya. Mmekula nyama yake).** Anahadithia Aisha "radhiyallahu anha" kwamba siku moja nilikuwa na mtume wa allah "swallallahu alayhi wasallam" na nikamueleza kuwa mwanamke fulani ni mrefu. Akaniambia **"Tema kilichomo mdomoni mwako".** Nikatema na kikatoka kipande cha nyama mdomoni mwangu. Allahu taala ni mwenye uwezo wa kuonesha sifa na miundo katika hali ya maumbo kwa namna atakavyo. Kusengenya ni kutaja mapungufu ya nduguyo muislamu au asie muislamu anaeishi chini ya dhima, hali ya kuwa hayupo, kwa jambo ambalo akilisikia hatopendezewa nalo. Allahu taala alimpa wahyi Musa "alayhi salaam" na kumwambia (Mwenye kusengenya halafu akaleta toba atakuwa ni wa mwisho kuingia peponi. Mwenye kusengenya halafu asilete toba atakuwa ni wa mwanzo kuingia kwenye Jahannam). Ibrahim Adham "rahimahullahu taala" alialikwa chakula. Baada ya kukaa, ikawa mmoja kati ya waalikwa bado hajafika na akasema mtu mmoja "Yule ni mzito kidogo". Ibrahim Adham "rahimehullahu taala" hapo hapo alinyanyuka na kuondoka na kusema kwamba huyo bwana amesengenywa. Katika hadithi sharif tunasoma kwamba **(Mapungufu anayotajwa nayo mtu ikiwa anayo huwa ni ghiba, na ikiwa hana inakuwa ni uzushi).** Kutaja mapungufu yake katika dini mfano kusema hasali, anakunywa pombe, anaiba au mfitinishi na kumtaja kwa mambo ya kidunia mfano kumtaja kuwa kiziwi au mwenye makengeza zote huwa ni kusengenya. Mapungufu ya kidini kama yatatajwa kwa nia ya kumtaja kwa ubaya itakuwa ni ghiba na kama yatatajwa kwa nia ya kutafuta njia ya kumnasihi itakuwa si ghiba. Kusema kwa lengo la kumsikitikia mtu pia si ghiba. Kuzungumza kwa ujumla kwa mfano kusema, hapa kijijini kuna asie

sali, au kuna mkoministi au kuna mwizi haitokuwa ghiba kwa sababu hakutajwa mtu maalum.

Mtu anaweza akawa anasali na kufunga lakini pia anawadhuru watu kwa mkono wake kama kuwapiga kuwanyanganya au kuwaibia mali zao, au anawadhuru kwa mdomo wake kama kuwasingizia kuwasengenya na kuwafitinisha. Makosa yenye kufanywa hadharani kuyataja sio ghiba. Wala sio dhambi kuyaripoti makosa kama haya kwa vyombo husika ili hatua zichukuliwe. Ikiwa mtu anafanya haram kwa siri na ukajua kuwa baba yake akijua anaweza kumzuia, basi kumjulisha baba yake kwa mdomo au kimaandishi si ghiba. Lakini ikiwa unajua kuwa hatoweza kumzuia basi haitofaa kumwambia kwa sababu hilo litasababisha uadui wa bure. Kutaja maovu ya mtu kutokana na kumhurumia yeye au kuwalinda wengine na madhara yake haiwi ghiba. Ila kumtaja kwa lengo la kumtia ubaya ndio ghiba. Katika hali sita zifuatazo, itakuwa si ghiba kutaja maovu ya mtu: kwa kumhurumia mtendaji, kwa kuwaepusha wengine na madhara, kwa lengo la kumzuia, kwa ajili ya kutafuta fatwa, ikiwa amepewa jina kutokana na jambo fulani kutumia hilo jina na kutaja maovu na bida'a zenye kufanywa wazi wazi. Kumtaja mtu kwa uovu kutokana na kughadhibika pia ni ghiba. Mali inayouzwa kuitaja mapungufu yake kwa mnunuzi huwa si ghiba kwa muuzaji. Kumtajia mwanamme mapungufu ya mchumba anaetaka kumuoa si ghiba bali ni nasaha. Kumnasihi mtu kwa jambo asilolijua ni wajibu. Mtu ambae anafanya haram fulani hadharani, kuyataja mambo yake mengine ambayo hayafanyi hadharani basi hiyo ni ghiba. Hadithi sharif inasema **(Sio ghiba kusema mambo ya mtu aliejivua jokho la haya).** Kujivua jokho la haya maana yake kufanya maovu hadharani. Hadithi sharif inamtaja mtu huyo kuwa amekosa haya. Imam Ghazali na baadhi ya wanazuoni "rahimahumullahu taala" wanasema kwamba ghiba ni kule kutaja mapungufu ya mtu tu na wala haishurutishi kuwa unamtaja kwa nia ya kumtia ubaya.

Hivyo inalazimu kujiepusha sana na kusengenya. Mambo yanayomfanya mtu kusengenya ni mengi. Hapa tutayataja mambo kumi na moja yenye kumpelekea mtu kusengenya: uadui dhidi ya mtu mwengine, kuunga mkono fikra za wengine, kumtia ubaya mtu asiependwa, kutambulisha kuwa dhambi fulani wewe huna, kujionesha kuwa uko bora kuliko mwengine, husda, kuchekesha wengine, kufanya mzaha, kumdhihaki mtu mwengine, kuonesha mshangao juu ya haramu anayoifanya mtu usiemtegemea na

kutambulisha huzuni na huruma zako, kuelezea chuki zako dhidi ya mtu mwenye kufanya haram.

Ghiba humsababisha mtu kupungua thawabu zake na kupewa dhambi za mtu mwengine. Hili inataka kila wakati mtu alikumbuke ili aweze kujizuia na kufanya ghiba.

Ghiba ziko za aina tatu. Aina ya kwanza ni pale mtu anaposema "Mimi sisengenyi. Ninayasema yaliyopo tu". Kusema hivyo ni kufur kwa sababu lile lijulikanalo kuwa ni haramu unakuwa umelihalalisha. Ya pili ni kusengenya na akasikia yule aliesemwa. Hii ni haramu kubwa. Inalazimu kuleta toba na kumuomba msamaha yule aliesemwa. Ya tatu ni kusengenya bila ya habari kumfikia yule aliesemwa. Hapa inalazimu kuleta toba na kumuombea dua ya kheri yule uliemsema.

Iwapo unamsikia mtu anasengenya ni wajibu kumzuia. Katika hadithi sharif tunasoma **(Yeyote atakaemsaidia nduguye muislamu bila ya yeye kuwa na habari, basi Allahu taala nae atamsaidia duniani na akhera).** Na katika hadithi sharif nyengine **(Yeyote ambae anamsikia ndugu yake muislamu anasengenywa, ikawa uwezo wa kuzuia anao lakini asifanye hivyo, basi dhambi zake zinamtosha duniani na akhera).** Na katika hadithi sharif nyengine **(Yeyote yule atakaelinda heshima ya nduguye muislamu isivunjwe, Allahu taala nae atampelekea malaika atakaemlinda na adhabu ya moto).** Na katika hadithi sharif nyengine **(Yeyote atakaeilinda heshima ya ndugu yake muislamu isivunjwe, Allahu taala nae atamkinga na moto wa Jahannam).** Wakati usengenyaji unafanyika ikiwa hukuuzuwia kwa mdomo ukiweza au alau kuchukia kwa moyo, basi nawe utapata sehemu ya dhambi ya ovu hilo. Ima amkatishe maneno msemaji au aondoke sehemu hiyo. Kukataza kwa mkono, kichwa au macho haitotosheleza, ni lazima amtake msemaji anyamaze.

Kafara ya ghiba ni kujuta, kuleta toba na kumtaka msamaha aliesemwa. Kuomba msamaha hali ya kuwa huna majuto ni riya ambayo pia ni dhambi. [Kumsengenya maiti au kafiri alie chini ya dhima pia ni haramu. Hayo ameyataja Ibn Abidyn katika kitabu chake juzuu ya tano ukarasa wa 263.]

## KUTOKULETA TOBA

40. Hili ni gonjwa la arobaini. Toba ni kujutia haram uliyoifanya, kumuogopa Allahu taala na kuazimia kutokufanya tena. Kujuta kwa kuogopa kufikwa na maafa ya kidunia hio haiitwi toba. Ni sahihi toba ya mtu ambae anafanya aina nyingi za madhambi akaleta toba kwa

baadhi na akaendelea kufanya mengine. Mtu alieleta toba kisha akarejea kosa na kuleta tena toba basi pia itakuwa sahihi toba yake. Pia ni sahihi kama atarejea kosa na kuleta toba mara kadhaa. Ili kusamehewa madhambi makubwa ni shuruti kuleta toba. Ibada kama sala tano na sala ya ijumaa, kufunga, kuhiji, kuleta istighfar na kujiepusha na madhambi makubwa kunapelekea kusamehewa madhambi madogo. Toba iliyokamilisha masharti yake kwa uhakika inamfanya mtu asamehewe dhambi na kufuru alizozitenda. Hija iliyokamilisha masharti na ikawa imefanywa kwa ikhlas huitwa **Hajjul mabrur**. Hija hii pia humfanya mtu kusamehewa madhambi yake yote isipokuwa yale ya ibada za fardhi alizoziacha na yale ya kudhulumu haki za waja wengine. Ili kusamehewa hayo madhambi mawili yaliyobaki ni wajibu kuzilipa hizo ibada na kurejesha hizo haki. Pamoja na kwamba dhambi za kuacha ibada ya fardhi hazisamehewi kwa hija, dhambi ya kucheleweshа au kutokuifanya ibada hiyo kwa wakati wake inasamehewa. Baada ya hija kama hakuanza mara moja kuzilipa hizo ibada basi dhambi za kuchelewesha zinaanza tena na baada ya muda zitakuwa zimeongezeka maradufu. Hadithi sharif isemayo **(Mwenye kufanya Hajjul mabrur hufutiwa madhambi yake, na huwa kama ndio kwanza anazaliwa)** inafahamisha kwamba ukiacha ibada za fardhi zilizoachwa na haki ya mja, madhambi mengine yote husamehewa. Na hivi ndivyo alivyotambulisha Mtume wa Allah „swallallahu alayhi wasallam" katika dua alizoziomba kwa kuwatakia maghfira mahujaji usiku wa Arafa na Muzdalifa. Wapo wanazuoni waliosema kuwa ibada za fardhi na haki ya mja pia husamehewa ila hii inakusudiwa ni kwa wale walioleta toba lakini ikawa hawawezi kuzilipa hizo ibada walizoziacha na hizo haki walizozichukua. Tunasoma katika Surat Hud aya ya 115 katika maana ya aya **(Hakika mema huondoa maovu).** Aya hii ina maana kwamba ikiwa ibada italipwa basi dhambi yake inasamehewa. Mwenye kufanya ghiba na yule msemwaji akasikia basi huhuzunika sana. Hii ni dhambi kubwa kwa mwenye kufanya ghiba na ili asamehewe inalazimu kumuomba msamaha huyo aliemsengenya.

Kuleta toba mara tu baada ya kufanya dhambi ni fardhi na kuchelewesha toba ni dhambi kubwa kuliko kufanya dhambi zenyewe kwa sababu dhambi za kuchelewesha toba zinaengezeka siku hadi siku. Na hizi dhambi za kuchelewesha toba pia inatakiwa ziletewe toba ila wakati mtu anapotubia kwa dhambi fulani na zile dhambi za ucheleweshaji wa toba kwa kosa lile pia husamehewa. Toba ya kutokutekeleza fardhi haikamiliki ila kwa kuitekeleza ile fardhi. Ili kusamehewa kwa dhambi yoyote ile, kuleta toba moyoni, istighfar

ulimini na kulipa kwa kiwiliwili ni lazima. Kuleta tasbih mara mia kwa kusema **(Subhanallahi wabihamdihi subhanallahil adhym)**, kutoa sadaka na kufunga siku moja inazidisha uzuri wa istighfar.

Tunasoma katika suratu Nur aya ya 31 katika maana ya aya **(Enyi waumini! Tubieni kwa Allah)** na tunasoma tena katika Suratu Tahrim aya ya 8 katika maana ya aya **(Enyi mlioamini! Fanyeni tawbatan nasuha).** Neno Nasuh limepewa maana 23. Iliyo mashuhuri katika hizo ni ile maana inayosema, kujuta, kuleta istighfari na kunuia kuto kurejea. Katika suratul bakara aya ya 222 katika maana ya aya tunaambiwa **(Allahu taala anawapenda wenye kutubia).**

Na hadithi sharif inasema **(mbora wenu ni yule ambae huleta toba mara tu anapofanya dhambi).** Dhambi kubwa ni kukufuru, unafiki na kurtadi. Mtu ambae si muislamu na hajawahi kuwa muislamu huitwa kafir.

[Yule mwenye kuwahadaa waislam kwa kudhihirisha Uislam hali ya kuwa yeye ni **kafiri** basi huyo huitwa **Mnafiki (mzandik)**. Na yule ambae ni muislamu kisha akawa kafiri huyu huambiwa amertadi naye huitwa **Murtadi**. Kutoka katika makundi haya matatu, yeyote atakaeamini imani ya kweli baadae, basi huyo huwa muislamu.

Katika **Barika** na **Hadika** mlango wa maafa ya ulimi, pia katika **Majmaul anhur** imesemwa (Muislamu mwanamke au mwanamme iwapo atasema neno au kufanya jambo kwa makusudi na kujua, neno au jambo ambalo wanazuoni wamekubaliana kusemwa kwake au kufanywa kwake ni ukafiri au akafanya jambo lenye sifa hiyo kwa ajili ya kuwachekesha wengine, hata kama hakufikiria maana yake, basi atakuwa **Murtad**. Hii huitwa **kufru ya inadi**. Na ikiwa hajui kuwa hilo linasababisha kurtadi, na akalifanya kwa hiari yake basi pia atakuwa Murtadi na hii huitwa kufru kwa ujinga. Kwa vile haya ni mambo ambayo ni lazima kwa muislamu basi ni fardhi kujifunza. Kutokujua si udhuru, ni dhambi kubwa. Yule aliyeritadi kwa kufru ya inadi au **kufru ya ujahili**, ndoa yake pia huvunjika. Inabidi achukue uwakala kwa mkewe na mbele ya mashahidi wawili au mbele ya jamaa msikitini analazimika kufunga tena ndoa yake. Hailazimiki **Hulla** kwa kufunga tena ndoa kwa zaidi ya mara mbili. Ikiwa neno linalopelekea ukafiri limesemwa kimakosa kwa ulimi kuteleza au kwa kukusudia neno lenye maana nyengine, au kwa kutozwa nguvu kusema au kufanya jambo husika, basi mtu hatokuwa Murtad na ndoa yake haibatiliki. Kusema neno ambalo wanazuoni wamekhitilafiana kwamba linasababisha ukafiri au la, kwa makusudi, pamoja na kwamba msemaji hatokuwa

amertadi, lakini kuleta istighfari na kufunga upya ndoa yake ni jambo linalopendekezwa. Haidhaniwi kwa muislamu anaekwenda msikitini kuwa anaweza kufanya kufru inady au kufru jahily. Lakini hii aina ya pili (kufru jahily) kwa vile mtu anaweza kuanguka ndani yake bila ya kujua, imam msikitini alete dua ya kutengeneza tena imani na kurudisha ndoa na maamuma wafuatishe. Dua yenyewe ni hii **(Allahumma inny uridu an ujaddidal iman wa nikah tajdydan bikawli laa ilaaha illallah Muhammadu rasulullah).** Katika hadithi sharif tunasoma **(Zifanyeni mpya imani zenu kwa kusema la ilaaha illallah).** Hadithi hii inatuamrisha kuzitengeneza upya imani zetu. Kila wakati kila mke inatakiwa amwambie mumewe “nimekupa uwakala wa kuifanya upya ndoa yetu” na mume anatakiwa ajibu “nimeukubali uwakala huu” Baada ya sala ya ijumaa imam anatakiwa aisome dua ya kutengeneza upya imani na maamuma waitikie.Kwa kufanya hivyo wote imani zao na ndoa zao zitakuwa zimetengenezeka upya.]

Itikadi yoyote isiyoafikiana na mafunzo ya ahli sunna „rahimahumullahu taala“ huitwa **bid’a** na **upotofu**. Hii ndiyo dhambi kubwa baada ya ukafiri. Wale ahli bid’a wenye kuchanganyika na waislam na wakafanya kazi ya kueneza bid’a hiyo basi huwa wanapata dhambi nyingi zaidi. Dola inatakiwa iwaadhibu watu hawa, wanazuoni wao inatakiwa wanasihiwe kwa maneno na kwa maandishi na watu wasio na elimu wanatakiwa wasikutane na watu hawa na wala wasisome vitabu na majarida yao. Inabidi kuwa na hadhari ili tusidanganyike na uongo na uzushi wao na mazungumzo yao ya hamasa. Wasio na madhehebu, wafuasi wa Maududi, wafuasi wa sayyid Kutub, kundi la tabligh, mawahabi, shia, nusayry na makundi mengi ya kitarika yaliyojitokeza hivi sasa na mashekhe bandia wanatumia kila njia kueneza imani na itikadi zao potofu. Kutokana na uovu wao wa nafsi na kwa kusaidiwa na shetani na Uingereza wanatumia njia ambazo haziwezi kufikiriwa kwa lengo la kuwahadaa waislamu, kuwakandamiza na kuwaangamiza ahli sunna. Wanatumia mamilioni katika mali zao ili kuwapiga vita baridi ahli sunna. Inahitaji vijana wasome njia ya haki ya dini ya kiislam na vitabu vya maulamaa wa ahli sunna. Wasiosoma watakumbwa na mafuriko ya ukafiri na bid’a, watazama na watakumbwa na maafa ya duniani na akhera. [Hakikat kitabevi wanaeneza vitabu vya wanazuoni wa ahli sunna tu. Hongera kwa wale wenye kusoma vitabu hivi.] Viongozi wa makundi ya bid’a hutoa tafsiri zisizosahihi za aya za Kur-an Karim na hadithi sharif kisha huzitumia tafsiri hizo kutolea dalili itikadi zao potofu. Wale wenye kusoma vitabu vya ahli sunna huifahamu haki na huokoka na

ubabaishaji wa watu hao. Kwa wale wasiojua haki, ni muhali kuokoka na mitego ya upotofu ya watu hao. Iwapo itikadi zao hazitawiana na yale yaliyowekwa wazi na Kur-an Karim na sunna, yakakubalika kwa kauli moja na maimamu mujtahid na yakaenea kwa waislam, basi imani zao hizo zitakuwa kufr. Aina hii ya kufru huitwa **ilhad** na makafiri hawa huitwa **Mulhid**. Hawa mulhid kufuatana na vitabu vya tawhid wametajwa kuwa ni mushrik,makafiri wasio na kitabu.]

Wale waliortadi miongoni mwa watu wa bid'a, toba yao inakubaliwa. Hawa toba yao ni kusoma vitabu vya itikadi ya ahli sunna na kuamini, na kuachana na itikadi zao mbovu na kujuta.

Mtu ambae fardhi anazipa umuhimu ila hazitekelezi kutokana na uvivu, huyo hawi Murtadi. Ila mtu mwenye kuacha fardhi kwa uvivu huwa amefanya madhambi mawili sambamba. Dhambi ya kwanza ni kuichelewesha fardhi kupita wakati wake yaani kupitisha wakati wa fardhi bila ya kufanya ibada yake. Hili linahitaji kuleta toba kwa kujuta na kuhuzunika na kuamua kuwa hatoichelewesha tena fardhi kwenye wakati wake. Dhambi ya pili ni kutoitekeleza fardhi yenyewe. Dhambi hii toba yake ni kuitekeleza (kuilipa) hio fardhi mara moja. Kuchelewa kuilipa pia nayo ni katika dhambi.

[Mwanazuoni mkubwa wa Uislam, Mujaddid wa karne ya kumi na nne, mwenye elimu za dhahiri na batini, mwalimu wa madrasatul mutakhasisyna, gwiji la tassawuf, Profesa Sayyid Abdulhakim Efendi „rahimahullahu taala", mara kwa mara katika darsa zake na waadhi wake alikuwa akisema "Farz moja, kutoitekeleza kwa wakati wake ni dhambi kubwa." Vile vile imetambulishwa katika vitabu mbali mbali kwamba kutokuilipa mara moja baada ya kupitwa na wakati pia nayo ni katika dhambi. **(Wakati wa fardhi fulani unapomalizika, fardhi ile lazima ilipwe. Kwa mfano ikiwa fardhi ile inachukuwa dakika 6 kutekeleza, hivyo baada ya wakati wake kutoka, zikipita dakika 6 bila ya kulipwa, unapata dhambi za kuchelewesha kulipa. Na kwa kila mzunguko wa dakika sita unaopita utakuwa unakupa dhambi za kuchelewesha kulipa. Hivyo dhambi zisizohesabika wala kufikirika zinaweza zikapatikana katika jambo hili).** Hivyo ndivyo dhambi zinavyoongezeka kwa ibada ya kulipa inapocheleweshwa. Kwa vile sala tano, kila moja ni fardhi kwa kila siku, hivyo dhambi za kila sala ambayo haikulipwa hujirejea kila siku. Na ikiwa sala zote tano hazikusaliwa basi muongezeko wake wa dhambi unafanana kwa kila sala moja. Hali itakuwaje basi kwa sala ambazo hazikusaliwa kwa miezi au miaka kadhaa. Kuokoka na jambo hili zito na la kutisha, inahitaji kutumia njia zote zenye kuwezekana. Yule mwenye imani na akili inafaa asali sala

za kulipa (kadha) usiku na mchana ili kuepuka adhabu za kuacha sala huko akhera. Kwani imeelezwa kwamba swala iliyoachwa kwa uzembe bila ya udhuru itamuingiza mtu motoni kwa miaka sabini na tano elfu. Muumini wa kweli mwenye kuzingatia adhabu zilizotajwa hapo juu zinazotokana na kuacha sala, hawezi kupata usingizi wala hatamani kula wala kunywa. Dunia yake inakuwa ni kama jela. Yule mwenye kuacha sala sababu ya kutokuipa umuhimu, basi huyo huwa ni murtad, kafir. Murtad atakaa daima ndani ya moto. Huyu Murtad tokea hapo yeye haamini Jahannam wala adhabu wala hayapi umuhimu mambo ya kusali. Anaishi duniani kama mnyama akitumikia matashi yake na kwenda mbio kukusanya mali na pesa. (Lolote litakalotokea na litokee,atakaedhurika na adhurike, ila mimi lazima nipate). Yuko tayari kuangamiza kila kitu ili kuridhisha matamanio yake. Hana imani wala akili. Watu kama hawa hawana huruma na ni hatari kuliko wanyama. Mtu kama huyu kumzungumzia ubinadamu, huruma na wema ni sawa na kuandika maandishi hewani. Ameanguka katika mtego wa kukidhi matamanio yake ya kinyama.

Kuzilipa sala ambazo hazikusaliwa siku nyingi inaonekana kama haiwezekani. Kwa vile watu wameacha kufuata yale yaliyoamrishwa na Uislam, na wameikengeuka ile njia ya utulivu na salama iliyofunzwa na Uislam, basi baraka katika maisha imepotea na riziki zimepungua. Tunasoma katika surat Taha aya ya 124 katika maana ya aya **(mkinisahau, nitapunguza riziki zenu).** Kutokana na hilo rizki ya imani, rizki ya afya, rizki ya chakula, rizki ya utu, rizki ya huruma na aina nyingi nyengine za rizki zimepungua. (Allahu taala hamdhulumu mja wake. Kila mtu linalomfika ni kutokana na makosa yake). Msemo huu umechukuliwa kutoka katika maana ya suratu Nahl aya ya 33. Kutokana na kufuru na kuacha mafunzo ya dini baraka imepotea na leo watu wanafanya kazi usiku na mchana, kike kwa kiume kwa ajili ya kutimiza mahitaji ya familia; lakini pia hayatimii. Bila ya kumuamini Allahu taala, kufuata mafunzo yake, kufuata tabia njema za mtume wake na kutekeleza sala tano alizoamrisha; maafa na maovu hayawezi kumalizika.

Ili kuweza kuzilipa sala za kadha alizonazo mtu pale anaposali sunna ya kablia basi pia atie nia ya sala ya kadha ya wakati ule (isipokuwa kwa sala ya asubuhi). Kwa mtindo huo atakuwa ameswali sala ya sunna pia amelipa kadha za siku moja. Mchanganuo na namna ya kusali sala ya kadha kwa mtindo huu umeelezwa kwa kirefu katika kitabu kiitwacho **Saadatul abadiyya.** Kuleta toba mara moja kutatosha kwa kusamehewa madhambi yote. Toba ya kuacha sala ili iwe sahihi,

zile sala zote zilizoachwa inalazimu zisaliwe. Mtu aliyeleta toba na kuanza kusali kadha, huwa amenuia kusali kadha kwa umri wake wote, yaani mpaka sala zake za kadha zimalizike. Mtu huyu akifa, Allahu taala humsamehe kutokana na nia yake hiyo. Na kwa mfano huu huu mwenye kuendeleza kuleta istighfar, na kafiri anaposilimu dhambi zake zote zilizopita husamehewa na yule kafiri asieamini basi hudumu motoni.

Wakati vilipoandikwa vitabu vya fikh karne nyingi zilizopita, imani za waislam wakati huo zilikuwa ni zenye nguvu na wakimuogopa sana Allahu taala na adhabu ya Jahannam. Ilikuwa haiwajii katika akili kwamba atatokea mtu asisali au aache kipindi cha sala bila dharura. Wakati huo ni mara chache sana mtu kupitwa na sala kwa sababu ya dharura maalum na hilo lilikuwa ni jambo lenye kuwapa huzuni sana. Nyudhuru za sala ni kulala, kusahau, kuwa vitani au njiani na kushindikana kusali hata kwa kukaa. Inapopatikana dharura moja kati ya hizi, kuipitisha sala haiwi dhambi. Dharura inapoondoka tu ni lazima kuilipa sala bila kuichelewesha. Inaruhusika kuchelewesha kwa kiasi ya muda wa kutafuta mahitaji ya lazima kwa ajili ya watoto. Sala zilizoachwa kwa dharura hazisaliwi badala ya sunna zilizokokotezwa. Kulipa kadha wakati wa sunna zilizokokotezwa imetajwa kwenye vitabu vya fikhi kuwa ni kwa zile kadha za sala zilizoachwa bila ya udhuru. Sala iliyoachwa bila ya udhuru lazima ilipwe haraka. Hii inaweza kusaliwa badala ya sunna. Anasema Imam Rabbany katika barua ya 123 (Ikiwa ibada ya sunna itasababisha kuacha fardhi, hiyo huwa si ibada. Huwa ni upuuzi wenye dhara).]

[Mwanazuoni mkubwa Ibn Abidin “rahmatullahi alayh” anasema (Unapoingia msikitini ni sunna kuswali rakaa mbili. Hii huitwa **tahiyyatul masjid**). Unapoingia msikitini ukaswali sala ya fardh, sunna, kadha au sala nyengine yoyote basi hiyo huchukuwa nafasi ya sala ya tahiyyatul masjid. Hii hailazimishi kuchanganya na nia ya tahiyyatul masjid wakati unapoziswali pamoja. Kikawaida, ikiwa utachanganya nia ya kusali sala ya sunna na sala ya fardhi iliyo kwenye wakati wake, hilo haliwezekani na hapo ni sala ya fardhi tu ndiyo inayohesabiwa. Lakini kwa sala ya tahiyyatul masjid, unapoingia msikitini ukasali sala yoyote ile, unakuwa pia umesali tahiyatul masjid bila ya kuleta nia mbali. Abdulhakim efendi “rahmetullahi alaih” alisema, lakini kuweza kupata thawabu zake lazima nayo itiliwe nia kwa sababu ibada yoyote isiyo na nia haina thawabu. Sala ya sunna maana yake ni sala isiyo ya fardhi inayosaliwa. Ikiwa sala ya kadha itasaliwa badala ya sunna ya kabla ya sala (kabliya) au sunna ya baada ya sala (baadiya), ikiwa

itasaliwa kwa mtiririko unaotakiwa basi sala ya sunna pia itakuwa imesaliwa. Hapa inafahamika kwamba kusali kadha badala ya sunna inakuwa hukuacha sunna na kama nia ya sunna pia itapatikana basi na thawabu zake zitapatikana.]

Mtu ambae ametia nia na ameanza kulipa sala kama tulivyoelezea hapo juu wakati anapopata maradhi thakili, inapasa ausie kutolewa kafara ya sala hizo baada ya kifo chake na wale waliousiwa wanatakiwa watekeleze wasia huo. Ikiwa wakati wa kusali moja kati ya mambo ya wajibu limeachwa au kufanya jambo la makruh, basi sala hiyo itabidi isaliwe tena. Hata kama sala ni ya sunna ikiwa litafanyika jambo lenye kuharibu sala basi ni wajibu kuirejea sala hiyo. Zaka, zakatul fitri, nadhiri na ibada ya kuchinja vyote vinalazimika kulipwa ikiwa havikufanyika kwa wakati wake. Ikiwa mtu atapatwa na ufakiri baadae asiweze kulipa basi anaweza kutumia njia ya kisheria iitwayo **Hilai Shar-iya.** Na kama atakuwa si fakiri basi haitojuzu kutumia njia hii.

Madhambi ambayo yanamhusu binadamu na mola wake tu bila ya kuingia haki ya mja mwengine, inatosha kuleta toba ya siri. Hailazimiki kumpa taarifa mtu mwengine kama imam au kiongozi wa dini. Kutoa pesa kwa ajili ya kufanyiwa toba hayo ni mafunzo ya kikristo na wala hayapatikani katika Uislamu. Kusoma Kur-an Karim ukiwa na janaba na kukaa msikitini, kuzungumzia mambo ya kidunia msikitini na kula, kunywa au kulala, kushika msahafu bila udhu, kupiga ala za muziki, kuzini, kulewa na kinamama kutoka nje bila ya stara ya kisheria ni mfano wa dhambi ambazo hazikuchanganya haki za mja mwengine. Ni uzito kusamehewa dhambi zilizohusiana na haki za wanyama. Mnyama kumuua bila ya haki, kumpiga, kumtembeza masafa marefu asiyoyaweza, kumtwisha mzigo mkubwa asiouweza, kutokumlisha kwa wakati stahiki, haya yote ni madhambi. Madhambi haya yanataka kuleta toba na kuomba kwa kuleta istighfar.

Haki za mja ni aina tano. Mali, nafsi, dini, heshima na Mahram. Wizi, unyanganyi, kuuza mali kwa hadaa na udanganyifu, kuharibu mali ya mtu mwengine, kutoa ushahidi wa uongo au kumpa taarifa dhalim na kutoa rushwa ni miongoni mwa haki za mja zinazohusu mali. Shilingi moja au chembe ya nafaka ya mtu uliyoichukua ni lazima kuleta toba na kufahamiana na mwenyewe. Ikiwa haitolipwa na muhusika akafa basi watoto wake wanalazimika kumlipia. Haki ambayo haikulipwa duniani basi akhera hulipwa kwa kuchukuliwa thawabu za mdaiwa na kupewa mdai. Ikiwa aliedhulumiwa ameshakufa basi watalipwa warithi wake. Ikiwa hana warithi basi ile haki itatolewa sadaka kwa mafakiri wema kwa nia ya kwamba thawabu za sadaka ile imfikie huyo

aliedhulumiwa. Iwapo hakuna mafakiri wema basi itatolewa kwa taasisi zenye kuuhudumia Uislam. Miongoni mwa mafakiri wema inafaa kuwapa katika jamaa zake mwenyewe huyo mdaiwa walio wema. Kitu anachopewa fakiri kama zawadi huwa ni sadaka na kwao hupatikana thawabu. Ikiwa atashindwa kufanya moja kati ya haya basi aombe dua ya kusamehewa kwa ajili yake yeye binafsi na kwa huyo aliemdhulumu. Ni wajibu kwa kafiri vile vile kufikia muwafaka nae unapomchukulia haki yake na lisipopatikana hili inakuwa ni uzito siku ya kiama.

Dhulma ya nafsi ni kumuua mtu au kumkata kiungo. Kwanza ni lazima kuleta toba na kisha kwenda kujisalimisha kwa walii wake. Walii wake akitaka atamsamehe au atafanya nae suluhu kwa kumlipisha mali. Akipenda pia anaweza kumkabidhi mahakamani ili apewe adhabu stahili. Haijuzu adhabu kutolewa na huyo walii. Haki ya heshima ni pamoja na kumtukana, kumsingizia, kumsengenya, kumdhihaki na mengineyo. Kuleta toba na kumuomba samahani muhusika ni lazima. Haitojuzu kuja kumuomba msamaha mrithi wake.

Haki ya maharam ni kumfanyia maovu mke wa mtu au watoto wake. Kuleta toba na istighfar ni lazima. Na ikiwa haitaleta fitna inapasa kumfata muhusika na kumuomba msamaha. Na ikiwa italeta fitna basi na amuombee dua huyo mdhulumiwa na kutoa sadaka kwa ajili yake. Haki ya dini ni kule kuacha kuwapa elimu ya dini wale walio chini ya amri yake. Kuwazuia watu kupata elimu ya dini na kutekeleza ibada au kumwita mtu kafir au fasik ni miongoni mwa haki hizo. Wakati wa kuomba radhi inatosha kumwambia ulie mkosa naomba radhi kutokana na haki zako, bila ya kulitaja kosa lenyewe.

Kumsamehe unae mdai ni katika tendo lenye thawabu nyingi.

Hadithi sharif inasema **(Mwenye kuleta toba ni sawa na kuwa hakufanya madhambi)** na katika hadithi sharif nyengine **(Kuleta istighfar kwa mdomo tu bila kujuta kunapeleka kuendelea kufanya maasi. Hii ni sawa na kumdhihaki Allah).** Kuleta istighfar maana ni kusema **(Astaghfirullah)** na maana yake ni kwamba (Nisamehe ewe mola wangu). Muhammed Othman Hindy „kuddise sirruh“[1] katika kitabu chake kilichoandikwa kwa kiajemi kiitwacho **Fawaid uthmaniyya** anasema (unataka nikuandikie dua ya kusoma kwa ajili ya kupata shifaa). (Yaani, **Astaghfirullâhal'adhîm alladhî lâ ilâha illâ hü al hayyul kayyûmu wa atûbü ilayh).** Ili kupata shifaa lete toba na usome

[1] Muhammed Osman alifariki mwaka 1314 (1896 m).

sana dua ya istighfar. Ukiachilia mbali mauti, itakukinga na shida zote na maradhi yote. Pia itakupunguzia machungu ya maradhi wakati wa kufa na utakufa kwa utulivu. Dua hii imeandikwa kwa urefu katika kitabu kiitwacho **Hak sozu vesikalari** ukarasa wa 344. Tunasoma katika surat Hud aya ya 52 katika maana ya aya **(Leteni istighfar. Nitakusaidieni)**. Na katika hadithi sharif **(Mwenye kuleta istighfar kwa kuendelea, Allahu taala humuondoshea mazito yake).** Ni vyema kila wakati na kila pahala, baada ya sala na kabla ya kulala kusema kwa mazingatio **(Astaghfirullah min kulli maa kerihallah)** au kwa kifupi **(astaghfirullah)**. Allahu taala atakupa shifa na mahitaji yako yote. Hazrat Muhamed Masum katika hadithi sharif iliyomo katika juzuu ya 6 barua ya 121 ameandika **(Juu ya moyo wangu kunafanya pazia hivyo kila siku ninaleta istighfar mara sabini).** Waadhini wa msikiti wa Khalid bin Zayad kila siku walikuwa wakisoma dua ifuatayo **(Rabbana amana bima anzalta wattabaana rasula faktubnaa maa shahidyn).**

Kila mwanamme anatakiwa asome dua hii **(Allahumma ghfir liabai wa ummahati waliabnaai wa banaty, wa liikhwaty wa akhwaaty wa liajdady wa jaddaty waliamamy wa ammaty wa liakhwali wa khalaty walizawjati wa abawayha waliustadhy wa lilmuuminina walmuuminati walhamdulillahi rabbil alamyn).** Ikiwa anaesoma ni mwanamke, sehemu ya zawjaty atasema zawjy.

Katika hadithi sharif tunasoma **(Allahu taala anamsamehe mja anaefanya kosa na akajuta hata kabla ya kuleta istighfar)** na katika hadithi nyengine **(Hata kama makosa yako yakiwa mengi yakagusa mbingu, basi ukileta toba Allahu taala anakusamehe).** Hadithi hii ni kwa yale makosa ambayo hayahusishi haki ya mtu mwengine. Katika hadithi sharif nyengine tunasoma **(Dhambi ziko za aina tatu. Kuna zile ambazo hazitasamehewa siku ya kiama, kuna ile ambayo duniani haikuachwa kufanywa (iliendelea) na kuna ile ambayo Allahu taala akipenda ataisamehe).** Dhambi ambayo haitasamehewa siku ya kiama ni shirki. Shirk hapa ina maana ni aina zote za kufr. Makosa ambayo Allahu taala hatayasamehe bila ya kutakana radhi ni yale yenye haki ya mja mwengine na deni la sala. Makosa ambayo Allahu taala akipenda atayasamehe ni yale makosa ambayo hayana haki za waja wengine.

## UZINDUZI MUHIMU

Iwe kwa mwanamke au mwanamme ni wajibu katika kila wanalosema na wanalotenda kuhakikisha kuwa wanafuata maamrisho ya Allahu taala na kuacha makatazo yake. Yule ambaye halipi umuhimu jambo la kuwa ni lazima kutekeleza fardhi na kuacha haramu, basi

imani yake hupotea na huwa kafir [adui wa Allah]. Mwenye kufa kafir hupata adhabu ya kaburini na akhera ataingia motoni. Ataungua katika moto daima na hakuna tamaa ya kusamehewa na kutolewa motoni. Kuwa kafiri ni jambo jepesi. Katika kila neno na kila tendo kuna uwezekano mwingi wa kuwa kafiri. Kujikinga na kufuru pia ni wepesi. Ukijua au usipojua kuwa umeleta sababu inayopelekea ukafiri, kila siku inafaa kusema (Ya Rabbi! Ikiwa nimefanya kwa kujua au kwa kutokujua, jambo au neno linalosababisha ukafiri, basi ninajuta. Naomba unisamehe) na kuleta toba. Kumuomba Allahu taala katika hali kama hii basi atakusamehe na utaokoka na kuingia motoni. Ili usiingie motoni inalazimu kuleta toba kila siku. Hakuna jambo muhimu zaidi ya kuleta toba. Tunazidi kuzindua tena kwamba dhambi ambayo ina haki ya mja ndani yake ni wajibu kuilipa hiyo haki wakati wa kuleta toba. Na sala ambazo ziliachwa ni wajibu kuzilipa. Soma kitabu kiitwacho **Saadati abadiyya** kutoka ukurasa wa 276 hadi ukurasa wa 287.

## MAADILI YA KIISLAM

## SEHEMU YA PILI

Maadili ya kiislam yanatafitiwa katika vigawanjo vitatu. Lakini vigawanyo hivyo vitatau ili uweze kuvielewa vyema inabidi upate elimu saidizi ya awali. Kutokana na hilo haya maandishi yetu tutayaweka katika utangulizi ukifuatwa na vigawanyo vitatu. Ila katika kitabu chetu hiki tutaelezea  kigawanyo cha mwanzo tu.

## UTANGULIZI

Elimu ya maadili husomwa kwa kutaka kwake mtu mwenyewe bila ya kulazimishwa. Kazi yoyote ya hiari inawezekana baada ya kujua mambo mawili. Kujua uhalisia wa hilo jambo ni nini, na kujua faida zake. Na la tatu liliongezeka ni kwamba ili uweze kujifunza elimu yoyote ile inafaa kwanza kupata elimu ya utangulizi. Katika utangulizi tutayaelezea haya makusudio matatu katika hatua tatu  kisha tutatoa na nyongeza mbili.

**HATUA YA KWANZA:** maadili ya kiislam yanagawika katika sehemu tatu.

1. Elimu ya tabia: Hii ni elimu inayomuwezesha mtu anapokuwa pekee bila ya kujali uwepo wa wengine, kujua uzuri au ubaya wa jambo. Elimu hii inamuwezesha mtu kutekeleza kwa namna

anavyojua, hata kama atakuwa haonekani na mtu. Mtu ambaye ni mpole, karimu na mwenye haya, tabia zake huwa ni hizo hizo akiwa mbele ya watu au pekee. Kwa Hivyo elimu hii humfunza mtu mambo kama haya ambayo hayabadiliki.

2. Usimamizi wa familia: Hii ni elimu inayofundisha namna ya kuwasimamia wale waliokulazimu ndani ya nyumba.

3. Mwenendo katika jamii: Hii inafunza namna ya kusimamia majukumu katika jamii na namna ya kuchukua tahadhari katika kuamiliana na watu katika jamii.

Katika kitabu kiitwacho **Akhlaki Nashiri** muandishi anasema: Tabia yoyote ya binaadamu, iwe ni nzuri au mbaya, lazima kuna sababu ambayo kwao ndiyo hufanywa. Sababu hiyo ima ni ya kimaumbile au ni amri, yaani kanuni. Sababu ya kimaumbile ni ile yenye kufanya mambo kwa kufuata akili, fikra na uzoefu. Mambo haya hayaathiriwi wala kubadilishwa na wakati au pahala. Sababu ya pili ambayo ni amri au kanuni inaweza kuwa ni ada iliyojengeka katika jamii iliyozaliwa na dhana ya pamoja ya wanajamii fulani au taifa. Vile vile inaweza kuwa imewekwa na alim anaekubalika, mzoefu au mwenye nguvu na amri katika jamii husika. Mitume "alayhimussalavatu wataslimat", maawliya, wafalme na madikteta wanaingia katika kundi hili. Amri za Allahu taala zilizotambulishwa na mtume, mawalii na wanazuoni nazo zina vitengo vitatu. Kitengo cha kwanza ni zile amri zinazomhusu kila mtu, mmoja mmoja peke yake. Hizi huitwa **ahkam** au **ibada**. Cha pili ni zile amri zinazohusu yale mambo wanayofanyiana watu baina yao. Hizi ni katika mambo ya ndoa **(munakahat)** na maingiliano mengine ya lazima katika kukidhi mahitaji yao binadamu ndani ya jamii kama biashara n,k **(muamalaat)**. Cha tatu ni zile amri zinazohusu nchi na taasisi. Hizi huitwa **Hudud** (mipaka) ambazo ndani yake kuna **siasa** na **sharia**. Elimu za vitengo hivi vitatu kwa pamoja ndio huitwa elimu ya **Fiqh**. Amri ambazo zitaweza kusimamia na kuifanya elimu ya dini ifatwe, zinaweza kutafautiana kulingana na wakati na nchi. Mabadiliko haya ni lazima yaletwe na Allahu taala mwenyewe. Kwa hivyo mabadiliko na mageuzi anayoyaleta Allahu taala yamekuja katika amri kama hizo. Mfano, wakati wa Adam „alayhi salaam" ilikuwa ni lazima watu kuongezeka. Hivyo mwanamme aliruhusiwa kumuoa nduguye wa kike. Idadi ya watu ilipoongezeka uhitaji uliondoka hivyo amri hiyo nayo ikabadilika na kuwa haramu.

**HATUA YA PILI:** Tuelezee faida za elimu ya tabia.

Binaadamu amezungukwa na vitu vingi vikiwemo sayari na nyota ambazo kwa karne nyingi sasa zinaelea bila kugongana. Joto, unyevu,

hewa, maji na vyenginevyo vilivyomo ardhini vimewekwa katika kiwango cha kuweza kukidhi uwezekano na uhitaji wa maisha. Binadamu, wanyama, mimea na viumbe visivyo na uhai, punje ndogo za uhai na kila tunachosoma katika skuli za sekondari na vyuo vikuu, vinathibitisha ustadi mkubwa uliotumika katika kuviumba viumbe visivyo na idadi na kuweka nidhamu, mpangilio na uwiano baina yao. Haya yote yanathibitisha na kulazimisha kwa kila mwenye akili kuamini kuwepo kwa muumbaji ambae ana uwezo na elimu isiyo na mipaka. Katika mwaka 1966 wakati Profesa wa falsafa wa Switzerland alipokua akijibu maswala ya waandishi wa habari alisema (baada ya kusoma vitabu vya kiislam kwa uchunguzi, nimeweza kuiona njia ya haki. Nimeufahamu utukufu wa wanazuoni wa kiislamu. Lau kama dini ya kiislam ingeelezewa kama uhalisia wake ilivyo, basi watu wote wenye akili duniani wangeingia Uislam kwa kupenda).

Iwapo mtu, mara tu baada ya kufanya utafiti na kuingia katika Uislam, atasoma vitabu vya ahli sunna “rahimahumullahu taala” vinavyoelezea maisha na mwenendo mwema wa Mtume “swallallahu alayhi wasallam”, basi imani yake itaongezeka. Akisoma elimu ya tabia, atafahamu juu ya tabia njema na mbaya na mambo yenye dhara na faida. Atafanya mambo mema na kuwa mja mkamilifu mwenye kima hapa duniani. Mambo yake yatakuwa ni mepesi na yenye nidhamu. Ataishi duniani kwa raha na utulivu na kila mtu atampenda. Allahu taala anamuia radhi na huko akhera atapata rehema na malipo kutoka kwa Allahu taala. Tukumbushe tena kwamba ili furaha ipatikane panahitajika mambo mawili ambayo mtu lazima ayafikie. La kwanza ni kuwa na elimu na imani sahihi. Hii hupatikana kwa kusoma elimu za sayansi na elimu ya maisha na mwenendo wa Mtume swallallahu alayhi wasallam. La pili ni kuwa na mwenendo mwema na vitendo vizuri. Hii itapatikana kwa kusoma na kufuata elimu ya tabia na elimu ya fiqh. Mwenye kuyapata mawili haya basi atapata radhi na mapenzi ya allah. Allahu taala ni mwenye elimu isiyo na mipaka na amewapa malaika na mitume elimu nyingi. Wao hawana aibu wala pungufu lolote. Elimu ya binaadamu ni chache na imani yao ima ni potofu au imeambukizwa na tabia mbaya au vitendo viovu. Kwa hivyo binaadamu yuko mbali na Allahu taala, malaika na mitume na amekosa utukufu wa kuwa karibu nao. Iwapo mtu atabakia kuwa mvivu, asichunguze na kuzingatia elimu za sayansi na maumbile atabakia kuwa jahil na hatoweza kufikia imani ya kweli na hatoweza kumfahamu kikweli Mtume swallallahu alayhi wasallama na kuongeza imani yake. Atabakia kuwa aliepata maafa na hasara ya milele. Iwapo

atapata imani sahihi na akafuata maamrisho ya Allahu taala badala ya matamanio ya nafsi yake, hawezi kukosa kabisa kabisa rehema za Allahu taala na msamaha wake na furaha ya milele. Anaweza akapata adhabu kutokana na makosa yake, na mwanzo ikawa uzito kupata rehema za Allahu taala, lakini kwa vile ni mwenye imani hatimae atapata rehema za Allahu taala na kuingizwa peponi.

Kama inavyofahamika ni kwamba ufunguo wa mafanikio na furaha ni kuwa na imani kamili. Kila mtu analazimika kuiokoa nafsi yake na itikadi zisizo sahihi na shubha. Mtu ambae atakuwa na imani kamili na mwenendo wake na matendo yake yakawa mema basi atawakaribia wenye roho zilizotukuka yani malaika, mitume na maawliyaa. Nao watamvuta karibu yao kama vitu vinavyovutana kwa nguvu za usumaku. Atapita katika sirat kama umesa na kuingia peponi na kuneemeka na neema zilizomo ndani yake.

Elimu ya tabia maana yake ni elimu ya kuutakasa moyo na roho. Inafanana na tiba ya mwili iliyo kwenye elimu ya utabibu. Tabia mbaya ni maradhi ya roho na moyo na matendo maovu ni dalili za maradhi hayo. Elimu ya tabia ni muhimu, yenye utukufu na kima kwa sababu uovu wa roho na moyo husafishwa na elimu hii. Moyo kuwa na tabia njema na kuwa na siha na nguvu unasaidiwa na elimu hii. Moyo unazidi kuwa msafi na mzuri kutokana na baraka za elimu hii.

[Moyo na roho ni vitu viwili tofauti vyenye kufanana. Ndani ya kitabu hiki tunapotumia neno roho tunakusudia vyote viwili.]

Je tabia inabadilika? Je binaadamu anaweza kuacha tabia moja na akachukua nyengine? Suala hili lina fikra kadhaa tafauti ambazo zote zimejikusanya katika nukta tatu.

1. Binadamu hawezi kubadilisha tabia kwa sababu ni kitu alichoumbwa nacho.

2. Tabia ziko za aina mbili. Ya kwanza ni ya kimaumbile na hii haibadiliki. Ya pili ni ile iliyopatikana baadae kwa mazoea. Hii inaweza kubadilika.

3. Tabia zote ni mambo tunayojifunza baadae na zinaweza kubadilika. Athari zake za nje zinaweza pia kubadilika.

Wengi wa wanazuoni wa kiislam wamejumuika katika hii nukta ya tatu. Dini za mitume "alayhimu salaam" zimesimama katika ukweli wa nukta hio. Wakuu wa tasawwuf na wanazuoni wameweka misingi ya malezi ya wanafunzi wao chini ya mwongozo wa nukta hio.

Je ni tabia gani ambazo binaadamu anazaliwa nazo? Suala hili nalo pia jawabu lake bado halijapatikana. Kufuatana na wanazuoni wengi, binaadamu anazaliwa na tabia ya kutenda wema na kupanda daraja kuelekea mambo mazuri. Kisha baadae kutokana na matamanio ya nafsi, kutopata mafunzo ya maadili mema au kushirikiana na marafiki wabaya ndiyo anaangukia kwenye tabia mbaya. Katika hadithi sharif tunasoma kwamba **(Kila mtu anazaliwa hali ya kuwa ni muislamu. Kisha mama na baba ndio wanawafanya wawe wayahudi, wakristo au wasio na imani).**

Baadhi yao wanasema kwamba roho ya binaadamu inakuja duniani hali ya kuwa ni ovu. Hata kama ilikuwa ni njema kiasili, lakini inapochanganyika na kiwiliwili, hupotea njia wakati wa kuyahudumia mahitaji ya kiwiliwili. Baadae, wale waliopata uongofu wa Allahu taala huwa wema na hawabakii waovu kama walivyozaliwa.

Wengine wanasema kuwa roho inapokuja duniani haiwi njema wala ovu, ila baadae ndio huweza kuelekea katika moja ya hali hizo mbili. Yule atakaejifunza mwenendo mwema na akatenda mazuri basi hupata furaha na ukamilifu. Ama ikiwa atachanganyika na watu waovu basi bila ya shaka naye mwenendo wake na matendo yake yatakuwa maovu, atakabiliwa na mashaka na kuwa mtu muovu.

Kufuatana na tabibu wa kigiriki bwana Calinusa yeye anasema roho zimegawika makundi matatu. Kuna zile ambazo zimeumbwa njema na zile ambazo zimeumbwa ovu. Kuna na zile ambazo hazimo katika makundi haya mawili lakini zinaweza baadae zikaangukia katika moja ya makundi haya. Wale walioumbwa kuwa ni wema ni wachache ila walioumbwa kuwa ni waovu na wenye kupendezewa na kufanya maovu ni wengi. Na wale wa hali ya katikati wengi wao pia ni baina ya hayo makundi mawili. Kwa mtizamo wa mgawiko huo wako baadhi ya watu ambao tabia zao zinaweza kubadilika ila wengi wao hawabadiliki. [Wanafalsafa wa kigiriki hawakuwa na habari ya kuwa mbali ya roho, binaadamu pia ana moyo. Hivyo katika maandishi yao waliitaja roho tu. Kuna baadhi ya waandishi wa kiislam ambao pia wamechukua fikira hii ya wanafalsafa wa kigiriki.]

Kufuatana na wanazuoni wengi, kila mtu tabia yake inaweza kubadilika. Hakuna mtu ambae tabia yake inabaki kama alivyozaliwa; bali hubadilika baadae. Lau kama tabia zingekuwa haziwezi kubadilika basi dini walizokuja nazo mitume „alayhimu salaam“ zingekuwa hazina faida wala ulazima. Na ile misingi ya malezi na adhabu iliyowekwa na wanazuoni kwa maafikiano ya kauli moja, basi ingekuwa ni upuuzi.

Wana elimu wote wamewapa watoto wao elimu na malezi na faida ya malezi imeonekana katika tabia zao. Hivyo jambo la kuwa tabia ni kitu kinachobadilika liko wazi kama jua na linaonekana na kila mtu. Ziko baadhi ya tabia ambazo mtu ameshikamana nazo sana na ambazo inakuwa ni uzito kuzibadilisha. Tabia kama hizo mara nyingi huonekana kwa watu majahili walio waovu. Ili kuweza kubadilisha tabia kama hizo **Riyadha** na **Mujahada** mkubwa unahitajika. Riyadha ni jitihada inayofanyika kuikatalia nafsi kufanya maovu. Mujahada ni jitihada ya kuilazimisha nafsi kutenda mazuri yenye faida. Watu majahil kwa madai ya kwamba tabia haziwezi kubadilika, hawafanyi mujahada wala riyadha, na hawabadilishi tabia zao mbaya. Lau kama itaachiwa kama hivi, kila mtu afanye kufuatana na matashi yake na wenye makosa wasiadhibiwe, ubinaadamu utaelekea kubaya. Kutokana na hili Allahu taala ameshusha rehema zake kwa waja wake na kuwashushia mitume "alayhimu salaam" ili kuwafunza yepi ni mazuri na yepi ni maovu. Miongoni mwa walimu hao, yule aliye mbora zaidi ni kipenzi chetu **Muhammad** „swallallahu alayhi wasallama". Kwa dini yake yeye amebadilisha dini zote zilizopita na yake kuwa ni ya mwisho. Kwa hivyo mazuri yote na tabia njema zote zimekusanyika katika mafunzo yake. Wale wote wenye busara inafaa kuchukua mafunzo ya mwenendo mwema yaliyomo ndani ya vitabu vya dini hii, ili kuweza kubagua mema na maovu na kuweza kuweka misingi ya maisha ya familia na jamii na hatimae kufikia furaha, utulivu na uokovu wa hapa duniani na huko akhera. Huu ndio wadhifa wa kwanza wa binaadamu. Hivyo, inafaa mtu kukisoma kitabu chetu hichi cha **Maadili ya kiislam** ili kiweze kumsaidia kufikia malengo hayo kwa msaada wa Allah.

**HATUA YA TATU:** Maadili ya kiism tumeyagawa sehemu tatu. Ili kuweza kuyafahamu vyema, tutavitaja visaidizi vyake. Elimu yoyote ina matawi yake. Matawi yote hayo hukutana katika nukta moja ambayo ndiyo maudhui makuu ya elimu hiyo. Mfano elimu ya utabibu ina matawi mbali mbali. Kila tawi linajishughulisha na kujua maradhi na afya ya binaadamu. Kwa hivyo hiyo ndiyo maudhui kuu ya elimu ya tiba. Ili elimu iweze kufahamika vyema, lazima maudhui yake makuu yajulikane. Maudhui makuu ya elimu ya maadili ni roho. Elimu hii huisafisha roho [moyo], kutokana na tabia ovu na kuipamba kwa tabia zilizo njema. Hivyo kwanza ni lazima kujifunza ili kujua roho ni nini na kisha kujifunza hizo tabia nzuri ni zipi na zilizo ovu ni zipi.

Ili kuweza kuilezea roho na moyo kwa kadri inavyowezekana, kuzichanganua nguvu zinazoonekana na zile za siri, na kuweza kueleza furaha na maafa ni vitu gani, nitaandika katika visimamo vitatu.

**KISIMAMO CHA KWANZA:** Moyo na roho ni nini? Vitu viwili hivi kufuatana na wanafilosofi wa kigiriki wameviita **Nafsi Natika** au pia wameiita Nafsi. [Ila gwiji wa elimu ya tasawuf na tabia **Imam Rabbani** “rahimahullahu taala” anasema ya kwamba roho, moyo na nafsi ni vitu vitatau tafauti.] Tunasoma katika suratul Israa aya ya 85 katika maana ya aya **(Wanakuulizia kuhusu roho. Wambie roho ni miongoni mwa viumbwa vya Allah).** Aya hii tukufu inakataza kuulizia juu ya roho kuwa ni kitu gani. Kutokana na hilo mashekhe wa tarika za juu na wanazuoni wengi wamejizuia kuzungumzia suala la roho ni nini. Ila kilichowazi katika Kur-an Karim ni kwamba katazo limekuja kutokutaka kujua roho ni nini tu, ila kuzungumzia sifa zake na mambo yake maalum haikukatazwa. Kwa hivyo wanazuoni wengi wanapoulizwa hujibu kuwa moyo na roho ni vitu visivyo na maumbile yenye kugusika. Vitu hivi viwili ndivyo vyenye kufahamu elimu inayokuja kwenye akili, hisia zifikazo kwenye ubongo zitokazo kwenye viungo vya hisia na ndivyo vyenye kudhibiti nguvu na harakati za kiwiliwili. Hivyo ndivyo walivyosema viongozi wa elimu ya tasawuf na elimu ya kalam. [Ili kupata maelezo zaidi juu ya roho na moyo unaweza kusoma kitabu kiitwacho **Awariful maarif** kilichoandikwa na shekhe wa kishafii Shihabudin Omar Shuhureverdy, aliezaliwa mwaka 539 hijria [1145 miladiya] na kafia Baghdad mwaka 632 hijria [1234 miladiya]. Alichukua faydh kutoka kwa Abdulkadir Jaylany. Vile vile unaweza kusoma kitabu kiitwacho **Maktubaat** cha Imam Rabbany Ahmed Faruky Serhendy aliyezaliwa India katika mji wa Serhendy mwaka 971 hijria [1563 miladia] na akafia huko mwaka 1034 hijria [1624 miladia ]. Abdulqadir Jaylani alikufa Baghdad mwaka 561 hijria.]

Roho na moyo vinaweza kuelezewa chini ya mada sita.

1. Kwanza tutambue kwamba moyo na roho vipo. Suala la kuwepo kwa roho liko wazi na kila mtu analifahamu. Kwa hivyo hili halihitaji kuthibitishwa. Jambo ambalo liko wazi kwa binaadamu mwenyewe ni uwepo wake. Binaadamu haitokei wakati wowote akajisahau. Akiwa amelala au amelewa, roho haijisahau. Hapahitajiki kuletwa ithbat yoyote kwa binaadamu ili aweze kujitambua yeye mwenyewe. Je roho ni kitu chenye umbile au la? Ipo katika hali ya kujitegemea au inategemea uwepo wa kitu chengine?, au uwepo wa sifa zake fulani? Pamoja na kwamba sifa zake nyingi ni zenye kutambulika, bado upo uhitaji wa kuzikumbusha. Na hayo ndiyo yatakayopatikana katika mada tano zilizobaki.

2. Roho na moyo vipo kwa nafsi yake (Jawhar). Wakati mnyama anapokufa tunasema kwamba **roho** imetoka kwa maana ya kwamba

roho imeufariki mwili. Viumbe ima ni Jawhar au Aradh. **Jawhar** ni vile viumbe ambavyo kuwepo kwake hakutegemei uwepo wa kitu chengine. **Aradh (sifa)** kuwepo kwake kunategemea uwepo wa vitu vyengine. Vitu na viumbe ni Jawhar. Rangi, ladha na shakli ni Aradh (sifa) na zinategemea kuwepo kwa Jawhar ili viwepo. Rangi haiwezi kuwepo bila ya kupatikana kitu fulani. Jawhar nazo ziko aina mbili. Ya kwanza ni mujarrad, yaani visivyo na jumbile. Hivi havina uzito, shakli, rangi na haviathiriwi na viungo vya hisia. Ya pili ni vile vitu vyenye umbile (visivyo mujarrad). **Mujarrad** havuhisiki kwa viungo vya hisia wala havigawanyiki vikawa vipande vipande. Akili na roho vimo ndani ya kundi hili. Vitu vyenye jumbile vinahisika kwa viungo vya hisia na vinagawika vipande vipande. Jumbile huchukua shakil maalum kuainisha kitu fulani. Kuna njia nyingi zinazothibitisha kuwa roho ni Jawhar (na wala sio sifa). Njia nyepesi ya kulithibitisha hili ni kwamba sifa (aradh) inabebwa na Jawhar. Roho inabeba vitu vyenye kuhisiwa na kufikiriwa. Kwa hivyo roho na moyo ni Jawhar sio sifa (aradh). Mjadala huu unazidi kunoga pale inapotajwa kwamba sifa pia inaweza kubeba sifa nyengine. Mfano sifa ya kasi kubwebwa na sifa ya mwendo. Haya ni madai ya wale wanaosema kwamba roho ni sifa (aradh) inayobeba sifa nyengine.

3. Roho na moyo ni vitu **hafifu** kwa maana ya kwamba havigawanyiki wala kuachana achana. Kinyume cha hafifu ni kile kilichofanyika kwa mchanganyiko wa vitu. Umbo dogo la kikemia linafanyika kwa mshikano kwani hata atom au molikuli ya gesi vinaweza kuachana (sababu sio hafifu). Uhafifu wa roho unatambulika kwa kuweza kuwepo katika vitu hafifu vyengine. Lau kama roho au moyo vingelikua ni vitu vilivyoshikana na kwamba vinaweza kugawika vipande vipande basi visingeweza kuwemo katika vitu hafifu vyengine. Hii ni kwa sababu wakati wa mgawiko wake basi hicho kitu hafifi chengine nacho pia kingelazimika kugawika, na hili ni kinyume na sifa za vitu hafifu.

4. Roho na moyo havina jumbile. Vitu vyenye urefu, upana na mnyanyuko, yaani vyenye shakil fulani, huwa vina maumbo. Kitu kinachopatikana ndani ya maumbo huitwa **Jismani** (jumbile dogo) na mfano wake ni sifa (aradh) za hayo maumbo.

5. Roho na moyo ndiyo vyenye uelewa na ndio viendeshaji. Pia vinajielewa vyenyewe. Vinaweza kufahamu rangi kwa kupitia macho na sauti kwa kupitia masikio. Vinaifanyisha kazi mishipa ya fahamu na kuifanyisha harakati misuli. Kwa ujumla vina uongoza na kuufanyisha kazi mwili. Harakati hizi ndio huitwa harakati za kukusudia (za hiari).

6. Roho haihisiwi kwa viungo vya fahamu. Majumbile na majumbile madogo huwa na hisia. Roho kwa vile si jumbile wala si jumbile dogo, haina hisia.

**KISIMAMAO CHA PILI:** Mtu akifa roho huwaje? Mtu akifa na mwili unapooza, roho na moyo haviozi. Roho na moyo hufarikiana na kiwiliwili na kuingia kwenye ulimwengu wa vitu visivyo na maumbile. Havitoweki hadi siku ya kiama. Wanazuoni, wanafalsafa na wanasayansi waadilifu wote wamekubaliana katika hilo. Baadhi ya wana elimu ya kimaumbile hawakuafiki rai hii na wameipinga. Kwao wao binaadamu ni kama majani yaliyo jangwani. Huota, hukua kisha hutoweka. Roho haibakii. Kutokana na kauli yao hii walipewa jina la **wanahashash** (yaani **majani**). Wataalamu wa dini na wanafalsafa walizipinga fikra hizi za wanahashash kwa dalili tafauti.

[Inatambulika leo kwamba Allahu taala ameumba elementi 105 na kuzipa sifa tafauti. Kila elementi imefanyika kwa atom nyingi. Kila atom imehifadhi nguvu ndani yake. Atom zikiungana ndio hufanya molikuli au ion ambazo kwazo majumbile na viungo mbali mbali viliumbwa na kupangwa na kufanyishwa kazi zake kwa ustadi wa hali ya juu kabisa. Mfano seli ndogo ambayo haiwezi kuonekana ila kwa darubini, imethibitishwa kuwa utendaji wake kazi ni sawa na kiwanda chenye mashine kadhaa. Kiwiliwili cha binaadamu ambacho kimefanyika kwa mamilioni ya seli kinahitaji kupatikana mazingira wezeshi ya ndani na nje ili kiweze kufanya kazi. Mazingira hayo yanapokosekana basi na kazi za kiwiliwili hazitokwenda sawa. **Allahu taala** mwenye uwezo na elimu ya hali ya juu ndiye mwenye kuweka mazingira wezeshi ili kiwiliwili kiweze kufanya kazi zake. Roho na moyo ni kama waya za umeme zenye kukipatia kiwiliwili nguvu. Kama ambapo waya za umeme katika mashine zikiharibika mashine hushindwa kutembea, basi ni hivyo hivyo kwa kiwiliwili cha binaadamu. Linapotokea tatizo lolote, na mazingira wezeshi ya ndani au ya nje yakakosekana, basi roho na moyo hukifariki kiwiliwili na binaadamu hufa. Hakuna mashine yoyote inayofanya kazi daima duniani, lazima siku moja itakongoweka kuharibika au kuvunjika. Hiyo ndio kanuni ya kawaida. Mwili nao vile vile huzeeka na kuoza. Wakati mwili unapooza ndani ya kaburi elementi zake hazitoweki. Kuoza ni mabadiliko ya kifizikia na kikemia ambayo huufanya mwili kugeuka kwenye elementi mbali mbali. Leo inafahamika kwa uhakika kwamba mabadiliko ya kifizikia na kikemia hayakifanyi kitu kitoweke. Mkemia wa kifaransa Bwana Laviosier anasema **(Mabadiliko ya kikemia hayakifanyi kitu kilichopo kipotee, wala kitu kisichokuwepo kabla**

**kizuke).** Kutokana na uthibitisho wake huu na kudhani kuwa vitu vyote vimeumbwa kutokana na mabadiliko na kanuni za kikemia alisema (Maumbile hayawezi kuumba kitu kipya wala kukiangamiza kiliopo). Lakini leo baada ya kupatikana maendeleo makubwa katika elimu ya nyuklia, inafahamika wazi kwamba, jumbile linaweza kugeuka nguvu na likatoweka kabisa. Hii inathibitisha kuwa Laviosier alikosea. Leo hii kila elimu ya sayansi inaposonga mbele na kupiga hatua, ndio na dini inazidi kupata nguvu kuuzima uzushi wa maadui wa Uislam na kuzidi kuwaadhiri wale wenye kuabudu vitu mbali mbali. Ila kwa bahati mbaya kuna wale wanadini ambao baada ya kujisomea elimu za sayansi, wameanza kuupiga vita Uislam chini ya mwamvuli wa sayansi. Makafiri hawa waliobeba shahada, wanawadanganya vijana wa kiislam kuwa Uislam ndiyo sababu ya kubaki nyuma na kwamba wakristo wanasonga mbele katika kila fani kama tiba, ulinzi na mawasiliano na kwamba eti inafaa tuwafuate wao. Hivyo wanawahadaa vijana kuacha maadili mema ya kiislam na udugu na kuwataka wafate Ulaya na Amerika eti kwa sababu ya kupata maendeleo. Wanawafanya vijana wawe maadui wa Uislam kama wao wenyewe na kuwaongoza kwenye maangamizi. Uhakika ni kwamba Uislam unatuamrisha kujifunza sayansi na sanaa. Wanayoyafanya wakristo na makafiri wengine ni yale waliyojifunza kwa wazee wao na walimu wao. Wanaengeza vitu vidogo tu juu ya yale yaliyokuwa yakifanywa na vizazi vilivyopita. Lau kama vizazi vilivyopita visingekuwa vimefanya basi hawa kwa nafsi zao wasingeweza kufanya kitu. Historia inaonesha kwamba magunduzi mapya ya kisayansi yote yalifanywa na waislam. Elimu na vifaa vya kisayansi hadi karne iliyopita viliendelezwa na kufikishwa daraja hilo na Uislam. Mafanikio hayo yalifikiwa kutokana na dini ya Uislam na dola ambazo zilikuwa zikifuata dini hiyo. Wakristo hawakuweza kuzipiga vita na kuzivunja dola za kiislam kwa silaha hivyo wakaanza kuzipiga vita vya ndani kwa kutumia hila, uongo na mbinu za kisiasa. Wamefanya hayo kwa kuanzisha serikali za kisekula na za kimasoni katika nchi za waislam. Pamoja na hayo uislam hawakuweza kuuangamiza. Kisha yale mavumbuzi ya kisayansi yaliyokuwa katika mikono ya waislam wakayachukua na kuengeza yao machache na kudai kuwa hayo ni mavumbuzi yao. Kwa vile wameyafanya hayo kwa ajili ya manufaa na matashi yao, ule Uislam ambao unaamrisha kusoma sayansi na sanaa leo wanauita kuwa ni dini ya kubaki nyuma. Mayahudi, wakristo na hata wanaoabudu masanamu wanaamini kuwepo kwa pepo na moto na wanajazana kwenye makanisa na mahekalu ya ibada. Ikiwa hawa waumini hawawaiti kwamba ni wajinga waliobaki nyuma, hivyo

inaonesha maendeleo kwao sio sanaa wala sayansi bali ni matashi na maadili maovu. Mashambulizi ya kutumia madai hayo yasiyo ya haki wala ya msingi yalianzishwa na Waingereza. Soma kitabu chetu kiitwacho **(Confessions of a British spy).** Waislam wanalazimika kushikamana tena upya kama mababu zao, washikamane na dini yao na wajiendeleze katika sayansi na sanaa, waanzishe viwanda na wazalishe ala za kisasa, wawe juu kuliko wakristo na warejeshe furaha kwa viumbe wote.

Vitu vinavyopatikana katika mwili wa binaadamu vimetengenezwa kutokana na dongo, maji na hewa. Vitu vyenye uhai vinapata mahitaji yao yote kutokana na vyanzo hivyo vitatu. Wakati binadamu anapooza mwili wake unarejea katika vyanzo hivyo vitatu na wakati wa kufufuliwa atafufuliwa kutokana na vitu hivyo na vile vilivyofanana navyo.

Roho, moyo na malaika katika hali zake za kiasili havina sifa ya kuweza kupanda daraja na kufikia makamu ya juu, vinabaki katika makamu yalivyoumiwa. Wakati roho na moyo vinapoungana na kiwiliwili vinapata sifa mpya inayoviwezesha kupanda daraja au kuwa kafiri, kutenda maovu na kushuka daraja ya chini kabisa.

Katika dunia kila kitu kina sifa maalum zinazokitambulisha kitu hicho. Sifa hizo zinatokana na aina za elementi zilizochanganyika na kufanya kitu hicho. Ikiwa mchanganyiko wa elementi utabadilika, kitu hicho kitatoweka na kupoteza sifa zake, na kitu kingine kipya chenye sifa tafauti kitapatikana. Pamoja na kwamba mabadiliko haya ya mara kwa mara hayavifanyi vifaa asili kupotea, ila vitu hubadilika na kupotea baada ya muda. Zamani vitu (mada) vikiitwa Khayulaa na Jumbile (umbile, umbo) yaani shakli ya vitu ikiitwa **Surat**.

Kwa vile moyo na roho havigawiki vikawa vipande vipande, wala havikutokana na mkusanyiko wa vipande vipande (ni Mujarrad) hivyo havibadiliki, haviharibiki wala havitoweki. Baadhi ya vitu hubadilisha shakli zake kwa mabadiliko ya kifizikia. Mfano maji yakipata moto hugeuka mvuke. Yanabadilika kutoka hali ya umaji kuwa hali ya gesi. Jumbile la maji linatoweka na lile la gesi linatokea. Mabadiliko ya kikemia hubadilisha muundo wa kitu. Inabadilisha vifaa vilivyounda hicho kitu na kuvifanya viwe vifaa tafauti. Katika mabadiliko ya kifizikia kitu hubadilika kwa ujumla ila vifaa vilivyofanya kitu kile havibadiliki. Katika mabadiliko ya kikemia kitu hutoweka ila vifaa vinavyotengeneza hubadilika tu. Katika mabadiliko yote mawili vifaa asili havitoweki.

Katika mabadiliko ya kinyuklia vifaa asili pia hutoweka na kugeuka kuwa nguvu.]

**KISIMAMO CHA TATU:** Moyo na roho ni vitu vyenye nguvu. Nguvu hizi hazifanani na nguvu za mimea au wanyama. Mimea na wanyama vyote vina roho. Moyo unapatikana kwa binaadamu tu. Kila kiumbe kina **roho ya mimea**. Kuzaliwa, kukua, kula, kutoa uchafu mwilini, kuzaliana, na kufa ni mambo ya uhai wa roho ya mimea. Mambo haya yanapatikana kwa binaadamu, Wanyama na mimea. Haya yanasomeshwa katika elimu za mazingira. Miongoni mwa haya, sifa ya kukua haiendelei kwa uhai wote, ila kiumbe husika kifikiapo kiwango maalum ukuwaji unasita. Kwa binaadamu kiwango hicho ni miaka ishirini na nne. Kunenepa sio kukua. Kula kunaendelea hadi mwisho wa maisha kwa sababu bila chakula hakuna uhai.

Wanyama na binaadamu pia wanazo **roho za kinyama**. Hii ipo kifuani. Roho hii ndiyo inayowafanyisha matendo hiari. Kwa binaadamu roho hii hufanya hayo chini ya amri ya moyo.

Kwa binaadamu pia kunapatikana roho nyengine ambayo roho hii inapotajwa hufahamika kwa pamoja na moyo. Kutumia akili, kufikiria na kucheka ni mambo yanayofanywa na roho hii. Roho ya kinyama ina nguvu mbili; nguvu ya kudiriki na nguvu ya kufanya harakati. Nguvu ya kudiriki ni ile ipelekayo kufahamu vitu nayo inafanya kazi katika njia mbili. Njia ya kwanza ni kwa kupitia viungo vya hisia vya dhahiri vionekanavyo. Njia ya pili ni ile ya kutumia viungo vya hisia vya siri visivyoonekana. Viungo vya hisia vinavyoonekana ni vitano. Kiungo cha kwanza ni ngozi ambayo kwao joto, baridi, unyevu, ukavu, ulaini na ugumu vinaweza vikafahamika. Kiungo cha pili ni kile cha kupokea harufu ambayo hufanyika kwa pua. Kiungo cha tatu ni kile cha kuonjea ladha ambacho ni ulimi. Kiungo cha nne ni cha kusikilizia sauti ambacho ni sikio. Kiungo cha tano ni jicho ambalo hutumika kuonea.

Viungo vya hisia vya siri visivyoonekana ni vitano. Ya kwanza ni **Hissi mushtarak.** Hii sehemu yake ni sehemu ya mbele ya ubongo. Athari zote za nje zinazotoka kwenye viungo vya hisia kuja kwenye ubongo hukusanyika hapa. Ya pili ni **Hayal**. Hii sehemu yake ni mbele ya uwazi wa mwanzo wa ubongo. Zile hisia zilizofika kwenye Hissi mushtarak baada ya kukusanywa na kufahamika, zinahifadhiwa katika sehemu hii. Wakati mtu anapoangalia kitu, hisia hupatikana kwenye Hissi mushtarak. Wakati kitu kile kinapotoweka mbele ya macho, hisia pia huondoka katika eneo la Hissi mushtarak na picha yake hupelekwa kwenye eneo hili na kuhifadhiwa kwa muda mrefu. Lau kama si hichi

kitendo cha kuhifadhiwa picha katika eneo hili basi watu wasingeweza kukumbukana. Ya tatu ni **Wahima**. Hii inachambua hisia ambazo hazitokani na viungo vya hisia ila maana yake huweza kupatikana kutokana na uzoefu au yaliyosikikana. Mfano ni uadui au ukweli hatuwezi kuuhisi kwa viungo vya hisia. Rafiki au adui anaweza kuonekana ila urafiki na uadui ndivyo vinavyohisiwa na hii hisia ya Wahima. Lau kama si hii hisia ya Wahima basi kondoo asingejua kuwa mbwa mwitu ni adui yake na wala asingemkimbia. Wala asingelinda watoto wake. Ya nne ni **Hafidha**. Maana zilizofahamika na Wahima zinahifadhiwa hapa. Ya tano ni **Mutasarrifa**. Zile hisia zilizofahamika na maana zake zinalinganishwa ili kuweza kutoa maana mpya. Washairi ni watu wenye nguvu ya hisia hii.

Nguvu ya pili ya roho ya kinyama ni nguvu ya kufanya harakati ambayo nayo ni aina mbili. Ya kwanza ni nguvu ya **shahawa**. Nguvu hii huwafanya wanadamu na wanyama kutaka yale yenye kuwapa ladha na yale mengine ambayo ni ya lazima kwao. Hii pia huitwa nguvu ya **kihayawani** (kinyama). Yapili ni **ghadhabu**. Hii huwapelekea kuvifukuza na kuviweka mbali vitu viovu na vitakavyowapa madhara.

Nguvu ya harakati inahitaji uwepo wa nguvu ya kudiriki kwa sababu kwanza lazima kwa kutumia viungo vya hisia ijulikane kwamba kitu husika ni kizuri au kibaya ili kiweze kukaribishwa au kufukuzwa. Hisia hizi zote zinafanyika kwa kupitia mishipa ya fahamu (nerves). Moyo na roho ya kibinaadamu hupatikana kwa binaadamu tu (haipatikani kwa Wanyama wala mimea). Roho hii nayo ina nguvu mbili. Kupitia nguvu mbili hizi ndio binaadamu hutafautiana na wanyama. Ya kwanza ni nguvu ya kujua na kupambanua na ya pili ni ya kusababisha na kutekeleza. Nguvu ya kujua na kupambanua pia huitwa busara. Nguvu hii ina matawi mawili makuu. Ya kwanza ni upambanuzi wa nadharia ambayo inahusika na kujua elimu zenye majaribio au sayansi na ya pili ni upambanuzi wa vitendo amabayo inahusiana na maadili. Upambanuzi nadharia unaohusiana na kujua sayansi ni muhimu katika kuulewa ulimwengu na vilivyomo. Kwa upande wa pili upambanuzi wa vitendo unaoshughulikia maadili ni muhimu kwa kuweza kupambanua yale yaliyo mazuri na yale yaliyo maovu.

Nguvu ya kutenda ndio inayotumika katika utekelezaji wa yale yanayofanyika. Inatekeleza kwa kutumia elimu iliyopatikana kupitia nguvu ya kujua. Wakati nguvu za harakati za roho ya kinyama inategemea yale yaliyo katika wahimu ambayo yanaeleza kwamba jambo hilo ima linaleta ladha hivyo lifanyike au machungu hivyo likimbiwe; nguvu za harakati za roho ya kibinadamu zinatekeleza

kutegemea na busara. Ikiwa busara itaeleza kuwa hilo jambo lina faida basi **akili** ya kibinaadamu hufanya na ikiwa busara itaeleza kuwa hilo jambo lina dhara akili ya kibinaadamu italikimbia. Pamoja na haya pia inadhibiti nguvu za shahawa na za ghadabu zilizo katika roho ya kinyama.

Watu wengi hutenda kwa kupitia roho zao za kinyama. Matendo yao yanahukumiwa zaidi na Waham na Hayal.

Imam Muhammad Al-Ghazali na mabwana wengine wakubwa wa tasawwuf wanasema "Nguvu hizi za roho ni malaika. Allahu taala kwa utukufu wake na rehema zake kwa waja wake amewaweka malaika chini ya amri ya roho. Na wanabakia chini ya amri ya roho hadi siku roho inapotoka." Zipo hadithi sharif zenye kuashiria haya. Pia mambo ambayo hufanywa na watu wa kawaida tu, ambayo kwa kawaida yako nje ya uwezo wao, hata kuweza kuwafanya magwiji washangae, ni dalili pia ya hilo. Ukamilifu wa mwandadamu, unapatikana kwa nguvu mbili za roho.

**UZINDUZI:** Hadhrat Muhammed Maasum anasema katika **Maktubat** juzuu ya pili barua ya 80 (Ili kuepuka balaa na misiba inalazimu kuleta **istighfar**. Faida ya hili imeshaonekana kwa vitendo na hadithi sharif inaashiria hayo. Fakiri huyu (muandishi) kila baada ya sala ya fardhi analeta dua ya istighfar mara tatu **(Astaghfirullahal`adhim alladhi la ilaha illa huwal hayyul kayyum wa atubu ilayhi).** Kisha anasoma **(astaghfirullah)** mara 67).

## NYONGEZA YA KWANZA YA UTANGULIZI

Nyongeza hii itaelezea utukufu na heshima ya binaadamu kati ya viumbe wote.

Maumbo hayatafautiani chini ya mtizamo wa vitu yalivyoumbiwa. Vyote vina uzito na kuchukua nafasi. Kwa mtizamo huo binaadamu na wanyama hawana tafauti na viumbe visivyo na uhai. Ila maumbo yanatafautishwa kwa sifa zake.

[Kila umbo limetengenezwa kwa **atomi**. Vumbi ni mkusanyiko wa mamilioni ya atom. Wakati idadi maalum ya atom inapoungana hufanya **molikuli**. Maumbo yanagawika sehemu mbili; **safi na mchanganyiko**. Maumbo safi ni yale yenye sifa mahsusi mfano waya wa shaba au maji ya mvua. Hii ni kwa sababu popote pale duniani na wakati wowote ule uwe, vitu hivi sifa zake zinajulikana na hazibadiliki. Joto lake la kuyayuka na kuchemka linajulikana na wala halibadiliki. Vitu ambavyo havina sifa mahsusi huitwa **mchanganyiko**. Maziwa,

ubao, mafuta na maji ya bahari ni mfano wa hayo. Hivi vinabeba sifa tafauti. Havina daraja la joto la kuyayuka na kuchemka linalojulikana. Maziwa ya n'gombe ni tafauti na yale ya kondoo. Maji ya Bahari Nyeusi yana chumvi chache ukilinganisha na yale ya Bahari ya Mediterrenian.

Vitu safi navyo ni vya aina mbili. Vile ambavyo havigawiki kutupa vipande vidogo zaidi vyenye sifa tafauti, hivi huitwa **elementi**. Oksijen, iod na dhahabu ni mfano wa vitu hivyo. Leo zipo element 105 zinazotambulika. Vile ambavyo vinagawika kutupa vipande vidogo zaidi vyenye sifa tafauti, hivi huitwa vitu mshikamano mfano sukari na alkohol. Sukari ikiingizwa motoni inatoa kabon, maji na vipand e vyengine. Maji nayo kwa msaada wa nguvu za umeme yanagawika kutupa gesi za aina mbili, oksijin na hydrojin. Vitu mshikamano hufanyika kwa kushikamana atom za elementi mbili au zaidi.

Kitu kimoja kinaweza kupatikana katika hali ya ugumu (solid) umajimaji (liquid) au hali ya gesi (gas). Mfano maji yanaweza yakawa barafu au yakawa mvuke. Gesi haina shakil maalum na huelea hewani.

Elementi inagawika makundi matatu:

1. Metali

2. Zisizo metali

3. Nusu metali

Metali halisi ni 78. Katika hali ya kawaida 77 ziko katika hali ya ugumu. Isipokuwa mercury iko katika hali ya umaji. Inachemka katika nyuzi joto 357.3 na inaganda katika nyuzi joto -39.4. Vitu vigumu vikivunjwa kwa nyundo havigeuki vumbi bali vinababataa na kubadilika shakli. Atom ya metali moja ikiungana na atom nyengine huchukua alama chanya ya umeme (+) na wala haichukui alama hasi (-). Kwa hivyo metali mbili haziwezi kuungana kwa sababu atom mbili zenye alama chanya hazikaribiani bali zinaepukana.

Zisizo metali ziko 17. Moja iko katika hali ya umaji, tano ziko katika hali ya ugumu na kumi na moja ni gesi. Zilizo katika hali ya ugumu zinapovunjwa hugeuka vumbi wala hazibabatai na kugeuza shakli. Makaa ya mti yaliyo safi ni miongoni mwa zisizo metali. Kwa lugha ya kikemia huitwa karbon. Zisizo metal zinaweza kuchukua alama umeme chanya au hasi. Hivyo baadhi ya zisizo metali zinaweza kuungana na kufanya molikuli.

Kuungana kuko kwa namna mbili. Pale ambapo zilizoungana ni Karbon na hydrogen huitwa organic. Hivi vinaweza kuunguana na hupatikana kwenye viumbe hai. Leo baadhi yao vinaweza

kutengenezwa viwandani. Mafuta, sukari, aseton na kwinini ni mfano wa **organik**. Vile ambavyo havina hydrojen na carbon kwa pamoja katika mchanganyiko wake huitwa **inorganik**. Hivi hupatikana katika ardhi na vyengine vimeyayuka katika bahari. Chumvi ya kupikia, maji, chokaa, mchanga ni mfano wa vitu hivi.

Vitu hivi vyote visivyo na roho huchanganyika na kufanya **cell** ambayo ndio msingi wa kutengenezea vitu vyenye uhai. Cell ni kitu chenye uhai. Cell ya mimea haifanani na ile ya binaadamu. Cell ya binaadamu inafanana na ya wanyama. Cell huungana pamoja katika kutengeneza kiungo fulani cha mwili. Viungo vinapoungana ndio hupatikana mwili. Muungano huu ndio unaoleta kupatikana **mimea, wanyama** na **binaadamu**.

Viumbe vyote vinagawika mafungu matatu; **wanyama, mimea na viumbe visivyo na uhai.** Katika kundi la wanyama, binaadamu ndie mbora kuliko wote. Kila fungu lina yule kiumbe alie juu zaidi na yule alie chini zaidi. Na haya mafungu pia kuna lililo bora zaidi na duni zaidi. Alie chini zaidi katika kundi moja anakaribiana kisifa na yule alie juu kabisa katika kundi la chini yake. Mfano chaza inafanana na jiwe lakini inazaliana na kukua kama kiumbe chenye uhai. Mfano mtende na mkamata wadudu vinahisia kama za wanyama. Mitende iko jike na dume. Mtende dume unapinda kuuelekea mtende jike. Iwapo mtende jike haukupata maji maji kutoka kwa mtende dume basi hauwezi kuzaa. Uhakika ni kwamba mimea yote inayo hali ya kuhitaji kupeana mbegu za uzazi ila mtende ndio unaonekana kuwa na hali hii zaidi. Inaelezwa kwamba katika mtende kuna kitu cheupe kinachofanya kazi kama moyo wa mnyama. Sehemu hiyo ikijeruhiwa au kukaa maji basi mtende hukauka. Katika hadithi sharif tunasoma **(Uheshimuni mtende; ni shangazi yenu huo. Kwani mtende wa mwanzo uliumbwa kutokana na dongo lililobakia katika kuumbwa [baba yenu] Adam)**. Hii inathibitisha kuwa miongoni mwa mimea huu ndio wa daraja la juu.

Miongoni mwa wanyama yule alie duni kabisa ni yule anaeitwa sponji, anaetembea na kuishi majini. Kuna viumbe vingi duni ndani ya maji ambavyo kutokana na hivyo viumbe vyengine huumbwa. Mpangilio wa ubora wao umeainishwa katika vitabu vya biolojia. Kila kundi lina aina mbali mbali ya viungo kwa ajili ya kujipatia chakula na kujilinda vikiwemo upinde, meno, kucha, mbawa, hila na kadhalika. Kila kundi limepewa njia za kujikinga nafsi yake na kizazi chake kisipotee. Katika njia zao za maisha kuna mambo mengi yenye kushangaza akili ya binaadamu. Nyuki kama muhandisi mahiri wanatengeneza sega lenye muundo wa pembe sita. Lau kama

wangelitengeneza katika muundo wa silinda basi kungekuwa na uwazi baina yake. Prizma ya pembe sita haipotezi nafasi. Wangelitengeneza kwa pembe nne nafasi yake ingekuwa ndogo. Elimu hii binaadamu huipata kwa utafiti na kusoma. Asiesoma hawezi kuijua. Je! ni nani aliempa nyuki elimu hii? Allahu taala ndie aliempa nyuki **ilham** hii. Ilham leo inaitwa **hisi ya ndani**.

Na katika mpangilio wa madaraja ya wanyama, binaadamu ndiye wa daraja la juu kabisa. Kisha hufuata farasi, kima, tembo na katika ndege ni kasuku. Ufahamu wa nyani na tembo haukutafautiana sana na baadhi ya watu wengi. Darwin ameandika kwamba katika mpangilio wa daraja la wanyama nyani ndie wa juu. Hata wale wanasayansi waovu wapinzani wa Uislam wanadai kwamba, Darwin ameelezea chanzo cha binaadamu kuwa ni nyani ambae kwa muda aliendelea kukomaa na kuweza kuchukua umbile la binaadamu. Hawa wamesonga mbele zaidi na kusema kuwa Adam hakuumbwa kwa udongo na kuwadanganya watoto wa kiislam. Uhakika ni kwamba Darwin hakuandika katika kitabu chake kwamba wanyama huboreka, kukomaa na kuwa kabila nyengine. Alichoandika ni kwamba kuna mtiririko maalum wa ukamilifu katika kuumbwa kwao. Alichosema chengine ni kwamba wale wa daraja la chini huwa ni chakula kwa wale wa daraja la juu. Hali hiyo wanazuoni wa kiislam waliijua zamani, waliieleza na kuiandika. Darwin alizaliwa mwaka 1224 hijria [1809 miladia] na kufa 1299 hijria [1882 miladia]. Mpangilio huwo wa daraja za wanyama tuliouandika hapo juu ulielezewa zamani mno na Ali bin Amrullah „rahimahullahu taala" aliezaliwa mwaka 916 hijria na kufa mwaka 979 hijria [1570 miladia]. Ni wazi kwamba Darwin aliyachukua maandishi haya kutoka kwenye vitabu vya waislam.

Wale walio daraja la juu katika wanyama, huwa ni daraja la chini kwa binaadamu. Wale wanaoishi majangwani na misituni ni miongoni mwa binaadamu wa daraja la chini. Binaadamu wa daraja la juu ni wale wanaoishi mijini baina ya latitude 23 na 66.

Ukiachilia mbali hizi tafauti za kimaumbile pia hupatikana tafauti nyengine zinazotokana na kufanya jitihada katika kazi na kuboreka kihali na kitabia. Wengi wametumia akili zao kutengeneza ala mbali mbali na wengine wakapata maendeleo ya sayansi, teknolojia na elimu ya akili. Waliofikia daraja la juu kabisa ni wale ambao mbali ya kuendelea kisayansi na kiteknolojia, pia waliboresha tabia zao na kujikurubisha kwa Allahu taala hivyo kufikia daraja la juu kabisa la mwanadamu. Hawa huwaongoza wale walio chini yao ili nao wafikie daraja la juu. Walio juu kwa daraja ni mitume "alayhimusalawatu

wataslimat" ambao Allahu taala amewapa heshima ya kuwapelekea malaika Jibril aleyhi salaam kuwajusa amri na makatazo yake. Mambo haya yaliyoshushwa kwa mitume alayhimu salaam huitwa **wahyi**. Wahyi huu mitume "alayhimusalawatu wataslimat" waliufikisha kwa watu na hii ndio njia inayowawezesha kufikia daraja la juu kabisa la ubinaadamu. Njia ya kufikia daraja hilo huitwa **dini**. Binadamu wanaweza kuboreka na kupanda daraja hata kuipita daraja ya malaika. Daraja za mitume nazo ni nne. La kwanza ni **nabii**, la pilli ni **rasuli** na la tatu ni **ulul azmi** na katika daraja hili wapo **Adam, Nuh, Ibrahim, Musa, Isa** na **Muhammad** "alayhimu salaam". Daraja la nne ni khatamul anbiyaa yaani mtume wa mwisho. Daraja hili la juu kabisa ni mahsusi kwa Muhammad „swallallahu alayhi wasallama". **(Lau kama si wewe, lau kama si wewe, nisingeumba kitu chochote!)** sifa hii ni ushahidi kwamba binaadamu ni mtukufu kuliko malaika.

Daraja la binaadamu lipo katikati ya viumbe vyote. Ikiwa atafuata Uislam atapanda daraja na kuwapita malaika. Na akiuacha Uislam na kufuata marafiki waovu daraja yake itashuka na kuwa chini kabisa. Kama tulivyoelezea huko nyuma kwamba roho ni Mujarrad ila kiwiliwili ni mchanganyiko wa vitu vyenye sifa zilizotafautiana. Kiroho binaadamu anafanana na malaika ila kiwiliwili chake kinafanana zaidi na wanyama. Ikiwa upande wa roho utapata nguvu basi binaadamu huwakaribia zaidi malaika. Kupata nguvu kwa kiwiliwili kunamkaribisha zaidi binaadamu kwa wanyama na kumuweka mbali na malaika na kwenda kinyume na hilo ni kuwakaribia malaika. Malaika hawana umbile la kinyama na wema umeumbwa pamoja na malaika.

Iwapo mtu ataifuata nafsi basi atakuwa duni kuliko wanyama. Katika suratul Aaraf aya ya 178 na suratul Furkan aya ya 44 katika maana ya sehemu ya aya **(bali wao ni duni zaidi kuliko wanyama)** inaeleza uovu wa watu hao. Wanyama hawana akili wala hawana roho inayofanana na malaika. Kufuata matamanio sio kosa kwao. Binaadamu wamepewa muangaza wa akili hivyo kwa wao kufuata matamanio ya nafsi na kuiacha njia sahihi ni uovu mkubwa.

***Binadamu ni mchanganyiko, malaika na mnyama.***
***Amfatae malaika, nae hutukukuka bali hata kumpita***
***Awae na tabia za mnyama, ndie muovu wa viumbe wote.***

Mahitaji yote ya lazima kwa mnyama kama, hewa, maji, chakula, makazi na mwenza vyote vimeumbwa tayari.

[Miongoni mwa hivi cha lazima zaidi ni hewa. Haiwezekani kukaa bila hewa na kuikosa hata kwa muda mfupi, kiumbe hufa. Lau kama hewa nayo ingekuwa ni ya kutafuta na kuifanyia kazi basi muda

usingetosha kwa hilo, tayari kiumbe kingekuwa kimeshakufa. Kwa umuhimu wake, Allahu taala ameieneza hewa kila pahali na akaiwezesha kuingia katika mwili wa binaadamu hadi kufikia ndani ya mapafu yake. Maji si muhimu sana kama hewa na wanaadamu wanao wakati wa kutosha kuyatafuta. Wanyama kwa vile hawana akili na wala hawasaidiani, hawawezi kutayarisha chakula chao na kinywaji chao. Hawalazimiki kupika wala kuandaa chakula chao. Hata majani tu wanajilia. Wanajifunika kwa manyoya na sufi. Ala zao za kujilindia wameumbwa nazo. Wao si wenye kuhitajiana.

Binaadamu analazimika kuyafikiri yote haya na kuyatayarisha. Bila ya kulima nafaka, mkate wake haupatikani. Bila ya kushona nguo, cha kuvaa hakipatikani. Ili kujilinda wanalazimika kutumia akili zao, kusoma sayansi na teknolojia na kuanzisha viwanda. Uweledi aliopewa kila mnyama, umekusanyika kwa binaadamu na ili aweze kuutumia lazima aitumie akili yake kufikiri na kuihangaisha. Funguo za furaha na maangamizi zote ziko mikononi mwa binaadamu. Kutukuka au kudhalilika kumeachwa mikononi mwake. Ikiwa atatumia akili na maarifa aliyopewa, akaiona na kuifuata njia ya kuweza kutukuka basi atafikia hali hiyo. Atapanda ngazi kwa ngazi hadi kufikia daraja ya malaika. Lakini ikiwa atachagua kufuata matamanio ya nafsi yenye madhara, na akabakia katika daraja la wanyama kama alivyoumbwa basi hali inakuwa kinyume chake. Ataporomoka na kuporomoka hadi kufikia chini kuliko walio chini. Atafikwa na balaa moja kuelekea jengine hadi kubururwa na kuingizwa ndani ya Jahannam.

Kimaumbile binaadamu ana pande mbili. Anahitaji mwalimu (ustadh) ili kumsaidia kuugundua na kuuendeleza upande wake mwema. Baadhi ya watoto huongoka kwa nasaha, maneno mazuri na zawadi. Wengine ili kuwaongoza wanahitaji ukakamavu, maneno makali na adhabu. Ustadh anatakiwa awe mweledi kumjua mtoto ni wa aina ipi na ni njia ipi sahihi inayomfaa katika malezi; ya ukakamavu au ya ulaini. Akikosekana mkufunzi kama huyu basi malezi ya mtoto hayatokuwa sawa. Malezi yaliyo sahihi ndio yatakayomuokoa mtoto na maangamizi na kumuelekeza kwenye furaha.]

***Haku taala ameisifu elimu sehemu nyingi,kwenye kur-an***
***Maneno ya mtume yenye kuamrisha elimu yako wazi.***

***Elewa,adui mkubwa wa Uislam ni ujinga***
***Ujinga ni maradhi hatari ya vimelea vidogo***

***Mtume amesema penye ujinga dini hupotea***
***Hivyo apendae dini,apende elimu na sayansi***

*Je hadithi haikusema kuwa pepo iko chini ya upanga*
*Amri ya kurusha jeti na kutumia nguvu za atom iko wazi*

*Udhalili wa Uislam ni ujinga,ndio ila zote*
*Ewe janga la ujinga, haliko kwako taifa hili*

*Umelifikisha katika hali ya kwamba hakuna dini wala heshima*
*Ewe jinamizi jeusi ulieuangusha Uislam*

*Ewe adui haini,ilikuwa nikuue tangu mwanzo*
*Wewe ndie uliewafanya makafiri wawe juu yetu*

*Amka ewe taifa,unaangamia kwa ujinga wako*
*Umeshapewa jina kuwa Uislam ni kubaki nyuma*

*Ona haya alau kwa Allah.niachie dini yangu*
*Kama kinyesi utadidimia kwenye dongo*

*Lakini kwa maneno yangu tu,ujahili hauathiriki*
*Na ni elimu inayopelekea kuona haya kwa ajaili ya Allah.*[1]

## NYONGEZA YA PILI YA UTANGULIZI

Katika nyongeza hii tutaelezea maana ya roho kupanda daraja na kuporomoka.

Mambo ambayo yataipelekea roho kupanda daraja au kuporomoka tumeshaelezea kabla. Hapa tutaelezea zaidi. Kama ambavyo kila kitu kina sifa za jumla kama uzito na tambo, kitu hicho pia kina sifa mahsusi zinazo kitambulisha. Mfano kila kitu kina mchanganyiko wa kikemia unaojulikana. Kila maji yana daraja la ujoto la kuchemka na kuganda. Kila chuma kina daraja lake la joto la kuyayuka. Kila mwangaza una mawimbi yake yenye urefu maalum ujulikanao. Basi ni hivyo hivyo kwa vitu vyenye uhai, navyo vina wasifu na sifa maalum zilizo mahsus kwao. Kwa mfano majani yaitwayo dijitali yanafahamika kuwa na athari kwa moyo. Farasi anafahamika kwa

[1] Sadri Azam MustafaRashid Pasha alikuwa ni masoni.Kufuatia amri aliyopewa na waingereza akaondoa elimu ya sayansi katika maskuli. Wakakosekana wanasayansi. Silaha za kisasa zikashindwa kutengenezwa. Vito vilivyofuata vyote tukashindwaHuu ndio uadui mkubwa walioufanya Waingereza kwa Uislam.

utiifu kwa bwana wake na ukimbiaji wake. Lau kama farasi angelikuwa hana sifa hizo basi angelikuwa kama punda na kabebeshwa mizigo.

Pamoja na kwamba binaadamu ana sifa nyingi zinazofanana na wanyama, mimea bali hata viumbe visivyo na uhai, binaadamu pia ana sifa mahsusi zinazomtambulisha kama binaadamu. Sifa hizo ndizo zinazompa heshima ya kibinaadamu. Sifa hizi ni uwezo wa roho wa kufikiri na kuelewa **(Nutk)**. Hapa Nutk hatukusudii kuwa ni uwezo wa kuzungumza kwa sababu hata bubu nae ni binadamu kwa sababu anayo nutk; anazingatia na kuelewa. Kasuku anazungumza ila si binaadamu kwa sababu hana nutki, hazingatii, hana fikra na akili, wala haelewi. Hivyo kinachompambanulia tabia nzuri na mbaya, tendo zuri na baya ni hii Nutku. Allahu taala amempa hii binaadamu ili aweze kumjua muumba wake. Kwa kutumia nguvu hii ya moyo na roho, na kwa kutumia neema ya akili, binadamu anatakiwa kuangalia kwa mazingatio vilivyomo mbinguni na ardhini na kuweza kutambua uwepo wa Allahu taala na sifa zake zilizotukuka. Kisha atazifuata amri zake na kuyaacha makatazo yake na kuweza kufikia furaha ya duniani na akhera na kuokoka na maangamizi. Tunasoma katika suratu Dhariat aya ya 56 katika maana ya aya **(nimewaumba binaadamu na majini ili waniabudu).** Maana ya 'waniabudu' katika aya hii ni 'wanijue mimi. 'Yaani tumeumbwa ili tumfahamu Allahu taala na tumuamini. Upande ambao binadamu na wanyama wanafanana ni katika matashi ya kishahawa na ghadhabu yanayotokana na ile roho ya kinyama. Vitu hivi viwili si muhimu kwa roho ya kibinaadamu. Vinapatikana kwa wanyama vile vile na vina nguvu zaidi kwa wanyama kuliko kwa binaadamu. Mfano n'gombe na punda wanakula zaidi kuliko binaadamu. Nguruwe na ndege wana shahawa zaidi kuliko binaadamu. Simba, tembo na Nyati wana nguvu zaidi kuliko binaadamu. Chui na mbwa mwitu ni wapambanaji na wararuaji mahiri zaidi kuliko binaadamu. Panya, mbwa na paka wanaona hata kwenye kiza. Wanaweza kunusa harufu ya kitu kilicho mbali. Sifa hizi sizo zilizompa utukufu binaadamu. Lau kuwa utukufu unapatikana kwa sifa kama hizi basi wanyama hawa wangelikuwa watukufu zaidi ya binaadamu. Utukufu wa binaadamu unatokana na zile nguvu mbili alizonazo kwenye roho. Kwa elimu na nutku ya roho na moyo anayafahamu yenye fadhila na yaliyo matukufu na kwa nguvu za amali, anashikamana nayo na kujiepusha na maovu.

Kumfahamu Allahu taala na kumuamini hakutoshi kwa kutamka tu. Masharti sita ya imani yanatakiwa kuyaamini maana yake kwa

moyo. Sharti la tano ni kuamini siku ya **kiama**, kwa maana ya kwamba kuna kufufuliwa baada ya kufa.

Maadui wa kiislam wanasema kwamba (Neema za peponi zilizotajwa ni katika yale mambo yenye kusisimua shahawa za matamanio ya kinyama kama vile nyama za ndege, matunda, maziwa, asali safi, makasri na mahurul ayni; mambo ya kuupa ladha mwili. Kwa vile furaha ya moyo inaendana na mambo yaliyoamuliwa kwa elimu na busara yenye kumpandisha mtu daraja na mfano wa hayo, kufuatana na sifa za pepo zilizotajwa, haya yanaonekana kama yatasahaulika na yatakayokuwa mbele ni yale yanayohusu shahawa za kiwiliwili. Katika hali hii basi, wale waliokuwa watukufu hapa duniani kama mitume “alayhimusalawatu wataslimat” na mawalii “rahimahumullau taala”, watakuwa daraja la chini huko peponi hata kuwapita wanyama. Jambo jengine ni kwamba ili uweze kulifurahia jambo lazima kwanza uwe umepata machungu ya kulikosa jambo lile. Mfano ili ukifurahikie chakula, lazima kwanza upate machungu ya njaa. Ili uweze kuufaidi usingizi, lazima kwanza upate machungu ya uchovu. Lakini kwa vile peponi hakutakuwa na machungu yoyote basi haitowezekana kupata ladha ya vitu vipendezavyo). Pamoja na kwamba Ibni Sinaa anataja siku ya kiama katika vitabu vyake **Shifaa** na **Najaat** lakini katika kitabu chake **Muad** anaeleza wazi kwamba yeye haamini kufufuliwa. Nasirudyn Tusi nae vile vile ametaja mambo ya kufufuliwa katika baadhi ya sehemu za kitabu chake kiitwacho **Tajrid** ila katika sehemu nyengine ameeleza kinyume na hayo.

Wanazuoni wa ahli sunna kwa kauli moja wanasema kwamba hiki kiwiliwili kitarejeshwa tena siku ya kiama. Ladha za peponi kuzidhania kuwa zitakuwa ni ladha za kiwiliwili tu hilo ni kosa. Roho ambayo imeanza kupanda daraja hapa duniani, itakapoufariki mwili itaendelea kupanda daraja hadi siku ya kiama. Mwili utakapokuwa peponi ili uweze kudumu daima humo utabeba sifa tafauti na zile za duniani. Roho iliyopanda daraja itaungana tena na kiwiliwili katika maisha ya peponi. Ndani ya pepo, roho na mwili vitakuwa na neema na ladha tafauti tafauti. Wale wa daraja la juu, hata watakapokuwa peponi basi watazipa muhimu ladha za roho ambazo zitakuwa ni tafauti, na za daraja la juu zaidi kuliko zile ladha za kiwiliwili. Miongoni mwa ladha za roho iliyo tamu na bora zaidi ni kumuona Allahu taala. Baadhi ya wanazuoni wanajuzisha kuwa baadhi ya watu waliofikia daraja la juu la uchamungu wanaweza wakaingia pepo ya roho wakati bado wangali duniani. Pepo ya kiwiliwili haiwezi kufikiwa ukiwa bado duniani. Ladha za akhera si sawa na ladha za dunia na wala hazifanani. Allahu taala

anatuelezea ladha za peponi kwa mfano wa vile alivyoviumba katika dunia ili akili zetu ziweze kupata kukisia tu. Pia dai la kuwa ili kupata ladha huko akhera lazima kwanza itanguliwe na machungu pia si sahihi kwa sababu muundo wa kiwiliwili na sifa zake huko akhera utakuwa tafauti na huu wa kidunia. Kiwiliwili cha duniani kimeumbwa kwa kuzingatia kwamba siku moja kitatoweka na uzima wake hauzidi miaka mia. Kiwiliwili cha akhera kitaumbwa ili kiweze kuishi milele. Mfanano wa hivi viwili ni kama mfanano wa binadamu na sura yake anaposimama mbele ya kioo. Akili ya binaadamu haiwezi kuyafahamu yale ya siku ya kiama. Akili ya binaadamu inafahamu yale yanayohisika kwa viungo vya fahamu na mfano wake. Kuzifananisha neema za peponi na ladha za duniani na kujaribu kutumia fikira na mantiki katika kuzijadili na kuzihukumu, itakupelekea kwenye matokeo mabovu na yasio sahihi. Kufananisha baina ya kitu ukijuacho na kile usichokijua si jambo sahihi.

Kufuatana na magwiji wa tasawwuf na baadhi ya wanazuoni wa kiislam "rahimahumullahu taala" ndani ya dunia hii kuna dunia nyengine iitwayo ya mfananisho **(Alam Mithal).** Haikufanywa kwa vitu kama ulivyo ulimwengu wa vitu wala haikufanywa kwa Mujarrad kama ulivyo ulimwengu wa kiroho. Upo kati ya hali hizo mbili. Viumbe vilivyoko katika ulimwengu huo vinafanana na vile vya ulimwengu wa vitu kwa vile vinaweza kugawika na kuwa vipande vipande ila vinatafautiana kwa vile havina uzito wala havichukui nafasi. Kila kitu cha hapa duniani na kila maana basi mfano wake huko unapatikana. Maji ya hapa duniani ni sawa na ya huko. Elimu mfanano wake huko ni maziwa. Tabia njema na matendo mema huko huwa ni tikiti, mauwa na matunda mazuri mazuri. Mifarakano na matendo maovu ya duniani huko hufananishwa na kiza, nyoka, ng'e na vitu vyengine vyenye kumpa binaadamu dhiki. Ndoto zote tunazoziona zinatoka katika ulimwengu huo. Kufuatana na wataalamu wa tasawwuf hii Alam mithali nayo inagawika sehemu mbili. Ikiwa wataalamu hawa wataingia ulimwengu huo kwa nguvu za fikira tu hapo huitwa ulimwengu wa mfanano wa kufikirika. Na iwapo wataalamu hao watauingia ulimwengu huo sio kwa fikra na wala sio kwa hisia za viungo vya hisia vya ndani basi huo huitwa ulimwengu wa mfanano wa uhakika. [Katika kitabu cha **Maktubat** juzuu ya pili barua ya 58 ulimwengu huu wa mfanano umeelezwa kwa kirefu. Tarjama ya barua hiyo refu inapatikana katika kitabu **Saadat abadiyya** sehemu ya kwanza mada ya 39.] Baadhi ya wanatasawwuf kwa kufanya **riadha** na **mujahada** wameweza kuingia katika ulimwengu huo na kuelezea

habari zake. Wanazuoni wametaja juu ya kuwepo ulimwengu huu na siri zake. Abdullah ibn Abbas “radiyallahu anhu” anasema (Kuna ulimwengu mwengine mbali na huu tunaouona. Huko kila tukionacho hapa mfano wake upo. Huko hata Abdullah ibn Abbas kama mimi pia yupo).

Magwiji wa Tasawwuf “rahimahumullahu taala” wanasema, binaadamu anapokufa roho inaufariki mwili. Wakati mtu anapokuwa duniani, mambo mema anayoyafanya, imani na tabia njema, hivi huchukua sura ya nuru, mwangaza, mauwa, makhuri, makasri na mapambo. Mambo ya kijahili, maovu na tabia mbaya nayo huchukua sura ya moto, kiza, nyoka, nge na kadhalika. Roho yenye imani na mwenendo mwema huvipeleka vitu vyake vya peponi yenyewe na ile roho ya kafir na fasik huvipeleka vitu vyake vya motoni yenyewe. Wakati roho inapoendelea kuwepo katika ulimwengu huu wa vitu haiwezi kuyaelewa haya. Kushikamana kwake na kiwiliwili na kuzama katika ulimwengu huu wa vitu unaizuia roho isiyajue haya. Wakati roho inapoufariki mwili, kizingiti hiki kinaondoka na kuanza kuiona ile mizigo ya mema na maovu iliyoitanguliza. Maisha ya kidunia ni sawa na hali ya kulewa na mauti ni sawa na kutoka kwenye ulevi. Mlevi kama atajiwa na mtu ampendae au zawadi azipendazo hawezi kujua. Kadhalika kama nyumbani mwake mtaingia nyoka na nge hawezi kujua. Anapotoka katika ulevi ndio anayaona haya na kufahamu. Hii hali ya akhera ni kama hali ya Alem mithali. Sadedyn Teftazani “rahimehumullahu taala” katika kitabu kiitwacho **Sharhul makasid** baada ya kuieleza hii Alam mithali anasema kuwa kwa vile mambo haya yamekosa ithbat na dalili, wanazuoni wa kweli hawakuyapa umuhimu. Wanazuoni wa kweli anakusudia ni wale ambao katika mambo ambayo akili inakubali, basi wao huyathibitisha kiakili. Hata hivyo kitu ambacho akili haikifikii, hata kama hukiafiki, usikatae kuwa hakipo. Hata Ibni Sinaa ambaye ni mmoja wa wenye kufuata akili anasema (Kitu ambacho hakiwezi kuthibitishwa kuwa hakipo, Hakiwezi kuambiwa kuwa hakipo. Kwa sababu kukataa kuwepo bila ya kuthibitisha ni kukanusha kutokufahamu kwako, jambo ambalo ni aibu na upungufu).

Shihabudyn Shuhreverdi “rahmatullahi alayhi” anasema (Kama ambavyo tunaamini, bila ya kuona, maneno ya wataalamu wa astronomi kwamba kuna mamilioni ya nyota na zinatembea pamoja kwenye anga bila ya tatizo, basi inalazimisha vile vile kuamini ulimwengu wa roho na Alam mithali vilivyogunduliwa na wataalam wa Tasawuf). Lililo sahihi ni kuwaamini wanosema sio wanaokataa.

[Mwenye akili na aliyesoma sayansi, ni rahisi kuthibitisha uwepo na upweke wa Allahu aala. Kuamini akhera hakuko hivyo. Huku kunahitaji kuamini yale ambayo Allahu taala ameyatolea habari.]

Watu wanagawika makundi manne:

1. Wanaoamini mitume na kuwafuata. Hawa hupata raha na utulivu duniani na khera huingia peponi moja kwa moja. Zile dhambi walizozipata kwa kufuata matashi ya dunia, wanaleta toba kwa moyo na istighfar kwa ulimi, wanayakabili mazito ya dunia na kusamehewa dhambi zao. Wataingia peponi moja kwa moja na watakaa humo milele.

2. Wanaoamini mitume na kuwafuata. Wanaishi duniani kwa shida, matatizo na maradhi. Wanafanya subira kwa matatizo wayapatayo na wanashukuru. Kutokana na subira zao, neema zao za kudumu zinaongezeka. Hawa hawafuati matashi ya nafsi. Hawa ni mawalii na ni wachache sana.

3. Wanaoamini mitume lakini wanafuata nafsi zao. Wanapata matatizo duniani. Akhera wataadhibiwa kutokana na madhambi yao waliyoyatenda kwa kufuata matashi ya nafsi zao, ila hatimae wataingizwa peponi. Hawa huitwa waja fasik. Ama wale ambao watachukia alau moja ya amri za Uislam basi hao ni makafiri na hawatoingia peponi.

4. Wasioamini mitume. Wale makafiri ambao kwa kutumia akili zao tu hufanya na kufuata mambo kama yale yaliyoamrishwa na uislam au hufanya kwa kuwaiga waislam basi hao watapata furaha ya duniani.

## ELIMU YA MAADILI NA MALEZI KATIKA UISLAM

Elimu inayoelezea hali ya roho na moyo huitwa **elimu ya tabia**. Wakati mtu anapokuwa peke yake, hali hizi zimeelezwa katika milango tisa. [Sisi katika kitabu hiki tutaelezea milango sita tu.]

## MLANGO WA KWANZA

Katika mlango huu aina za tabia, mambo mema na maovu yatatajwa. Tabia ni mazowea ambayo yanamuwezesha mtu kufanya jambo bila hata kufikiria. Tabia iliyokwisha kuwa ya kudumu huitwa **Malaka** na ile ya mpito tu huitwa **Hali**. Mfano kucheka, kuona haya hizi ni Hali. Ukarimu na ushujaa ni mifano ya Malaka. Wakati inaposemwa tabia hufahamika kuwa ni Malaka. Wakati mwengine kufanya wema haina maana kuwa ndio tabia yako. Ikiwa kila wakati mtu atakuwa anafanya wema ndio ataambiwa ni tabia yake. Na ikiwa atakuwa

anafanya kila wakati lakini kwa kujilazimisha basi hiyo pia haijafikia kuitwa tabia. Ili iambiwe kuwa ndio tabia yako inatakiwa uwe unaifanya kwa mapenzi.

Tabia inapelekea kufanya zuri, baya au kufanya jambo la kawaida lisilo zuri wala baya. La kwanza huitwa **tabia njema**, mfano ukarimu, ushujaa na upole. La pili huitwa **tabia mbaya** mfano woga kwa mwanamme. La tatu si tabia njema wala mbaya. Ushoni, kilimo ni mfano wa mambo hayo. Katika kitabu hiki tutataja yaliyo katika fungu la kwanza na la pili.

Tumezungumza katika utangulizi kwamba moyo na roho vina nguvu aina mbili. Ya kwanza ni nguvu ya kujua na kudiriki ambayo tuliita **Nutki** au **akili**. Kwa nguvu hii ndiyo vinafahamu vitu vinavyochanganuliwa na akili. Ya pili ni nguvu ya utekelezaji. Kila moja ya hizi aina mbili za nguvu nayo inagawika sehemu mbili. Aina ya kwanza inagawika kwenye **hikma ya kinadharia** na **hikma ya kivitendo**. Aina ya pili inagawika kwenye **shahawa**, ambayo ni nguvu inayosukuma kuyaelekea mambo yenye kuleta ladha na sehemu ya pili ni **ghadhabu** ambayo ni nguvu yenye kuyasukuma mbali yale tusiyoyapenda. Nguvu nne hizi zinatekeleza mambo tafauti. Mambo haya ikiwa yatakuwa yenye kuafikiana na akili, mazuri, yasiyo na mapungufu wala ziada, basi mwenye kuyafanya huwa ni mtu wa tabia njema. Yule ambae kutakuwa na mapungufu au ziada katika utendaji wake basi atakuwa ni mtu wa tabia mbaya. **Hikma** ya kinadharia ikiwa nzuri hiyo huitwa busara na hikma ya kivitendo ikiwa nzuri hiyo huitwa **Uadilifu**. Iwapo miongoni mwa nguvu za utekelezaji, nguvu za shahawa zikiwa ni nzuri basi hiyo huwa ni **Iffat** na sehemu ya ghadhabu ikiwa nzuri huo huwa **Ushujaa**. Misingi ya wema ni haya mambo manne. Uadilifu hakuna uchache na mwingi. Hayo matatu yaliyobaki kuzidi au kupungua daraja ya wastani inakuwa ni tabia mbaya. Hekima ikiwa nyingi ni ujuaji na ikiwa chache ni ujinga. Uadilifu hakuna mwingi uliopita daraja wala mchache. Isipokuwa kuna kinyume cha uadilifu ambayo ni **dhulma**. Iffat ikiwa nyingi huitwa **Fujur** na iwapo chache huitwa **Humud**. Ushujaa ukiwa mwingi unakuwa ni ushupavu, na ukiwa mchache unakuwa ni woga. Mgawiko huu wa kitabia ameuainisha Imam Nawawy katika kitabu chake cha **Ihya**. Abdulghani Nablushy aliyefariki huko Sham mwaka 1143 hijria [1731 miladia] pia ameyaandika haya katika kitabu chake kiitwacho **Hadikatun nadiyya.** Kitabu hiki ni cha kiarabu na kilichapishwa Istanbul na Hakikat Kitabevi. Baadhi ya wengine wanasema kwamba hekima, ushujaa na iffat vikikusanyika pamoja ndio hufanya **uadilifu**.

Mwenye tabia ya ujuaji huitumia nguvu ya akili kwa kufaya hila, kusengenya na maskhara. Mwenye tabia ya ujinga hafahamu uhakika wa mambo. Hawezi kupambanua mazuri na mabaya. Mwenye tabia ya ushupavu huweza kujiingiza kwenye hatari kwa kupambana na adui ambae amemzidi sana kinguvu. Mwoga hawezi kusubiri wala havumilii. Hawezi kugombania haki yake. Mwenye tabia ya Fujur huwa ni mtu wa kula, kunywa na kuogelea kwenye mambo ya makruh na haram. Anatumia matashi yake kwenye vitu viovu na vibaya. Na yule Humud hujinyima hata yale halali na yaliyoruhusiwa miongoni mwa mambo matamu. Ima ataiangamiza nafsi yake au kizazi kitakatika.

Tabia njema zote za binaadamu zinazalika kutokana na tabia njema kuu nne zilizotajwa hapo juu. Kila mtu anajifakharisha kwa sifa nne hizi. Hata yule anayejifakharisha kwa ukoo wake na jamaa zake basi anajifakharisha kwa sifa nne hizi.

## MLANGO WA PILI

Hapa tutavitaja vigawanyo vya tabia njema kuu nne. Vigawanyo vinavyozaliwa na tabia kuu nne hizi ni vingi visivyo idadi. Kukielezea kila kimoja haiwezekani. Hapa tutayataja yale yaliyo mashuhuri katika waliyoyataja mabingwa wa elimu ya maadili ya kiislam.

Hekima inakuja na tabia njema saba:

1. **Zakaa:** Ni malaka (tabia ya kudumu) Ni mazoea. Kwa msaada wa hili binaadamu huwa na uwezo wa kuyagundua yasiyojulikana kutoka katika yanayojulikana Huweza kukusanya dalili na kulifichua linalotafutwa. Ili kuweza kufikia hili kwa msaada wa vitu maalum, ni lazima kutafiti vitu visivyojulikana na kufanya maswala ya kihisabati na ya kijometri.

Watu wanatafautiana katika zakaa yao. Wenye zakaa ya hali ya juu kabisa ni wale watu wanaotajwa kuwa na akili nyingi. Zakaa hupimwa kwa kipimo kiitwacho **IQ Test.** Msaikolojia maarufu wa karne ya ishirini, mmarekani aitwae Terman. Terman alikuwa hai katika mwaka 1380 (1960 m) anasema kwamba kipimo cha kwanza cha kupima zakaa kilifanywa na dola ya kiothmani. Jeshi la Othman lilikuwa linasonga mbele na Viyena inatekwa. Ikitekwa Viyena, basi kuiteka Ulaya yote itakuwa ni wepesi. Dola ya Othman ilikuwa inaupeleka ustaarabu wa kiislam huko Ulaya. Kiza na kupooza kulikosababishwa na ukiristo kunabadilishwa kuwa muamko, utulivu na furaha kwa kutumia mwangaza wa elimu, sayansi na tabia njema. Maisha ya kikandamizaji na kishupavu yaliyokuwa yakiendeshwa huko ulaya chini ya madikteta, mabepari na mapapasi, yamebadilishwa na kuwapa

watu haki zao kupitia elimu, maadili na haki za kiislam. Madikteta wa Ulaya wakiongozwa na kanisa wanatumia jitihada yao ya mwisho kuzuia jeshi la Dola ya Othman. Usiku mmoja, balozi wa Uingereza aliyepo Istanbul anapeleka barua ya kihistoria huko London. **NIMESHAGUNDUA…NIMESHAGUNDUA…** Sababu inayolifanya jeshi la Othman lisonge mbele nimeshaijua. Njia ya kulizuia nimeshaijua.

Aliandika yafuatayo (Dola ya Othman wanapouteka mji wowote ule, huwapima watoto zakaa yao bila ya kujali dini au kabila na wale walio na zakaa ya juu wanawachukua na kuwapeleka katika madrasa, wanawasomesha na kuwapa malezi ya kiislam. Na wale wanaowachagua miongoni mwa hawa huwapeleka katika madrasa ya juu iitwayo **Enderun** iliyo ndani ya ikulu na huko hupewa elimu ya juu zaidi. Hivyo wanasiasa na makamanda wa dola ya Othman ndio hawa wateule wenye zakaa ya hali ya juu. Kina Sokullu na Kopru wametokea katika kundi hili. Ili kuzisitisha nguvu za kuenea kwa dola ya kiothman na kuuhami ukristo ni lazima vyuo na madrasa ya Enderum visambaratishwe). Baada ya barua hii huko Uingereza walifungua wizara mpya ya nchi, kitengo cha makoloni. Majasusi, wamishionari na wamasoni waliofunzwa chini ya kitengo hichi walitumika kuwadanganya na kuwahadaa baadhi ya watumishi wa dola ya Othman kwa kuwaahidi maisha mazuri. Kisha walifanya ushawishi ndani ya dola ili vibaraka wao hawa wapate nyadhifa za juu. Kisha wakawatumia vibaraka hawa kujaribu kuondosha masomo ya sayansi, maadili na hata elimu za dini katika madrasa na kuwaacha waislam wajinga. Harakati hizi za chini chini zilipata mafanikio baada ya mageuzi ya kisiasa. Wakaivunja dola ya kiislam na kuisitisha nuru ya uislam iliyokuwa ikieneza furaha na utulivu.

2. **Ufahamu wa haraka:** Kuweza kufikiri haraka na kutekeleza katika hali ya dharura, tukio au mjadala na mazungumzo. Hii ni hali inayomwezesha mtu kufahamu namna ya kujibu haraka na sahihi kila inapohitajika. Hii pia inamuwezesha mtu anaposikia jambo kuweza kujua na kinyume chake. Inakichunguza kitu kinachotambulika kwa undani na kuweza kutoa matokeo yasiyotambulika. Ufahamu wa haraka pia unaonekana katika mambo mengine mbali na kufikiri.

3. Akili makini: Kuweza kujua ukitakacho kwa haraka na kukipata.

4. Wepesi wa kuelimika: Kutokuzipa kikwazo fikra na kuziachia zielekee kule zinakotaka.

5. Mipaka ya kufikiri: Wakati unapojifunza kitu muhimu, kubakia ndani ya mipaka ya hicho kitu. Ina maana kujishughulisha na lililo muhimu na kuacha lisilo muhimu.

6. Kuhifadhi: Kutosahau vitu. Roho haitakiwi isahau mambo yliyotambuliwa na akili.

7. Kukumbuka: Kuweza kuyakumbuka mambo uliyoyahifadhi kila unapotaka.

Mambo yanayopatikana kutokana na tabia ya ushujaa ni kumi na moja:

1. Kichwa kitulivu: Haathiriki na kusifiwa au kutolewa makosa. Tajiri na maskini huwa sawa kwake. Habadilishwi na matamu na machungu. Hatetereshwi na mabadiliko ya hali wala vitisho na shida.

2. Jasiri: Anasubiri na kuthubutu katika hali za vitisho na shida. Hapigi mayowe na kupayuka wala hafanyi yasiyofaa.

3. Mwenye Himma na jitihada: Hashughulishwi na cheo, ulwa, kupanda na kushuka au mali.

4. Uthabiti: Kuweza kuvumilia mazito na kuweza kuvuka vizingiti mbali mbali katika kufikia lengo.

5. Hilmi: Utulivu wa roho, kuwa na murwa na kuepuka ghadhabu.

6. Ukakamavu: Kuwa na nguvu za kusubiri na kuthubutu na kuleta upinzani wakati wa mapambano kwa ajili ya nchi, dini na kutojiachia kuwa kichekesho kwa adui.

7. Shahama: Hali ya kutaka kufikia nafasi ya juu kwa ajili ya kutoa huduma bora. Hali ya kutaka kukumbukwa kwa wema na kujisisitiza kutenda wema ili kupata thawabu.

8. Uvumilivu: Kutokutetereka wala kuchoka wakati wa kutekeleza mambo mema.

9. Tawadhuu: Kutokujitukuza mbele ya wengine kutokana na cheo cha kidunia kwa sababu cheo kimetokana na Allah, hakuna alichokipata kwa mkono wake. Wenye vyeo na mali inabidi waoneshe tawadhuu. Ni jambo la thawabu. Kuonesha tawadhuu kwa ajili ya kupata maslahi fulani au kwa kuepuka dhara fulani kama vile wafanyavyo omba omba ni dhambi.

10. Himaya: Kuihami na kuilinda dini na nchi. Kutokufanya uzembe na kufanya hima kwa kutumia nguvu zako zote.

11. Rikkat: Kutokuhuzunika kutokana na madhara anayotendewa na wengine na kutokuacha kutenda wema.

Iffat nayo inakuja na tabia nzuri kumi na mbili:

1. Haya: Kuhisi haya unapofanya jambo ovu.

2. Rifk: Rifki ni kufuata Uislam.  Maana ya neno ni huruma na kutenda wema.

3. Hidaya: Kujitahidi kuwa na tabia njema.

4. Upatanishi: Kutokuleta malumbano wakati fikra zinapotafautiana. Kutokuwa mgumu, kutokuleta ubaguzi na mifarakano na kuwa mbele kuleta suluhu na umoja.

5. Kudhibiti nafsi: Wakati unapokumbwa na shahawa, kuweza kuzidhibiti na kuziweka chini ya amri yako.

6. Subira: Ni kujiepusha na maasi na kutokuiachia nafsi kuelekea kwenye matashi maovu. Kuyakwepa yale mambo ambayo hatimae yatakupa majuto. Subira inagawika sehemu mbili. Kufanya subira kwa kutokufanya makosa. Binadamu anapata vishawishi vingi kutokana na nafsi yake na wale marafiki waovu. Kutovisikiliza vishawishi hivyo na kujizuia kufanya maovu ni thawabu. Subira inayoelezwa hapa ndio ya aina hii. Aina nyengine ya subira ni ile ifanywayo wakati wa shida na balaa mbali mbali. Wakati inapotajwa subira wengi wanafahamu aina hii. Hii pia ni subira yenye thawabu. Aina zote mbili za subira ni fardhi.

7. Kinaa: Kutosheka na mahitaji ya lazima na kutotaka ziada. Na wala sio maana yake kutokupokea unachopewa. Hiyo huitwa Taktir nayo si tabia njema. Ni jambo ambalo halipendezi kiakili na Uislam pia haukulipenda. Kinaa ni tabia njema. [Yale anayoyahitaji mtu ili asife au asipoteze kiungo huitwa mahitaji ya **dharura**. Yale yanayohitajiwa kwa matumizi ya kila siku na kukilinda kiwiliwili na madhara huitwa **mahitaji ya lazima**. Yale yaliyozidi mahitaji ya lazima, mambo yenye kupendeza, matamu yenye kupandisha hadhi na heshima yake mtu huitwa mapambo. Kutumia mapambo kwa ajili ya kutafuta kusifiwa, kujionesha na kujitukuza huwa ni kujifakharisha. Mahitaji ya dharura na yale ya lazima, ni fardhi kuyakidhi. Yale yaliyo juu ya mahitaji ya lazima kama pesa ya dawa na daktari ni sunna kuyakidhi. Mapambo ni halali. Fakhari ni haramu.]

8. Wakar: Kutokufanya pupa katika kutafuta mahitaji na vitu vyengine. Huu ni utulivu wa kutenda mambo na wala sio uvivu na kupoteza fursa.

9. Waraa: Kujiepusha na mambo yaliyoharamishwa na yale yenye shubha na kuyafanya yale yaliyoamrishwa na yenye faida kwa kila mtu. Kujiepusha na kuwa mzembe na mapungufu.

10. Nidhamu: Kufanya kazi kwa mpangilio maalum.

11. Uhuru: Kuchuma mali kwa njia za halali na kuzitumia kwa njia za halali. Kuzingatia haki ya kila mtu. Uhuru haina maana kwamba kila jambo liachiwe lifanywe.

12. Sahawa: Kupenda kutoa pesa na mali katika njia za kheri. Kutoa kwa mapenzi katika mambo ambayo Uislam umeamrisha. Sahawa maana yake ni kuwa karimu. Ni moja katika tabia njema ya

daraja la juu kabisa. Imesifiwa na aya tukufu na hadithi sharif. Kutoka katika sahawa huzaliwa tabia njema nyingi. Miongoni mwa hizo, nane zilizo maarufu ni hizi:

1. Ukarimu: Kupenda kutoa msaada wa mali katika mambo yenye faida.

2. Ithaar: Kumpa mtu mwengine mali ambayo wewe unaihitaji nawe ukabaki kufanya subira. Ni tabia njema ya daraja la juu na imesifiwa na aya karim.

3. Kusamehe: Kuacha kulipiza kisasi hali ya kuwa uwezo wa kufanya hivyo unao. Kulipa wema baada ya kutendewa uovu ni bora zaidi kuliko msamaha.

4. Murwa: Kuwapa mahitaji ya lazima wale wanaohitaji. Kupenda kuwasaidia wengine.

5. Wafaa: Kuwasaidia jamaa na marafiki katika jambo la kujikimu.

6. Muwasat: Kugawana na ndugu na jamaa neema uliyonayo. Kuishi nao vyema.

7. Samhat: Kutoa kwa kupenda vitu ambavyo huna wajibu wala ulazima kuvitoa.

8. Msamaha: Jambo ambalo si lazima kuliacha, ukaliacha kwa ajili ya faida ya mtu mwengine. Kuyafumbia macho makosa ya mtu mwengine.

Chini ya uadilifu zinazaliwa tabia kumi na mbili:

1. Urafiki: Kumpenda rafiki yako. Kumpendelea mema na mazuri na kumkinga na maovu. Kujipendekeza kwake.

2. Ulfat: Uwepo wa uwiano na ushirikiano kwa wana jamii juu ya fikra za kidini, kidunia na imani yao.

3. Wafaa: Kusaidiana na kuishi vyema. Pia hutumika kwa maana ya kutimiza ahadi.

4. Huruma: Kuhuzunika kutokana na shida na maafa yaliyowafika wenzio. Kusaidia katika kumuondoshea mwengine shida na madhila.

5. Kuunga ukoo: Kuwaangalia ndugu na jamaa, kuwasaidia na kuwatembelea. Katika hadithi sharif tunasoma **(Nimetumwa ili kuyavunja masanamu na kuwatendea wema jamaa).**

6. Mukafaa: Kulipa wema unapotendewa wema.

7. Ushirika mwema: Kuzingatia haki na kutenda kwa uadilifu.

8. Maamuzi mema: Kila wakati kuzingatia haki ya kila kitu na kutokufanya jambo ambalo litakupa majuto baadae.

9. Tawaddud: Kuwapenda marafiki zako na kuwapa zawadi. Kujipendekeza kwao.

10. Kujisalimisha: Kuyafuata maamrisho yote ya Uislam na kuyaacha makatazo yote ya Uislam, na kufuata maadili ya kiislam hata katika yale yaliyo mazito.

11. Kutawakal: Yale mambo ambayo yako nje ya uwezo wa binaadamu na ambayo hawezi kuyabadilisha, basi inafaa kuyakubali kuwa yametokana na Allah na yaliamuliwa toka Azali hivyo kuyakabili kwa subira bila kuhuzunika.

12. **Ibada:** Ni kutekeleza yale yaliyoamrishwa na kuyaacha yale yaliyokatazwa na Allahu taala alieviumba viumbe hali ya kuwa havikuwepo, mwenye kuvilinda na balaa na ajali, na mwenye kuvipa neema na mazuri kadhaa. Kutokufanya mapungufu katika kutekeleza anayoyataka. Kufanya jitihada ya kufanana na wale waliopata radhi za Allahu taala katika mitume „alayhimu salawatu wasallamu“ na mawalii “rahmatullahi alayh“ na wanazuoni.

[Waislam wanagawika makundi mawili. Wenye elimu na watu wa kawaida. Katika kitabu kiitwacho **Durr-i-yekta** kilichoandikwa kwa kituruki tunasoma (Watu wa kawaida ni watu wasiojua asili na misingi ya elimu za nahw, sarf na fasihi. Hawa hawawezi kufahamu vitabu vya fatwa. Hawa wanalazimika kuuliza na kujifunza elimu za **imani** na **ibada**. Wenye elimu wanalazimika kuwafunza hawa misingi ya imani kisha misingi mitano ya dini, kwa maelezo, mawaidha na maandishi. Katika vitabu viitwavyo **Zahire** na **Tatarhaniye** inaelezwa kwamba kusoma sharti za imani na itikadi ya ahli sunna ndiyo jambo la mwanzo kwa watu hawa). Ndio maana mwanazuoni mkubwa, gwiji wa elimu za dhahiri na batini Sayyid Abdulhakim Arwasy „rahimatullahi alayhi“, kabla ya mauti yake alisema (Kwa miaka thalathini sasa, katika misikiti mbali mbali ya Istanbul nimekuwa nikifundisha imani iliyoandikwa katika vitabu vya wanazuoni wa ahli sunna tu. Yaani nikielezea mafunzo ya itikadi ya ahli sunna na mafunzo ya mwenendo mwema wa kiisalam). Hii ni kwa sababu wanazuoni wa ahli sunna wameipata elimu hii kwa masahaba ambao nao wamejifunza kutoka kwa Mtume swallallahu alayhi wasallama. Elimu ya imani huitwa **Akaid** au **iitikad**. Kutokana na hilo ndio maana na sisi katika vitabu vyetu vyote, tunasisitiza ulazima wa kufuata iitikadi ya ahli sunna, kuwa na mwenendo mwema wa kiisalam na kuisaidia serikali. Wajinga wa dini kama sayyid Kutub na Mawdudy, na watu wa bid’a kama kundi la tabligh na wale wapinzani wa madhehebu ambao wanaandika maandishi ya kuipinga serikali, kugombanisha ndugu kwa ndugu na kuwagawa, sisi hatuyaungi mkono maandishi yao. Mtume „swallallahu alayhi wasallama“ aliposema **(Dini iko chini ya kivuli cha upanga)** ina

maana kwamba waislam wataishi kwa utulivu chini ya uangalizi wa sharia na kanuni za nchi. Serikali ikiwa na nguvu, utulivu ndio unapozidi. Waislam wanaoishi nchi za kikafiri kama Amerika na Ulaya, ambao wanaishi kwa utulivu na wanatekeleza ibada zao kwa uhuru, wanatakiwa wasivunje sharia za nchi, wasilete upinzani wala wasizue fitna dhidi ya serikali inayowapa uhuru huo. Wanazuoni wa ahli sunna „rahimahumullahu taala“ wanatuamrisha hivyo. Moja kati ya ibada kubwa ni kutokucheza na moto wa kuleta fitna na ufisadi na kutokuwa kibaraka, msaidizi wa wapinzani na wenye kuzua fitna. Tusome **itikadi ya ahli sunna** na tuiweke sawa imani yetu ifuatane na hayo ili tuwe mbali na yale makundi sabini na mbili ya kibid'a, kisha ibada zetu pia tuziepushe na bid'a. Mambo ambayo Uislam haukuamrisha ukayafanya kwa kudhania kuwa ni ibada hiyo huitwa bid'a ya ibada. Amri za Allahu taala na makatazo yake huitwa **hukmu za kiisalam**. Kuzifuata hukumu za kiislam ndio huitwa ibada. Kuna **madhehebu** manne yanayoelezea njia sahihi za kutekeleza ibada. Yote haya manne ni ya haki na yako sahihi. Madhehebu hayo manne ni Hanafi, Maliki, Shafi na Hanbali. Kila muislam anatakiwa kusoma kitabu cha mafunzo ya dini kutoka katika moja ya madhehebu haya manne na kutekeleza ibada zake kwa kufuata mafunzo hayo. Hivyo atakuwa ni mfuasi wa dhehebu hilo. Wasiofuata madhehebu haya huitwa **wasio na madhehebu**. Wasio na madhehebu si ahli sunna nao huwa ni watu wa **bid'a** au makafiri.

Hadhrat Ali "Karamullahu wacheh" anasema (Utakapokutana na anayepinga kufufuliwa mwambie "Mimi ninaamini kufufuliwa. Ikiwa rai yako wewe itatokea kuwa sahihi, mimi haitanipa dhara yoyote. Ila ikiwa rai yangu mimi ndio sahihi, basi wewe utadumu milele katika Jahannam"). Huko Ulaya na Amerika, wanasayansi wote, viongozi wa nchi wote, maprofesa na makamanda wa jeshi wote wanaamini maisha ya akhera. Wanakwenda makanisani kuabudu. Mayahudi, Mabuda, Berehmen, waabudia moto na waabudia masanamu, waliostaarabika na wasiostaarabika, wote wanaamini maisha ya akhera. Wasioamini hili ni wachache tu miongoni mwa wale viongozi waongo, madhalimu, madikteta wenye kuongoza nchi za kikoministi na vibaraka wao waliowazunguka na wale wanaowalipa walio katika nchi nyengine. Je inawezekana kuwa hawa majahili wachache, wasaka tonge, watumwa wa matamanio ya nafsi wakawa ndio wa kweli dhidi ya asilimia zaidi ya tisini ya wakazi wa hii dunia?! Mtu asieamini anapokufa, kufuatana na imani yake binafsi, atatoweka; ila kufuatana na imani ya waumini huyu ataingia katika Jahannam milele. Mtu mwenye kuamini anapokufa, kufuatana na mtu asie amini, huyu pia

atatoweka; ila kufuatana na yule anaeamini huyu atadumu katika neema na mazuri yasiyo na mwisho. Kwa mtu mwenye akili kamilifu ni lipi atachagua kati ya haya makundi mawili? Bila ya shaka atachagua kundi la pili. Nidhamu ya dunia na vitu vilivyomo ndani yake vinatoa habari ya wazi juu ya kuwepo kwa Allahu taala. Kwa hivyo yeyote mwenye elimu lazima aamini kuwepo kwa Allah na upekee wake. Kutokuamini ni ujinga. Kumuamini Allahu taala maana yake ni kuamini **sifa zake za Uluhiyya**, yaani **sifa zake za Dhatiyya** na zile **za Thubutiyya**, kuamini habari alizozitoa na kufuata dini yake. Mwenye kuufuata Uislam anaishi kwa raha na furaha duniani na anamfanyia wema kila mtu. Allahu taala kwa huruma yake kwa viumbe ndio amewaamrisha kufanya mambo ya **fardhi** na kuwakataza yale yenye dhara nao, ndiyo hayo ya **haram**. Fardhi na Haram kwa pamoja ndio huitwa **Ahkam Islamiyya**. Dini ni rehema ya Allahu taala kwa viumbe wake. Mwenye kuamini na kufuata dini, atapata ihsan ya Allahu taala na kuishi maisha mema duniani na akhera. Yule asieamini, na kwa akili yake tu akayafahamu yenye faida na kuyatekeleza, basi atapata raha za dunia tu. Hivi sasa Ulaya wanaishi kwa raha kwa sababu hii na waislam wanaishi maisha dhalili yaliyo duni kutokana na kuuacha Uislam wao.

## MLANGO WA TATU

Hapa tutaelezea tabia mbaya. Kama ambavyo msingi wa tabia nzuri ni tabia nne, basi na msingi wa tabia mbaya pia ni tabia nne.

1. Ujinga ni kinyume cha busara.
2. Woga ni kinyume cha ushujaa.
3. Fujur, kuifuata nafsi, kufanya maovu ni kinyume cha Iffat.
4. Dhulma na jeuri ni kinyume cha uadilifu.

Dhidi ya kila tabia njema kuna tabia mbaya zisizo na idadi kwa sababu tabia njema ndio njia ya katikati, na kuwa kushoto au kulia ya njia hii ni kukengeuka wema. Kila unapokuwa mbali kutoka kati basi na usahihi ndio unavyopungua. Njia sahihi ni moja tu, lakini njia za uovu ni nyingi. Uovu hauna mipaka. Baada ya kuingia katika njia ya haki, kudumu na kutokutoka katika njia hiyo nalo ni jambo zito lenye kuhitaji azma kubwa. Tunasoma katika Surat Hud aya ya 113 katika maana ya aya **(Na kuweni katika njia sahihi mlioamrishwa).** Mtume „swallallahu alayhi wasallama" anasema **(Surat Hud imenitoa mvi katika ndevu zangu).** Jambo la kuwa kwenye njia sahihi kama ilivyoamrisha aya liliwahamanisha mitume, mawalii na watu wema hata mtume „swallallahu alayhi wasallama" akatoka mvi kwenye ndevu zake

kutokana na woga wa amri hiyo. Kwa vile kuwa katika njia sahihi ni uzito ndio maana ikasemwa **(Daraja la Sirat ni jembamba kuliko nywele na kali kuliko upanga).** Tunasoma katika suratul Fatiha katika maana ya aya **(Tuongoe njia iliyonyooka).** Katika dunia hii ni lazima binaadamu ashikamane na njia iliyonyooka na hilo ndilo litakalomuwezesha kupita katika daraja la Sirat siku ya kiama.

Mmoja kati ya maawliyaa wakubwa „rahimahullahu taala“ anasema, yale yote aliyoyaeleza msema kweli (Mtume) "swallallahu alayhi wasallama", katika neema na adhabu za huko akhera ni sura na muonekano wa huko wa yale binaadamu aliyoyafanya hapa duniani miongoni mwa tabia, mwenendo na amali. Kuwa katika mwenendo mwema na amali njema hapa duniani, sura na muonekano wa huko akhera utajitokeza kwenye Daraja la Sirat. Wale ambao walikua katika njia sahihi na kuufuata Uislam hapa duniani watapita haraka kwenye daraja hilo, wataingia pepo za maarifa na ukamilifu, na mabustani ya matendo mema. Wale ambao walikuwa ni wavivu katika utekelezaji wa majukumu yao ya kidini, watapita kwenye daraja kwa uzito. Na wale ambao hawakuwa wakitekeleza majukumu yao, watashindwa kuvuka daraja hili na wataangukia ndani ya moto wa Jahannam.

Katika surat Zukhruf aya ya 36 katika maana ya aya **(Wale wenye kuzifuata nafsi zao na wakaigeuzia uso dini ya Allahu taala, tutawasalitishia shetani hapa duniani).** Kufuatana na aya hii wamesema baadhi ya wanazuoni kwamba matendo mema na ya kheri yanafanyika kwa kupitia malaika na yale ya shari na maovu yanafanyika kwa kupitia shetani. Mmoja kati ya hao ndio atakuwa rafiki yake siku ya kiama. Kwa hivyo kila mtu kwa kutizama mwenendo na amali zake tu, atafahamu ni rafiki wa aina gani atakuwa nae siku ya kiama.

Tunaposema njia ya kati mambo mawili yanafahamika. Ya kwanza ni ile ambayo kila mtu anaifahamu nayo ni katikati ya kitu fulani, kama ilivyo kati kati ya duara. Ya pili ni ile maana ya kati ya kukadiria, yaani inaainisha kati kwa mtizamo wa kitu fulani na hailazimishi kwamba iwe ni kati kwa vitu vyengine vile vile. Hii maana ya pili ndiyo inayokusudiwa katika elimu ya maadili. Kwa hivyo, tabia njema ina maana tafauti kwa mtu mmoja na mwengine, bali pia inaweza ikawa tafauti kufuatana na pahali na wakati. Kile amabacho ni tabia njema kwa mtu mmoja inaweza kisiwe hivyo kwa mtu mwengine. Jambo ambalo lilikuwa likionekana ni zuri wakati fulani, linaweza lisionekane zuri katika wakati mwengine. Kwa hivyo tabia njema si kuwa kati hasa bali ni kuwa kwenye wastani. Na tabia mbaya nayo vile vile ni kukengeuka huo wastani. Hadithi isemayo **(Uzuri wa jambo ni kuwa**

**kwa wastani)** ndio anafahamisha hilo. Kwa hivyo kila tabia njema moja ina tabia mbaya mbili dhidi yake. Kwa hivyo kuna tabia nane mbaya za msingi dhidi ya tabia nne njema za msingi:

1. Ujuaji ni kuwa na hekima zaidi ya kiwango kinachotakiwa. Kutumia nguvu za upembuzi na uchunguzi wa mambo katika hali isiyotakiwa. Mfano wake ni kufanya hila, kudanganya na kueneza maasi. Kutumia nguvu za kisayansi zilizomo akilini sio ujuaji wala si vibaya. Kutafiti mambo ya elimu za dini, sayansi na hesabati kwa lengo la kuziendeleza elimu hizo ni jambo linalotakiwa.

2. Ujinga ni kutokutumia akili. Kuwa na uzito katika kujifunza na makosa katika kutekeleza. Kushindwa kupambanua jema na ovu. Tabia hii imetajwa sana katika Kur-an Karim na hadithi sharif.

3. Ushupavu ni kufurutu ada katika ghadhabu. Ni ushujaa uliopita wastani unaotakiwa. Kufanya mambo ambayo watu wenye akili timamu hawatoyafanya. Kuuchosha mwili na roho katika mambo yasiyo na faida.

4. Woga ni upungufu wa ushujaa kuwa daraja la chini kuliko wastani. Ni kuogopa katika hali ambazo kikawaida hazitakiwi uogope.

5. Fujur ni kuvuka daraja la Iffatt na kuwa mwenye kupenda mno ladha za kidunia. Kufanya yale mambo ambayo Uislam na akili hauyapendelei.

6. Humud ni kuwa chini ya wastani wa daraja la Iffat na kuyaacha hata yale matashi na ladha ambazo Uislam umeyatolea ruhusa. Matokeo ni kupoteza nguvu za mwili, kuwa mgonjwa au hata kizazi kutoweka.

7. Dhulma ni kuvuka mipaka ya uadilifu na kuingilia haki za wengine. Kudhuru roho, mali na heshima ya wengine.

8. Ubwege ni kukubali dhulma, mateso na matusi yanayofanywa dhidi yake. Ni kupungua kwa uadilifu. Kama ambavyo kwenye uadilifu yanakusanyika mazuri yote, basi na kwenye dhulma vile vile yanakusanyika maovu yote. Mfano ni yale aliyoyasema Abdullahi Ansari:

***Walio katika njia ya haki, hawawaudhi wengine.***
***Kwani hakuna ovu kubwa kama hilo.***

Abdullahi Ansari alikuwa ni mwanazuoni wa sufiyyal aliyya. Alikuwa ni shaykhul islam. Alizaliwa mwaka 396 hijria huko Hirat na kufia huko mwaka 481 hijria [1088 miladia]. Baadhi ya watu waovu hawakuyafahamu maneno ya mwanazuoni huyu. Wao waliyafahamu ya kwamba kufanya lolote unalotaka ni ruhusa, muhimu usimuudhi

mtu mwengine tu. Hivyo wakaacha ibada, na kutenda kila ovu hali ya kuwa wakijisifu kwamba wao ni wema kwa sababu hawamdhuru mtu yeyote. Hata wakafika kusema:

***Ukitaka kuwa kafiri, ukitaka ichome Kaaba,***
***Ukitaka kunywa pombe, ila usimuudhi mwengine***

Na kwa dhana hio wakatoka katika uislam. Kiuhakika kila lililoharamishwa na dini ni dhulma. Iwe ni kwa watu wengine au kwa nafsi yako, kila kilichoharamishwa ni dhulma. Wengi wa madhalimu ni watu wenye mali, ufalme na vyeo. Wenye kudhulumiwa wengi ni mafakiri. Wengi wa walio hali za kati ni wale ambao wanazingatia uadilifu.

Tabia njema zote ni zile zilizo katika hali ya wastani. Na kwa kila moja yao, kile kinachozidi au kupungua basi kitakua ni tabia mbaya. Hizi tabia mbaya pengine majina yake hayapatikani katika kila lugha, ila kwa kuzingatia maana yake inafahamika kwa wepesi.

Kuna miongoni mwa tabia njema ambazo zinaweza zikadhaniwa kuwa kila zikizidi na uzuri ndio unazidi, hali ya kwamba uhakika hauko hivyo. Kila tabia njema ina mipaka yake. Ikiwa mipaka hiyo itavukwa uzuri unaondoka na ubaya unaingia. Tabia hizi njema zipunguapo inafahamika kiwepesi kuwa utakuwa uovu ila zinapozidi ndio haifahamiki kuwa ni uovu pia. Mfano wa tabia hizo ni ushujaa na shahawa. Tabia hizi mbili zikizidi kiwango kitakiwacho husababisha ushupavu na israfu. Majahili, hasa wale wasiojua maadili ya kiislam, mwenye kufanya israfu wanamdhani kuwa ni karimu sana na wana msifu. Yule mwenye kufanya ushupavu pia wanamdhani ni shujaa. Ila mtu aliye mwoga au mchoyo hakuna anaemdhani kuwa ni shujaa au karimu.

Miongoni mwa tabia njema pia kuna zile ambazo zikiwa chini ya wastani inadhaniwa kuwa ndio uzuri, jambo ambalo pia si sahihi. Hizi zikiwa nyingi ni rahisi kufahamika kuwa ni mbaya ila zikiwa chache ndio haifahamiki kuwa ni uovu pia. Mfano ni tawadhuu, yaani mtu kutokuwa na kiburi. Hii inapopungua inakuwa ni kujidhalilisha. Ni vigumu kutafautisha kati ya kujidhalilisha na tawadhuu. Hata kuna wenye kuchanganya kati ya kujidhalilisha kwa mtu omba omba na tawadhuu ya mwanazuoni. Hii ni kwa sababu omba omba nae hana kiburi, hivyo huo nao hudhaniwa ni uzuri.

# MLANGO WA NNE

Katika mlango huu tutaelezea zile tabia mbaya ambazo zinafanana na tabia nzuri na namna ya kuzipambanua.

Kuna watu wengi ambao hawawezi kupambanua baina ya dhahabu safi na ile bandia. Kuna wanaodhani shanga kuwa ni vito vyenye thamani. Mfano wa hili pia kuna wanaozidhani baadhi ya tabia mbaya kuwa ni nzuri. Kwa hivyo ili kuweza kuzigundua tabia mbaya, kuziona aibu na mapungufu yaliyomo inahitaji kuisoma vyema elimu ya tabia na kuwa bingwa katika somo hilo.

1. Tunataja tabia mbaya yenye kufanana na hekima: Kuna watu ambao huchukua vipengele vichache au maneno machache ya busara ya kidini au ya kisayansi kutoka kwa wajuzi, redio au magazeti na kuyakariri mara kwa mara kwa watu wenye elimu chache bali hata kushiriki katika malumbano na mijadala ili kujijengea picha tafauti kwa watu. Hatimae watu huwadhania kuwa ni wenye elimu na mabingwa katika sayansi fulani au tawi fulani la dini. Kiuhakika ni kwamba watu kama hawa hawana wanachokijua wala hawawezi kutoa mwongozo wa utatuzi katika hiyo sayansi, wala hawana maarifa katika elimu ya tasawwuf. Mfano wao na wanasayansi au wanazuoni ambao wanajaribu kuvaa koti lao ni sawa na mfano wa binaadamu na kasuku katika uwezo wa kuzungumza. Hekima imo ndani ya akili na moyo. Nuru na kazi zake ziko nje ya uwezo wa kufikirika. Kuna watu wengi wanaoambiwa wameendelea lakini hawana habari na hekima na thamani yake. Watu wa aina hii kiuhalisia ni wajinga wasio na maadili mema. Hawana habari juu ya elimu na maadili wala hawataji tabia njema. Kubwa walijualo ni kuvaa mavazi mazuri na kuwaamkia kwa unyenyekevu waheshimiwa. Utawakuta wakitumwa kwenye hafla na mikusanyiko yenye dansi na ulevi. Hatimae siku moja utawakuta nao wamepewa vyeo vya mjumbe wa kamati, mshauri au mwenyekiti.

2. Kuna sifa mbaya ambayo inafanana na Iffat. Watu hawa hawafanyi mambo maovu. Hawakimbilii matashi ya nafsi. Wanaonekana ni watu wenye fadhila, watulivu na wenye elimu. Wanasifiwa na kuheshimiwa na kila mtu. Zawadi, zaka na sadaka zinamiminika kwao. Kikawaida ni wazembe mno wa kutekeleza fardhi na sunna, ila wanapokua mbele za watu hujionesha kwa ibada nyingi hadi miili yao huchoka. Nafsi iamrishayo maovu imewatawala. Ni waaminifu mbele za watu lakini ni wahaini mbele ya Allah. Mashekhe bandia wa kitarika na baadhi ya viongozi wa dini wasaka tonge ndio mfano mzuri wa kundi hili.

Baadhi ya watu wa vijijini hawali chakula cha mjini. Baadhi ya watu hawakotayari kutumia pesa zao kwa kujinunulia chakula bora. Hawa ukiwaona utadhania ni madarweshi wenye kinaa na iffat. Uhakika hawa si watu wenye kinaa wala iffat. Yote wanayoyafanya ni kujionesha, uwongo na riyaa.

3. Kuna tabia mbaya inayofanana na Sahawa. Mtu huyu mali hakuichuma kwa jasho lake. Ima amepata urithi, ameshinda bahati nasibu au katumia njia nyengine za kimagendo. Uchungu wa mali haujui. Huitumia mali katika njia za haramu na kwenye mahali musio na lazima. Huangamiza mali yake kwenye mambo ambayo akili na Uislam hauyakubali. Wajinga wanamdhania huyu kuwa ni karimu. Kuchuma mali ni sawa na kupandisha jiwe juu mlimani wakati kugawa mali ni sawa na kuliwacha jiwe mviringo lishuke mlima. Ufakiri umewazuia wengi kuwa watu wema. Kutokana na shida za ufakiri, kuna watu wengi ambao wamepoteza imani zao na kuwa murtad. Hadithi sharif iliyo katika **Ramuzul ahadith** inasema **(Ufakiri ni furaha kwa masahaba zangu. Zitakapofika zama za mwisho utajiri utakuwa ndio furaha).**

***Baada ya uzoefu wa muda mrefu,***
***nimeweza kufahamu,***
***Ubinaadamu hupimwa kwa elimu,***
***na elimu hupimwa kwa mali***

Ni uzito kuchuma mali kwa njia ya halali ambayo imeridhiwa na Uislam. Mali ichumwayo kwa njia ya halali hudondoka kwa matone wakati ile ichumwayo kwa njia ya haramu humiminika kama mafuriko. Kupenda kutoa mali ni jambo zuri ila kufanya israf ndio uovu. Sahawa ni kuokoka na tabia mbaya ya ubakhili kwa kujizowesha kutoa. Kutoa kwa ajili ya kupata kitu au kwa ajili ya kukidhi matashi maovu huwa sio Sahawa.

4. Kuna tabia mbaya inayofanana na ushujaa. Katika hali hii mtu hafanyi ushujaa kwa lengo la kuepukana na sifa mbaya za woga na ushupavu bali anajitumbukiza kwenye hatari kwa ajili ya kutafuta maslahi ya kidunia na cheo au kwa kupata umaarufu. Ili kujipatia mali, anahatarisha maisha yake kwa kuvunja majumba ya watu au kuwakaba jiani na kuwanyanganya mali zao na wanyama wao. Wafuasi wa watu kama hawa baadhi ya wakati huwa wajinga mno na kuwadhania hawa wenzao kuwa ni wajasiri hivyo hukataa kutoa ushahidi dhidi yao, hata kama watapata mateso au kupoteza mali na uhai wao kwa hilo. Kwa uhakika waovu hawa hawana hata harufu ya ushujaa. Mwenye ushujaa ni yule mwenye kujitokeza kwa ajili ya

kuyatekeleza mambo ambayo akili na dini vinayakubali. Hujitoa kuihudumia jamii na taifa. Hutaka kufikia sifa ya ushujaa ili apate radhi za Allahu taala. Uvamizi wa mbwa mwitu na simba pia ni kujitoa muhanga ila hauitwi ushujaa. Ni shambulio tu linalotokana na nguvu na hisia za kimaumbile. Si kitu kinachofanywa kwa nia njema na kutaka radhi za Allahu taala. Ni shambulio linalofanywa na mwenye nguvu dhidi ya dhaifu. Shambulio la mtu mwenye silaha dhidi ya dhaifu asie na silaha linafanana na hilo. Huu hauitwi ushujaa. Ushujaa ni pale ambapo kwa kutumia akili na fikra imeamulika kuwa kushambulia ndio tendo sahihi, sio kwa lengo la kutafuta maslahi ya kidunia, bali ni kwa lengo la kujivisha tabia njema ya ushujaa na kujiepusha na tabia mbaya za woga na ushupavu. Mtu kama huyu anahiyari kufa kuliko kutenda jambo lisilo sahihi. Anahiari kufa kiheshima kuliko kuishi kwa udhalilifu. Anahiari kufa na kukumbukwa kwa wema kuliko kuishi na uso wenye doa jeusi. Kwa vile ushujaa unaendana na hatari ya kujeruhiwa na kufa, mwanzo unaweza usiwe jambo la kupendeza. Lakini mwisho wake unapendeza kutokana na ladha za dunia na akhera na utamu wa ushindi. Ladha inayopatikana kwenye kifo kinachotokana na kuulinda Uislam na kuieneza dini ya Allahu taala, haipatikani popote pengine. Tunasoma katika surat Ali Imran aya ya 169 katika maana ya aya **(Msiwadhanie wale waliotoa roho zao katika njia ya Allah ni wafu. Wako hai na wananeemeka kwa mola wao)**. Hadithi sharif zilizousifu ushujaa ni nyingi sana. Kukimbia jihadi hakumkingi mtu na kifo wala hakumuongezei umri. Kukabiliana na maadui hakumfanyi mtu afe wala hakumpunguzii umri. Anasema hadhrat Muawiya kwamba alinuia kukimbia katika vita vya Siffin lakini ikamjia katika akili hadithi sharif isemayo **(Wenye kufanya subira, wataokoka na balaa)**. Nilifanya subira nikawa thabit na namshukuru Allah nikaokoka na tendo la kukimbia. Kutokana na subira ile, leo nimekuwa khalifa.

Msingi wa ushujaa ni kukubali kudra ya Allahu taala, kutawakal kwake na kumtegemea. Simba wa Allah, chanzo cha ushujaa, waridi la bustani ya uwalii, Hadhrat Ali "radhiyallahu anhu" alikuwa akikimbilia kuhujumu maadui katika vita vya Siffin huku akizisema beti hizi:

***Kuna siku mbili ambazo si sahihi kukikimbia kifo***
***Siku ambayo ahadi yako imefika, na iwapo bado.***
***Ikiwa ahadi imefika, kukimbia hakutokupa faida yoyote.***
***Ikiwa ahadi yako bado, huna sababu ya kukimbia.***

Wale wanaojiua kwa kupoteza mali au cheo au kwa kutekwa na adui, hao si mashujaa ni waoga. Kwa ujinga wao wanadhani kifo kitawaokoa na machungu. Ni wajinga sana. Kifo kama hicho kitazidi

kuwapa machungu na madhila. Kujiua ni dhambi kubwa kuliko kumuua mtu mwengine. Watapata adhabu kali kabisa. Yule ambae atajiua baada ya kupotelewa na akili hatopata adhabu hiyo. Mtu anapokuwa katika matatizo asiombe mauti, bali aombe siha na afya kutoka kwa Allahu taala.

5. Kuna tabia mbaya inayofanana na uadilifu. Hii imefanana na tabia mbaya inayofanana na Iffat. Mtu muovu asie na uadilifu huusifu uadilifu na kuutundikia mabango kwenye ukuta wa ofisi au nyumba yake. Anazungumzia juu ya uadilifu na kuandikia makala juu yake. Na lililo ovu zaidi atachukua dhamana zenye kuhitaji uadilifu na ataandamana na watu waadilifu ili nae aonekana ni miongoni mwao. Lakini uhakika ndani ya nafsi yake amejaa dhulma na visasi. Uadilifu ni kwenda sawa kwa namna akili na dini inavyotaka. Undani wako uwe sawa na uonekanavyo nje. Unapokuwa peke yako iwe sawa na unapokuwa mbele za watu. Kuwa na sura mbili si uadilifu,ni unafiki.Ubeti unasema:

***Ibada lazima iambatane na nia njema***
***Vyenginevyo haitofaa, kama kokwa iliotupu ndani.***

## MLANGO WA TANO

Sasa tuelezee uadilifu ni nini: Uadilifu ndio tabia njema yenye heshima kabisa. Mtu muadilifu ni mtu bora kabisa miongoni mwa watu. Uadilifu ni itifaki na usawa. Vitu viwili huwa sawa ima kwa dhati yao au kwa sifa yao. Maeneo yanayofanana yanaungana. Hii ni kusema uadilifu unatokana na umoja na muungano. Umoja ni sifa yenye heshima ya hali ya juu kwa sababu viumbe vyote vimetokana na yule alie mmoja, pekee. Muungano wowote uliopo duniani unatokana na kitu hakika kimoja. Kama ambavyo kila kiumbe kimetokana na muumba mmoja, basi ni hivyo hivyo kila umoja unatokana na kitu kimoja. Katika elimu ya vipimo na mlinganisho, usawa ndio matokeo yenye thamani. Jambo hili linasomwa kwa undani na kupewa umuhimu katika somo la muziki. Hivyo uadilifu ndio tabia tukufu miongoni mwa tabia njema zote. Ni kosa kumuhisabu mtu kuwa muadilifu ikiwa hayupo kwenye hali ya wastani. Katika maeneo matatu uadilifu lazima uwepo:

1. Wakati unapogawa mali au neema yoyote lazima uadilifu upatikane.

2. Katika kuuza na kununua uadilifu ni lazima.

3. Katika kutoa adhabu lazima kuwe na uadilifu. Ikiwa mtu alimtishia na kumhujumu mwengine naye apate lipizo linalowiana.

[Ifahamike kwamba adhabu hizi hutolewa na serikali. Haifai mtu kuchukua sharia mikononi mwake, inabidi apeleke madai kwenye vyombo vinavyohusika. Muislam anafuata mafunzo ya dini hivyo hafanyi dhambi na anafuata kanuni za nchi hivyo havunji sharia.] Panapokua na uadilifu watu wote wanaishi bila khofu. Uadilifu huondoa khofu.

Uadilifu ni nini? Kwa vile hili litakuwa ni shida kwa akili ya binaadamu kulifahamu, Allahu taala kwa rehema zake akawaletea binadamu sharia ili zitumike katika nchi zao. Sharia hizi za kiungu zinafanya wepesi kuupima uadilifu. Sharia hio ndio hii dini aliokuja nayo Mtume Muhammad swallallahu alayhi wasallama, ambayo ipo leo na itaendelea kuwepo hadi siku ya kiama. Baada ya sharia hii, kipimo cha pili kikaletwa ambacho ni jaji mwenye mamlaka. Binaadamu ameumbwa ili astaarabike kwa maana ya kwamba achanganyike na kuishi pamoja na binaadamu wengine na wasaidiane. Wanyama hawakuumbwa kuwa viumbe vyenye ustaarabu. Hawakuwekewa kuishi kwenye miji iliyojengwa. Binaadamu ni kiumbe tafauti. Chakula chake, mavazi yake na malazi yake yanahitaji matayarisho. Wanahitaji sanaa na kwa hivyo wanalazimika kusoma kutafiti, kugundua na kufanya kazi.

[Uislam unahimiza sayansi teknolojia, kufanya kazi na tabia njema. Waingereza na wakomunisti wanautuhumu Uislam kuwa ni ushenzi. Wanautuhumu Uislam kwa kuwafanya watu wapooze na wasitake kufanya kazi. Wamewawinda na kuwadanganya baadhi ya watu katika nchi za kiislam, wanawalipa pesa nyingi vibaraka hao na kuwafikisha kwenye vyeo vikubwa ili nao wauzungumze ubaya Uislam. Wanawezaje waovu hawa kuusingizia Uislam mambo haya wakati kuna aya nyingi na hadithi zinazohimiza kujifunza sayansi, elimu na kufanya kazi kwa bidii. Waingereza wanaupiga vita Uislam kwa kujipenyeza ndani na kuuvunja Uislam ndani kwa ndani. Ili uongo wao uweze kuenea kirahisi kwa vijana, elimu na vitabu vya kiislam wanaviangamiza. Ili kuuangamiza Uislam, huko London waliunda idara maalumu katika wizara ya nchi, na hapo ndipo walipokuwa wakipanga mipango yao ya kihaini. Miongoni mwa wale walioanguka kwenye mtego wao ni kiongozi wa dini asie na nasabu, mnajdy, aitwae Muhammad bin Abdulwahab na amiri wa Dariyya Muhammed Suudi, ambao walishirikiana na wakatumia mamilioni ya pesa na nguvu za kijeshi kuanzisha kundi la kibid'a la **Wahabi**. Wakaivunja dola ya Othman ambayo ilikuwa ndio mlinzi wa Uislam. Soma kitabu chetu kiitwacho **KUUNGAMA KWA JASUSI WA KIINGEREZA!**

Katika kitabu kiitwacho **Alemi islam** kilichoandikwa na Abdulrashid Ibrahim Efendi, katika chapisho la kituruki lililochapishwa huko Istanbul mwaka 1328 hijria [1910 miladia], kwenye kichwa cha habari kisemacho uadui wa waingereza; ameandika (Kuuondosha ukhalifa wa kiislam ilikuwa ndio ajenda yao kuu. Kuanzisha vita vya Kirim na kuwa upande wa waturuki ilikuwa ni hila tu ya kuuhujumu ukhalifa. Nia ya hila hiyo ilikuwa ni kuleta yale makubaliano ya Paris. [Mada za siri zilizoandikwa katika makubaliano ya Lozan mwaka 1923, yanadhihirisha uadui wao huu]. Maafa yanayowafika waislam wakati wowote, kwa namna yoyote ile yatakavyogubikwa, mwisho inadhihirika kuwa yalitokana na Waingereza. Msingi wa siasa ya Waingereza ni kuuangamiza Uislam kwa sababu wanauogopa Uislam. Ili kuwadanganya waislam wanatumia vibaraka walionunuliwa kwa pesa. Hawa wanajaribu kutambulishwa kwenye Ulimwengu wa kiislam kama mashujaa. Mwisho wa maneno yetu ni kwamba adui mkubwa wa Uislam ni Waingereza.) Abdulrashid Efendi alikufa Japan mwaka 1363 hijria [1944 milady].

Je, Uislam kweli unakataza sayansi, teknolojia na kufanya kazi? Binaadamu analazimika kutayarisha mahitaji yake yote. Ili kufanya matayarisho hayo anahitaji sayansi, sanaa na kufanya kazi. Mtu hawezi kujifunza kila aina ya fani. Kila fani husomewa na watu maalum na wakaifanyia kazi. Mwenye kuihitaji fani hiyo huchukua kwa watu hao, na wao wanapohitaji fani nyengine huchukua kwa watu wengine. Kwa namna hiyo ndiyo binaadamu hukidhiana mahitaji yao. Hivyo binaadamu hawezi kuishi peke yake. Ni lazima aishi na wenziwe katika jamii. Ustaarabu maana yake ni kuishi pamoja yaani **Tamiri bilad watarfihi ibad.**]

Binaadamu wanapoishi pamoja wale wenye tamaa huanza kuzikodolea macho mali za wengine. Hutokea watakaofanya dhulma kwani kila nafsi hutaka kupata kile inachokitamani. Hivyo hufanya jitihada ili ikipate. Kama mbwa wanavyogombea mzoga, hubwekeana kisha wakaanza kugombana. Hawa wanahitaji muamuzi mwenye nguvu. Katika biashara kila mtu cha kwake ndio anakiona kina thamani zaidi. Lazima kuwe na uadilifu wa kuweza kuzipa bidhaa thamani yake halisi. Kitu kinachotumika kupima na kutia thamani baina ya bidhaa ni dhahabu na fedha yani pesa. Dhahabu na fedha huitwa sarafu. Pesa za noti zinazotumika na kila nchi ni mkabala wa dhahabu kwa maana kwamba kila nchi ikiwa na dhahabu nyingi zaidi basi inaweza kuchapisha noti zaidi. Nchi yenye dhahabu chache ikichapisha noti nyingi huwa hazina thamani kwa sababu Allahu taala ameziumba

dhahabu na fedha ili ziwe pesa. Hakuna kinachoweza kuchukua nafasi ya dhahabu kwa hiyo zaka hutolewa kwa hesabu ya dhahabu na fedha. Bidhaa zinalazimika kutiwa thamani na hakimu muadilifu kwa kutumia dhahabu au fedha. Hakimu anaetajwa hapa ambae anakuwa na mamlaka ni serikali.

Hii ni kusema kwamba kuna mambo matatu yanahitajika ili kuleta uadilifu katika jamii nayo ni sharia ya Allahu taala, mamlaka ya binadamu na mizani ya dinari. Lililo kuu na muhimu zaidi miongoni mwa haya ni sharia ya mola yaani Uislam. Dini ni kanuni zilizotumwa na Allahu taala ili kuleta uadilifu. Kanuni hizi zimeletwa ili mahakimu wahukumu kwa uadilifu. Tunasoma katika suratul Hadid aya ya 25 katika maana ya aya **(Tumewapelekea kitabu na mizani, ili wahukumu kwa haki).** Hapa kitabu maana yake ni dini kwa sababu dini ni yale maamrisho na makatazo yaliyomo ndani ya Kur-an Karim. Mizani hapa inaashiria dhahabu kwani dhahabu hupimwa kwa uzito. Wasioyapenda maamrisho na makatazo ya Uislam ni makafiri na wanafiki. [Muislam hatakiwi apingane na kanuni zilizopo akiwa katika nchi za kikafiri]. Asie kubaliana na thamani ya dhahabu huwa haini na mwizi.

**TANBIHI:** Kwanza binaadamu lazima afanye uadilifu kwake binafsi kwa harakati zake na kwa viungo vyake. Kisha afanye uadilifu kwa watoto wake, jirani na marafiki zake. Wanasheria na watumishi wa serikali nao wafanye uadilifu kwa wananchi. Hii ni kusema kwamba ili mtu aweze kuwa muadilifu basi kwanza lazima uadilifu upatikane kwenye harakati zake na viungo vyake. Kila kiungo na kila nguvu aitumie kufuatana na sababu yake ya kuumbwa. Asibadilishe matakwa ya Allahu taala na kuvitumia kinyume na maarisho ya Uislam na akili. Ikiwa ana watoto basi aishi nao kwa namna dini na akili vinavyokubali na asiende nao kinyume na mwenendo mwema wa kiislam, ili nao waweze kukua na mwenendo mwema. Mahakimu, makamanda na magavana na yeyote yule mwenye amri basi atekeleze ibada zake na kuwataka wengine nao watekeleze. Kwa mtindo huo ndio atakuwa katekeleza wajibu wake wa kuwa khalifa katika hii ardhi na ataweza kupata malipo watakayopewa watu waadilifu siku ya kiama. Ni bahati kiasi gani kwa mtu mwenye sifa kama hizi ambae hueneza baraka katika sehemu anayoishi ambayo husababisha kuenea riziki kwa watu, wanyama na hata mimea. Lakini kama itakuwa wakuu wa nchi si waadilifu, si wenye huruma, na wakawa wenye kuvamia mali za watu, madhalimu na watesaji, basi hawa si wadau wa uadilifu bali ni marafiki wa ibilisi na wenza wa shetani. Mshairi anasema:

***Usihadaiwe na makasri na mapambo yake***
***Mabustani ya makasri yao yananyeshwa kwa machozi ya wanyonge.***

Yule ambae hatowarehemu walio chini ya amri yake basi nae hatorehemewa na Allahu taala siku ya kiama.

Imesemwa kwamba

***Man la yarham la yurham!***

yenye maana kwamba asie waonea huruma wengine basi nae hatoonewa huruma. Hawa ni wale ambao kwa ajili ya matashi ya miaka michache ya maisha ya dunia hii ya kupita, huwatesa mamilioni ya watu. Ila hawataondoka duniani bila ya kupata adhabu zitokanazo na dhulma zao. Pamoja na kwamba wanaonekana wanaishi maisha ya anasa na raha, matatizo kadha wa kadha huwa hayawaondokei. Na huo ufalme haudumu mikononi mwao, na mara nyingi ufalme huo huingia mikononi mwa maadui zao. Tunasoma katika surat Maryam aya ya 81 katika maana ya aya **(Na tutayarithi yale yote anayoyataja kuyamiliki. Na tutamleta mbele yetu akiwa pekee).** Kama inavyoelezwa hapa, hawa watafikishwa mbele ya mahakama ya Allahu taala na nyuso duni, huku wakibururwa. Wote watapata adhabu yenye kuumiza. Dhulma walizozifanya na mateso yatawagubika kwenye kiza kizito wasione mbele. Wataingizwa kwenye Jahannam ili nao wakapate adhabu katika mikono ya malaika ambayo itakuwa ni kubwa kuliko waliyoyafanya wao. Kwa kutokuipenda sharia ya Allah na kuisema kuwa ni sharia ya kishenzi,basi huko hawatopata rehema zozote.

## MLANGO WA SITA

Katika mlango wa sita wa kitabu kiitwacho **Ahlakul aala** aina za tabia njema zimeelezwa. Miongoni mwa hizo sisi tutaelezea uadilifu tu. Uadilifu unagawika sehemu tatu:

Sehemu ya kwanza ni kutekeleza wajibu wa utumishi wako kwa Allahu taala aliyekuumba. Ihsani, rehema na huruma za Allahu taala zimeenea kwa kila kiumbe. Neema iliyo kubwa kabisa ni ile ya kuwaonesha waja wake njia ya furaha. Amewaumbia kwa uzuri kabisa haki zao, hali ya kwamba zilikuwa hazipo. Amewapa mema na neema nyingi za kudumu. Mja huyu ni lazima kwake kumuabudu yule aliyemuumba na kumshukuru yule aliyempa neema hizo zote. Uadilifu ni kumpa kila mwenye haki, haki yake. Kila aliyeumbwa ana deni kwa muumbaji wake, na kulipa deni lake ni lazima.

Sehemu yapili ya uadilifu ni kutekeleza haki za binaadamu wengine. Kutokwenda kinyume na serikali na viongozi, kutokupinga

sharia, kuwaheshimu wanazuoni, kutekeleza amana, kufanya haki katika biashara na kutimiza ahadi ni mambo ya lazima.

Sehemu ya tatu ni kutekeleza haki za waliokwisha kufa. Kuwalipia madeni yao, kutekeleza wasia wao, kuhifadhi wakfu zao na kuyaendeleza yale mema na mazuri waliyoyaacha. Mwenye kumtendea wema mwenziwe, nae amlipe kwa mali au huduma. Isipowezekana basi shukurani na dua pia zitatosha. Anaefanyiwa wema halafu asiulipe wema huo, hulaumiwa na kusemwa kwa ubaya kwa sababu kulipa wema ni wadhifa wa kibinaadamu.

Allahu taala ndie aliyefanya wema mkubwa, muhimu wao ikawa kuleta uhai hali ya kuwa haukuwepo. Yeye ndiye aliyekipa kila kitu maumbile mema na akawapa viumbe viungo vya lazima na nguvu na akakipa kila kiungo uwezo wa kutekeleza majukumu yake. Ni yeye aliyewapa binaadamu akili na ufahamu, akawapa watoto, makazi, chakula, maji na mahitaji mengine na akawaumbia mavazi. Ametoa neema hizi bila ya sababu wala kutaka ujira bali pia hutoa ulinzi dhidi ya maangamizi, maadui na maradhi nae hahitajii kitu kutoka kwetu. Mwenye uwezo na nguvu ni yeye. Basi ni uovu mkubwa kiasi gani kwa mja kutokumshukuru Allahu taala na kutokulipa deni lake kwa muumba wake. Ni ushenzi wa kiasi gani! Kama haitoshi, mja hufikia daraja ya kukataa kuwa neema hizo zinatoka kwake Allahu taala au hata kudai kuwa kuna mwengine ndie aliezileta. Bila ya shaka huu ni ukomo wa dhulma na wizi mkubwa wa fadhila. Leo hii kama utajuwa kuwa kuna mtu kila mwezi anakupa mahitaji yako ya lazima na pesa, mtu huyo kwa kiasi gani utakuwa ukimsifia? Je hutojitahidi usiku na mchana kujipendekeza kwake? Je hutojitahidi kumuondoshea matatizo na kumsaidia katika mazito yake? Je hutokuwa tayari hata kujiingiza kwenye matatizo kwa ajili ya kumuhudumia yeye? Na usipofanya hivyo, na ukaacha kumthamini huyo mwenye kukufanyia ihsan watu hawatokuaibisha? Je jamii haitokuhukumu kwa kuacha kutekeleza wajibu wako wa kibinaadamu? Kwa hivyo ikiwa wema wa binadamu unazingatiwa na kuthaminiwa kiasi hiki, basi ni vipi inatakiwa iwe kwa Allahu taala ambae ndie aliyeumba neema zote? Je hailazimu kwake kushukuriwa na kutendewa yale anayoyapenda!? Bila shaka ni haki zaidi kushukuriwa yeye, kutiiwa yeye na kuabudiwa yeye. Hii ni kwa sababu ukilinganisha neema zake na wema wa wengine haufikii hata tone dhidi ya bahari. Lakini la uhakika zaidi ni kwamba hata hayo mazuri wanayoyafanya wengine basi yanatokana na yeye. Neema za Allahu taala nani anaweza kuzihisabu? Nani anaweza kuzishukuru neema zake alau kwa moja kati ya milioni?

Kufuatana na watu wengine, kumshukuru Allah ni kufahamu kuwa neema zimetoka kwake na kumshukuru na kumsifu kwa ulimi.

Kwa wengine kumshukuru Allah ni kutekeleza maamrisho yake na kujiepusha na makatazo yake.

Kwa wengine binaadamu kwanza ajitakase yeye mwenyewe binafsi na amkabili Allah katika hali hiyo.

Kwa wengine binaadamu ajaribu kuwaongoza wengine wenye kuhitaji kuongozwa kwenye njia sahihi. Awasaidie wengine ili wawe watu wema.

Kwa wengine, hakuna njia maalum ya kumshukuru Allah, kila mtu anaweza akafuata njia tafauti.

Wale waliokuja baadae wamesema wadhifa wa binaadamu kwa Allahu taala umegawika mafungu matatu. La kwanza ni ibada zinazofanywa kwa kiwiliwili kama sala na funga. La pili ni ule wadhifa unaotekelezwa na roho nayo ni kuwa na itikadi sahihi. Kuamini kama ilivyoelekezwa na wanazuoni wa ahli sunna. La tatu ni kujikurubisha kwa Allahu taala kwa kuwatendea waja wake uadilifu. Hii nayo huwa kwa kuhifadhi amana, kunasihi watu na kuwapa elimu ya dini.

Kutokana na yote haya inafahamika kwamba dini inagawika sehemu tatu. Itikadi sahihi, maneno sahihi na matendo sahihi. Hayo mambo mawili ya mwisho, pale ambapo hapakupatikana amri iliyo wazi kabisa, basi yanaweza kubadilika kufuatana na wakati na pahala. Allahu taala ndie pekee mwenye mamlaka ya kufanya mabadiliko hayo na huyafanya kupitia mitume "alayhimusalawatu wataslimat" wake. Binaadamu hana mamlaka ya kubadilisha ibada. Mtume swallallahu alayhi wasallama na warithi wake, wanazuoni wa madhehebu ya ahli sunna "rahimahumullahu taala", wameelezea kwa ufasaha juu ya namna ya utekelezaji wa ibada hizo. Kila mtu anatakiwa kujifunza mambo haya na kuyafuata.

Ningependa kufupisha maneno kwa kusema kwamba kiini cha wadhifa wa muislam ni kuwa na itikadi sahihi, kusema yaliyo sahihi na kufanya yaliyo sahihi.

Wanazuoni wa kiislm na magwiji wa kisufi "rahimahumullahu taala" wanasema kwamba wajibu wa kwanza wa binaadamu ni kuwa na imani, amal na ikhlas. Furaha ya duniani na akhera inapatikana kwa haya matatu. Amal hufanyika kwa moyo na ulimi, yaani mambo yanayofanyika kwa maneno na vitendo. Kazi ya moyo ni tabia. Ikhlas maana yake ni kufanya mambo yote na amali zote kwa ajili ya kupata radhi za Allahu taala na mapenzi yake.